# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

## Kikao chacha Thelathini na Tatu – Tarehe 21 Mei, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**NAIBU SPIKA:** Hati za kuwasilisha Mezani Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa niaba yake Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mheshimiwa Exaud Kigahe.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**
Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Fakharia Shomari.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu utekelezaji wa majukumu na bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali na tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 272

### Hitaji la Wodi ya Wanaume, Akina Mama na Watoto Frelimo Iringa

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wanaume, akina mama na watoto katika Hospitali ya Wilaya ya Frelimo katika Manispaa ya Iringa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Iringa (Frelimo) imeanza kufanya kazi kama Hospitali ya Halmashauri mwezi Februari, 2012 na kusajiliwa rasmi mwaka 2013. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali iliipatia Halmashauri ya Manispaa ya Iringa shilingi milioni 400 kwa ajili ya upanuzi wa hospitali ambapo jengo la maabara na jengo la mionzi yalijengwa na kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu iliyopo katika Hospitali ya Frelimo ni pamoja na jengo la utawala, jengo la huduma za wagonjwa wa nje *(OPD),* jengo la huduma za maabara, jengo la huduma za mionzi, jengo la kufualia na jengo la huduma za afya ya uzazi na mtoto. Miundombinu inayokosekana katika hospitali hii ni pamoja na jengo la upasuaji, wodi za kulaza wagonjwa, jengo la kuhifadhi maiti na jengo la kutunzia dawa. Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imetenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya watoto, wodi ya wanaume na wodi ya wanawake magonjwa mchanganyiko *(medical ward).*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini niseme kwamba Hospitali ya Frelimo ilijengwa ili kupunguza msongamano mkubwa sana uliopo katika Hospitali yetu ya Mkoa na mpaka sasa hivi tunashukuru kwamba tumeweza kupata milioni 500, lakini

hakuna hata wodi moja toka mwaka 2012 imeanzishwa, lakini pia tushukuru kwa hizi shilingi milioni 400 ambazo tumepewa kwa ajili ya kujenga majengo ya maabara na uchunguzi.

Sasa ni lini Serikali italeta vifaa kama vya *X-Ray, MRA, CT Scan* ili sasa wananchi wa Iringa wasiendelee kwenda kwenye Hospitali ya Mkoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Swali langu la pili, Sera ya Serikali ni kujenga vituo vya afya kila kata. Lakini Manispaa yetu ya Iringa ina kata 18 na ina vituo viwili tu vya Ngome na Ipogolo, vituo ambayo kwa kweli ni vichakavu mno na havijawahi kufanyiwa ukarabati wowote toka vimeanzishwa. Na tulitegemea kwamba hivi vituo…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati uliza swali.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Kuna *population* karibu ya watu laki mbili.

Je, ni lini Serikali sasa hivi itaboresha hivi vituo vya afya ili viweze kufanya huduma ya upasuaji ili kupunguza msongamano mkubwa uliopo katika Hospitali yetu ya Mkoa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru kwa kutambua kwamba Serikali imeendelea kuwekeza fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Hospitali hii ya Manispaa ya Iringa - Frelimo inatoa huduma na kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimhakikishie kwamba, kama ambavyo tumeweka katika mipango yetu katika mwaka wa fedha ujao tutaendelea kutenga fedha kwa awamu ili kuhakikisha wodi zote katika hospitali ile zinajengwa, zinanakamilika ili ziweze kutoa huduma bora zaidi kwa wananchi wa Manispaa ya Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimhakikishie kwamba vifaa tiba ni moja ya kipaumbele cha Serikali na ndio maana katika bajeti yetu 2021/2022 tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 14 kwa ajili ya kununua vifaa tiba katika vituo vyetu na hospitali zetu. Kwa hiyo, nimuhakikishie hospitali hii pia itapewa kipaumbele kuhakikisha kwamba tunakwenda kupeleka vifaa tiba katika hospitali ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatu kuhusiana na vituo vya afya tutaendelea kujenga na katika mwaka wa fedha ujao Manispaa ya Iringa ni moja ya Manispaa ambazo zitajengewa vituo vya afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hali inayoonekana Manispaa ya Iringa yaani inafanana moja kwa moja na hali iliyopo kwenye Halmashauri ya Masasi. Kwa sababu ni kata 18 kama ilivyo, lakini hali kadhalika vituo vya afya viwili na hali ni mbaya kabisa.

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu je, ni lini Serikali itatuwezesha kuwa na vituo vya afya zaidi, maana yake vituo viwili vya afya ni vichache?

Lakini pili, je,...

**NAIBU SPIKA:** Unauliza swali moja tu la nyongeza Mheshimiwa. Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, asante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mchungahela, Mbunge wa Jimbo la Lulindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri ya Masasi Vijijini katika mwaka wa fedha kuna fedha ambazo zimetengwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa ajili ya kujenga vituo vya afya. Kwa hiyo, naomba nimuhakikishie kambwa pamoja na bajeti yetu 2021/2022 kutenga fedha kwa ajili ya kujenga vituo vya afya kwa mapato ya ndani lakini pia kwa fedha za Serikali Kuu tutaendelea kutenga fedha kuhakikisha jimbo hilo pia linapata vituo vya afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali fupi.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa swali la nyongeza.

Kama ulivyosimamia hospitali ya Makandana na kupata wodi ya wanawake bado tunashida ya *x-ray* wananchi wanaambiwa waende hospitali ya Igogwe. Ni lini Serikali itatupatia *x-ray* mpya katika hospitali ya Makandana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Wazir,i Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la nyongeza la

Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hospitali ya Halmashauri ya Rungwe maarufu kama Makandana ina tatizo la *x-ray* pamoja na juhudi za Serikali za kuboresha miundombinu mingine, kipaumbele pia ni kupeleka vifaa tiba zikiwemo *x-ray*. Na katika mipango ya fedha ya miaka ijayo tutahakikisha pia hasa mwaka ujao katika mgao wa *x-ray* lakini na vifaa tiba vingine tunaipa kipaumbele Halmashauri ya Rungwe kwa maana ya Hospitali ya Makandana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Hospitali hiyo inahudumia Wilaya ya Kyela, Ileje wote wanakwenda kutibiwa hapo, Busokelo, kwa hiyo kama hakuna *x-ray* tafadhali ufanye bidii kupeleka hapo hiyo *x-ray*.

Mheshimiwa Mwita Kembaki Michael, Mbunge wa Tarime Mjini sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 273

## Ardhi ya Mlima Nkongore Iliyokabidhiwa kwa Jeshi la Magereza

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI** aliuliza:-

Je, ni sheria ipi ambayo ilitumika kuchukua ardhi ya Mlima Nkongore kutoka kwa wananchi na kulipatia Jeshi la Magereza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa David Ernest Silinde majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**, **(MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi. Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali

la Mheshimiwa Mwita Kembaki Michael, Mbunge wa Jimbo la Tarime Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mlima Nkongore upo katika Halmashauri ya Mji Tarime na una eneo lenye ukubwa wa ekari 266.65. Eneo hilo halina mchoro wa mipango miji na halijamilikishwa. Wananchi wanaozunguka eneo hilo walikuwa wakiutumia Mlima Nkongore kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo ukataji kuni, uchomaji mkaa na kilimo, shughuli ambazo zilikuwa zinahatarisha mazingira ya Mlima Nkongore.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Novemba, 2017 Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Tarime ilikabidhi eneo hilo kwa Jeshi la Magereza ili kuhakikisha kuwa eneo hilo linalindwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 kwa maana ya *Environmental Management Act, 2004;* kifungu cha 58(1) na (2) ambacho kinazuia kufanya shughuli zozote zinazoweza kusababisha hifadhi ya mlima kuharibiwa. Halmashauri ya Mji Tarime kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inakamilisha taratibu za kulifanya eneo la Mlima Nkongore kuwa hifadhi. Hivyo, eneo la Mlima Nkongore litaendelea kuwa chini ya uangalizi wa Magereza hadi hapo taratibu zitakapokamilika na kulitangaza kuwa eneo hilo kuwa hifadhi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Kembaki. Michael, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza.

Ningependa kujua, kwasababu wamesema kwamba wananchi wale ambao walikuwa wanalima katika mlima ule walikuwa wanaharibu mazingira na bado magereza ambao wanapewa eneo lile wameendeleza kilimo kama walivyokuwa wanafanya wananchi.

Sasa ningependa kujua kilimo cha wale waliopewa Magereza wao hawaharibu mazingira au wananchi ndio wanaharibu mazingira?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ningependa kujua kama Mlima Nkongole ndio pekee ambao Serikali imeona kwamba uhifadhi lakini ukienda maeneo kama Mwanza wananchi wanaishi mlimani.

Je, ni mlima Nkongole peke yake ndiyo imeonekana ni hifadhi au iutumie au kwa milima yote ambayo ipo katika nchi hii ndiyo inayohifadhiwa na Serikali? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwita, Mbunge wa Tarime Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ajenda ya uharibifu wa mazingira, haijalishi mtu ama taasisi kama watu binafsi wanaharibu mazingira, kama Jeshi la Magereza linaharibu mazingira ama taasisi yoyote inaharibu mazingira wote ni waharibifu wa mazingira. Kwa haina *excuse* ya aina yoyote na kutokana na jibu la msingi Naibu Waziri, Ofisi ya Rais - TAMISEMI alivyokuwa akijibu hapa alieleza wazi kama eneo hilo lipo katika mchakato katika maeneo lindwa. Sio eneo hilo peke yake, isipokuwa kuna maeneo mengine ya fukwe na maeneo mengine ambayo sisi Serikali tumeona kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 sasa kuna mchakato wa kuainisha maeneo hayo yote.

Kwa hiyo, tuseme kama Jeshi la Magereza licha ya kukabidhiwa wanaharibu mazingira maana yake jambo hilo halifai na ofisi yetu inasema jambo hilo tutaendelea kulisimamia kwa karibu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa nini maeneo mengine watu bado wanaendelea kujenga nyumba. Tumesema sasa hivi tutakuwa nimetoa maelekezo mahasus katika upande wa mazingira na ndio maana katika suala zima ambalo tutalizindua siku ya tarehe 5 Juni, 2021 Kampeni Kabambe ya Kimazingira miongoni mwa mambo hayo tutakayokwenda kuyaainisha ni suala zima la utoaji elimu katika suala zima la utunzaji wa mazingira.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge sote tushirikiane pamoja katika ajenda kubwa ya kulinda mazingira hususan kuilinda nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, tuendelee na swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 274

**Kuipandisha Hadhi Hospitali ya Mji Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Hospitali ya Mji Tarime isipandishwe hadhi na kuwa Hospitali ya Kanda Maalum ya Tarime na Rorya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mji Tarime ina Wodi nane na vitengo mbalimbali vya huduma ikiwemo maabara, jengo la mionzi, chumba cha upasuaji, huduma za mama

na mtoto, chumba cha dawa, chumba cha magonjwa ya akili, macho, duka la dawa lakini pia miundombinu mingine. Hospitali hii inahudumia wastani wa wagonjwa 140 wa nje *(OPD),* lakini inahudumia wagonjwa 70 wanaolazwa kwa siku. Hospitali ina jumla ya vitanda 180.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanda ya Ziwa tayari ina Hospitali ya Rufaa ambayo ni Hospitali ya Bugando iliyopo Mkoa wa Mwanza. Hivyo, Serikali haikusudii kuipandisha hadhi Hospitali ya Mji Tarime kuwa Hospitali ya Rufaa ya Kanda Maalum ya Tarime na Rorya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko swali la Nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mji wa Tarime mpaka leo imesajiliwa kama Hospitali ya Wilaya na kiuhalisia inahudumia wananchi wote wa kutoka Tarime Vijijini kwa huduma za upasuaji, kutoka Rorya, lakini pia watu wengine wanatoka nje ya nchi kwa maana ya kule Kenya tuko mpakani.

Ningetaka kujua ni kwa nini Serikali haijaifanya hospitali hii ili iweze kupata stahiki kama Hospitali ya Wilaya kama vile ilivyo Hospitali ya Kahama Mjini ambayo inahudumia Ushetu na Msalala, kama vile ilivyo Hospitali ya Nzega Mjini ambayo inahudumia Bukene na Nzega Vijijini ili sasa ihudumie sio kwa idadi ya watu wa Tarime Mji bali kwa idadi ya watu halisia wa kutoka Wilaya nzima ya Tarime na wengine kutoka Rorya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kupelekea kupokea watu wengi nje ya Tarime Mji, hospitali ile inaelemewa, haina matabibu wa kutosha, na kama nilivyosema awali wanaleta fedha chache, leo hata ukienda *mortuary* unakuta ina *burst* kwa sababu inachukua watu wote kutoka nje.

Ningetaka kujua ni lini Serikali itapanua chumba cha kuhifadhi maiti ili sasa wakati mkibadilisha usajili kuwa wa Wilaya na kuweka stahiki za Wilaya ili *mortuary* ile iweze kupokea Watanzania ambao wamekutwa wamefariki na kuja kuhifadhiwa pale Tarime Mji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba hospitali ya Mji wa Tarime inahudumia pamoja na wananchi wa kutoka katika Halmashauri za jirani na Tarime na ni utaratibu wa kawaida katika hospitali zetu ambazo mara nyingi zipo mipakani, lakini hata zile ambazo zinahudumia wananchi ambao wapo karibu na Halmashauri hiyo.

Kwa hiyo, kuna baadhi ya hospitali za Halmashauri nchini kote ambazo pamoja na wananchi wa ndani wa Halmashauri husika pia zinahudumia wananchi wanaotoka katika Halmashauri nyingine, ni suala la kawaida na utaratibu wetu sisi katika afya hatuna mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nitambue kwamba ni kweli tunafahamu hospitali hii inazidiwa na wagonjwa, lakini takwimu zimeonesha kwa wastani kwa siku wagonjwa wanaolazwa ni 70 lakini pia 140 wa *OPD*. Na Serikali inatambua kwamba tunahitaji kuendelea kuboresha miundombinu katika hospitali hii na sisi tutaendelea kuhakikisha kwamba tunaongeza idadi ya watumishi kwa maana ya waganga na wauguzi ili waweze kuendana na mzigo wa hospitali hii. Lakini pia ujenzi wa *mortuary* ni kipaumbele katika Serikali yetu, lakini pia katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili nilichukue ili twende na sisi tukalifanyie tathmini kuona kwa maana Serikali Kuu na Halmashauri namna gani tutafanya ili tuweze kuondoa adha ya kuwa na *mortuary* ndogo na kuboresha huduma hizi kwa wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, swali fupi la nyongeza.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotokea Tarime hata Maswa kinatokea hicho kwamba Hospitali ya Maswa inazidiwa kwa wagonjwa na imekadiriwa kwanza kuwa Hospitali ya Wilaya, lakini inahudumia zaidi ya Wilaya moja. Kuna wagonjwa wanatoka Itilima, wagonjwa wanatoka Wilaya ya Meatu na wagonjwa wa Wilaya ya Maswa. Hospitali inaonekana kama ya Wilaya lakini inazidiwa kwa sababu watu wengi wanakwenda pale.

Kwa hiyo nilikuwa naomba aji-*commit* Mheshiwa Naibu Waziri je, na Maswa atai-*consider* na yenyewe iweze kuongezewa hadhi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameongea kuhusiana na Hospitali ya Halmashauri ya Maswa ni hospitali ambayo ni kongwe, lakini ina hudumia wananchi wengi wa ndani ya Halmashauri ya Maswa, lakini pia na Halmashauri zingine kama Itilima na

Meatu. Lakini naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali iliona hilo na imelifanyia kazi. Kwanza kwa kujenga Hospitali ya Halmashauri katika Halmashauri ya Wilaya ya Itilima ili kuhakikisha wananchi wa Itilima ambao walikuwa wanalazimika kufika Maswa sasa watatibiwa Itilima, lakni pia imeboresha sana hospitali ya Halmshauri ya Meatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na hayo bado tunatambua kwamba kuna kazi ya kufanya katika Hospitali ya Halmashauri ya Maswa na ni muhakikishie tunaji-*commit* kwamba tutaendelea kuhakikisha tunaboresha miundombinu, vifaa tiba na upatikanaji wa wataalam ili tuhakikishe hospitali ile inatoa huduma bora zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali fupi la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Wilaya ya Urambo ina hospitali ya wilaya iliyojengwa mwaka 1975 na hali yake siyo nzuri. Je, Serikali yetu inayosikiliza maombi ya wananchi ni lini itakuja kuingalia itengenezwe upya ili iende na wakati? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Halmashauri ya Urambo ni kweli ni hospitali kongwe sana ambayo imejengwa mwaka 1975 na bahati njema katika ziara yangu pia nilifika katika hospitali ile tukashirikiana vizuri sana na Mheshimiwa Mama Margaret Sitta, tukaikagua hospitali ile na kuona kwa

kweli tunahitaji kuweka mpango mkakati wa kuzikarabati hospitali kongwe zote nchini ikiwepo ya Hospitali hii ya Urambo.

Kwa hiyo, naomba nimuhakikishie kwamba mipango ya Serikali tumeshapanga katika mwaka ujao wa fedha kuanza kukamilisha ujenzi wa Hopitali za Halmashauri katika Halmashauri zote ambazo hazina Hospitali za Halmashauri. Lakini baada ya hapo tutakwenda kwenye awamu ya kukarabati au kujenga kulingana na tathmini hospitali nyingine za Halmashauri katika Halmashauri zenye hospitali kongwe sana ikiwepo Urambo.

Kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba suala hili tunalifanyia kazi na tutahakikisha kwamba tunalitekeleza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, swali fupi.

**MHE. VITA RASHID KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa Serikali ilitufanyia kazi nzuri sana Jimbo la Namtumbo kutujengea Kituo cha Afya cha Mtakanini na kukarabati Kituo cha Afya cha Mji wa Namtumbo lakini vituo vya afya hivi viwili havina watumishi.

Je, Serikali ipo tayari sasa kutupangia watumishi ili ifanye kazi kama ilivyokusudiwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi ofisi ya Rais - TAMISEMi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipokee shukrani nyingi za Mheshimiwa Mbunge wa Namtumbo kwa kazi kubwa sana ambayo Serikali imefanya kuhakikisha inakarabati na kujenga vituo vya afya katika Jimbo la Namtumbo. Lakini nimhakikishie kwamba Serikali inatambua sana kwamba tuna upungufu wa watumishi katika vituo vile vya afya. Lakini kama tunavyoona, hivi sasa Serikali imetangaza ajira 2,796 za wataalam wa afya, lakini pia katika mwaka wa fedha tutakwenda kuomba vibali kuhakikisha kwamba tuna ajiri watumishi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba Jimbo la Namtumbo litapewa kiupaumbele kuhakikiha tunaendelea kupelekea watumishi pale na kuboresha huduma za afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante tuendelea na swali la Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini kwa niaba yake Mheshimiwa Joseph Mhagama.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba namba ya swali.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Namba 275.

Na. 275

**Kutatua Migogoro ya Mipaka ya Kiutawala**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA - K.n.y. MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua migogoro ya mipaka ya kiutawala baina ya Mikoa, Wilaya na Vijiji hapa nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutatua migogoro ya mipaka ya kiutawala baina ya Mikoa, Wilaya na Vijiji hapa nchini Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kusambaza Matangazo ya Serikali kwa maana ya *Government Notices au GN* yanayoonesha mipaka ya Wilaya na Mikoa kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote nchini; kKuunda vikundi kazi na kuvipeleka kwenye maeneo yenye migogoro ya mipaka ili kutatua migogoro; kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Matumizi Bora ya Ardhi nchini kwa kuhakikisha Vijiji, Kata na Wilaya zinaandaa na kutekeleza Mipango ya matumizi ya ardhi, kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera na Sheria za ardhi, kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba katika Halmashauri, kurasimisha makazi na kumilikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kutatua migogoro ya mipaka ya kiutawala baina ya Mikoa, Wilaya na Vijiji hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mhagama swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo, nilikuwa na swali la nyongeza.

Kwa vile migogoro hii kwa sehemu kubwa inachangiwa sana na kutokamilika kwa utengenezaji wa mipango bora ya matumizi ya ardhi katika Mikoa, Wilaya na Vijiji vyetu. Ni lini basi Serikali itakamilisha upimaji na utekelezaji

wa sera ya kuwa na mipango ya kuwa na matumizi bora kwa kila Kijiji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais–TAMISEMI, Mheshimiwa Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joseph Mhagama, Mbunge wa Madaba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge alikuwa anauliza kwamba moja ya sababu kubwa ya hii migogoro ni sisi ama Serikali kushindwa kwa wakati kukamilisha hii mipango ya matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwambie tu jambo moja kwamba ili Serikali iweze kupima hizo ardhi katika maeneo mengine yote. Ni lazima ngazi za Halmashauri zote nchini zipange bajeti ili watu/sisi kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi tuje tupime hayo maeneo ili kuhakikisha kabisa tunaondoa hiyo kero iliyopo.

Kwa hiyo, nizitake Halmashauri zote nchini kuhakikisha katika bajeti zao wawe wanatenga fedha kwa ajili ya upimaji wa ardhi ili kuhakikisha kwamba hii migogoro tunaiondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya ardhi katika ngazi za vijiji nafikiri ni kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba tutaendelea kuhamasisha ngazi za Halmashauri kuhakikisha wote wanafuata sheria lakini tutaendelea kutenga fedha na kuainisha maeneo yote ili kuondoa hii migogoro ambayo inaendelea kujitokeza kila wakati. Kwa sababu hilo ndiyo lengo la Serikali kuhakikisha kwamba migogoro hii ya mipaka pamoja na maeneo inatatuliwa kabisa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa jitambulishe.

**MHE. BAKARI HAMAD BAKARI:** Mheshimiwa Bakari Hamad Bakari.

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba yake, Mheshimiwa Bakari Hamad Bakari.

Na. 276

**Bima ya Afya Kwa Wahitimu wa Elimu ya Juu**

**MHE. BAKARI HAMAD BAKARI - K.n.y MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuwapatia Bima ya Afya wanafunzi wa elimu ya juu na wanaosubiri kupata ajira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMISI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuboresha huduma za bima ya afya kwa kuongeza kitita cha huduma na upatikanaji wa huduma kwa wanachama kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa kutekeleza mikakati mbalimbali yenye lengo la kuwawezesha wananchi wengi

kujiunga katika mfumo wa bima ya afya na hivyo kuwa na uhakika wa kumudu gharama za matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati inayotekelezwa ni pamoja na utekelezaji wa bima ya afya kwa wanafunzi wa elimu ya juu ambao hujiunga kwa kuchangia na kunufaika na huduma za bima ya afya kwa mwaka mzima. Vilevile kwa wale wanaosubiri kupata ajira, Mfuko wa Maendeleo wa Bima ya Afya una utaratibu wa umeandaa utaratibu wa vifurushi ambavyo vimezingatia uhitaji wa aina ya huduma, umri na ukubwa wa familia kwa kuwapatia wanachama wigo na kuchagua aina ya kifurushi kwa kulinganisha na mahitaji yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa kutambua umuhimu wa kila mwananchi kuwa na Bima ya Afya, Serikali inakamilisha rasimu ya muswada wa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambao utawasilishwa Bungeni mwezi Juni, 2021. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakari Bakari ameelewa majibu na ameridhika.

Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la nyongeza Je, Serikali iko tayari kushughulikia masuala ya bima za afya kwa wauguzi wastaafu wakianzia na Hospitali ya Mkoa wa Iringa ili watibiwe bila usumbufu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na wtoto majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni sahihi kwenye mwelekeo wetu huu wa Bima ya Afya kwa Wote tutachukua makundi yote, hakuna atakayebaki nyuma yakiwepo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Kichiki Lugakingira, Mbunge wa...

Samahani, Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 277

**Wanawake Kugharamia Matunzo ya Watoto**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwakomboa wanawake wanaobebeshwa mzigo mkubwa wa kugharamia matunzo ya watoto bila msaada wa baba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Mwanaidi Khamisi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMISI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu maswali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Viti Maalum kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kulithibitishia Bunge lako tukufu kuwa Serikali inatambua na kuthamini mchango mkubwa wanaotoa wanawake tangu enzi za kupigania uhuru na maendeleo ya nchi kwa ujumla hadi kufikia hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwakomboa wanawake hawa wanaobebeshwa mimba na kuachwa bila matunzo, Serikali imeandaa Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 ambayo pamoja na masuala mengine inatoa maelezo kuhusu matunzo kwa mtoto kutoka kwa wazazi wote wawili. Sheria hii kupitia kifungu cha 7(1), kifungu cha 8(1)(a)

mpaka (g), kifungu cha 8(2) na kifungu cha 9(3)(a) na (b) imetoa maelezo kwa wazazi kuhakikisha kuwa watoto wanapata mafunzo yote ya stahiki ili kuhakikishiwa kuwa haki sawa na ustawi wake vinatimizwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hii pia kupitia kifungu cha 44 (a) mpaka (e) na kifungu cha 45(1) pia imetoa maelezo endapo wazazi wa mtoto kama hawaishi pamoja na kama mtoto atakuwa anaishi na mzazi wake wa kike yaani mama, basi mzazi wa kiume atawajibika katika kugharamia malezi ya mtoto kulingana na kipato alichonacho na mazingira anayoishi mtoto husika. Aidha, sheria hii pamoja na kanuni zake imekuwa ni msaada mkubwa katika kuhakikisha kuwa mzigo wa kugharamia malezi ya watoto unawagusa wazazi wa pande zote mbili yaani baba na mama wa mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe rai kwa wananchi wote kuwa jukumu la kutunza familia ni la lazima watu wote wawili na asitokee mmojawapo kutegea kwa kutotoa matumizi. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema Lugangira swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, sheria zilizopo bado kuna changamoto kubwa sana katika eneo hili na ndiyo maana hata Chama cha Mapinduzi kwenye Ilani yake ya Uchaguzi ya mwaka 2020/2025 kimeliona hili na kimeahidi kwamba kitaelekeza Serikali kwenye ukurasa wake wa 145 inasema hivi; “Chama cha Mapinduzi kitaelekeza Serikali kuimarisha huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na matunzo kwa watoto.” Kwa msingi huu naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, je, Serikali haioni saa ipo haja ya kurekebisha sheria zilizopo ili gharama ya matunzo ya watoto iendane na hali ya uchumi wa sasa na maisha ya sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili kwa kuwa vitendo vya masuala ya familia vimezidi kushamiri; je, Serikali haioni sasa iko haja ya kuanzisha Mahakama ya Familia *(Family Court)* kama walivyofanya kwenye Mahakama ya Ardhi ili masuala haya ya matunzo ya watoto yaweze kubebwa kwa uzito unaostahili na kupanua wigo wa haki? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Mwanaidi Khamisi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMISI)**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaungana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna haja ya chombo maalum kitakachokuwa kinashughulikia masuala ya familia. Ushauri wake tumeupokea na tutaufanyia kazi kulingana na sheria zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, Serikali iweke kiwango cha matunzo kitakachozingatia hali ya uchumi ya sasa kusaidia matunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi kuwa huduma za matunzo ya watoto umetolewa kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019 kifungu cha 44(a) na (e) sheria hii imeipa mamlaka Mahakama kufanya maamuzi ya kuzingatia mambo yafuatayo; kuangalia kipato cha wazazi wote wawili, ulemavu wowote na uwezo wa kipato cha mzazi katika jukumu la kutunza mtoto, wajibu wa majukumu ya mzazi katika kutoa matunzo kulinganisha na majukumu ya kutoa matunzo kwa watoto, gharama za maisha katika eneo ambalo mtoto anaishi na

haki nyingine za kisheria ambazo mtoto anahitaji kupatiwa. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, akina mama kwenye swali hili tuwakilishwe na akina baba, Mheshimiwa Zacharia Issay swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kupitia Naibu Waziri, tatizo hili la watoto kutelekezwa limekuwa kubwa sana kuzalisha watoto wa mitaani.

Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kutazama upya sheria za kuzuia uwepo wa watoto wa mitaani kwa ajili ya wale wanaotelekeza watoto? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Issaay kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali inatambua kwamba tatizo hili ni kubwa na tunakiri kwamba kuna haja ya kufanya kitu cha ziada hapa kuweza kulidhibiti. Niseme kuelekea tarehe 16 Juni, 2021 tunapokwenda kuadhimisha siku ya Mtoto wa Afrika, hili nalo tutaliangalia tuliwekeje. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa kuwa limeonekana tatizo hili la kuongezeka kwa watoto wa mitaani na mimi siamini wanandoa kama wanaweza kutelekeza kulea watoto, ninaomba sasa akina mama wajaribu kupata elimu ama itolewe elimu zaidi wapunguze na wao ile huruma ili kupunguza watoto wa mitaani. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, nadhani ule ulikuwa ni ushauri. Serikali itoe elimu.

Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, changamoto ya wanawake kutelekezewa watoto imekuwa kubwa sana; je, Serikali haioni umuhimu wa kubadilisha kuleta mabadiliko ya Sheria ya Ustawi wa Jamii Bungeni ili iendane na hali halisi ya maisha ya sasa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Mwanaidi Khamisi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. MWANAIDI ALI KHAMISI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelipokea ombi la Mheshimiwa Mbunge na tutalifanyia kazi kwa mujibu wa sheria zilizopo ili wanawake waweze kupata haki zao kikamilifu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Mwandabila, swali kwa kifupi.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunduma ni sehemu mojawapo ambayo tunapata changamoto sana ya kuwa na idadi kubwa ya watoto waliotelekezwa na mara nyingi watoto hawa waliotelekezwa huwa wanakimbilia Ofisi ya Ustawi wa Jamii. Wanapofikiwa kule, Afisa wa Ustawi wa Jamii anapaswa kuwahudumia kwa huduma zote yule mtoto anazokuwa anahitaji mpaka atakapopata kituo cha kumpeleka. Lakini changamoto wanayoipata ni kwamba hawana fedha za kuwahudumia watoto hawa.

Je, ni lini Serikali itakuja na fungu maalum kwa ajili ya Maafisa wa Ustawi wa Jamii kuweza kuwahudumia watoto wao. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Dkt. Dorothy Gwajima majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea swali la nyongeza la Mheshimiwa Neema Mwandabila; ni kweli, Serikali inatambua kwamba bado hatujawekeza vya kutosha kwenye eneo hilo kuwawezesha Maafisa Ustawi wa Jamii wetu waweze kufanya kazi hizi. Naomba niahidi kwamba tutafanya tathmini tuone ili kwenye kipindi kijacho cha bajeti tuweze kuanzisha namna gani ya kuwawezesha hawa Maafisa Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wanawake chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Shally Raymond ni vizuri pengine na sisi tuchukue hatua kwenye mambo haya kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Hussein Amar, lazima wanawake tuondokane na hii dhana ya mtu kubebeshwa mimba kwa sababu yeye ndiye anayebeba mimba.

Kwa hivyo, lazima sisi tuzungumze na wanawake watumie ule uwezo walionao, aidha ule wa ushawishi au wafanye hayo mambo ya kubeba mimba kwa watoto wanaoweza kuwalea hata kama huyo mwanaume hayupo. Lazima tufikie huko, kwa sabbau tusiwe kila saa tunafikiri kwamba watoto kuwepo mtaani ni halali kwa sabbau kuna mwanaume ameondoka kwenye maisha ya mwanamke, hapana. Nadhani ni kazi yetu Mama Shally Raymond lazima hawa wanawake ambao wanatutegemea kule nje tuweke msingi mzuri. *(Makofi)*

Watoto wetu wa kike hawataweza kufika sehemu kubwa hizi tunazozungumzia Rais mwanamke sasa hivi, hatuwezi kupata mwanamke Rais kama tunafikiria watoto wa mitaani watajaa tu huko kwa sababu kuna wanaume

wanakimbia majukumu yao. Kwa hiyo, tuwafundishe vizuri wanawake wafanye maamuzi sahihi. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea na swali la Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe sasa aulize swali lake.

Na. 278

**Mpango wa Kuwafutia Wafanyabiashara wa Ndani Madeni ya Nyuma**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufuta madeni ya muda mrefu kwa wafanyabiashara wa ndani yatokanayo na ukosefu wa elimu juu ya matumizi sahihi ya mashine za *EFD* wanayodaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Masauni, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Henry Maganga, Mbunge wa Mbogwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali ilitoa msamaha kwa wadaiwa wa kodi ili kuongeza makusanyo. Msamaha huu ulihusisha riba na adhabu zilizoambatana na madeni yote yaliyolimbikizwa kwa miaka ya nyuma. Msamaha huu ulilenga kusamehe malimbikizo ya nyuma ya riba na adhabu kwa kiwango cha asilimia 100 kwa wafanyabiasha wote hapa nchini ambao walikuwa na malimbikizo ya madeni ya kodi. Msamaha huo ulitolewa kwa kipindi cha miezi sita kilichoanzia tarehe 1 Julai, 2018 mpaka tarehe 31 Desemba, 2018 ambapo kutokana na kusuasua kwa utekelezaji wake, Serikali iliongeza muda wa msamaha huo kwa miezi sita ili wafanyabiashara

waliokuwa na madeni hayo kuweza kukamilisha malipo husika yaliyotokana na msamaha huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hiyo ya marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438 ilitarajiwa kuongeza mapato ya Serikali na kukusanya malimbikizo ya madeni ya nyuma ya kodi pamoja na kuinua kiwango cha ulipaji kodi kwa hiyari kwa zaidi ya asilimia 10.

Hata hivyo, licha ya nia nzuri ya Serikali ya kufuta riba na adhabu ili kuwawezesha walipa kodi wenye madeni sugu ya kodi kuyalipa kwa awamu ili kurahisisha mwendelezo wa biashara zao, wengi wao hawakulipa kodi hizo hata baada ya kuingia mikataba na *TRA* na hata baada ya Serikali kuongeza muda wa ziada wa kufanya malipo ya kodi husika yaliyotokana na msamaha huo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Henry Nicodemus Maganga swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nimesikia majibu ya Serikali lakini ukweli bado wafanyabiashara wana kilio hapa nchini, hawana raha na Serikali yao kulingana na madeni hayo maana hawakuwa na elimu ya hizi mashine za *EFD.* Hivyo sasa, naomba Mheshimiwa Waziri utoe kauli ili nchi nzima wajue kwamba walishasamehewa hayo madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili je, ni lini sasa Serikali itafuta madeni ya mgodi wa Bulyanhulu ili waweze kutimiza makubaliano yao katika mkataba wao wa ujenzi wa barabara itokayo Kahama ya lami kwenda Bulyanhulu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la nyongeza la pili unao uhuru wa kujibu kama majibu unayo; kama huna, utampatia majibu kwa maandishi kwa sababu ni swali mahsusi kwa ajili ya hiyo kampuni kufutiwa madeni.

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango ya Mheshimiwa Nicodemus Maganga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza suala la kauli ya Serikali kuhusu kusamehe madeni haliwezi kutolewa kwa utaratibu huu. Msamaha wa madeni unatokana na uko kwa mujibu wa sheria, hata yale maamuzi ambayo yalisababisha kusamehe madeni ya kipindi kile yalitokana na utaratibu wa kisheria ambao ulipitishwa na Bunge hili. Kwa hiyo, hatuwezi kusimama hapa tukatoa tu tamko la kusema tunamsamehe nani madeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili vilevile kuhusiana na kusamehe madeni na kwenyewe kuna *repercussions* zake. Kwa mfano, *best practice* wataalam wanasema kwamba utaratibu ule wa kusamehe madeni hauwezi kufanywa kila wakati kwa sababu unaathiri wigo mpana wa ukusanyaji kodi chini.

Kwa hiyo, lengo kubwa lilikuwa ni kuhakikisha kwamba kwanza tunawasaidia wale ambao walikuwa na madeni ya muda mrefu, lakini la pili ilikuwa ni kuhakikisha kwamba tunakusanya kwa kipindi kile ambacho maamuzi yale yalitoka kwa haraka.

Kwa hiyo, ili msamaha mwingine utoke, lazima tukae chini na kuweza kufanya tathmini na utafiti wa kina kupima athari na faida za kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusiana na hoja ya Bulyanhulu napokea maelekezo yako nadhani ni suala mahsusi kwa hiyo basi tutalifanyia kazi na kumpatia majibu Mheshimiwa Mbunge baada ya kupata hizo takwimu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, sasa aulize swali lake.

Na. 279

**Kuwaandaa Wakulima Wadogo wa Miwa – Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaandaa wakulima wadogo wa miwa *(outgrowers)* wa Bagamoyo ili kuwa na uzalishaji mkubwa na wenye tija?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Sukari cha Bagamoyo kimejiwekea mipango inayotekelezwa kwa awamu. Awamu ya Kwanza, kiwanda kinatarajia kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 2,050 za mashamba yake. Hadi kufika mwezi Desemba, 2020 jumla ya hekta 1,700 zimelimwa, kati ya hizo hekta 750 zimewekewa mfumo wa umwagiliaji wa matone.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wadogo wa miwa *(outgrowers scheme)* watahusishwa katika utekelezaji wa Awamu ya Pili ambayo inatarajia kuanza mwaka 2022/2023. Katika awamu hiyo, Serikali kwa kushirikiana na mwekezaji imetenga eneo lenye hekta 3,600 kwa ajili ya wakulima wa miwa *(outgrowers)* ambao watazalisha na kuuza miwa yao katika Kiwanda cha Miwa cha Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwanda unategemewa kukamilika ifikapo Juni, 2022 kwa hiyo miwa ya wakulima itakomaa wakati kiwanda kimeanza kufanya kazi. Hivyo, wakulima hao watakuwa na uhakika wa soko la miwa watakayozalisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Muharami Shabani Mkenge, swali la nyongeza.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi huu ni mpya kabisa katika Ukanda wetu wa Pwani ya Bagamoyo na Kata za Yombo, Magomeni, Nia Njema, Makurunge pamoja Fukayosi, wamejiandaa kuupokea mradi huu kwa ajili ya kilimo cha miwa. Sasa, je, ni lini Serikali itawapa mafunzo hawa watu, ili waweze kuzalisha kilicho bora kwa ajili ya kupeleka kiwandani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali namba mbili; katika jibu la msingi Serikali imetenga hekta 3,600 kwa ajili ya *outgrowers.* Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza akanionesha hizo hekta kusudi nisikae katika mikutano ya watu nikawaambia kwamba tumetengewa hekta 3,600 wakati mimi mwenyewe Mbunge sijazijua bado? Yuko tayari kwenda kunionesha ili nikienda katika mikutano niwaambie wananchi wangu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Muharami, Mbunge wa Bagamoyo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo yataanza hivi karibuni ambayo tutashirikiana na mwekezaji katika wakulima wote watakaoingia katika hiyo *scheme. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwa niko tayari kwenda, baada ya Bunge hili tutakwenda pamoja tutafanya ziara na tutaelekezana wapi hiyo *scheme* ya *outgrowing* itafanyika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 280

**Ukarabati wa Meli ya Mv. Liemba**

**MHE. IRENE A. NDYAMKAMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakarabati Meli ya Mv. Liemba pamoja na kujenga meli mpya ambazo zitachochea ukuaji wa uchumi wa Mkoa wa Rukwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabhe Waitara, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, asante. kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Kampuni ya Huduma za Meli imetenga kiasi cha shilingi bilioni 135 katika mwaka huu wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kutekeleza miradi tisa ya ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli katika Ziwa Victoria na Tanganyika. Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na mradi wa ukarabati wa meli ya Mv. Liemba ambayo tayari umeshapata mkandarasi na taratibu za kusaini mkataba zinakamilishwa na itasainiwa mwanzoni mwa mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na kutekeleza mradi wa ukarabati wa meli ya Mv. Liemba katika Ziwa Tanganyika, Serikali pia imepanga kutekeleza miradi ya ujenzi wa meli mpya ya kubeba abiria 600 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Tanganyika, ujenzi wa meli mpya ya kubeba shehena ya

mizigo katika Ziwa Tanganyika na ukarabati mkubwa wa meli ya kubeba shehena ya mafuta ya MT. Sangara katika Ziwa Tanganyika. Mikataba ya miradi hiyo ipo katika hatua za mwisho kusainiwa mapema mwanzoni mwa mwezi Juni, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumai yangu kuwa, kukamilika kwa miradi hii kutaondoa adha ya usafiri kwa njia ya maji katika Ziwa Tanganyika na mikoa jirani na Kigoma. Aidha, kutaimarisha na kuifanya nchi yetu kuwa kiungo kikubwa cha soko pana la pamoja linalokisiwa kuwa na idadi ya watu takribani milioni 10 wanaoishi pembezoni mwa ziwa hili katika nchi za Mashariki na Kati ya Afrika ikijumuisha nchi ya Tanzania, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Burundi na Zambia, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Irene Ndyamkama, swali la nyongeza.

**MHE. IRENE A. NDYAMKAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa meli hii imedumu takribani miaka 100 na ilikuwa mkombozi wa Wana-Ziwa Tanganyika, nikimaanisha Rukwa, Katavi na Kigoma. Je, ni lini sasa Serikali itakarabati meli hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Ziwa Tanganyika lina uchumi mkubwa na Serikali imetujengea bandari mbili, Bandari ya Kasanga na Bandari ya Kabwe. Ni lini Serikali itatujengea meli mpya Mkoa wa Rukwa kama mikoa mingine ili wananchi wa Mkoa wa Rukwa wafaidike na Serikali yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Waitara, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, asante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu maswali

mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Irene Ndyamkama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba, tayari Mv. Liemba ipo kwenye hatua nzuri kwa sababu mkandarasi amekwishapatikana na mwezi ujao tuna-*sign* mkataba ili kazi iendelee. Kwa hiyo, katika hili la Mv. Liemba kama ambavyo Wabunge wengi wa Mkoa wa Katavi na maeneo ya jirani walizungumza wakati wa bajeti, tumezingatia linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali la pili tumepokea hoja yake ya kupata meli ya Mkoa wa Katavi kama mikoa mingine. Tutalifanyia kazi kadiri ambavyo Serikali itapata fedha za kutekeleza hilo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Maji. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mbunge wa Msalala, sasa aulize swali lake.

Na. 281

**Hitaji la Maji – Msalala**

**MHE. IDDI K. IDDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kusambaza maji kutoka Mradi wa Maji Mhangu – Ilogi katika Kata za Lunguya, Ikinda, Shilela, Sogese na Mega katika Halmashauri ya Msalala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Msalala, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa

Maji wa Mhangu – Ilogi awamu ya kwanza ambayo ilihusisha ujenzi wa bomba kuu kutoka Mhangu hadi Ilogi umbali wa kilometa 56 kwa gharama ya shilingi bilioni 13.86 na kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi huu kwa awamu ya pili ambayo itahusisha usanifu wa miundombinu ya usambazaji maji na ujenzi wa miundombinu hiyo katika kata zote tano ambapo mradi unatarajiwa kuanza mwanzoni mwa mwaka 2022.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, swali la nyongeza.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nilitaka niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko juu ya ongezeko la bili za maji katika Kata ya Isaka, Kata ya Bugarama; je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuunda tume na niombe au Waziri mwenyewe husika uweze kufika katika Kata ya Bugarama na Kata ya Isaka, ili kuweza kubaini nini chanzo cha ongezeko la gharama za maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kuna fedha iliyobaki katika mradi ambao unatoka Kagongwa – Isaka; je, Serikali ina mpango gani wa kutumia fedha hizo kuweza kuanza kusambaza maji katika Kata ya Mwakata? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Iddi kwa kazi kubwa, nzuri anayoifanya katika Jimbo lake la Msalala, lakini kubwa ambalo nataka kulisisitiza ni haki ya mwananchi wa Tanzania kupatiwa maji na mwananchi naye asisahau kwamba ana wajibu wa kulipia bili za maji. Sisi kama Wizara

ya Maji tutasimamia bili hizo zisiwe bambikizi. Tumetoa maelekezo mahususi kwa Taasisi ya *EWURA* yenye jukumu la kuidhinisha bili za maji na ripoti wamenikabidhi hivi karibuni, tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu swali lake la pili, tunakiri kuna fedha ambazo zimebaki katika mradi wa Isaka – Kagongwa. Tumetoa maelekezo mahususi kwa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira - Kahama, kufanya kazi ile kwa *force account* kuhakikisha vijiji vyote ambavyo vimebaki vipatiwe huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante; nilikuwa naomba kuuliza ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi wa Mradi wa Maji ya Kikafu ambao unalenga kuhudumia Kata ya Masama Kusini, Muungano, Bomang'ombe na *KIA?* Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Hai, kiukweli amekuwa mfuatiliaji mkubwa sana, ni mradi ambao amekuwa akiupigia kelele.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa tumekwishatoa kibali na tumetoa maelekezo kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira - *MUWSA,* Moshi kuhakikisha kwamba anatangaza kazi hiyo na mkandarasi apatikane mara moja kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, nikiwa mwakilishi wa Jimbo la Kawe mwaka 2010 mpaka 20 tulifanikiwa kwa kiwango kikubwa sana kupunguza tatizo la maji, lakini kuna kata kadhaa ambazo zimebaki bado ni sugu sana. Kata ya Wazo, hususan maeneo ya Nyakasangwe, Mivumoni, Salasala, Kata ya Mbezi Juu eneo la Mbezi Mtoni na Sakuvede. Sasa nataka tu *commitment* ya Waziri ni lini changamoto hii itafikia ukingoni? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nijibu swali na ninashukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kukiri kwamba kuna jitihada kubwa ambayo Serikali imefanya katika Jiji la Dar es Salaam na nikiri bado kuna changamoto katika eneo la Mivumoni na maeneo ambayo ameyataja ya Wazo, lakini kuna kazi kubwa ambayo inafanywa juu ya utandazaji wa miundombinu na usambazaji wa maji inayofanywa na *DAWASA,* zaidi ya kilometa 1,600 ambazo tutaenda kutekeleza. Nataka nimhakikishie sisi kama Wizara tutasimamia kuhakikisha maeneo haya yanapata maji kwa haraka na wananchi waweze kupata maji, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumalizie swali la mwisho. Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali, kwa niaba yake swali litaulizwa na Mheshimiwa Masache Kasaka.

Na. 282

**Kukamilisha Ujenzi wa Mradi wa Maji Luguda – Mawindi – Mbarali**

**MHE. MASACHE N. KASAKA K.n.y. MHE. FRANCIS L. MTEGA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji Ruduga – Mawindi ili kuwatua ndoo kichwani akina mama wa Mbarali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, majibu.

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha wananchi wa Wilaya ya Mbarali wanapata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza, Serikali ilianza ujenzi wa Mradi wa Maji wa Luduga – Mawindi kwa lengo la kuhudumia vijiji sita vya Kangaga, Mkandami, Itipingi, Manienga na Ipwani kwa gharama ya jumla ya shilingi bilioni. 9.66. Utekelezaji wa mradi huo umepangwa kwa awamu *(lots)* tano. Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa awamu zote ni ujenzi wa banio la maji, mtandao wa bomba jumla ya kilometa 139, matanki sita yenye ujazo wa lita 150,000 moja, lita 100,000 matatu na lita 75,000 mawili na vituo vya kuchotea maji 119.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa banio la maji, mtandao wa bomba jumla ya kilometa 54 na tanki la kuhifadhia maji la lita 150,000, ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 12. Kwa kazi zilizokamilika wananchi wa Kijiji cha Kangaga wameanza kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 utekelezaji wa mradi utakamilika na huduma ya maji itapatikana katika vijiji vyote na kunufaisha wananchi zaidi ya 26,000. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masache Kasaka, swali la nyongeza.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri.

Naomba niulize maswali madogo mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali ilitenga fedha kujenga visima nane vya maji katika Wilaya ya Chunya katika Kata za Sangambi, Shoga, Matunda, Skambikatoto, Rualaje, Nkung'ungu na Soweto mpaka Itumbi, lakini mpaka sasa hivi fedha hizo hazijatoka.

Je, ni lini fedha hizi zitatoka ikiwa imebakia takribani siku 40 mwaka huu wa fedha uishe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwenye chanzo cha maji cha Chunya Mjini kuna takribani visima nane vilichimbwa, lakini visima viwili pekee ndivyo vinavyofanya kazi.

Je, ni kwa nini visima hivi vingine, takribani sita, havifanyi kazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu kwa maswali hayo.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Mbarali kuwa miongoni mwa Wabunge ambao wamepitisha bajeti yetu na kutupatia fedha zaidi ya shilingi bilioni 680. Kwa hiyo, jukumu letu sisi kama Wizara ni kuhakikisha tunakwenda kutatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu fedha ambazo kwa ajili ya uchimbaji wa hivyo visima; nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya Saa 07:00 naomba tukutane ili tuweke *commitment* ya Wizara tuweze kuku-*support* kuhakikisha wananchi wako wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu suala zima la visima pale katika eneo la Chunya Mjini, kuna visima nane, viwili vinafanya kazi. Nimetoa maelekezo mahususi. Wizara ya Maji inafanya mageuzi makubwa katika kuhakikisha

Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama kama Mheshimiwa Rais maelekezo yake ametupatia sisi Wizara ya Maji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, maelekezo ambayo tumeyatoa kwamba, kwa wataalam wetu wote kusimamia na kufuatilia, hususan aidha visima ama miradi ya maji, kuhakikisha vyote vinafanya kazi na wananchi waende kupata huduma ya maji safi, salama na yenye kutosheleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipatia nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Muleba iko pembezoni mwa Ziwa Victoria, lakini inalo tatizo kubwa la uhaba wa maji na tunao mradi mkubwa ambao usanifu na upembuzi yakinifu umekamilika.

Je, ni lini sasa Serikali itaanza kujenga mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwa ajili ya kata sita za Wilaya ya Muleba; Kata ya Gwanseri, Kata ya Muleba Mjini, Kata ya Magata Karutanga, Kikuku, Kagoma na Buleza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Muleba kwa namna bora na nzuri ambayo kwa kufuatilia wananchi wake waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa ambalo sisi kama Wizara na Bunge lako tukufu, sisi kama Wizara ya Maji tumesema hatuna sababu tena ya Watanzania kulalamika suala la maji. Mwenyezi Mungu ametupa rasilimali toshelevu, tuna rasilimali ya maji mita za ujazo zaidi ya bilioni 126. Tuna mita za ujazo bilioni 105 juu ya ardhi ikiwemo mito pamoja na mabonde na bilioni 21 ambayo iliyokuwa chini ya ardhi.

Kwa hiyo, mkakati ambao tumeuweka sisi kama Wizara na katika bajeti yetu kutumia maziwa, rasilimali toshelevu, kuhakikisha kwamba tunatatua tatizo la maji na moja ya maeneo ambayo ya kipaumbele ni vijiji ambavyo vipo kandokando ya mito ama maziwa. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi ni Wizara ya Maji si Wizara ya ukame. Tunakwenda kutatua tatizo la maji kwa wananchi wako, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi wa chujio wa Maswa, Kata ya Zanzui, umeshakamilika na mradi ule unategemewa kusambaza maji katika vijiji kumi, Maswa Mashariki vijiji vitano na Maswa Magharibi vijiji vitano.

Ni lini sasa maji yale yatasambazwa ili wananchi wa Maswa na akinamama wa Maswa wapumzike na adha ya maji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu kwa swali hilo.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli anatosha mpaka chenji inabaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa namna nyingine ambayo nataka kusema wananchi wa Maswa changamoto kubwa sana ilikuwa ni chujio kwamba wanapata maji, lakini sio safi na salama na yenye ubora. Kwa hiyo, tumepata fedha, chujio lile tumelikamilisha kazi iliyobaki na ninatoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa pale na tumekwishamthibitisha, kipimo chake cha kwanza ni kuhakikisha maeneo ambayo

Mheshimiwa Mbunge ameyaeleza kuhakikisha wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara tutampatia fedha kuhakikisha kwamba anatimiza majukumu yake na wananchi wanapata huduma ya maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru; kwa kuwa Jimbo la Kibamba sasa changamoto yake kubwa ni usambazaji wa mabomba tu katika maeneo mbalimbali. Je, Serikali sasa iko tayari kutoa kauli au maelekezo ya utoaji wa mabomba yale ili wananchi wa maeneo mengi wapate maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji, majibu.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kidhati ya moyo nikupongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Mbunge, kaka yangu Mtemvu. Moja katika bajeti yako umeonesha masikitiko yako eneo ambalo halina maji na tumekwishakubaliana na *commitment* yangu mimi baada ya Bunge tunakwenda Kibamba tunakwenda kumaliza kabisa tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na tumeshatoa maelekezo mahususi kwa *DAWASA,* wamefanikiwa maeneo mengi sana, walipe kipaumbele Jimbo la Kibamba katika kuhakikisha kwamba, tunaenda kumaliza kabisa tatizo la maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwa Wabunge na majibu kutoka kwa Serikali, nitaleta matangazo niliyonayo hapa mezani.

Tangazo la kwanza ni tangazo linalohusu wageni, tutaanza na wageni waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika,

nao ni wageni 108 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambaye ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambao ni familia yake, Watendaji Wakuu wa Wizara, Waheshimiwa Madiwani na Wakuu wa Idara wa Halmashauri ya Ushetu.

Tutaanza na Dkt. Faraji Mnyepe ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana, lakini pia ameambatana na Luteni Jenerali Yacoub Mohamed ambaye ni Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Brigedia Jenerali Rajabu Mabele ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, karibu sana, tunaye pia Meja Jenerali Richard Makanzo ambaye ni Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Wanamaji, karibu sana, tunaye pia Meja Jenerali Jacob Mkunda ambaye ni Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi kavu, karibu sana. Tunaye pia Meja Jenerali George Igram ambaye ni Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Meja Jenerali Mkingule ambaye ni Mdhibiti Mkuu wa Jeshi, karibu sana; tunaye Meja Jenerali Paul Simuli ambaye ni Mkuu wa Utumishi Jeshini, karibu sana, tunaye pia Brigedia Jenerali Ramson Mwaisaka ambaye ni Mkuu wa Kamandi ya Makao Makuu ya Jeshi, karibu sana; tunaye pia Meja Jenerali Amri Mwami ambaye ni Mkuu wa Tiba Jeshini karibu sana. Tunaye pia Ndugu Obedi Sayore ambaye ni Kamishna wa Sera na Mipango karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ambao ni Majenerali watano wanawake na hawa ni Meja Jenerali Hawa Kodi, karibu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunaye pia Brigedia Jenerali Pili Kambenga, karibu sana, tunaye pia Brigedia Jenerali Anna Mkinga Karibu sana, tunaye pia Brigedia Jenerali Korotina Nshushi karibu sana, tunaye pia Brigedia Jenerali Agatha Katua karibu sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, nadhani Mheshimiwa Waziri aliwaalika hawa mahsusi ili tujue Jeshini wamekamilika, akina mama wapo vizuri Jeshini. *(Makofi/Vigelegele)*

Hata mimi kuna siku nilikuwa ninatafakari kwenda kujiunga na Jeshi lakini sasa naona nimechelewa kidogo labda nitapeleka..., hapa ninakumbushwa umri jamani.

Haya, wageni wengine watatu wa Mheshimiwa Waziri moja ni Mke wake Dkt. Marceline Mumbee, karibu sana, ameongozana na mtoto wake Ndugu Jacquiline Kwandikwa, karibu sana, lakini pia ameongozana na Ndugu Joseph Nyanda Shilole karibu sana.

Sasa asimame Dkt. Marceline Mombee, Mke wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana, jamani nadhani tumemuona wifi yetu na shemeji. *(Makofi)*

Haya Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Waziri hajamaliza bado orodha ya wageni, anao wageni wengine 26 ambao ni Madiwani kutoka Ushetu wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Igwamanoni, Mheshimiwa Gagi Lali, karibuni sana Waheshimiwa Madiwani, ninaamini mnafanya kazi nzuri ya kumlindia Jimbo Mheshimiwa Waziri akiwa na majukumu mengine makubwa ya Kitaifa. Nataka kuamini kati yenu hamna ambaye ana mpango wa kumtoa Mheshimiwa Waziri, *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, anao pia wageni sita tena Mheshimiwa Waziri ambao ni Wakuu wa Idara kutoka Halmashauri ya Ushetu wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Ndugu Michael Matomora, karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini pia anao wageni wengine 19 ambao ni kikundi cha *Super Queens Generation* kutoka Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Mwenyekiti wa kikundi hicho Eliza Thomas karibuni sana sana. *(Makofi)*

Hawa *Super Queens Generation* wamependeza na sare lakini sijapewa taarifa za ziada kwamba wanafanya nini,

lakini sare tu zinaashiria mambo anayoyafanya ni mazito kwa hiyo tunawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge wengine kwanza ni wageni 17 wa Mheshimiwa Doto Biteko ambaye ni Waziri wa Madini na hawa ni watendaji kutoka Wilaya ya Bukombe wakiongozwa na Ndugu Issa Shaaban, karibuni sana wageni wetu kutoka Bukombe. *(Makofi)*

Lakini pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ambaye ni Waziri wa Viwanda na Biashara na huyu ni mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Ndugu Steven Wassira. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sio kawaida sana mgeni kupigiwa makofi na Wabunge wote humu ndani, lakini Mheshimiwa Wassira amepata mengi sana hasa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya. *(Makofi/Kicheko)*

Ahsante sana na karibuni sana, kwa wale vijana wa siku hizi mbili, tatu wanaweza wakawa hawamfahamu vizuri Mheshimiwa Wassira, lakini yule ni Mbunge wa siku nyingi na kukaa kwakwe pale ninauhakika anakumbushia mambo mengi humu ndani anakikumbuka na kiti anachokuwa anakaa, karibu sana Mheshimiwa Steven Wassira. *(Makofi)*

Lakini wapo pia wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii na hawa ni kikundi cha wadau wa Utalii nchini wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Petro Mponzi, karibuni sana wadau wa utalii. *(Makofi)*

Lakini pia wapo wageni 19 wa Mheshimiwa Mwita Waitara ambaye ni Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na hawa ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mkoani Mara wakiongozwa na ndugu Mwita Ryoba, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 21 wa Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde ambao ni Wanamaombi na Wainjilisti kutoka Kanisa Anglikana Chimuli la Jijini Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Leonard Mtembwe, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Neema Lugangira ambaye ni Rais wa Tanzania Adventist nchini Marekani na huyu ni Dkt. Michael Mwasumbi, Dkt. Mwasumbi kwa maelezo yaliyopo hapa ni mtaalam wa mambo ya usingizi wa Hospitali ya St. Joseph ya nchini Marekani, karibu sana sana. *(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Rashid Rashid ambaye ni kaka yake kutoka Mjini Magharibi Zanzibar na huyu anaitwa Isihaka Khamis, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Masache Kasaka ambao ni wachungaji wa Kanisa la Morovian kutoka Jijini Dodoma na Dar es Salaam wakiongozwa na Mchungaji Aswile Mwakabumbi, karibuni sana wachungaji watu jamani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mmemuona pale kuna Mchungaji mwana mama sijapata jina lake, zote hizo ni ishara akina mama tupo vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni wawili kutoka Ubalozi wa Marekani nchini ambao ni Ndugu Kristin Mencer - Mkurugenzi wa Kitengo cha Siasa na Ndugu Chikulupi Kasaka ambaye ni Afisa Msaidizi wa Masuala ya Siasa ambao wamekuja Bungeni kwa ziara ya kikazi na kujifunza namna Waheshimiwa Wabunge wanavyofanya kazi zao, karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini pia tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambao ni wadau wake kutoka Dar es Salaam na hawa ni Ndugu Manase Michael na Ndugu Boniface Magesa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo pia tangazo lingine mtakumbuka kwamba siku ya jana tarehe 20 Mei, 2021

tuliahirisha shughuli za Bunge kufuatia msiba wa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Khatib Said Haji ili kuweze kuombeleza msiba huo, lakini pia kushiriki mazishi. Kutokana na kuahirisha shughuli za Bunge kwa siku hiyo ratiba ya Mkutano wa Bunge itakuwa na mabadiliko kama ifuatavyo:-

Leo tarehe 21 Mei, 2021 tutakuwa na mjadala wa hotuba ya Bajeti ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kesho Jumamosi 22 Mei, 2021 tutakuwa na Kikao cha Bunge kujadili hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara; na kuanzia Jumatatu tarehe 24 Mei, 2021 ratiba itaendelea kama ilivyokuwa awali.

Hivyo baadaye nitamuita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ili aweze kutengua Kanuni ili Bunge liweze kukutana kesho siku ya Jumamosi tarehe 22 Mei, 2021.

Sasa nimuite Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu ili atoe Hoja ya Kutengue Kanuni za Bunge.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu siku ya jana Bunge la Jamhuri ya muungano wa Tanzania lilipata msiba mzito wa kupotelewa na Mbunge mwenzetu ambaye amezikwa siku hiyo ya jana katika Visiwa vya Pemba kule Zanzibar, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema, peponi, Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwakuwa kwa mujibu wa kanuni za Bunge jana hatukuwa na shughuli zozote; na kwa mujibu wa maelekezo na maelezo ambayo umekwisha kuyatoa ya kikanuni; ninawaomba Waheshimiwa Wabuge

sasa turidhie kwa pamoja siku ya kesho Bunge liweze kuketi na kufanya kazi siku ya Jumamosi toka saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Niabu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeunga mkono na sasa kwa utaratibu wetu nitawahoji.

Nadhani walioafiki wameshinda, kwa hiyo waheshimiwa Wabunge kesho tutaendelea na shughuli za Bunge.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu!

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Mhandisi Elias John Kwandikwa ili aweze kuwasilisha hoja yake.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati

ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti...

**NAIBU SPIKA:** Majenerali naona mnaondoka kabla bajeti haijasomwa, naomba mrejee pale bajeti itakapomalizwa kusomwa ndio mtaelekea hicho chumba kingine kama ndiko mlipokuwa mnapelekwa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyetujalia uzima na afya njema na kuendelea kuijalia nchi yetu amani na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, na kwako Naibu Spika, Mheshimiwa Spika, Wabunge, Serikali, familia za marehemu na Watanzania wote, kwa misiba iliyolikumba Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 17 Machi, 2021, Taifa liliondokewa na Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, na tarehe 24 Julai, 2020 Taifa liliondokewa na Hayati Benjamin William Mkapa, aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 17 Februari, 2021, Taifa liliondokewa na Hayati Maalim Seif Shariff Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Mhandisi Balozi John William Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, natoa pole kwa kuondokewa na Atashasta Justus Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe, aliyefariki tarehe 12 Februari, 2021 na Martha Jachi Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, aliyefariki tarehe 21 Januari, 2021 na Khatib Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde aliyefariki jana tarehe 20 Mei, 2021. Namuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa pole kwa wananchi waliopata majanga na kuondokewa na ndugu, jamaa na marafiki kutokana na matukio mbalimbali yaliyosababishwa na madhara ya mvua kubwa, ajali na magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Namtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake mapya. Aidha, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuniamini na kuniteua kuiongoza Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, kwa kuteuliwa kushika wadhifa wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge lako tukufu kumpitisha kwa asilimia 100. Pia napenda kumpongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kushika wadhifa huo kwa awamu ya pili.

Kwa ujumla ninawashukuru kwa uongozi wao makini na maelekezo wanayonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukupongeza wewe, napenda kumpongeza Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Mbunge na Spika wa Bunge hili, wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu Mbunge, Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa mafanikio makubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa maarifa, busara, hekima na nguvu ili muendelee kuliongoza Bunge letu vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie pia fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Balozi Hussein Athuman Kattanga, kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Pia nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na Kuteuliwa kulitumikia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge, ambayo kwa kipindi chote imesimamia na kufuatilia shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara na kutoa ushauri maoni na ushauri wa Kamati wakati wakichambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na mapendekezo ya mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 umesaidia kuboresha mapendekezo na makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wote Kamati hii imeendelea kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kuimarisha utendaji wa vyombo vya ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dira, dhima malengo na majukumu ya Wizara yameelezwa katika aya ya 13 hadi ya 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama yaliyotolewa katika Mkutano wa 19; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipitia na kujadili utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kutoa maoni, ushauri maelekezo kwa Wizara yaliyolenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu yake.

Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi na kuzingatiwa wakati wa kuandaa na kukamilisha mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 inayowasilishwa leo hapa Bungeni kama ilivyooneshwa katika Kiambatisho Namba 1.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi mwaka 2020/2025 na Dira ya Taifa ya mwaka 2025 kwa mwaka wa fedha 2021; Wizara imeendelea kutekeleza mipango yake kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025 Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2016/2017 – 2020/2021). Maelekezo ya Ilani kwa Wizara yameainishwa bayana kwenye sura ya tano Ibara ya 105 ya Ilani ya CCM na utekelezaji wake umeoneshwa katika Kiambatisho Namba 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kushirikiana kikamilifu na mamlaka nyingine za kiraia katika kukabiliana na majanga kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 107 ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi; katika mwaka wa fedha 2021 hali ya mipaka

ya nchi yetu yenye jumla ya urefu wa kilometa 5461.2 ambayo inahusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji imeendelea kuwa shwari katika kipindi hicho hapakuwa na matukio ya uhasama yaliyoripotiwa baina ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo. Hata hivyo zipo changamoto za kiusalama katika baadhi ya mipaka yetu iliyohitaji kuchukuliwa hatua ili kuimarisha ulinzi wa mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni baadhi ya maeneo ya mipaka kutokuwa na barabara za ulinzi na zilizopo kuharibika, vitendo vya kigaidi, biashara ya madawa ya kulevya, usafirishaji haramu wa binadamu, uhamiaji haramu na ujambazi wa kutumia silaha katika baadhi ya nchi tunazopakana nazo. Hali hiyo imevilazimu vyombo vya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na nchi jirani kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wa Kaskazini; mpaka huu una urefu wa kilometa 1281.2 ambapo Tanzania inapakana na nchi za Kenya na Uganda; hali ya usalama katika mpaka kwa ujumla ni shwari, hata hivyo mpaka umeendelea kukumbwa na changamoto ya uhamiaji haramu na ni njia ya usafirishaji haramu wa binadamu kutoka nchi za Ethiopia, Eritrea na Somalia. Changamoto nyingine ni wafugaji kutoka baadhi ya nchi tunazopakana nazo kuendelea kuingiza mifugo yao ndani ya Ranchi ya Taifa ya Misenyi iliyoko Wilaya ya Misenyi Mkoa wa Kagera kwa ajili ya kutafuta malisho na maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wa Mashariki; mpaka huu una urefu wa kilometa 1421 ambapo Tanzania inapakana na nchi za Kenya, Visiwa vya Shelisheli, Comoro na Msumbiji. Ulinzi katika mipaka umeendelea kuwa imara na hali ya usalama ni ya kuridhisha. Pamoja na hali hii kuwa tulivu katika eneo hili mpaka huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo; uvuvi haramu katika Bahari ya Hindi, biashara ya magendo na kutumika kama mapito ya wahamiaji haramu, usafirishaji wa madawa ya kulevya na usafirishaji haramu wa binadamu. Jeshi la Wananchi wa

Tanzania kwa kushirikiana na vyombo vingine vya usalama vinaendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili kukabiliana na changamoto hizo kwa kufanya doria za mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wa kusini mpaka huu una urefu wa kilometa 1,536 ambapo Tanzania imepaka na nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia. Hali ya ulinzi na usalama katika mpaka huu kwa ujumla ni shwari, hata hivyo usalama wa mpaka huu unatishiwa na uwepo wa kundi la kigaidi la *Ansar Al-suni Wal Jamaa* iliyopo katika Jimbo la Kabo Delgado Msumbiji linalopakana na Mkoa wa Mtwara Tanzania kundi hilo mwezi Oktoba na Disemba, 2020 lilifanya mashambulizi katika baadhi ya vijiji vya Mkoa wa Mtwara mashambulizi hayo yalisababisha vifo na uharibifu wa mali. Katika hali ya kuimarisha ulinzi wa mpaka huo Serikali imepeleka vikundi vya ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama wa mpaka wa Tanzania na Malawi imeendelea kuwa shwari kwani hakuna tishio la wazi dhidi ya nchi yetu. Changamoto katika mpaka huu ni kutokuhakikiwa kwa mpaka katika Ziwa Nyasa. Serikali yetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki imeendelea kutumia njia za kidiplomasia ili kulipatia suala hili ufumbuzi wa kudumu. Vilevile changamoto nyingine ni Mto Songwe ambao ni mpaka kati ya Tanzania na Malawi kuhamahama. Hali hiyo pia inaendelea kuleta changamoto za kimpaka baina ya nchi hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka wa Magharibi; mpaka una urefu wa kilometa 1,220 ambapo Tanzania inapakana na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hali ya ulinzi na usalama katika mpaka ni shwari.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za ulinzi na usalama katika mpaka huu ni zifuatavyo; sehemu kubwa ya mpaka huo kutokuhakikiwa, kuingia wahamiaji haramu ambao hujihusisha na matukio ya kihalifu kwa kutumia silaha, uvunaji wa mazao ya misitu na kuhamishwa kwa sehemu ya

Mto Malagarasi kutokana na shughuli za kibinadamu zinazoendelea hali inayosababisha maji ya mto huo kumomonyoa ardhi kwa upande wa Tanzania na kuendelea kwa hali hiyo kutasababisha mpaka baina ya nchi hizi kusogea kwa upande wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021; tathmini ya makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 85,103,000.00 kutoka katika mafungu yake yote matatu. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 Wizara imefanikiwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 103,091,528.83 sawa na asilimia 121.14 ya makadirio kwa mafungu yote matatu. Mchanganuo wa maduhuli katika kila fungu umeonyeshwa kwenye Jedwali Namba 1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo fedha zilizoidhinishwa; katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya shilingi 2,141,034,489,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika mafungu yake yote matatu, kati ya fedha hizo, shilingi 1,977,034,489,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 164,000,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu umeainishwa katika Jedwali Na. 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizopokelewa kuanzia Julai 2020 hadi Aprili 2021; hadi kufikia mwezi Aprili 2021, fedha zilizopokelewa zilikuwa ni shilingi 1,744,178,001,813.29 sawa na asilimia 81.46 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,647,178,500,215.32 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 96,999,501,597.97 ni kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo. Mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa mafungu matatu umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 3.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Aprili 2021, Wizara imepokea jumla ya shilingi

37,610,598,686.00 ikiwa ni ziada ya bajeti kwa ajili ya shughuli za matumizi mengineyo. Fedha hizo zimetolewa kwa Fungu 38 - Ngome na Fungu 39 – JKT ambazo zimetumika kwa ajili ya operesheni maalum za ulinzi wa mipaka ya nchi, kugharamia shughuli za uapisho wa Rais wa Awamu ya Tano na kugharamia mazishi ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa na Rais wa Awamu ya Tano Hayati John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara imepokea jumla ya shilingi 222,704,504,764.37 kwa ajili ya kulipa madeni ya wazabuni wa ndani na nje yaliyohakikiwa kwa mafungu yote matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zilizotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kutumia fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya kawaida; Wizara imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali kupitia fedha za matumizi ya kawaida ikiwemo; matunzo ya zana na vifaa vya Jeshi, kukamilisha mapendekezo ya mpango wa miaka kumi (2021/22 - 2030/31) kwa kuliimarisha Shirika la *Tanzania Automotive Technology Centre – TATC* ambapo mpango huo pamoja na Waraka wa Baraza la Mawaziri uliwasilishwa kwenye ngazi ya Kamati ya Makatibu Wakuu *(IMTC)* na kuendelea kukamilisha rasimu ya Sera ya Ulinzi wa Taifa, ambapo maoni ya wadau yaliyokusanywa yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli nyingine ambazo zimetekelezwa na Wizara kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida ni mafunzo ya kijeshi, mafunzo ya jeshi la akiba, huduma za afya na tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi husika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa kutoa huduma za matibabu kwa maafisa, askari, watumishi wa umma na familia zao, vijana wa JKT na wananchi wanaoishi

karibu na vituo vya tiba vya Jeshi hapa nchini. Aidha, Wizara imeendelea na maboresho ya huduma za matibabu kwa wanajeshi na familia zao, ambapo Halmashauri ya Majeshi ya Ulinzi imeidhinisha uanzishaji wa Huduma za Bima ya Afya Jeshini kuanzia Julai, 2020. Huduma hizo zimeanza kutolewa kuanzia tarehe 1Oktoba, 2020 ambapo kila afisa na askari anachangia asilimia tatu ya malipo yake ghafi ya kila mwezi. Huduma hiyo imeboresha matibabu kwa maafisa, askari, familia pamoja na wastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine; Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushirikiana na nchi mbalimbali katika masuala ya ulinzi na usalama katika baadhi ya maeneo ambayo ni mafunzo, misaada ya kitaalam, vifaa, zana na mitambo. Vilevile Jeshi la Wananchi wa Tanzania inashirikiana na Umoja wa Mataifa (*UN*), nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika katika mafunzo na ubadilishanaji wa wataalam. Pia Jeshi la Wananchi wa Tanzania inapata msaada wa mafunzo kwa Maafisa na Askari kutoka nchi za China, Urusi, Marekani, Misri, India, Ujerumani, Uingereza, Bangladesh, Morocco, Canada, Ufaransa, Uholanzi, Indonesia, Oman, Uturuki, Israel, Pakistan, Jordan na Sri Lanka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Ulinzi *(NDC)* inaendesha mafunzo ya Usalama na Stratejia kwa Maafisa wa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na watumishi wa umma wenye madaraka kuanzia ngazi ya Mkurugenzi Msaidizi. Mafunzo hayo hutolewa pia kwa washiriki kutoka nchi za China, Zimbabwe, Afrika Kusini, Kenya, Ghana, Misri, Nigeria, Rwanda, Malawi, Zambia, Namibia, Botswana, Uganda, Msumbiji, Burundi na Bangladesh. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Ujerumani kupitia *GAFTAG* imetoa msaada wa ujenzi wa majengo ya Idara ya Magonjwa Ambukizi katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, ujenzi wa mabweni na mabwalo katika Kituo cha Mafunzo ya Ulinzi wa

Amani katika maeneo ya Msata, Pwani na Kunduchi, Dar es Salaam.

Aidha, *GAFTAG* inashirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania katika maandalizi ya ujenzi wa Hospitali Kuu ya Jeshi – Msalato hapa Dodoma. Pia *GAFTAG* imewezesha ukarabati wa Kiwanda cha Uchapaji kilichopo Gongo la Mboto ambapo ulihusisha uwekaji wa mashine mpya za uchapaji. Vilevile Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Jeshi la Ukombozi la Watu wa China imewezesha awamu ya pili ya ujenzi wa *NDC* ambao ulihusisha jengo kuu la mafunzo na utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushiriki wa Jeshi katika shughuli za ulinzi wa aman;i Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa katika Operesheni za Ulinzi wa Amani katika nchi mbalimbali zenye migogoro kwa kupeleka vikosi, Waangalizi wa Kijeshi, Wanadhimu na Makamanda. Mpaka sasa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ina Vikosi vya Ulinzi wa Amani katika nchi za Lebanon, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Jamhuri ya Afrika ya Kati. Aidha, Jeshi lina Maafisa Wanadhimu, Waangalizi wa Kijeshi na Makamanda kwenye Operesheni za Ulinzi wa Amani nchini Lebanon, Sudan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan Kusini na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushirikiano na mamlaka za kiraia katika shughuli mbalimbali za Kitaifa; katika mwaka wa fedha 2020/2021 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika shughuli mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Baadhi ya maeneo ambayo Jeshi la Wananchi wa Tanzania imeshirikiana na mamlaka za kiraia ni kushiriki katika kuboresha huduma katika Taasisi za Serikali; kushiriki katika ujenzi wa *standard gauge* na Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere; kushiriki katika ulinzi wa maeneo ya kimkakati kwa nchi ikiwemo Mgodi wa *Tanzanite* uliopo Mererani, Mkoani Manyara na utoaji wa huduma za afya na tiba kwa wananchi ambapo takwimu zilizopo zinaonesha

kwamba asilimia 80 ya wanaopata huduma katika Hospitali za Jeshi ni raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa; katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2020 hadi Aprili, 2021 jumla ya vijana 21,370 wa mujibu wa sheria "Operesheni Uchumi wa Kati" walipatiwa mafunzo kwenye Kambi mbalimbali za Jeshi la Kujenga Taifa, kati yao 16,171 ni wa kiume na 5,199 ni wa kike. Aidha, mpango wa Wizara ni kuhakikisha vijana wote wanaohitimu kidato cha sita wanachukuliwa kuhudhuria mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafunzo kwa vijana, Jeshi la Kujenga Taifa liliendesha mafunzo kwa watumishi 41 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuwajengea maadili mema, ukakamavu na moyo wa kizalendo. Matumaini ya Wizara ni kuwa watumishi hao watakuwa mfano wa kuigwa katika utekelezaji wa majukumu yao. Pia naomba kutoa wito kwa Wizara na Taasisi kuleta maombi Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili watumishi wapate nafasi ya kufanya mafunzo yatakayowaimarisha kulitumikia vyema Taifa. Hapa Waheshimiwa Wabunge vijana wanaendelea kujiandikisha pia tutawapa dozi ya mafunzo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kwa upande wa magonjwa yasiyoambukizwa jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanyika ikiwemo kutoa elimu ya afya ili kupunguza magonjwa hayo na kupima afya mara kwa mara. Vilevile maafisa, askari na watumishi wa umma hushauriwa kuacha uvutaji wa sigara, unywaji pombe uliopitiliza na kufanya mazoezi ya mwili na michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utawala bora; Wizara imeendelea kutekeleza dhana ya Utawala Bora katika maeneo ya kazi kwa kushirikisha watumishi wake kupitia vikao mbalimbali vikiwemo vya Baraza la Wafanyakazi, Kamati ya

Ukaguzi, Kamati ya Maadili, Bodi ya Manunuzi na Kamati ya Ajira. Pia Wizara imeendelea kuimarisha jitihada za kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utunzaji wa mazingira kwa upande wa shughuli za utunzaji wa mazingira katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara kupitia Taasisi zake imeendelea na utunzaji wa fukwe katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ili kuzuia mmomonyoko wa udongo. Pia, imefanikiwa kupanda miti 99,851 kwa kutumia vitalu vilivyopo Ruvu JKT, Makutupora JKT, Rwamkoma JKT, Mafinga JKT na Nachingwea JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inamiliki maeneo makubwa yenye miti ya asili ambayo hutunzwa kwa kufanya doria mbalimbali, hivyo kufanya maeneo hayo yasivamiwe kwa shughuli za kijamii, mfano eneo la Pongwe, Msungura lililopo Mkoa wa Pwani na Ngerengere lililopo Mkoa wa Morogoro. Aidha, maeneo yote ya Jeshi yana zuio la ukataji miti na kuchoma mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika yaliyo chini ya Wizara *(TATC),* Mzinga na SUMAJKT yameendelea na uzalishaji kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za uhifadhi wa mazingira. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la *TATC* imefanikiwa kukamilisha utafiti wa mashine kwa ajili ya uzalishaji wa nishati mbadala. Mashine ambazo zinatumia mabaki ya mashambani ya vyakula, vumbi na makaa ya mawe na udongo wa mfinyanzi kutengeneza mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli za maendeleo kwa upande wa fedha za maendeleo, fedha zilizotolewa katika Fungu 57 - Wizara zimetumika katika ununuzi na ukarabati wa zana na vifaa vya Jeshi, kuwasha umeme kwenye Mradi wa Mawasiliano Salama Jeshini na usanidi wa mtandao, ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi ikiwa ni pamoja na Nyabange – Musoma, RAS – Mshindo - Kilwa na ununuzi wa malighafi za kuzalisha zao la msingi kwa Shirika la Mzinga. Aidha, *TATC* imenunua mitambo ya

kuyeyusha, kuchonga na kuchomelea chuma kwa ajili ya mradi wa kuzalisha nguzo za chuma na viambata vyake kwa matumizi ya Shirika la Umeme Tanzania na ukamilishaji wa uunganishaji na ukarabati wa magari ya zimamoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo kwa Fungu 38 - Ngome zimetumika kwa ajili ya ununuzi na matunzo ya zana na vifaa, kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa, ununuzi wa magari ya utawala, ununuzi wa vipuri vya mitambo ya kuchimbia visima vya maji safi, ujenzi wa maghala pamoja na miundombinu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo Fungu 39 - JKT zimetumika kwa ajili ya ukamilishaji wa miundombinu muhimu Makao Makuu ya JKT na baadhi ya vikosi. Vilevile fedha hizo zimetumika katika ulipaji wa fidia kwa eneo la Chamwino – Dodoma yalipo Makao Makuu ya JKT na kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Makao Makuu ya JKT, Chamwino – Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zilizotekelezwa na mashirika yanayosimamiwa na Wizara; Wizara kupitia mashirika yake ya *TATC,* Mzinga na SUMAJKT imeendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kwa kufanya tafiti na uhawilishaji wa teknolojia, nimeonyesha katika aya ya 57 hadi ya 77.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu changamoto za utekelezaji mpango wa bajeti.Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kubwa ikiwa ni ukomo mdogo wa bajeti na upungufu wa rasilimali watu.

Aidha, fedha za maendeleo zilizotolewa kwa kiasi kikubwa zimetumika kulipia mikataba michache ya ununuzi wa zana na vifaa na kutekeleza miradi mingine ya maendeleo. Hatua za kukabiliana na changamoto, hizo kwa kuchukuwa hatua mbalimbali kama ilivyoelekezwa katika haya ya 82, 84 na 85. Naomba kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kulipa baadhi ya madeni ya wazabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mpango wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka wa fedha 2021/2022 ni kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na ufasaha kulingana na dira na dhima ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa shughuli zinazokusudiwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2021/2022 utazingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo: kuliimarisha Jeshi kwa kulipatia zana na vifaa vya kisasa, kuendelea na jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka nchi yetu, kuboresha mazingira ya kazi makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi ya wanajeshi na watumishi wa umma, kuendelea kujenga uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa; kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia na kuimarisha na kuratibu mafunzo ya kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, kabla sijahitimisha hotuba yangu napenda kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa michango waliyotoa katika kutayarisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yangu. Namshukuru Katibu Mkuu Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe; Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Venance Salvatory Mabeyo; Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Luteni Jenerali Yacoub Hassan Mohamed; Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa Meja Jenerali Rajab Mabele. Nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshiiwa Mabele kwa sababu bado ni mpya mpya huyu na mimi namtakia kila kheri katika kutekeleza majukumu yake. Pia nawapongeza Wakuu wa Kamandi na Wakuu wa Mashirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo wa Wizara ya Ulinzi na JKT, Wakuu wa Matawi Makao Makuu ya Jeshi, Wakuu wa Idara, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma waliopo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kufanikisha majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya Serikali kutoa shukrani kwa Serikali za nchi mbalimbali na washirika wa maendeleo kwa ushirikiano walioipatia Wizara yangu. Serikali na washirika wa maendeleo hao ni pamoja na Jamhuri ya Watu wa China, Ujerumani, India, Marekani, Canada, Ufaransa na Uturuki.

Aidha, ninazishukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu za ulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Bangladesh, Falme za Kiarabu, Ghana, Indonesia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Uholanzi, Morocco, Nigeria, Uingereza, Urusi na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika yaani *SADC. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika ulinzi wa nchi yetu.

Kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru familia yangu, mke wangu, Watoto wangu, wazazi wangu, kwa uvumilivu na ushirikiano wanaonipa kuniwezesha niweze kufanya shughuli zangu kwa utulivu. *(Makofi)*

Napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Madiwani waliofika leo hapa Bungeni pamoja na wapiga kura wangu wa Jimbo la Ushetu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa tangu wanichague kuwawakilisha. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile natoa shukrani za dhati kwa Maafisa na askari walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uapisho na mazishi ya viongozi wetu wapendwa waliolitumikia Taifa letu kwa moyo wa uzalendo.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya makusanyo ya maduhuli; kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara inatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 85,103,000 kutoka katika mafungu yake matatu, kwa mchanganuo uliooneshwa katika katika Jedwali Namba Tatu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya kawaida na maendeleo; Wizara katika mwaka wa fedha 2021/2022 ili iweze kutekeleza majukumu yake inaomba iidhinishiwe na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi 2,358,694,986,000 kwa mafungu yote matatu. Kati ya fedha hizo shilingi 2,182,116,562,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 176,578,424,000 ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo. Mchanganuo wake mafungu umeainishwa katika Jedwali Namba Nne.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, nawashukuru Mawaziri wenzangu na Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii, inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo ni www.modans.go.tz. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA ELIAS JOHN KWANDIKWA (MB), WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na kupitisha Mpango na

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, aliyetujalia uzima na afya njema na kuendelea kuijalia nchi yetu amani na usalama.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** naungana na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwa **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwako Mhe. Spika, Wabunge, Serikali, Familia za Marehemu na Watanzania wote, kwa misiba iliyolikumba Taifa letu. Mnamo tarehe 17 Machi, 2021, Taifa liliondokewa na **Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli,** aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, na tarehe 24 Julai, 2020 liliondokewa na **Hayati Benjamini William Mkapa,** aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 17 Februari, 2021, Taifa liliondokewa na **Hayati Maalim Seif Sharif Hamad,** aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na **Mhandisi Balozi John William Kijazi,** aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** vile vile, natoa pole kwa kuondokewa na Atashasta Justus Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe, aliyefariki tarehe 12 Februari, 2021 na Martha Jachi Umbula aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, aliyefariki tarehe 21 Januari, 2021. Namuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, Amina.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutoa pole kwa wananchi waliopata majanga na kuondokewa na ndugu, jamaa na marafiki kutokana na matukio mbalimbali yaliyosababishwa na madhara ya mvua kubwa, ajali na magonjwa.

7. ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza **Mhe. Samia Suluhu Hassan,** kwa kuapishwa

kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Namtakia kila la kheri katika kutekeleza majukumu yake mapya. Aidha, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuniamini na kuniteua kuiongoza Wizara hii.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** nampongeza **Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango**, kwa kuteuliwa kushika wadhifa wa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Bunge lako Tukufu kumpitisha kwa asilimia 100. Pia, napenda kumpongeza **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi,** Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kushika wadhifa huo kwa awamu ya pili. Kwa ujumla nawashukuru kwa uongozi wao makini na maelekezo wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe, **Mhe. Job Yustino Ndugai (Mb),** Spika wa Bunge hili, **Mhe. Dkt. Tulia Ackson Mwansasu (Mb),** Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa mafanikio makubwa. Namuomba Mwenyezi Mungu azidi kuwapa maarifa, busara, hekima na nguvu ili muendelee kuliongoza Bunge letu vyema.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie pia fursa hii, kumpongeza **Mhe. Balozi Hussein Athuman Kattanga,** kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na kuteuliwa kulitumikia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na **Mhe. Mussa Azzan Zungu**

**(Mb),** ambayo kwa kipindi chote imesimamia na imefuatilia shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara na kutoa ushauri. Maoni na Ushauri wa Kamati wakati wakichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021 na mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 umesaidia kuboresha mapendekezo ya Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ninayowasilisha leo hapa bungeni. Wakati wote Kamati hii imeendelea kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kuimarisha utendaji wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama vya nchi yetu.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo, naomba uniruhusu nieleze kwa kifupi Dira, Dhima na Malengo ya Wizara.

## DIRA, DHIMA NA MALENGO YA WIZARA

13. ***Mheshimiwa Spika,*** **Dira** ya Wizara ya Ulinzi na JKT ni kuendelea kuwa Taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa letu. Aidha, **Dhima** ya Wizara ni kuendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani na nje ya nchi kwa kuhakikisha kuwa mamlaka na maslahi mapana ya nchi yetu yanakuwa salama.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha Dira na Dhima, Malengo ya Wizara yameendelea kuwa yafuatayo:

a. Kuwa na Jeshi dogo lenye wataalamu, zana na vifaa vya kisasa;

b. Kuendelea kuwapa Vijana wa Kitanzania ukakamavu, maadili mema, utaifa, moyo wa uzalendo na uwezo wa kujitegemea;

c. Kujenga uwezo katika tafiti mbalimbali na uhawilishaji wa teknolojia kwa matumizi ya Kijeshi na Kiraia;

d. Kuimarisha Jeshi la Akiba;

e. Kusaidia Mamlaka za Kiraia; na

f. Kudumisha amani na usalama kwa kushirikiana na nchi nyingine duniani.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia malengo hayo, Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake muhimu katika maeneo yafuatayo:

a. Kuliongezea uwezo wa kimedani Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia vifaa na zana bora pamoja na mafunzo;

b. Kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa Wanajeshi na Watumishi wa Umma;

c. Kuwapa Vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi na kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa;

d. Kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia;

e. Kuendelea kutoa mafunzo ya Jeshi la Akiba katika Mikoa yote; na

f. Kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine katika nyanja za kijeshi na kiulinzi.

## UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA YALIYOTOLEWA KATIKA MKUTANO WA 19

16. ***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipitia na kujadili utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na kutoa maoni, ushauri na maelekezo kwa Wizara yaliyolenga kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu yake. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni, ushauri na maelekezo yaliyotolewa yamefanyiwa kazi na kuzingatiwa wakati wa kuandaa na kukamilisha Mpango na Bajeti ya Mwaka wa

Fedha 2021/2022 ninayowasilisha leo hapa bungeni kama ilivyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 1**.

## UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM) 2020 - 2025 NA DIRA YA TAIFA 2025 KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza mipango yake kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020-2025, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021). Maelekezo ya Ilani kwa Wizara yameainishwa bayana kwenye **Sura ya Tano** Ibara ya 105 ya Ilani ya CCM katika vifungu vifuatavyo, naomba ninukuu:

*a. "Kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi na mipaka yake ili kudumisha Muungano, kulinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, umoja, mshikamano, amani na usalama wa raia na mali zao;*

*b. Kuendeleza jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka ya nchi yetu na nchi jirani;*

*c. Kuwezesha ushirikiano wa vyombo vya ulinzi na usalama kufanya utafiti na ubunifu kwa kushirikiana na taasisi za utafiti;*

*d. Kuhusisha kikamilifu Majeshi ya Ulinzi na Usalama katika kulinda miradi mikubwa ya kimkakati;*

*e. Kuhamasisha na kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi, uzalendo wa kitaifa, usalama na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi ikiwa ni pamoja na Jeshi la Akiba na ulinzi shirikishi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu;*

*f. Kuimarisha uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika kushiriki shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda katika sekta ya ulinzi na maeneo mengine ya kimkakati;*

*g. Kuimarisha viwanda vya NYUMBU na Mzinga ili viweze kutimiza azma ya kuanzishwa kwake;*

*h. Kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ili viwe vyombo vya kuwapatia vijana ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa na pia kuwa vyombo mahiri vya huduma na uzalishaji mali hasa katika ujenzi, kilimo, ufugaji na uvuvi;*

*i. Kupanua na kuongeza idadi ya kambi za JKT na JKU ili kuwezesha vijana wengi zaidi wakiwemo wahitimu wote wa kidato cha sita kupata fursa ya mafunzo ili kujenga uzalendo na moyo wa kujitolea; na*

*j. Kuboresha mazingira ya kazi kwa kuwapatia makazi bora na kuongezea uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia mafunzo ya kitaaluma na kitaalam, vitendea kazi na zana za kisasa zinazoendana na teknolojia ya kisasa".*

18. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana kikamilifu na mamlaka nyingine za kiraia katika kukabiliana na majanga kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 107 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ufanisi kama ilivyooneshwa katika **Kiambatisho Na. 2**.

## HALI YA ULINZI NA USALAMA WA MIPAKA YA NCHI

20. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, hali ya mipaka ya nchi yetu yenye jumla ya urefu wa kilomita **5,461.20** ambayo inahusisha eneo la nchi kavu na eneo la maji imeendelea kuwa shwari. Katika kipindi hicho hapakuwa na matukio ya uhasama yaliyoripotiwa baina ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo. Hata hivyo, zipo changamoto za kiusalama katika baadhi ya mipaka yetu zinazohitaji kuchukuliwa hatua ili kuimarisha ulinzi wa mipaka. Changamoto hizo ni pamoja na; kutohakikiwa kwa baadhi ya maeneo ya mipaka, tatizo la wafugaji kutoka nchi jirani

kuingiza mifugo yao kwa lengo la kupata malisho na maji nchini na wahamiaji haramu.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** changamoto nyingine ni baadhi ya maeneo ya mipaka kutokuwa na barabara za ulinzi na zilizopo kuharibika, vitendo vya kigaidi, biashara ya madawa ya kulevya, usafirishaji haramu wa binadamu, uhamiaji haramu na ujambazi wa kutumia silaha kutoka katika baadhi ya nchi tunazopakana nazo. Hali hiyo imevilazimu Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kushirikiana na nchi jirani kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka. Aidha, juhudi zinaendelea kufanyika kuhakiki na kuimarisha mipaka. Hali ya mipaka yetu katika kipindi husika imeendelea kuwa ifuatavyo;

**Mpaka wa Kaskazini**

22. ***Mheshimiwa Spika,*** mpaka huu una urefu wa kilomita **1,281.2** ambapo Tanzania inapakana na nchi za Kenya na Uganda. Hali ya usalama katika mpaka kwa ujumla ni shwari. Hata hivyo, mpaka umeendelea kukumbwa na changamoto ya wahamiaji haramu na ni njia ya usafirishaji haramu wa binadamu kutoka nchi za Ethiopia, Eritrea na Somalia. Changamoto nyingine ni wafugaji kutoka baadhi ya nchi tunazopakana nazo kuendelea kuingiza mifugo yao ndani ya Ranchi ya Taifa ya Misenyi iliyopo Wilaya ya Misenyi, Mkoa wa Kagera kwa ajili ya kutafuta malisho na maji. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ili kudhibiti hali hiyo. Naomba kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge na Viongozi waendelee kuwaelimisha wananchi hususan maeneo ya mipakani kutoa taarifa kuhusu wahamiaji haramu watakaoonekana katika maeneo yao.

**Mpaka wa Mashariki**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** mpaka huu una urefu wa kilomita **1,424** ambapo Tanzania inapakana na nchi za Kenya, Visiwa vya Shelisheli, Comoro na Msumbiji. Ulinzi katika mpaka umeendelea kuwa imara na hali ya usalama ni ya kuridhisha. Pamoja na hali kuwa tulivu katika eneo hilo, mpaka huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo: uvuvi haramu katika Bahari ya Hindi, biashara za magendo na kutumika kama

mapito ya wahamiaji haramu, usafirishaji wa madawa ya kulevya na usafirishaji haramu wa binadamu. JWTZ kwa kushirikiana na Vyombo vingine vya Usalama inaendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili kukabiliana na changamoto hizo kwa kufanya doria za mara kwa mara.

**Mpaka wa Kusini**

24. **Mheshimiwa Spika,** mpaka huu una urefu wa kilomita **1,536** ambapo Tanzania inapakana na nchi za Msumbiji, Malawi na Zambia. Hali ya Ulinzi na Usalama katika mpaka kwa ujumla ni shwari. Hata hivyo, usalama wa mpaka huu unatishiwa na uwepo wa kundi la kigaidi la *Ansar Al Sunnah Wa Jamaah* (AASWJ) lililopo katika Jimbo la Cabo Delgado, Msumbiji linalopakana na Mkoa wa Mtwara, Tanzania. Kundi hilo mwezi Oktoba na Desemba 2020 lilifanya mashambulizi katika baadhi ya Vijiji vya Mkoa wa Mtwara. Mashambulizi hayo yalisababisha vifo na uharibifu wa mali. Katika hatua ya kuimarisha ulinzi wa mpaka huo, Serikali ilipeleka Vikundi vya Ulinzi.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya usalama wa mpaka wa Tanzania na Malawi imeendelea kuwa shwari kwani hakuna tishio la wazi dhidi ya nchi yetu. Changamoto katika mpaka huu ni kutokuhakikiwa kwa mpaka katika Ziwa Nyasa. Serikali yetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaendelea kutumia njia za kidiplomasia ili kulipatia suala hili ufumbuzi wa kudumu. Vile vile, changamoto nyingine ni Mto Songwe ambao ni mpaka kati ya Tanzania na Malawi kuhamahama. Hali hiyo pia inaendelea kuleta changamoto za kimpaka baina ya nchi hizi mbili.

**Mpaka wa Magharibi**

26. ***Mheshimiwa Spika*****,** mpaka una urefu wa kilomita **1,220** ambapo Tanzania inapakana na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hali ya Ulinzi na Usalama katika mpaka ni shwari. Changamoto za Ulinzi na Usalama katika mpaka huu ni ifuatavyo: Sehemu kubwa ya mpaka huo kutokuhakikiwa, kuingia wahamiaji haramu ambao hujihusisha na matukio ya kihalifu kwa kutumia silaha, uvunaji wa mazao ya misitu, na kuhamishwa kwa sehemu ya

Mto Malagarasi kutokana na shughuli za kibinadamu zinazoendelea hali inayosababisha maji ya mto huo kumomonyoa ardhi kwa upande wa Tanzania. Kuendelea kwa hali hiyo kutasababisha mpaka baina ya nchi hizi kusogea kwa upande wetu. Kwa upande wa mpaka wetu na Burundi wenye urefu wa kilomita 469.847, kazi ya uhakiki wa mpaka wenye urefu wa kilomita 135 imekamilika na alama zimewekwa. Pia, uhakiki wa mpaka wenye urefu wa kilomita 122 utafanyika wakati wowote baada ya makubaliano ya tarehe ya kikao baina ya nchi yetu na Burundi kufanyika. Vile vile, vikao vya ujirani mwema vinaendelea kufanyika ili kutatua changamoto katika mpaka huu.

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### Tathmini ya Makusanyo ya Maduhuli

27. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 85,103,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu; Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa **Shilingi 1,200,000.00,** Fungu 38 - NGOME **Shilingi 22,000,000.00** na Fungu 39 - JKT **Shilingi 61,903,000.00.**

28. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2021, Wizara imefanikiwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 103,091,528.83** sawa na **asilimia 121.14** ya makadirio kwa mafungu yote matatu, kwa mchanganuo ufuatao: Fungu 57 – Wizara, limekusanya jumla ya **Shilingi 8,262,000.00** ambazo zilitokana na huduma ya mtandao wa mawasiliano salama; Fungu 38 – NGOME, limekusanya jumla ya **Shilingi 45,322,528.83** ambazo zilitokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na malipo ya kamisheni zinazotokana na makato ya Bima kwa Wanajeshi kutoka makampuni mbalimbali na Fungu 39 - JKT limekusanya **Shilingi 49,507,000.00** zilizotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, mauzo ya mazao ya bustani (mboga mboga na matunda), mazao ya mifugo na mazao ya shambani. Mchanganuo wa maduhuli kwa kila fungu umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 1.**

**Jedwali Na. 1: Muhtasari wa Mapato na Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

| Fungu | Makadirio ya Mapato 2020/2021 | Makusanyo Julai 2020 hadi Aprili 2021 | Makusanyo (%) |
|---|---|---|---|
| 57 – Wizara | 1,200,000.00 | 8,262,000.00 | 688.50 |
| 38 – NGOME | 22,000,000.00 | 45,322,528.83 | 206.01 |
| 39 – JKT | 61,903,000.00 | 49,507,000.00 | 79.98 |
| **Jumla** | **85,103,000.00** | **103,091,528.83** | **121.14** |

**Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Fedha Zilizoidhinishwa**

29. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,141,034,489,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo katika mafungu yake matatu, ambayo ni Fungu – 57 Wizara ya Ulinzi na JKT, Fungu 38 – NGOME na Fungu 39 – JKT. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,977,034,489,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 164,000,000,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa Bajeti kwa kila fungu umeainishwa katika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

| Fungu | Matumizi ya Kawaida (TZS) | Matumizi ya Maendeleo (TZS) | Jumla (TZS) |
|---|---|---|---|
| 57 - Wizara | 19,634,547,000.00 | 150,000,000,000.00 | 169,634,547,000.00 |
| 38 - NGOME | 1,607,164,984,000.00 | 10,000,000,000.00 | 1,617,164,984,000.00 |
| 39 - JKT | 350,234,958,000.00 | 4,000,000,000.00 | 354,234,958,000.00 |
| **Jumla** | **1,977,034,489,000.00** | **164,000,000,000.00** | **2,141,034,489,000.00** |

**Fedha Zilizopokelewa Kuanzia Julai 2020 hadi Aprili 2021**

30. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2021, fedha zilizopokelewa zilikuwa ni **Shilingi 1,744,178,001,813.29** sawa

na **asilimia 81.46** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,647,178,500,215.32** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 96,999,501,597.97** ni kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo. Mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa mafungu yote matatu umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3.**

31. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Aprili 2021, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 37,610,598,686.00** ikiwa ni fedha nje ya Bajeti kwa ajili ya shughuli za matumizi mengineyo. Fedha hizo zimetolewa kwa Fungu 38 - NGOME na Fungu 39 – JKT ambazo zimetumika kwa ajili ya Operesheni maalum za ulinzi wa mipaka ya nchi, kugharamia shughuli za uapisho wa Rais wa Awamu ya Tano na kugharamia mazishi ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa na Rais wa Awamu ya Tano Hayati John Pombe Joseph Magufuli.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 222,704,504,764.37** kwa ajili ya kulipa madeni ya Wazabuni wa ndani na nje yaliyohakikiwa, ambapo **Shilingi 175,401,424,719.60** zimetolewa kwa Fungu – 57 Wizara, **Shilingi 47,228,036,544.77** zimetolewa kwa Fungu – 38 NGOME na **Shilingi 75,043,500.00** zimetolewa kwa Fungu – 39 JKT.

***Shughuli Zilizotekelezwa***

33. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali kwa kutumia fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo.

**Matumizi ya Kawaida**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanikiwa kutekeleza shughuli mbalimbali kupitia fedha za matumizi ya kawaida ikiwemo; matunzo ya zana na vifaa vya Jeshi, kukamilisha Mapendekezo ya Mpango wa Miaka Kumi (2021/22 - 2030/31) wa Kuliimarisha Shirika la *Tanzania Automotive Technology Centre – TATC* ambapo Mpango huo pamoja na Waraka wa Baraza la Mawaziri uliwasilishwa kwenye ngazi ya Kamati ya Makatibu Wakuu (IMTC) na kuendelea kukamilisha Rasimu

ya Sera ya Ulinzi wa Taifa, ambapo maoni ya wadau yaliyokusanywa yanaendelea kufanyiwa kazi.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli nyingine ambazo zimetekelezwa na Wizara kwa kutumia fedha za Matumizi ya Kawaida ni:

**(a)Mafunzo ya Kijeshi**

36. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia JWTZ imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi katika Shule na Vyuo vya Kijeshi ndani na nje ya nchi, kwa ajili ya kuwapatia Wanajeshi mafunzo ya awali na kuwaendeleza katika taaluma mbalimbali na uongozi.

Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara kupitia JWTZ kwa kushirikiana na Chuo cha Uhasibu - Arusha imefanikiwa kufanya mahafali kwa wahitimu wa kwanza wa Shahada ya Sayansi ya Kijeshi (Bachelor of Military Science – BMS).

**(b) Mafunzo ya Jeshi la Akiba**

37. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia JWTZ imeendesha mafunzo kwa Jeshi la Akiba kwa wananchi katika ngazi ya awali. Mafunzo hayo yameendelea kufanyika katika Mikoa yote ya Tanzania. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili, 2021 jumla ya wananchi walioandikishwa na kuhitimu mafunzo hayo ni **13,808,** kati ya hao wanaume ni **11,800** na wanawake ni **2,008.** Vile vile, JWTZ kupitia Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya, imeendelea kuelimisha wananchi juu ya masuala ya Ulinzi na Usalama.

**(c) Huduma za Afya na Tiba**

38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi husika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa Maafisa, Askari, Watumishi wa Umma na Familia zao, Vijana wa JKT na Wananchi wanaoishi karibu na vituo vya tiba vya Jeshi hapa nchini. Aidha, Wizara imeendelea na maboresho ya huduma za matibabu kwa Wanajeshi na familia zao, ambapo Halmashauri ya Majeshi ya Ulinzi imeidhinisha uanzishaji wa Huduma za Bima ya Afya Jeshini kuanzia Julai 2020. Huduma hizo zimeanza kutolewa

kuanzia tarehe 01 Oktoba, 2020 ambapo kila Afisa na Askari anachangia asilimia tatu (3%) ya malipo yake ghafi ya kila mwezi. Huduma hiyo imeboresha matibabu kwa Maafisa, Askari, Familia pamoja na Wastaafu.

**(d)Ushirikiano wa Kiulinzi na Kijeshi na Nchi Nyingine**

39. ***Mheshimiwa Spika,*** JWTZ imeendelea kushirikiana na nchi mbalimbali katika masuala ya ulinzi na usalama katika baadhi ya maeneo ambayo ni mafunzo, misaada ya kitaalam, vifaa, zana na mitambo. Vile vile, JWTZ inashirikiana na Umoja wa Mataifa (UN), nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) katika mafunzo na ubadilishanaji wa wataalam. Pia, JWTZ inapata msaada wa mafunzo kwa Maafisa na Askari kutoka nchi za China, Urusi, Marekani, Misri, India, Ujerumani, Uingereza, Bangladesh, Morocco, Canada, Ufaransa, Uholanzi, Indonesia, Oman, Uturuki, Israel, Pakistan, Jordan na Sri Lanka.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC) inaendesha mafunzo ya Usalama na Stratejia kwa Maafisa wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na Watumishi wa Umma wenye madaraka kuanzia ngazi ya Mkurugenzi Msaidizi. Mafunzo hayo hutolewa pia kwa washiriki kutoka nchi za China, Zimbabwe, Afrika Kusini, Kenya, Ghana, Misri, Nigeria, Rwanda, Malawi, Zambia, Namibia, Botswana, Uganda, Msumbiji, Burundi na Bangladesh.

41. ***Mheshimiwa*** **Spika,** naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Ujerumani kupitia *German Armed Forces Technical Advisory Group* (GAFTAG) imetoa msaada wa ujenzi wa majengo ya Idara ya Magonjwa Ambukizi katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, ujenzi wa mabweni na mabwalo katika Kituo cha Mafunzo ya Ulinzi wa Amani (Peacekeeping Training Centre) katika maeneo ya Msata, Pwani na Kunduchi, Dar es Salaam. Aidha, *GAFTAG* inashirikiana na JWTZ katika maandalizi ya ujenzi wa Hospitali Kuu ya Jeshi – Msalato, Dodoma. Pia, *GAFTAG* imewezesha ukarabati wa Kiwanda cha Uchapaji kilichopo Gongo la Mboto ambao ulihusisha uwekaji wa mashine mpya za uchapaji. Vile vile,

Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Jeshi la Ukombozi la Watu wa China (PLA) imewezesha awamu ya pili ya ujenzi wa NDC ambao ulihusisha Jengo Kuu la Mafunzo na Utawala.

**(e)Ushiriki wa JWTZ Katika Shughuli za Ulinzi wa Amani**

42. ***Mheshimiwa Spika,*** JWTZ imeendelea kushirikiana na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) katika Operesheni za Ulinzi wa Amani katika nchi mbalimbali zenye migogoro kwa kupeleka vikosi, Waangalizi wa Kijeshi, Wanadhimu na Makamanda. Mpaka sasa JWTZ ina Vikosi vya Ulinzi wa Amani katika nchi za Lebanon, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Jamhuri ya Afrika ya Kati. Aidha, Jeshi lina Maafisa Wanadhimu, Waangalizi wa Kijeshi na Makamanda kwenye Operesheni za Ulinzi wa Amani nchini
Lebanon, Sudan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan Kusini na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

**(f)Ushirikiano na Mamlaka za Kiraia Katika Shughuli Mbalimbali za Kitaifa**

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia katika shughuli mbalimbali kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Baadhi ya maeneo ambayo JWTZ imeshirikiana na Mamlaka za Kiraia ni: kushiriki katika kuboresha huduma katika Taasisi za Serikali; kushiriki katika ujenzi wa Reli ya *Standard Gauge* na Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (Julius Nyerere Hydro Power Project – JNHPP); kushiriki katika ulinzi wa maeneo ya kimkakati kwa nchi ikiwemo; Mgodi wa *Tanzanite* uliopo Mirerani, Mkoani Manyara na utoaji wa huduma za afya na tiba kwa wananchi ambapo takwimu zilizopo zinaonyesha kwamba **asilimia 80** ya wanaopata huduma katika
Hospitali za Jeshi ni raia.

**(g)Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana**

44. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kuwapatia Vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa.

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Aprili 2021 jumla ya Vijana **21,370** wa Mujibu wa Sheria "Operesheni Uchumi wa Kati" walipatiwa mafunzo kwenye Kambi mbalimbali za Jeshi la Kujenga Taifa, kati yao **16,171** ni wa kiume na **5,199** ni wa kike. Aidha, Mpango wa Wizara ni kuhakikisha vijana wote wanaohitimu kidato cha sita wanachukuliwa kuhudhuria mafunzo hayo.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafunzo kwa vijana, Jeshi la Kujenga Taifa liliendesha mafunzo kwa Watumishi 41 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili kuwajengea maadili mema, ukakamavu na moyo wa uzalendo. Matumaini ya Wizara ni kuwa, watumishi hao watakuwa mfano wa kuigwa katika utekelezaji wa majukumu yao. Pia, naomba kutoa wito kwa Wizara na Taasisi kuleta maombi Wizara ya Ulinzi na JKT ili Watumishi wapate nafasi ya kufanya mafunzo yatakayowaimarisha kulitumikia vyema Taifa.

**(h)Mapambano Dhidi ya Magonjwa Ambukizi na Yasiyoambukiza**

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza na kusimamia mikakati ya kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, kwa kutoa elimu ya jinsi ya kujikinga ili kuzuia maambukizi mapya na kupunguza vifo vitokanavyo na UKIMWI na pia kushiriki mafunzo kwa wataalamu mbalimbali wa tiba na kutoa ushauri nasaha kwa walioambukizwa. Wizara imekuwa ikihimiza upimaji wa hiari kwa Maafisa, Askari, Watumishi wa Umma na Vijana wa JKT. Kwa wale ambao wamethibitika kuwa na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI wamekuwa wakipatiwa dawa za kufubaza virusi katika Vituo vya Huduma na Matibabu na posho kwa ajili ya lishe.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, kwa upande wa magonjwa yasiyoambukizwa jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanyika ikiwemo kutoa elimu ya afya ili kupunguza magonjwa hayo na kupima afya mara kwa mara. Vile vile, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma hushauriwa kuacha uvutaji wa sigara, unywaji pombe uliopitiliza na kufanya mazoezi ya mwili na michezo. Aidha, Wizara inaendelea

kuchukua tahadhari kwa ajili ya kujikinga na maambukizi mapya ya Homa kali ya Mapafu inayosababishwa na Virusi vya Corona (COVID – 19) kulingana na miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**(i)Utawala Bora**

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza dhana ya Utawala Bora katika maeneo ya kazi kwa kushirikisha watumishi wake kupitia vikao mbalimbali vikiwemo vya Baraza la Wafanyakazi, Kamati ya Ukaguzi, Kamati ya Maadili, Bodi ya Manunuzi na Kamati ya Ajira. Pia, Wizara imeendelea kuimarisha jitihada za kupambana na rushwa. Kwa upande wa mapambano dhidi ya rushwa, taarifa za kila robo mwaka zimekuwa zikiandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika. Aidha, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma wameendelea kuhimizwa kuzingatia sheria, kanuni na maadili ya utendaji kazi bila kusahau uzalendo na weledi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

**(j) Utunzaji wa Mazingira**

49. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za utunzaji wa mazingira katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara kupitia Taasisi zake imeendelea na utunzaji wa fukwe katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ili kuzuia mmomonyoko wa udongo. Pia, imefanikiwa kupanda miti 99,851 kwa kutumia vitalu vilivyopo Ruvu JKT, Makutupora JKT, Rwamkoma JKT, Mafinga JKT na Nachingwea JKT.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inamiliki maeneo makubwa yenye miti ya asili ambayo hutunzwa kwa kufanya doria mbalimbali, hivyo kufanya maeneo hayo yasivamiwe kwa shughuli za kijamii, mfano eneo la Pongwe Msungura lililopo Mkoa wa Pwani na Ngerengere lililopo Mkoa wa Morogoro. Aidha, maeneo yote ya Jeshi yana zuio la ukataji miti na kuchoma mkaa.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** Mashirika yaliyo chini ya Wizara, *Tanzania Automotive Technology Centre* (TATC), MZINGA na SUMAJKT yameendelea na uzalishaji kwa kuzingatia sheria,

kanuni na taratibu za uhifadhi wa mazingira. Uzalishaji huo hutumia njia za kisasa za kutibu maji yenye kemikali (water treatment) yanayotoka viwandani. Vile vile, viwanda vimeendelea na utaratibu wa kuwapa wafanyakazi wake vifaa kinga na vyenye mfumo wa kudhibiti sauti ili kuzuia kelele.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara kupitia Shirika la *TATC* imefanikiwa kukamilisha utafiti wa mashine kwa ajili ya uzalishaji wa nishati mbadala. Mashine hizo ni za *Agrowaste briquette* na *Coal briquette* ambazo zinatumia mabaki ya mashambani, vyakula, vumbi la makaa ya mawe na udongo mfinyanzi kutengeneza mkaa.

**Shughuli za Maendeleo**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa fedha za maendeleo, fedha zilizopokelewa na Fungu 57 - Wizara zimetumika katika ununuzi na ukarabati wa zana na vifaa vya Jeshi, kuwasha umeme kwenye Mradi wa Mawasiliano Salama Jeshini na usanidi wa mtandao, ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi ikiwa ni pamoja na Nyabange – Musoma, Ras – Mshindo - Kilwa na ununuzi wa malighafi za kuzalisha zao la msingi kwa Shirika la Mzinga. Aidha, *TATC* imenunua mitambo ya kuyeyusha, kuchonga na kuchomelea chuma kwa ajili ya mradi wa kuzalisha nguzo za chuma na viambata vyake kwa matumizi ya Shirika la Umeme Tanzania na ukamilishaji wa uunganishaji na ukarabati wa magari ya zimamoto. Pia, fedha hizo zimetumika kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara na Taasisi zake.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo kwa Fungu 38 - NGOME zimetumika kwa ajili ya ununuzi na matunzo ya zana na vifaa, kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa, ununuzi wa magari ya utawala, ununuzi wa vipuri vya mitambo ya kuchimbia visima vya maji safi, ujenzi wa maghala pamoja na miundombinu yake.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** fedha zilizopokelewa kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo kwa Fungu 39 - JKT zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu muhimu Makao Makuu ya JKT na baadhi ya Vikosi. Vile vile, fedha hizo zimetumika katika ulipaji wa fidia kwa eneo la Chamwino – Dodoma yalipo Makao Makuu ya JKT na kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Makao Makuu ya JKT Chamwino – Dodoma.

### Shughuli Zilizotekelezwa na Mashirika Yanayosimamiwa na Wizara

56. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia mashirika yake ya *TATC,* MZINGA na SUMAJKT imeendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/ 2021) kwa kufanya tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma mbalimbali kwa matumizi ya kijeshi na kiraia.

### Shirika la *Tanzania Automotive Technology Centre – TATC*

57. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 *TATC* imepokea jumla ya **Shilingi 6,707,810,282.00** kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo. Fedha hizo zimetumika katika usanifu wa mitambo ya kuvunja chuma (cast iron crusher); na kuanza ujenzi wa kiwanda cha uundaji wa nguzo za chuma zinazotumika kusambaza umeme na viambata vyake kwa ajili ya matumizi ya Shirika la Umeme Tanzania, ambapo uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Septemba 2021. Aidha, Shirika limefanya ukarabati wa magari matano (5) ya zimamoto kutoka katika Manispaa na kutengeneza vipuri mbalimbali kwa ajili ya sekta za usafirishaji, kilimo, madini, maji na ulinzi.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** matengenezo ya magari matano (5) ya viwango vya Manispaa yaliyokarabatiwa na kukamilika yamegharimu kiasi cha **Shilingi 444,289,200.00** na iwapo Serikali ingeamua kununua magari mapya ya aina hiyo ingetumia **Shilingi 3,951,900,000.00.** Hivyo, Shirika la TATC limefanikiwa kuokoa kiasi cha fedha **Shilingi 3,507,610,800.00.**

**Shirika la MZINGA**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Shirika limepokea kiasi cha **Shilingi 4,000,000,000.00** zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya uzalishaji wa zao la msingi kwa matumizi ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Aidha, Shirika limefanya ukarabati wa silaha kutoka katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama, kuzalisha vipuri kwa ajili ya mashine za uzalishaji wa zao la msingi na uzalishaji wa mabomu ya kufukuzia wanyama (thunderflash), ambayo yanatumiwa na Mamlaka ya Hifadhi za Taifa.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Mzinga katika jitihada za kujiongezea mapato, limeendelea na utengenezaji wa samani za aina mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Ofisi za Serikali na watu binafsi. Vile vile, kupitia Kampuni Tanzu ya *Mzinga Holding*, Shirika limeendelea na ukamilishwaji wa miradi ya ujenzi katika maeneo mbalimbali yakiwemo: Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi - Singida, Ofisi za Wakurugenzi wa Mbulu - Manyara, Ushetu – Shinyanga, Nzega – Tabora na Hosteli ya Watawa wa Kike wa Kashozi - Bukoba. Vile vile, *Mzinga Holding* imekamilisha ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Bukoba na Kahororo zilizopo Mkoani Kagera na ukamilishaji wa mradi wa *Cottages* Magadu - Morogoro.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Shirika la Mzinga, imeendelea kusimamia na kutunza zana na silaha zinazomilikiwa na makampuni yanayofanya ulinzi katika meli zinazotia nanga kwenye bandari zetu.

**Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMAJKT)**

62. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 SUMAJKT imeendelea kutumia Kampuni Tanzu na Viwanda vyake kutekeleza shughuli za kibiashara ili kuipunguzia Serikali gharama za uendeshaji wa mafunzo ya Vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa. Shughuli hizo ni ujenzi, uanzishaji na uendelezaji wa Viwanda, kilimo na mifugo, ulinzi na mradi wa matrekta na zana za kilimo.

***Shughuli za Ujenzi***

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Ujenzi ya SUMAJKT (SUMAJKT Construction Company Ltd) inaendelea kutekeleza ujenzi wa majengo mbalimbali yakiwemo; Maabara ya Sayansi katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine – Morogoro, Jengo la Halmashauri ya Kibaha Mkoani Pwani, Ofisi za Halmashauri ya Ruangwa Mkoani Lindi, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi, Ukuta kuzunguka Mgodi wa Irasaniro – Butiama Mkoani Mara, Hospitali ya Uhuru – Chamwino Mkoani Dodoma na Majengo ya Makao Makuu ya Uhamiaji – Dodoma.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** vile vile, SUMAJKT *Construction Company Ltd* inakarabati baadhi ya majengo yakiwemo; makazi katika Kampasi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Jengo la Utawala Bungeni – Dodoma, Ofisi za Wakala wa Usajili wa Kampuni zilizopo Dar es Salaam, miundombinu ya Taasisi ya Ubaharia – Dar es Salaam na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa.

65. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021 miradi ya ujenzi iliyoainishwa hapo juu inatarajia kuliingizia Shirika kiasi cha mapato ya **Shilingi 160,816,142,707.17**, ambapo faida inayotarajiwa kupatikana ni **Shilingi 24,122,421,406.08**.

***Shughuli za Uanzishaji na Uendelezaji wa Viwanda***

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Kiwanda cha Samani - Chang'ombe (Chang'ombe Furniture Factory) kilichopo Dar es Salaam kinaendelea na utengenezaji wa samani za taasisi mbalimbali za Serikali na watu binafsi katika mikoa mbalimbali ya Tanzania. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 kiwanda kinatarajia kupata mapato ya **Shilingi 1,640,000,000.00** ambapo faida inayotarajiwa kupatikana ni **Shilingi 127,950,000.00.**

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Kiwanda cha Maji ya Kunywa (SUMAJKT Bottling Plant) kinaendelea na uzalishaji wa maji ya *Uhuru Peak* ambayo yanasambazwa katika Mikoa mbalimbali. Aidha, Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha wastani

wa katoni 2,500 za ujazo wa nusu lita na katoni 4,400 za ujazo wa lita moja kwa siku. Kiwanda kinahudumia wateja kutoka Serikalini na Taasisi binafsi ikiwemo; baadhi ya Vikosi vya JKT, Makao Makuu ya Magereza Dodoma, Shirika la Ndege Tanzania na Ukumbi wa Kimataifa wa Mwalimu Nyerere (Julius Nyerere International Convention Centre – JNICC). Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 kiwanda kinatarajia kupata mapato ya **Shilingi 1,527,000,000.00** ambapo faida inayotarajiwa kupatikana ni **Shilingi 143,901,708.38**.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Kiwanda cha Ushonaji (National Service Garments Factory) kina uwezo wa kuzalisha Kombati 300 hadi 400 kwa siku. Wateja wakuu wa bidhaa zinazozalishwa na Kiwanda ni; JWTZ, SUMAJKT *Guard Ltd*, Jeshi la Akiba, *TANESCO,* Mamlaka ya Bandari Tanzania, Mahakama Kuu – Kanda ya DSM, Wakala wa Huduma za Misitu, Idara ya Uhamiaji, Mamlaka ya Uhifadhi wa Wanyama Pori, Polisi Jamii na Shirika la Kazi Duniani. Katika kipindi hicho Kiwanda kimeweza kupata mapato ya **Shilingi 3,284,000,000.00** na faida ya **Shilingi 191,764,469.60**.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Kiwanda cha Kuchakata Nafaka – Mlale JKT kina uwezo wa kuchakata tani 20 kwa siku. Wateja wa mazao ya kiwanda hiki ni; Mzabuni wa Kikosi, Vikosi vya Jeshi *Base* ya Songea na wateja binafsi katika Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Kiwanda kinatarajia kupata mapato ya **Shilingi 453,263,200.00** ambapo faida inayotarajiwa kupatikana ni **Shilingi 45,326,320.00.**

70. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Kauli Mbiu ya Tanzania ya Viwanda, Wizara kupitia SUMAJKT imeendelea kuanzisha viwanda vipya kwa kutumia vyanzo vya ndani vya fedha pamoja na ubia. Viwanda ambavyo vimeanzishwa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na viko mbioni kuanza uzalishaji ni pamoja na Kiwanda cha Taa za *LED* kilichopo Dar es Salaam na Kiwanda cha Bati kilichopo Dodoma. SUMAJKT imeendelea na jitihada za kutafuta fedha kutoka katika taasisi mbalimbali za kifedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati. Aidha, Shirika limeendelea

kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwemo Vyuo Vikuu, Taasisi za Utafiti pamoja na Wizara na Idara mbalimbali za Serikali ili kuhakikisha miradi yote itakayoanzishwa inatekelezwa kwa ufanisi na tija.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** baadhi ya Wizara, Taasisi na Idara za Serikali ambazo zimeshirikiana kwa karibu na JKT ni pamoja na Wizara ya Kilimo, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Taasisi ya Utafiti ya Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA).

***Shughuli za Kilimo***

72. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha JKT inajitosheleza kwa chakula, umeandaliwa Mkakati wa Kilimo (2019/2020 – 2024/2025) ambao unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao na kujitosheleza kwa chakula. Mkakati huu unatekelezwa kwa Awamu Mbili. Awamu ya Kwanza imehusisha; upimaji wa mashamba na afya ya udongo katika maeneo ya mradi, upatikanaji wa pembejeo, usanifu na uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji, barabara za shambani, ujenzi wa maghala, karakana na viwanda vya kuchakata mazao na kuandaa watendaji.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Awamu ya Kwanza imeanza kutekelezwa mwaka 2019/2020 katika vikosi vya Chita – Morogoro na Milundikwa – Rukwa. Kikosi cha Chita kililima ekari 1,000 za mpunga kwa kutumia gharama ya **Shilingi 755,648,065.00.** Kutokana na uwekezaji uliofanyika, kikosi kilifanikiwa kuvuna tani 972.8 za mpunga sawa na tani 0.97 kwa ekari. Mazao hayo endapo yangeuzwa kwa bei ya soko yangezalisha mapato ya **Shilingi 778,240,000.00** na faida ya **Shilingi 22,591,935.00**. Kikosi cha Milundikwa kililima ekari 1,000 za mahindi na 200 za maharage kwa gharama ya **Shilingi 571,211,000.00** na kuvuna tani 630.5 za mahindi sawa na wastani wa tani 0.63 kwa ekari. Mavuno ya maharage yalikuwa tani 8.7 kutokana na mvua kuwa nyingi. Endapo mazao hayo yangeuzwa kwa bei ya soko, zingepatikana **Shilingi 647,900,000.00** na faida ya **Shilingi 76,689,000.00**.

Aidha, katika kipindi husika vikosi mbalimbali vya JKT vilifanikiwa kulima ekari 6,217.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Awamu ya Pili ambayo imeanza kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2020/2021 itaendelea hadi mwaka 2024/2025. Katika awamu hii mpango utahusiha Vikosi kumi (10) vifuatavyo; Chita – Morogoro, Milundikwa na Luwa – Rukwa, Mlale – Ruvuma, Itaka – Songwe, Oljoro – Arusha, Kanembwa - Kigoma, Mgambo na Maramba – Tanga na Msange – Tabora ambapo vitalima ekari 12,831. Aidha, mkakati huu utagharamiwa kwa kutumia vyanzo vya ndani vya JKT, Bajeti ya Serikali na Taasisi za Kibenki.

***Shughuli za Ulinzi***

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Kampuni ya Ulinzi (SUMAJKT Guard Ltd) imeendelea kutoa huduma ya ulinzi katika Taasisi mbalimbali za Serikali na watu binafsi. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Aprili 2021 Kampuni imefanikiwa kuongeza malindo kutoka **455** hadi kufikia malindo **551,** ambalo ni ongezeko la malindo **96**. Pia, hadi Aprili 2021 Kampuni imeajiri Vijana **13,119** nchi nzima. Aidha, Kampuni imeendelea kuboresha huduma zake kwa kuongeza vitendea kazi mbalimbali ikiwemo magari ya kusafirishia fedha, magari na pikipiki kwa ajili ya doria, kununua silaha na kuanzisha ulinzi kwa kutumia mbwa. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Kampuni ya Ulinzi inatarajia kupata mapato ya **Shilingi 34,770,375,312.25,** ambapo faida inayotarajiwa kupatikana ni **Shilingi 7,885,754,530.28.**

***Mradi wa Matrekta na Zana za Kilimo***

76. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika kupitia Mradi wa matrekta limeendelea kuagiza na kuuza Matrekta, vipuri na zana zake kwa bei nafuu ili kumfanya mkulima kuweza kumudu kununua. Vile vile, kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 Mradi wa matrekta ulipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 5,170,000,000.00** kwa kuuza matrekta, zana na vipuri na unatarajia kupata faida ya **Shilingi 186,715,933.00.**

77. ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzia Julai 2020 hadi Aprili 2021 jumla ya **Shilingi 465,147,158.00** zimekusanywa ikiwa ni madeni kutoka kwa washitiri mbalimbali waliokopa matrekta na zana

zake. Mradi unaendelea na juhudi za ukusanyaji wa madeni kutoka kwa wadaiwa sugu, ambao miongoni mwao walikuwa Watumishi wa Umma pamoja na watu binafsi.

## CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali kubwa ikiwa ni ukomo mdogo wa bajeti na upungufu wa rasilimali watu. Kwa upande wa rasilimali fedha, kiasi cha fedha za maendeleo na matumizi mengineyo kilichoidhinishwa ni pungufu ikilinganishwa na kiasi kinachohitajika kutekeleza majukumu ya msingi ya Wizara. Aidha, fedha za maendeleo zilizotolewa kwa kiasi kikubwa zimetumika kulipia mikataba michache ya ununuzi wa zana na vifaa na kutekeleza miradi mingine ya maendeleo.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** kupatiwa ukomo mdogo wa bajeti ya maendeleo kumepelekea Wizara kutofikia malengo ya utekelezaji kwa baadhi ya maeneo hususan; ununuzi wa zana na vifaa vya Kijeshi, utafiti na uzalishaji wa mazao ya msingi katika viwanda vya Kijeshi, kuboresha makazi, kambi na ofisi. Maeneo mengine yaliyoathirika ni upimaji, uthamini na kulipa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi, kuboresha Mawasiliano Salama Jeshini, kugharamia matengenezo ya zana na vifaa. Vile vile, Wizara haijakamilisha baadhi ya miradi ya kuboresha Kambi za JKT na miundombinu yake.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** changamoto nyingine ni uwezo mdogo kifedha wa; kugharamia matunzo ya zana na vifaa, kufanya mafunzo na mazoezi ya Kijeshi inavyostahili, kugharamia uendeshaji wa Ofisi za Waambata Jeshi, kugharamia uondoshaji wa vifaa bandarini na katika Viwanja vya Ndege, kugharamia upatikanaji wa Sare kwa Wanajeshi, kugharamia likizo na uhamisho kwa Wanajeshi na Watumishi wa Umma, kugharamia huduma za chakula kulingana na mahitaji halisi na kulipa madeni ya wazabuni na wakandarasi waliotoa huduma mbalimbali.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa SUMAJKT, changamoto inayolikabili Shirika ni ukosefu wa mitaji kwa ajili ya kuanzisha miradi mikubwa.

**Hatua za Kukabiliana na Changamoto**

82. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kukabiliana na changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha, kwa kuendelea kutumia vizuri kiasi kinachotolewa kutekeleza majukumu yake. Aidha, Wizara inaipongeza Serikali kwa kusisitiza matumizi ya *Force Account* katika kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi na hivyo kupunguza gharama. Pia, Wizara imeendelea kukutana na wazabuni pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango kwa lengo la kupitia na kukubaliana namna ya kulipa madeni husika hasa ya Kimkataba.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa kulipa baadhi ya madeni ya Wazabuni.

84. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto ya Rasilimali Watu, Wizara imeendelea kuwasiliana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupata vibali vya ajira kuziba nafasi zilizo wazi katika Mashirika ya MZINGA na *TATC*. Aidha, Mashirika yameendelea kutumia wataalamu kutoka JWTZ kuziba baadhi ya nafasi zilizo wazi kwa dharura.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa mitaji, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango inaendelea na jitihada za kuiwezesha SUMAJKT kutumia rasilimali zake kama dhamana ya kupata Mikopo katika taasisi za fedha.

**MPANGO NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

86. ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ni kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na ufasaha kulingana na Dira na Dhima ya Wizara.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** mwelekeo wa shughuli zinazokusudiwa kufanyika katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 utazingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo:

a. Kuliimarisha Jeshi kwa kulipatia zana na vifaa vya kisasa, mawasiliano, rasilimali watu pamoja na kutoa mafunzo kwa wanajeshi ili kuliongezea uwezo na weledi wa kiutendaji na utayari kivita;

b. Kuendeleza jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka ya nchi yetu na nchi jirani;

c. Kuboresha mazingira ya kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa umma;

d. Kuendelea kujenga uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa zana na vifaa vya kilimo ili liweze kujitosheleza kwa chakula na kuboresha miundombinu katika vikosi ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi na kutoa mafunzo ya uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa na stadi za kazi;

e. Kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia;

f. Kuimarisha na kuratibu Mafunzo ya Jeshi la Akiba;

g. Kuimarisha ushirikiano na Jumuiya za Kimataifa, Kikanda na nchi moja moja katika nyanja za kijeshi na kiulinzi;

h. Kuendelea kushirikiana na Mamlaka za Kiraia; na

i. Kufanya upimaji, uthamini na ulipaji fidia ya ardhi katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

## SHUKRANI

88. ***Mheshimiwa Spika,*** kabla sijahitimisha Hotuba yangu napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Viongozi na watendaji wa Wizara na Taasisi zake kwa michango waliyotoa

katika kutayarisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu. Namshukuru Katibu Mkuu **Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe,** Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi **Jenerali Venance Salvatory Mabeyo,** Mnadhimu Mkuu wa Jeshi **Luteni Jenerali Yacoub Hassan Mohamed,** Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa **Meja Jenerali Charles Mang'era Mbuge,** Wakuu wa Kamandi na Wakuu wa Mashirika.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** pia napenda kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo (Wizara ya Ulinzi na JKT), Wakuu wa Matawi (Makao Makuu ya Jeshi), Wakuu wa Idara (Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa), Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma waliopo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kufanikisha majukumu ya Wizara.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya Serikali kutoa shukrani kwa Serikali za nchi mbalimbali na washirika wa maendeleo kwa ushirikiano walioipatia Wizara yangu. Serikali na washirika wa maendeleo hao ni pamoja na; Jamhuri ya Watu wa China, Ujerumani, India, Marekani, Canada, Ufaransa na Uturuki. Aidha, tunazishukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu za Ulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Bangladesh, Falme za Kiarabu, Ghana, Indonesia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Uholanzi, Morocco, Nigeria, Uingereza, Urusi na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kuwashukuru wananchi wote kwa ushirikiano wanaoutoa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania katika ulinzi wa nchi yetu. Kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru Waheshimiwa Madiwani waliofika leo hapa bungeni pamoja na wapiga kura wangu wa Jimbo la Ushetu kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa tangu wanichague kuwawakilisha. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

92. ***Mheshimiwa* Spika,** vile vile, natoa shukrani za dhati kwa Maafisa na Askari walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uapisho na mazishi ya viongozi wetu wapendwa waliolitumikia Taifa hili kwa moyo wa uzalendo.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba uniruhusu kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/ 2022.

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli**

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara inatarajia kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 85,103,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu, kwa mchanganuo ufuatao katika **Jedwali Na. 3.**

**Jedwali Na. 3: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

| Fungu | Makadirio ya Maduhuli 2021/2022 |
|---|---|
| 57 – Wizara | 1,200,000.00 |
| 38 –NGOME | 22,000,000.00 |
| 39 – JKT | 61,903,000.00 |
| **Jumla** | **85,103,000.00** |

**Matumizi ya Kawaida na Maendeleo**

95. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika Mwaka wa Fedha 2021/ 2022 ili iweze kutekeleza majukumu yake inaomba iidhinishiwe na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 2,358,694,986,000.00** kwa mafungu yote matatu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,182,116,562,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 176,578,424,000.00** ni kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo. Mchanganuo kwa kila Fungu umeainishwa katika **Jedwali Na. 4.**

**Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Bajeti kwa Kila Fungu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

| Fungu | Matumizi ya Kawaida (TZS) | Matumizi ya Maendeleo (TZS) | Jumla (TZS) |
|---|---|---|---|
| 57 - Wizara | 20,166,322,000.00 | 140,000,000,000.00 | 160,166,322,000.00 |
| 38 - NGOME | 1,779,475,285,000.00 | 32,578,424,000.00 | 1,812,053,709,000.00 |
| 39 - JKT | 382,474,955,000.00 | 4,000,000,000.00 | 386,474,955,000.00 |
| **Jumla** | **2,182,116,562,000.00** | **176,578,424,000.00** | **2,358,694,986,000.00** |

**MWISHO**

96. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mawaziri wenzangu na Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii, inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo ni ***www.modans.go.tz***

97. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa Hoja.

**KIAMBATISHO NA. 1**

**UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA YALIYOTOLEWA KATIKA MKUTANO WA 19**

**Agizo 1:** Serikali iongeze ukomo wa bajeti kwa mafungu yote matatu ili kuwezesha kukabiliana na changamoto zenye umuhimu zaidi kutatuliwa.

**Utekelezaji:** Serikali imekuwa ikiongeza ukomo wa Bajeti kwa mafungu yote ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kuzingatia hali ya uchumi wa nchi kwa kila Mwaka wa Fedha. Katika mwaka 2020/2021 bajeti ya Wizara kwa mafungu yake yote imeongezeka kwa **asilimia 15.5**.

**Agizo 2:** Serikali itoe fedha zinazohitajika katika ujenzi wa Makao Makuu ya Jeshi – Kikombo, Dodoma ili ujenzi huo uendane na wakati.

**Utekelezaji:** Hadi sasa Serikali imekwishatoa jumla ya **Shilingi 10,000,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi

wa Taifa. Serikali itaendelea kutoa fedha za ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa hadi hapo utakapokamilika kwa kuzingatia bajeti ya utekelezaji wa mradi huo.

**Agizo 3:** Serikali ipatie fedha Wizara hii kwa ajili ya kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yamechukuliwa na yanayotarajiwa kuchukuliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi.

**Utekelezaji:** Katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 na 2020/2021, Serikali ilitoa jumla ya **Shilingi 6,924,544,927.00** na **Shilingi 1,418,562,566.00** mtawalia kwa ajili ya upimaji, uthamini na ulipaji fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi.

**Agizo 4:** Serikali ione umuhimu wa kufanya ukarabati wa haraka wa nyumba za makazi ya wanajeshi kwa kuanzia na zile ambazo zipo katika hali isiyoridhisha, ili kuepuka gharama kubwa inayoweza kujitokeza ya kuzijenga upya.

**Utekelezaji:** Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za makazi kwa Wanajeshi. Aidha, Wizara inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kupata fedha za kufanya ukarabati wa nyumba hizo.

**Agizo 5:** Serikali iongeze bajeti ya vijana wanaohitajika kujiunga na JKT na kuweka utaratibu utakaowawezesha vijana hao kupata ujuzi na uzoefu wa kazi za kujitegemea unaotambulika baada ya mafunzo yao.

**Utekelezaji:** Serikali imeongeza bajeti ya kuhudumia vijana wanaoudhuria mafunzo ya JKT.

Vijana wanaendelea kupatiwa mafunzo ya stadi za kazi kupitia shughuli mbalimbali zikiwemo Kilimo, Uvuvi, Ufugaji na Ufundi. Mashamba darasa yaliyopo makambini yanasaidia Vijana kujifunza mbinu mbalimbali za kilimo na ufugaji zitakazowawezesha kujitegemea mara wamalizapo mafunzo. Aidha, JKT imeingia makubaliano na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) yanayolenga

kuwapatia elimu ya ujasiriamali Vijana waliopo katika mafunzo ya JKT.

**Agizo 6**: Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Serikali itoe kipaumbele cha kutoa fedha zilizoidhinishwa kwenye mafungu yake matatu.

**Utekelezaji:** Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Serikali imetoa fedha **asilimia 81.45** ya bajeti yote iliyoidhinishwa hadi kufikia mwezi Aprili 2021.

**Agizo 7:** Serikali iyapatie fedha za kutosha mashirika ya Mzinga na Nyumbu ili yaweze kuendeleza tafiti zake zinazoendelea na kuanzisha tafiti mpya zenye tija kwa nchi yetu kwani dalili njema zimeanza kuonekana kama vile utengenezaji wa magari ya zimamoto.

**Utekelezaji:** Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Serikali imeyapatia Mashirika ya *TATC* na Mzinga fedha za maendeleo jumla ya **Shilingi 10,707,810,282.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 6,707,810,282.00** sawa na **asilimia 89.44** ya bajeti iliyoidhinishwa zimetolewa kwa Shirika la *TATC* na **Shilingi 4,000,000,000.00** sawa na **asilimia 100** ya bajeti iliyoidhinishwa zimetolewa kwa Shirika la Mzinga.

**KIAMBATISHO NA. 2**

## UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI 2020 – 2025 KATIKA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Serikali kupitia Wizara inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025 sambamba na majukumu mengine ya Wizara. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara imetekeleza Ilani ya Uchaguzi ifuatavyo:

**Ibara 105 (a) Kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi na mipaka yake ili kudumisha Muungano, kulinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, umoja, mshikamano, amani na usalama wa raia na mali zao.**

**Utekelezaji**: Wizara kupitia JWTZ imeendelea kuimarisha vikosi vilivyopo mipakani kulingana na hali ya matishio na kuboresha mazingira ya kazi kwa Maafisa na Askari waliopo mipakani. Aidha, JWTZ imeendelea kuimarisha ushirikiano na Majeshi ya Nchi jirani na Jumuiya za Kikanda, katika mafunzo, mikutano ya pamoja na vikao vya ujirani mwema vinavyofanyika mara kwa mara katika Mikoa na Wilaya za mpakani kwa kushirikiana na Mikoa na Wilaya za nchi tunazopakana nazo.

**Ibara 105 (b) Kuendeleza jitihada za utatuzi wa changamoto za mipaka ya nchi yetu na nchi jirani.**

**Utekelezaji:** Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea kuchukua jitihada kuhakikisha changamoto za mipakani zinatatuliwa kwa njia ya mazungumzo. Changamoto ya mpaka kati ya Tanzania na Malawi inaendelea kutafutiwa ufumbuzi na Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kupitia Tume ya Usuluhishi inayoongozwa na Mheshimiwa Joachim Chissano, Rais Mstaafu wa Msumbiji. Kwa upande wa mpaka wetu na Burundi wenye urefu wa kilomita 469.847, uhakiki umefanyika ambapo sehemu ya Mpaka yenye urefu wa kilomita 135 imewekwa alama za mpaka. Pia, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Serikali za Tanzania na Burundi zimepanga kuendelea na kazi za uimarishaji wa sehemu ya mpaka yenye urefu wa kilomita 122. Aidha, changamoto za mipaka kati ya Tanzania na nchi za Uganda, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Rwanda na Kenya zinaendelea kujadiliwa katika vikao rasmi baina ya nchi husika.

**Ibara 105 (c) Kuwezesha ushirikiano wa vyombo vya ulinzi na usalama kufanya utafiti na ubunifu kwa kushirikiana na taasisi za utafiti.**

**Utekelezaji:** Wizara kupitia Taasisi yake ya Utafiti na Uhawilishaji wa Teknolojia ya Magari (TATC) imeendelea kushirikiana na Taasisi za utafiti ikiwemo Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO) ambapo wamefanikiwa kutafiti na kutengeneza mashine ya kuchakata nyuzi za

mkonge (Sisal Decorticator) ambayo inasubiri kuzalishwa kibiashara. Aidha, ushirikiano umeendelea kufanyika na Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo (TEMDO) na Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH) katika azma ya kuendeleza utafiti na kuongeza ubunifu kwa Shirika la *TATC*. Wizara imeanza ujenzi wa Idara ya Magonjwa Ambukizi katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo kwa ajili ya kufanya tafiti kwa kushirikiana na taasisi za utafiti wa magonjwa.

**Ibara 105 (d) Kuhusisha kikamilifu Majeshi ya Ulinzi na Usalama katika kulinda miradi mikubwa ya kimkakati.**

**Utekelezaji:** Wizara kupitia JWTZ imeendelea kushiriki katika ulinzi wa baadhi ya miradi ya kimkakati kwa nchi ikiwemo miradi ya Reli ya Kisasa (SGR) na Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP). Aidha, JWTZ imeendelea kushiriki katika ulinzi wa maeneo ya kimkakati kwa nchi ikiwemo; Mgodi wa *Tanzanite* uliopo Mirerani, Mkoani Manyara, Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Kampuni ya Simu (TTCL) na maeneo ya Viwanja vya Ndege ambapo Maafisa na Askari wa JWTZ wanashiriki kikamilifu.

**Ibara 105 (e) Kuhamasisha na kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi, uzalendo wa kitaifa, usalama na umuhimu wa kushiriki katika ulinzi ikiwa ni pamoja na Jeshi la Akiba na ulinzi shirikishi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.**

**Utekelezaji:** Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, Wizara kupitia JWTZ kwa kushirikiana na Kamati za Usalama za Mikoa na Wilaya, imeendelea kuelimisha wananchi juu ya masuala ya Ulinzi na Usalama. Katika kipindi hicho, Wizara kupitia JWTZ imeendesha mafunzo ya awali ya Jeshi la Akiba kwa Wananchi katika Mikoa yote ya Tanzania. Wananchi walioandikishwa na kuhitimu mafunzo hayo ni **13,808,** kati ya hao wanaume ni **11,800** na wanawake ni **2,008.** Wizara kupitia JKT imeendelea kuwapatia Vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2020 hadi Aprili 2021 jumla ya Vijana **21,370** wa Mujibu wa Sheria "Operesheni Uchumi wa Kati" walipatiwa mafunzo kwenye Kambi

mbalimbali za Jeshi la Kujenga Taifa, kati yao **16,171** ni wa kiume na **5,199** ni wa kike.

**Ibara 105 (g) Kuimarisha uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama katika kushiriki shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na kuanzisha viwanda katika sekta ya ulinzi na maeneo mengine ya kimkakati.**

**Utekelezaji:** Wizara kupitia JKT imeendelea kuanzisha na kuendeleza viwanda mbalimbali vikiwemo; Kiwanda cha Maji ya Kunywa, Kiwanda cha Ushonaji, Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi, Kiwanda cha Samani, Kiwanda cha kutengeneza taa zinazotumia nishati ya jua vilivyopo katika Mkoa wa Dar es Salaam, Kiwanda cha Kuchakata Nafaka kilichopo Mkoani Ruvuma na Kiwanda cha kutengeneza mabati kilichopo Mkoani Dodoma ambacho kinatarajia kuanza uzalishaji katika Mwaka wa Fedha 2021/2022. Aidha, Shirika la *TATC* limeanza ujenzi wa Kiwanda cha uundaji wa nguzo za chuma zinazotumika kusambaza umeme na viambata vyake kwa ajili ya matumizi ya Shirika la Umeme Tanzania, ambapo uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Septemba 2021.

**Ibara 105 (h) Kuimarisha viwanda vya NYUMBU na Mzinga ili viweze kutimiza azma ya kuanzishwa kwake.**

**Utekelezaji:** Wizara kupitia Shirika la *TATC* imeandaa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi (2021/22 - 2030/31) wa kuliimarisha Shirika ambao unalenga; kuendeleza wataalamu katika utafiti, ubunifu na utengenezaji wa magari na mitambo, kukarabati miundombinu ya teknolojia na kununua mitambo mipya, kuendeleza utafiti na uhawilishaji wa teknolojia za magari, kueneza matokeo ya tafiti kwa kuanzisha viwanda na kukuza masoko ya bidhaa. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Shirika la *TATC* limepokea **Shilingi 6,707,810,282.00** sawa na **asilimia 89.44** ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa. Shirika la Mzinga limepokea **Shilingi 4,000,000,000.00** sawa na **asilimia 100** ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa kwa ajili ya ununuzi wa malighafi zitakazotumika katika uzalishaji wa mazao ya msingi yatakayotumika na Vyombo vya Ulinzi na Usalama.

**Ibara 105 (i) Kuimarisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ili viwe vyombo vya kuwapatia vijana ujuzi wa kujiajiri na kuajiriwa na pia kuwa vyombo mahiri vya huduma na uzalishaji mali hasa katika ujenzi, kilimo, ufugaji na uvuvi.**

**Utekelezaji:** Wizara inaiimarisha JKT katika uzalishaji hususan kilimo, ambapo katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ilinunua zana mbalimbali ikiwemo matrekta kumi na sita (16) yenye thamani ya **Shilingi 1,965,227,080.00** na mitambo sita (6) yenye thamani ya **Shilingi 142,782,421.00** kwa kutumia vyanzo vya ndani. Aidha, JKT imeingia makubaliano ya awali na Wizara ya Kilimo na Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi kwa lengo la kuboresha shughuli za kilimo na kuwapatia vijana ujuzi, mtawalia. Vile vile, sekta ya ujenzi imeendelea kuimarishwa kwa zana na mitambo yenye thamani ya **Shilingi 4,986,436,266.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi. Vijana wanaendelea kushiriki katika miradi hiyo kwa lengo la kuwapatia ujuzi ili waweze kujiajiri baada ya kuhitimu mafunzo. Maboresho ya mitaala ya mafunzo ya vijana yanaendelea kufanyika ili kuwajengea uwezo wa kujiajiri. Pia, JKT imesajili na kuimarisha vyuo vyake vya Ufundi Stadi vilivyopo Vikosi vya Jeshi; 822KJ (Rwamkoma), 831KJ (Mgulani), 832KJ (Ruvu), 834KJ (Makutopora), 838KJ (Maramba) na 843KJ (Nachingwea). Sambamba na hayo eneo la ukubwa wa ekari 576 limenunuliwa katika Wilaya ya Kongwa - Dodoma kwa ajili ya kuanzisha Chuo cha Ufundi Stadi.

**Ibara 105 (j) Kupanua na kuongeza idadi ya kambi za JKT na JKU ili kuwezesha vijana wengi zaidi wakiwemo wahitimu wote wa kidato cha sita kupata fursa ya mafunzo ili kujenga uzalendo na moyo wa kujitolea.**

**Utekelezaji:** Wizara kupitia JKT inaendelea kupanua na kuongeza Kambi ili kuchukua vijana wengi zaidi. Uwezo wa Kambi za JKT kwa sasa ni kuchukua Vijana **50,000** kwa wakati mmoja. Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 mafunzo ya Mujibu wa Sheria yameendeshwa kwa Vijana **21,370** ambao ni asilimia **28.59** ya Vijana **74,753** waliohitimu kidato cha sita

katika kipindi husika. Idadi ya vijana wanaohudhuria mafunzo hayo itaendelea kuongezeka kadri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu. Aidha, Mpango wa Wizara ni kuhakikisha vijana wote wanaohitimu kidato cha sita wanachukuliwa kuhudhuria mafunzo hayo.

**Ibara 105 (l) Kuboresha mazingira ya kazi kwa kuwapatia makazi bora na kuongezea uwezo wa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia mafunzo ya kitaaluma na kitaalam, vitendea kazi na zana za kisasa zinazoendana na teknolojia ya kisasa.**

**Utekelezaji:** Katika kuboresha makazi kwa Maafisa na Askari, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa makazi. Wizara inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Fedha na Mipango ili kupata fedha za kukamilisha nyumba 3,936 katika Mradi wa Nyumba 10,000 za awali ambapo kati ya hizo Nyumba 6,064 zimekamilika. Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wa JWTZ kwa kutoa mafunzo ili kujenga Jeshi imara na lenye weledi utakaowezesha kukabiliana na matishio ya kiusalama. Mafunzo hayo yameendelea kutolewa katika Vyuo na Shule za Kijeshi ndani na nje ya nchi. Vile vile, JWTZ imeendelea kuimarishwa kwa kupatiwa zana za kisasa na kuboresha zilizopo kwa lengo la kuwa na utayari wakati wote.

**KIAMBATISHO NA. 3**

**MCHANGANUO WA FEDHA ZILIZOPOKELEWA KUANZIA JULAI 2020 HADI APRILI 2021**

| Fungu | Matumizi Yaliyoidhinishwa | Bajeti ya Mwaka 2020/2021 | Kiasi Kilichopokelewa Hadi Aprili, 2021 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 57 - Wizara | Mishahara (Wizara na Mashirika) | 9,693,002,000.00 | 6,855,709,000.00 | 70.73 |
| | Ruzuku (Mashirika na Majenerali) | 6,874,634,814.00 | 4,658,126,268.35 | 67.76 |
| | Matumizi Mengineyo | 3,066,910,186.00 | 2,662,085,269.30 | 86.80 |
| | Maendeleo | 150,000,000,000.00 | 83,803,992,017.65 | 55.87 |
| | **Jumla ya Fungu** | **169,634,547,000.00** | **97,979,912,555.30** | **57.64** |
| 38 - NGOME | Malipo na Posho (Pay and Allowance) | 1,290,280,923,000.00 | 1,069,155,517,568.67 | 82.86 |
| | Chakula | 219,284,700,000.00 | 180,346,517,833.00 | 82.24 |
| | Matumizi Mengineyo | 35,519,761,000.00 | 32,646,423,104.00 | 91.91 |
| | Misamaha ya Kodi | 62,079,600,000.00 | 49,156,200,000.00 | 79.18 |
| | Maendeleo | 10,000,000,000.00 | 9,694,160,292.32 | 96.94 |
| | **Jumla ya Fungu** | **1,617,164,984,000.00** | **1,340,998,818,797.99** | **82.92** |
| 39 - JKT | Malipo na Posho (Pay and Allowance) | 221,338,851,000.00 | 197,071,135,134.00 | 89.04 |
| | Chakula na Posho ya Chakula | 70,984,053,000.00 | 55,053,830,500.00 | 77.56 |
| | Matumizi Mengineyo | 30,419,054,000.00 | 25,472,955,538.00 | 83.74 |
| | Mafunzo ya Vijana kwa Mujibu wa Sheria | 16,000,000,000.00 | 16,000,000,000.00 | 100 |
| | Posho ya Msamaha wa Kodi | 11,493,000,000.00 | 8,100,000,000.00 | 70.48 |
| | Maendeleo | 4,000,000,000.00 | 3,501,349,288.00 | 87.53 |
| | **Jumla ya Fungu** | **354,234,958,000.00** | **305,199,270,460.00** | **86.16** |
| | **JUMLA KUU** | **2,141,034,489,000.00** | **1,744,178,001,813.29** | **81.46** |

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,WAZEE NA WATOTO**: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono ahsante sana Mheshimiwa Waziri, sasa kama ulivyo utaratibu wetu tunaendelea, nimuite sasa

Mwenyekiti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama. Kwa niaba yake Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. VINCENT P. MBOGO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Taarifa hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa mezani mapema asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nafahamu kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 175(1) na (2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Juni, 2020 inakataza kurejea kutoa salaam za pole au pongezi baada ya wewe au Waziri Mkuu kufanya hivyo, lakini kutokana na jukumu la msingi la Kamati hii hususan kwa Wizara hii naomba uniwie radhi na uniruhusu kutoa salaam za pole kwa kifo cha aliyekuwa Amiri Jeshi Mkuu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa kuwa leo ni siku ya kibajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati yangu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa jinsi alivyoanza vyema kwa kuchukua hatua muafaka za kuendeleza mipango ya kuliwezesha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama nchini katika nyanja zote ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Kwa hakika sote tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumzidishia hekima na busara katika kuliongoza vyema Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue kw nafasi ya kipekee kukupa pole pamoja na Wabunge wenzangu kwa msiba uliotufikia kwa Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali mema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya salaam hizo za rambirambi na pongezi, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya

Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa kifungu cha 6(6) na kifungu cha 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaju inajumuisha mafungu matatu ya kibajeti yafuatayo; Fungu 38 - Ngome; Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa; na Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne zifuatazo: matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo ukurasa wa 4 - 9; mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ukurasa wa 9 – 22; uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ukurasa wa 23-30; na maoni na ushauri wa Kamati ukurasa wa 30 - 35.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa Mradi Namba 6103 - *Defence Scheme* wa Fungu 57 - Wizara, katika maeneo mawili tofauti kwenye Mikoa ya Singida na Arusha. Kamati ilikagua Mradi wa Mawasiliano Salama Jeshini - Ikungi, Singida, na nyumba 112 za makazi katika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli, Arusha zilizojengwa katika awamu ya kwanza ya Mradi wa Nyumba 10,000 za makazi ya Wanajeshi. Aidha, Kamati ilitembelea na kukagua masuala ya kiulinzi katika machimbo ya madini ya *Tanzanite*, Mererani, Mkoani

Manyara ambapo changamoto zilizobainika zilitolewa ushauri mahsusi na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi hiyo kama yanavyoonekana katika ukurasa wa 7 na wa 8 wa taarifa hii, Kamati ilitowa maoni yafuatayo kuwa; ili kufanikisha adhma ya Serikali ya kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa changamoto ya makazi kwa wanajeshi, utengaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya ukarabati na ujenzi wa makazi hayo, na upatikanaji wake kwa wakati ni jambo muhimu na linatakiwa kupewa uzito unaostahili; upo umuhimu wa Serikali kubadilisha utaratibu wa kulipa kodi ya pango kwa kila mwezi kwa wananchi ambao maeneo yao yanatumiwa kwa ajili ya mradi wa mawasiliano salama Jeshini, na badala yake kuwe na utaratibu wa kulipa fidia ili maeneo hayo yamilikiwe na Jeshi. Ni vema Serikali ikaendelea kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ya sekta hii kutokana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ulilenga kulinganisha makusanyo ya mapato na lengo la makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukusanyaji wa mapato, naomba kutoa taarifa kuwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 85,103,000/= kwa mafungu yote matatu ya Wizara. Makadirio haya yalikuwa ni ongezeko la asilimia 4.7 ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ya shilingi 81,104,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa maelezo ya Wizara, hadi kufikia mwezi februari, 2021, kiasi kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa ni shilingi milioni 76,085,664.16 sawa

na asilimia 89 ya lengo la mwaka lililopangwa. Kamati ilibaini kuwa kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la asilimia 41.35 ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa Fungu 38 - Ngome na Fungu 39- JKT ndio yamechangia ongezeko hilo ambapo Fungu 38 - Ngome limekusanya asilimia 155 ya lengo lililowekwa na Fungu 39 - JKT limekusanya asilimia 68 ya makadirio yake. Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Fungu 57 Wizara halikukusanya fedha zozote kama ilivyokuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020. Kamati ilihoji kuhusu sababu za Fungu 57 kushindwa kukusanya na Wizara ilitoa maelezo kama inavyoonekana katika ukurasa wa 12 wa taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya ulinganisho wa malengo ya makusanyo kwa kila fungu ikilinganishwa na kiasi halisi kilichokusanywa. Ulinganisho huo umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo huu wa makusanyo ni mzuri na Wizara inaweza kufikia lengo la makusanyo ifikapo tarehe 30 Juni, 2021. Maelezo ya kina kuhusu uchambuzi wa makusanyo yanapatikana katika ukurasa wa 10 hadi wa 15 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina, Kamati ilifanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha fedha kilichotolewa hadi kufikia mwezi Februari, 2021. Aidha, Kamati ililinganisha uwiano wa bajeti za mafungu ya Wizara na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa mafungu hayo. Ulinganisho huo unaonekanaka katika majedwali namba 02 na Namba 03 ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia uchambuzi huo Kamati ilibaini masuala nane yakiwemo yafuatayo; hadi kufikia mwezi Februari, 2021 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mafungu yote matatu imepokea shilingi 1,404,135,476,314.81sawa na asilimia 65.58 ya fedha zilizoidhinishwa. Asilimia 92.67 ya fedha zilizopokelewa ni kwa

ajili ya matumizi ya kawaida na asilimia 7.33 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya shilingi 95,917,678,289.97 zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, asilimia 89.89 ya fedha hizo ni kwa ajili ya Fungu 57 la Wizara na asilimia 10.11 ni kwa ajili ya Fungu 38 - Ngome. Kati ya fedha za maendeleo zilizotolewa, Fungu 38 - Ngome limepokea asilimia 96.94 ya shilingi bilioni 10 ilizoidhinishiwa na Fungu 57 - Wizara limepokea asilimia 57.48 ya shilingi bilioni 150 zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 39 - JKT halijapokea fedha zozote za miradi ya maendeleo kati ya shilingi bilioni nne zilizoidhinishwa kwa ajili ya Fungu hilo. Katika fedha zilizoidhinishwa kwa kila fungu, Fungu 38 - Ngome lilipokea asilimia 65.62; Fungu 39 - JKT lilipokea asilimia 69.29 na Fungu 57 - Wizara lilipokea asilimia 57.48.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi huo unaonesha kuwa Serikali ilizingatia ipasavyo uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha bajeti. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na mtiririko wa utolewaji wa fedha za maendeleo kwa ajili ya Fungu 39 - JKT. Ni rai ya Kamati kuwa Serikali itoe fedha hizo za maendeleo kwa ajili ya Fungu 39 - JKT kwa mujibu wa ratiba ya utekelezaji wa miradi iliyowekwa ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kuchambua mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Kamati ilishauri masuala saba yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti hiyo kwa mafungu yote matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika masuala yaliyotolewa ushauri, masuala manne yametekelezwa kikamilifu, masuala mawili yanaendelea kutekelezwa, na suala moja bado halijatekelezwa kikamilifu kutokana na changamoto za

kibajeti kama inavyoonekana katika ukurasa wa 20 hadi 22 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiujumla, Kamati inaipongeza Wizara kuwa, pamoja na changamoto za kibajeti zilizojitokeza, imeendelea kutumia kiwango kilichotengwa kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujiridhisha na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na dira na dhima ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa majukumu yaliyopangwa yatawezesha ufikiaji wa malengo sita ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itatoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia mpango kazi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mafungu yote matatu 38, 39 na 57 inategemea kukusanya mapato ya jumla ya 108,104,000. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 21.28 ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2020/2021. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 38 - Ngome ambapo lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa asilimia 104.55.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia maoni ya Kamati kuhusu lengo la ukusanyaji wa mapato kwa kuzingatia uhalisia wa makusanyo yanayopatikana. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa uhalisia wa makusanyo kwa ajili ya Fungu 57 uangaliwe upya. Maelezo ya kina kuhusu makadirio ya

mapato ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/2022 yapo katika Ukurasa wa 24 hadi 27 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya kamati yalibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2021/2022, bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa Mafungu yote matatu ni shilingi 2,358,694,985,502. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,182,116,562,000 sawa na asilimia 92.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 176,578,423,502 sawa na asilimia 7.5 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukidhi mantiki ya masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

(a) Bbajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imeongezeka kwa shilingi 217,660,496,502 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021. Tofauti hiyo ni ongezeko la asilimia 9.23. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake wa mara kwa mara wa kuongeza kiwango cha Bajeti ya Wizara hii na vyombo vyake vyote inavyovisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kimeongezeka kwa shilingi 12,578,423,502 ambayo ni sawa na asilimia 7.12 ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika mwaka wa fedha 2020/2021. Fedha hizi zimeongezeka katika Fungu 38- Ngome. Kati ya fedha zilizoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo asilimia 18.45 ni kwa ajili ya Fungu 38 - Ngome; asilimia 2.27 ni kwa ajili ya Fungu 39 JKT na asilimia 79.24 ni kwa ajili ya Fungu 57 ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bunge lako Tufutu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga

Taifa kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yake kwa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati; kwa kuzingatia taarifa iliyotekelezwa na bajeti ya Wizara hii, na maoni yalitolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2020/2021 sambamba na majadiliano ya kina kuhusu bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 39 la JKT kwa mtitiriko uliopangwa. Hadi kufikia mwezi Februari, 2021 fungu hili lilikuwa halijapokea fedha zozote kwa ajili utekelezaji wa shughuli za maendeleo, aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 38 Ngome na Fungu 57 la Wizara ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Serikali itoe fedha zilizotengwa katika mwaka 2020/2021 kwa ajili ya ukarabati wa nyumba na makazi ya wanajeshi. Hadi kufikia mwezi Februari 2021 hakuna fedha zozote zilizotolewa kwa ajili ya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikamilishe na kuanza utekelezaji wa mpango wake wa miaka kumi 2021/2230 hadi 2031 wa kuimarisha Shirika na Nyumbu kuweza kukabiliana na changamoto ya uchakavu wa mitambo na teknolojia iliyopitwa na wakati, hii itawezesha shirika hilo kutekeleza shughuli zake za kimsingi kwa ufanisi zaidi na hivyo kuokoa fedha nyingi za Serikali. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 shirika liliokoa kiasi cha fedha shilingi bilioni 3.5 baada ya kutengeneza magari ya viwango vya manispaa kwa shilingi milioni 404.2 ambapo Serikali ingetakiwa kuyanunua hayo magari kwa shilingi bilioni 3.9. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe kuwa awamu ya pili ya huduma ya Bima za Afya Oktoba, 2021/ 2026 inatekelezwa kama ilivyopangwa kama ili kuwezesha wanajeshi kupata huduma za afya katika hospitali mbalimbali za Serikali hospitali binafsi, pamoja na mashirika ya kidini.

Serikali ikamilishe upatikanaji wa sera ya ulinzi ambayo Kamati imekuwa ikishauri kwa vipindi tofauti tofauti tangu Bunge la Tisa. Taarifa hiyo imewasilishwa mbele ya Kamati iliweka kuwa tayari maoni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yameshapokelewa na taratibu nyingine za kuwasilisha katika Baraza la Mawaziri zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iendelee kuimarisha miundombinu ya kiulinzi iliyopo katika mipaka yote ya nchi ikiwa ni pamoja na barabara, alama za mipaka na mengineyo. Pia Serikali iweke utaratibu wa kutoa fidia ya kulipa kodi ya pango katika maeneo ya wananchi ambayo yametwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara ya Mawasilisano Salama Jeshini kwa kufanya hivyo Serikali itamiliki maeneo hayo lakini pia itakuwa fedha nyingi ambazo zingeendelea kulipwa kama kodi ya pango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye tathmini ya mahitaji halisi ya nyumba za makazi kwa wanajeshi itakayojumuisha nyumba 3939 zilizobaki katika mradi wa nyumba 10,000 na kutenga bajeti ya utekelezaji wake ili kupunguza changamoto za nyumba na makazi kwa wanajeshi. Pamoja na nia njema ya Serikali ya kutafuta mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na makazi ya wanajeshi Kamati inashauri Serikali kuhakikisha masharti ya mikopo hiyo yanaruhusu Serikali kuchagua Mshauri Elekezi na Mkandarasi wa kujenga nyumba hizo ili kuhakikisha zinakuwa na viwango bora na vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya bajeti ya Shirika la Nyumbu na Mzinga kutoka shilingi bilioni 7.5 hadi bilioni tisa na shilingi bilioni 4 hadi bilioni 5.5 kwa mwaka 2021/2022. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha hizo kwa kadri inavyoidhinishwa na Bunge na kulingana ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kuwezesha tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ikamilishe mpango wake wa kuwapatia wahitimu wote wa kidato cha sita mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria, aidha, ili kufanikisha

mpango huo Serikali itenge na kutoa fedha kwa ajili ya kuongeza makambi na kuboresha miundombinu ya makambi yaliyopo. Serikali ikamilishe kwa haraka mpango wa kuwawezesha vijana wanaojitolea kwa ajili ya mafunzo ya JKT kupata mitaji kwa shirika, sekta binafsi na taasisi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii, aidha, kipee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni na ushaurikiano wao umewezesha kukamilisha kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge *(Hansard).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Elias Kwandikwa (Mbunge) kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Faraji Mnyepe pamoja na watendaji wote wa Wizara na kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai aliyekuwa Katibu wa Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kukumilisha kazi zake bila kukwama. Aidha, Kamati inampongeza Bibi Nenelwa Mwihambi aliyeteuliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama kuwa Katibu wa Bunge na kuapishwa rasmi tarehe 19 Mei, 2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ya Bunge Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhani Abdallah na Bibi Grace Bidya, akisaidiwa na Bibi Rehema Kimbe, kwa utaratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kuikubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (FUNGU 38, 39, 57) KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, awali ya yote nafahamu kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 175 (1) (2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Juni, 2020 [Kanuni za Bunge]inakataza kurejea kutoa salam za pole au pongezi baada ya wewe au Waziri Mkuu kufanya hivyo, lakini kutokana na Jukumu la Msingi la Kamati hii hususan kwa Wizara hii naomba uniwie radhi na uniruhusu kutoa salaam za Pole kwa kifo cha aliyekuwa Amiri Jeshi Mkuu Dk. John Pombe Joseph Magufuli, Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi – Ameen.

**Mheshimiwa Spika,** na kwa kuwa leo ni Siku ya kujadili Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati yangu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi alivyoanza vyema kwa kuchukua hatua mwafaka za kuendeleza mipango ya kuliwezesha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania pamoja na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama Nchini katika nyanja zote ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa. Kwa

hakika sote tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumzidishia hekima na busara katika kuliongoza vyema Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya salaam hizo za rambirambi na pongezi, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni 2020, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge. Kwa mujibu wa Kanuni hizo, kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT, kujadailiwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa Uchambuzi huo ulifanyika tarehe 28 Machi, 2021 baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117 (1) hadi 117 (2) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuweka bayana mawanda (scope) ya Taarifa hii, nitangulie kulikumbusha Bunge hili kuwa Wizara ya Ulinzi na JKT inajumuisha Mafungu Matatu (3) ya Kibajeti yafuatayo: -

i) Fungu 38- Ngome;
ii) Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa; na
iii) Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Wizara).

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu kuu nne (4) zifuatazo: -

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi namba 6103- *Defence Scheme* katika Mkoa wa Singida na Arusha. Maeneo yaliyotembelewa ni sehemu ya miradi inayotekelezwa na Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Taarifa hii inaeleza mambo makuu mawili:

a) Muhtasari wa maelezo ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021; na

b) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa Fedha ilizo ziidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

### 2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, Kama ilivyoelezwa awali, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa Mradi Na. 6103: *Defence Scheme* Mkoani Singida na Arusha. Miradi

iliyotembelewa na kukaguliwa inajumuisha Mradi wa Mawasiliano Salama Jeshini na Nyumba za Makazi ya Wanajeshi. Aidha, Kamati ilitembelea na kukagua masuala ya kiulinzi katika machimbo ya madini ya *Tanzanite*, Mererani Mkoani Manyara ambapo changamoto zilizobainika zilitolewa ushauri mahsusi.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo kuhusu maeneo yaliyokaguliwa ni kama ifuatavyo:-

**a) Mradi wa Mawasiliano Salama Jeshini, Ikungi-Singida**

Eneo la hili ni sehemu ya Mradi wa Mawasiliano salama Jeshini unaotekelezwa chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Fungu 57) tangu Mwaka 2009. Tangu kuanzishwa kwake, mradi huu umeendelea kuleta tija iliyokusudiwa.

**b) Nyumba 112 za Makazi katika Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Monduli, Arusha**

Ujenzi wa Nyumba 112 ulitekelezwa katika ya awamu ya kwanza ya Mradi wa Nyumba 10,000 za Makazi ya Wanajeshi uliojumuisha ujenzi wa nyumba 6,064 kwa gharama ya USD 300,000,000. Kati ya fedha hizo, USD 15,000,000 sawa na asilimia 5 ya fedha hizo zilitoka katika Bajeti ya Serikali na USD 285,000,000 sawa na asilimia 95, zilikuwa ni fedha za Mkopo wa masharti nafuu kutoka *Exim Bank* ya China. Mradi huu unatekelezwa chini ya Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na JKT.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hiyo, Kamati ilibaini mapungufu[1] katika nyumba hizo licha ya kuwa zimetumika kwa muda wa miaka minne tu tangu zilipokabidhiwa Mwaka 2016.

2.2 **Matokeo ya Ukaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya muhtasari wa miradi ya maendeleo iliyokaguliwa, sasa naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya uchambuzi wa miradi hiyo kwa kutaja yafuatayo:

---

[1] Nyufa, unyevu kwenye kuta na Misingi ya nyumba hizo kuachia.

i) Juhudi zinazofanywa na Serikali katika kujenga nyumba za makazi ya wanajeshi unapunguza changamoto ya makazi kwa wanajeshi na kuimarisha utaratibu wa kurejesha wanajeshi kwenye Makambi;

ii) Kutumia Wakandarasi wa ndani katika kutekeleza miradi hususan ya ujenzi wa nyumba za makazi ni suala linalotakiwa kupewa kipaumbele ili kuwa na uhakika wa ubora wa majengo unaohitajika;

iii) Wizara kutomiliki maeneo ya ardhi ambayo minara ya mawasiliano ya Jeshi imejengwa kunasababisha Serikali kuendelea kulipa kodi ya pango kwa kila mwezi jambo ambalo linasababisha Serikali kutumia pesa nyingi kwa ajili ya kulipa kodi hizo.

### 2.2.1 **Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati inamaoni yafuatayo:

i) Ili kufanikisha adhma ya Serikali ya kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa changamoto ya makazi kwa wanajeshi, utengaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya ukarabati na ujenzi wa makazi hayo, na upatikanaji wake kwa wakati ni jambo muhimu na linatakiwa kupewa uzito unaostahili;

ii) Upo umuhimu wa Serikali kubadilisha utaratibu wa kulipa kodi ya pango kwa kila mwezi kwa wananchi ambao maeneo yao yanatumiwa kwa ajili ya mradi wa mawasiliano salama Jeshini na badala yake kuwa na utaratibu wa kulipa fidia ili maeneo hayo yamilikiwe na Jeshi.

iii) Ni vema Serikali ikaendelea kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ya sekta hii kutokana na umuhimu wake.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, ulilenga kulinganisha Makusanyo ya Mapato na lengo la Makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za Matumizi Mengineyo na upatikanaji wa fedha za Maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kwa mafungu yote Matatu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Januari, 2021 na Machi, 2021 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo: -

#### 3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ilikadiria kukusanya Mapato ya jumla ya Shilingi **85,103,000.00** kwa Mafungu yote matatu (3). Makadirio haya yalikuwa ni ongezeko la asilimia 4.7% ikilinganishwa na Makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ya Shilingi **81,104,000.00.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa maelezo ya Wizara, hadi kufikia Mwezi Februari, 2021, kiasi kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa ni Shilingi **76,085,664.16** sawa na asilimia 89% ya lengo la Mwaka lililopangwa. Kamati ilibaini kuwa kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la asilimia 41.35% ikilinganishwa

na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ambayo yalikuwa Shilingi 53,826,000.00 sawa na asilimia 66 ya lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa Fungu 38- Ngome na fungu 39- JKT ndio yamechangia ongezeko hilo ambapo Fungu 38 (Ngome) limekusanya asilimia 155 ya lengo lililowekwa na Fungu 39 (JKT) limekusanya asilimia 68 ya makadirio yake.

Aidha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Fungu 57- Wizara halikukusanya fedha zozote kama ilivyokuwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Kamati ilihoji na kuelezwa kuwa sababu ya Wizara kutokukusanya maduhuli kumesababishwa na kufungwa kwa mgahawa ambao ulikuwa ndio chanzo cha mapato ya makusanyo hayo baada ya Watumishi waliokuwa wanapata huduma katika mgahawa huo kuhamia Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01 na Grafu Na. 01 hapa chini.

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Makadirio na Makusanyo ya Mapato**

| FUNGU | MAKADIRIO | % YA JUMLA YA LENGO | MAKUSANYO | % YA JUMLA YA MAKUSANYO | % YA LENGO LA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|---|---|
| 38- Ngome | 22,000,000.00 | 25.85 | 34,003,664.16 | 46.69 | 155 |
| 39- JKT | 61,903,000.00 | 72.74 | 42,082,000.00 | 55.31 | 68 |
| 57- Wizara | 1,200,000.00 | 1.41 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA** | **85,103,000.00** | **100.0** | **76,085,664.16** | **100.00** | **89** |

**Chanzo: Randama ya Wizara 2020/2021**


**Grafu Na. 1: Ulinganisho wa lengo na Makusanyo halisi ya Mapato**

**Chanzo: Randama ya Wizara 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, vile vile Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa Makusanyo yaliyopatikana kwa kila Fungu kufikia Mwezi februari 2021 na Makusanyo yaliyopatikana a 2020 kama -

**/2020 na**




**Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020 na 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kufanya Uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa: -

i) Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 25.85 lakini katika utekelezaji Fungu hilo limechangia kwa asilimia 155 ya kiasi kilichokusanywa.

ii) Makusanyo ya Fungu 39 –JKT yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 72.74, lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya JKT yamechangia kwa asimia 68.

iii) Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara, yalikusudiwa kuchangia kwa asilimia 1.41 kwenye mapato yote ya Wizara, lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 57 (Wizara) halikuweza kuchangia kutokana na sababu zilizoelezwa hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi halisi kilichokusanywa, umeisaidia kamati kubaini kuwa mwenendo huu wa makusanyo ni mzuri na Wizara inaweza kufikia lengo la Makusanyo ifikapo tarehe 30 Juni, 2021. Aidha, kamati inapongeza Serikali kwa kuweka makadirio kwa uhalisia ambapo hata Fungu 57- Wizara ambayo haikukusanya fedha yoyote, ilitarajiwa kukusanya asilimia 1.41 moja tu ya makadirio yaliyowekwa.

### 3.1.2 **Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2020/2021, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha Fedha kilichotolewa hadi kufikia Mwezi Februari, 2021.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa

kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/ 2021, Kamati ililinganisha uwiano wa Bajeti za Mafungu hayo na uwiano wa Fedha zilizopokelewa kwa Mafungu hayo . Ulinganisho huo unaonekanaka katika Jedwali Na. 02 na 03 hapa chini.

**Jedwali Na. 02: Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa miongoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**

| Fungu | Kiasi cha fedha zilizoidhinishwa | Asilimia ya fedha zilizoidhinishwa Kiuwiano | | Fungu | Kiasi cha fedha zilizotolewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa kiuwiano |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 38 | 1,617,164,984,000.00 | 75.53 | | 38 | 1,061,162,441,691.72 | 65.61 | 75.57 |
| 39 | 354,234,958,000.00 | 16.55 | | 39 | 245,463,546,058.00 | 69.29 | 17.48 |
| 57 | 169,634,547,000.00 | 7.92 | | 57 | 97,509,488,565.09 | 57.48 | 6.95 |
| | **2,141,034,489,000.00** | 100 | | | **1,404,135,476,314.81** | 65.58 | 100 |

Chanzo: **Randama ya Wizara 2020/2021**

**Jedwali Na. 03: Ulinganisho wa fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na zilizopokelewa miongoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57**

| Fungu | Kiasi cha fedha zilizoidhinishwa | Asilimia ya fedha zilizoidhinishwa kiuwiano | | Fungu | Kiasi cha fedha zilizotolewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa | Asilimia ya fedha zilizopokelewa Kiuwiano |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 38 | 10,000,000,000 | 6 | | 38 | 9,694,160,292.32 | 96.94 | 10.11 |
| 39 | 4,000,000,000 | 2 | | 39 | 0 | 0 | 0 |
| 57 | 150,000,000,000 | 92 | | 57 | 86,223,517,997.65 | 57.48 | 89.89 |
| | **164,000,000,000** | 100 | | | **95,917,678,289.97** | 58.4 | 100 |

Kupitia uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

i) Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu imepokea Shilingi **1,404,135,476,314.81** sawa na asilimia 65.58 ya fedha zilizoidhinishwa.

ii) Kati ya fedha zilizopokelewa Shilingi **1,308,217,798,025** sawa na asilimia 92.67 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **95,917,678,289.97** sawa na asilimia 7.33 ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

iii) Kati ya fedha zilizopokelewa, asilimia 76 ni kwa ajili ya Fungu 38 (Ngome), asilimia 17 ni kwa ajili ya Fungu 39 (JKT) na asilimia 7 ni kwa ajili ya Fungu 57 (Wizara)

iv) Kiasi kilichopokelewa na Wizara hii kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni pungufu ya asilimia 6.23 ikilinganishwa na Fedha zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2019/2020.

v) Kati ya Shilingi **95,917,678,289.97** zilizopokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, asilimia 89.89 ya Fedha hizo ni kwa ajili ya Fungu 57 (Wizara) na asilimia 10.11 ni kwa ajili ya Fungu 38 (Ngome). Aidha, Fungu 39 (JKT) halijapokea Fedha zozote za Miradi ya Maendeleo kati ya Shilingi **Bilioni 4** zilizoidhinishwa kwa ajili ya Fungu hilo.

vi) Fungu 38 (Ngome) limepokea Shilingi **9,694,160,292.32** sawa na asilimia 96.94 ya Shilingi **Bilioni 10** zilizoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo.

vii) Fungu 57 (Wizara) limepokea Shilingi **86,223,517,997.65** sawa na asilimia 57.48 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Fungu hilo.

viii) Katika Fedha zilizoidhinishwa kwa kila Fungu, Fungu 38 (Ngome) lilipokea asilimia 65.62, Fungu 39 (JKT) lilipokea asilimia 69.29 na Fungu 57- (Wizara) lilipokea asilimia 57.48.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huo unaonesha kuwa Serikali ilizingatia ipasavyo uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti. Kwa mfano, Bunge liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 (Ngome) ikiwa ni asilimia 75.53 ya Bajeti ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo ni asilimia 75.57 ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hadi kufikia mwezi Februari, 2021. Kwa

mwenendo huu, Kamati inaipongeza Serikali kutoa uzito stahiki kwa Bajeti ya Ngome, Jeshi la Kujenga Taifa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mwenendo huo mzuri, Kamati haijaridhishwa na mtiririko wa fedha za maendeleo kwa ajili ya Fungu 39 (JKT) ambapo hadi kufikia Mwezi Februari, 2021 Fungu hilo lilikuwa halijapokea fedha za maendeleo kati ya Shilingi **Bilioni 4** zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge.
Ni vema Serikali ikatoa fedha hizo za maendeleo kwa mujibu wa ratiba ya utekelezaji wa miradi iliyowekwa ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.

3.2 **Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ilishauri masuala saba (7) yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti hiyo kwa Mafungu yote matatu.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika masuala yaliyotolewa ushauri, masuala manne (4) yametekelezwa kikamilifu, masuala mawili (2) yanaendelea kutekelezwa, na suala moja (1) bado halijatekelezwa kikamilifu kutokana na changamoto za kibajeti. Masuala yaliyotolewa ushauri pamoja na utekelezaji wake yameambatishwa katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, miongoni mwa ushauri uliotekelezwa kikamilifu ni ule wa kuongeza ukomo wa Bajeti ambapo kwa mwaka ujao wa Fedha wa 2021/2022, Serikali imeongeza Bajeti ya Wizara hii kwa asilimia 10.17 ukilinganisha na bajeti ya Mwaka 2020/2021. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza ushauri huu na kuisisitiza kuendelea na utaratibu huu kwa bajeti za Wizara hii katika siku za usoni.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya ushauri unaoendelea kutekelezwa ni ule wa kuipatia Wizara hii fedha za ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa – Kikombo, Dodoma ambapo Serikali inaendelea kuipatia fedha Wizara hii kwa kuzingatia bajeti ya utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, suala ambalo halijatekelezwa kikamilifu ni ukarabati wa nyumba za makazi ya Wanajeshi. Maelezo yaliyotolewa na Serikali yalibainisha kuwa katika Mwaka wa fedha 2020/2021 hakuna fedha zozote zilizotolewa na Hazina kwa ajili hiyo. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuipatia Wizara fedha za kukabiliana na changamoto hii pamoja na kubuni utaratibu mzuri zaidi utakaowezesha kuboresha makazi hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kiujumla, katika utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Mwaka 2020/2021, Kamati inaipongeza Wizara kuwa, pamoja na Changamoto za kibajeti zilizojitokeza, imeendelea kutumia kiwango kilichotengwa kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na pongezi hizo, kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujatekelezwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

### 4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na Kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na Dira na Dhima ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu sita likiwemo la kuwapatia vijana wa kitanzania mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi na

kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa na kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi muhimu ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, majukumu yaliyopangwa yatawezesha ufikiaji wa malengo sita (6) ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa Fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia mpango kazi wake.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu (38, 39 na 57) inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 108,104,000.00** Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 21.28 ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Ongezeko hili linatarajiwa kuwa katika Fungu 38- Ngome ambapo lengo la makusanyo yake limeongezeka kwa asilimia 104.55.


| **Fungu** | **Makadirio** | | **Asilimia ya lengo la Wizara** |
|---|---|---|---|
| 38 - Ngome | Shilingi | 45,001,000.00 | 41.63 |
| 39 - JKT | Shilingi | 61,903,000.00 | 57.26 |
| 57 - Wizara | Shilingi | 1,200,000.00 | 1.11 |
| **JUMLA** | Shilingi | **108,104,000.0** | **100.00** |

[illegible] kuzingatia kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2021 Fungu 38- Ngome lilikuwa limeshakusanya asilimia 155 ya makadirio yaliyowekwa katika mwaka wa Fedha 2020/ 2021.Mchanganuo wa lengo hilo la Makusanyo na Sura ya mchanganuo wake inaonekana katika Jedwali Na. 04. Na Chati Na. 03 hapa chini: -

**Jedwali Na. 04: Mchanganuo wa Makadirio ya mapato**

**Chanzo: Randama ya Wizara 2021/2022**

**Chati Na. 3: Mchanganuo wa Makadirio ya Makusanyo 2021/ 2022**




**Chanzo: Randama ya Wizara 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

i) Lengo la makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara hii limeongezeka kwa asilimia 21.28 ikilinganishwa na lengo la Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha.

ii) Fungu 38 (Ngome) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha asilimia 41.63 ambapo Mwaka 2020/2021 lilitegemewa kwa asilimia 25.85.

iii) Fungu 39 (JKT) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha asilimia 57.26 ambapo Mwaka 2019/2020 lilitegemewa kwa asilimia 72.74.

iv) Fungu 57 (Wizara) linategemewa kwa makusanyo kwa kiasi cha asilimia 1.11 wakati Mwaka 2020/2021 lilitegemewa kwa asilimia 1.41. Hata hivyo, kiasi hicho cha Makadirio ya

Makusanyo kwa Fungu 57 kinalingana na Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia Maoni ya Kamati kuhusu lengo la ukusanyaji wa Mapato kwa kuzingatia uhalisia wa makusanyo yanayopatikana. Hata hivyo, kwa mara nyingine, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuwa uhalisia wa makusanyo kwa ajili ya Fungu 57 uangaliwe upya.

4.3 **Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa Mafungu yote matatu ni Shilingi **2,358,694,985,502.00.** Kati ya Fedha hizo, Shilingi **2,182,116,562,000.00** sawa na asilimia 92.5 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **176,578,423,502.00 sawa na asilimia 7.5** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mantiki ya Masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma (Items), Vifungu (Subvotes) na Mafungu (Votes) yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

a) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 imeongezeka kwa Shilingi **217,660,496,502.00** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021. Tofauti hiyo ni ongezeko la asilimia 9.23. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake wa mara kwa mara wa kuongeza kiwango cha Bajeti ya Wizara hii na vyombo vyake vyote inavyovisimamia.

b) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kimeongezeka kwa Shilingi **12,578,423,502.00** ambayo ni sawa na asilimia 7.12 ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2020/2021. Fedha hizi zimeongezeka katika Fungu 38- Ngome.

c) Kati ya Shilingi **176,578,423,502.00** zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo, asilimia 18.45 ni kwa ajili ya Fungu 38- Ngome, asilimia 2.27 ni kwa ajili ya Fungu 39- JKT na asilimia 79.28 ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa Mwaka ujao wa Fedha.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii na Maoni yaliyotolewa na Kamati yangu kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 sambamba na majadiliano ya kina kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 ikilinganishwa na Dhima ya Wizara ya kulinda Mamlaka, Maslahi na Mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati inatoa Maoni na Ushauri ufuatao: -

i) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 39- JKT kwa mtiririko uliopangwa. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021, Fungu hili lilikuwa halijapokea fedha zozote kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Maendeleo. Aidha, Serikali itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa kwa Fungu 38 (Ngome) na Fungu 57 (Wizara) ili kutoathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

ii) Serikali itoe fedha zote zilizotengwa katika mwaka 2020/ 2021 kwa ajili ya kukarabati nyumba za makazi ya wanajeshi. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021, hakuna fedha zozote zilizotolewa kwa ajili ya shughuli hiyo.

iii) Serikali ikamilishe na kuanza utekelezaji wa Mpango wake wa miaka kumi (2021/22-2030/31) wa kuliimarisha Shirika la NYUMBU kuweza kukabiliana na changamoto ya uchakavu wa mitambo na teknolojia iliyopitwa na wakati. Hii italiwezesha Shirika hilo kutekeleza shughuli zake za msingi kwa ufanisi zaidi na hivyo kuokoa fedha nyingi za Serikali.

Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Shirika liliokoa kiasi cha Shilingi Bilioni 3.5 baada ya kutengeneza magari ya Viwango vya Manispaa kwa Shilingi **Milioni 444.2** ambapo Serikali ingetakiwa kuyanunua ingetumia Shilingi **Bilioni 3.9**.

iv) Serikali ihakikishe kuwa Awamu ya Pili ya Huduma za Bima ya Afya (Oktoba 2021 hadi 2026) inatekelezwe kama ilivyopangwa ili kuwezesha Wanajeshi kupata huduma za afya katika Hospitali za Jeshi, Serikali, Hospitali Binafsi pamoja na Mashirika ya Dini.

v) Serikali ikamilishe upatikanaji wa Sera ya Ulinzi ambayo Kamati imekuwa ikishauri kwa vipindi tofauti tangu Bunge la Tisa. Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilieleza kuwa tayari maoni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yameshapokelewa na taratibu nyingine za kuwasilisha katika Baraza la Mawaziri zinaendelea.

vi) Serikali iendelee kuimarisha miundombinu ya kiulinzi iliyopo katika mipaka yote ya Nchi ikiwa ni pamoja na barabara, alama za mipaka na mengineyo.

vii) Serikali iweke utaratibu wa kutoa fidia badala ya kulipa kodi ya pango katika maeneo ya Wananchi ambayo yametwaliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara ya mawasiliano salama Jeshini. Kwa kufanya hivyo Serikali itamiliki maeneo hayo lakini pia itaokoa fedha nyingi ambazo zingeendelea kulipwa kama kodi ya pango.

viii) Serikali ifanye tathmini ya mahitaji halisi ya nyumba za makazi kwa Wanajeshi itakayojumuisha nyumba 3,936 zilizobaki katika mradi wa Nyumba 10,000 na kutenga bajeti ya utekelezaji wake ili kupunguza changamoto ya nyumba za makazi kwa Wanajeshi.

ix) Pamoja na nia njema ya Serikali ya kutafuta mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi ya wanajeshi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha masharti ya mikopo hiyo yanaruhusu Serikali kuchagua Mshauri elekezi na Mkandarasi wa kujenga nyumba hizo ili kuhakikisha zinakuwa na viwango vya ubora unaotakiwa.

x) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza makadirio ya Bajeti ya Mashirika ya NYUMBU na MZINGA kutoka Shilingi Bilioni 7.5 hadi bilioni 9 na Shilighi Bilioni 4 hadi Bilioni 5.5 mtawalia kwa Mwaka 2021/2022. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha hizo kwa kadri zitakavyoidhinishwa na Bunge na kulingana na ratiba ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa ili kuwezesha tija inayokusudiwa.

xi) Serikali ikamilishe Mpango wake wa kuwapatia wahitimu wote wa kidato cha Sita mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria. Aidha, ili kufanikisha mpango huo, Serikali itenge na kutoa fedha kwa ajili ya kuongeza Makambi na kuboresha miundombinu ya Makambi yaliyopo.

xii) Serikali ikamilishe kwa haraka Mpango wa kuwawezesha vijana wanaojitolea kwa ajili ya mafunzo ya JKT kupata mitaji kwa kushirikisha Sekta na Taasisi nyingine. Wakati wa majadiliano na Wizara hii Kamati ilielezwa kuwa Utekelezaji wa Mpango huu unasimamiwa na Wizara ya Ulinzi na JKT kwa kushirikisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kazi na Ajira, Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

## 6.0 **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard): -

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb - **Mwenyekiti**

2. Mhe. Vicent Paul Mbogo, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb- Mjumbe
5. Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Bonnah Ladislaus Kamoli, Mb- Mjumbe
7. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani - Mjumbe
8. Mhe. Janeth Maurice Masaburi - Mjumbe
9. Mhe. Cosato David Chumi, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb- Mjumbe
12. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb- Mjumbe
13. Mhe. Alexander Pastory Mnyeti, Mb- Mjumbe
14. Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb- Mjumbe
15. Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Muharami Shabani Mkenge- Mjumbe
17. Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa- Mjumbe
18. Mhe. Ali Juma Mohammed, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb- Mjumbe
22. Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi, Mb- Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Elias Kwandikwa (Mb) kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Faraji Mnyepe pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, napenda kumshukuru Ndg. Stephen Kagaigai aliyekuwa Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi zake bila kukwama. Aidha, nampongeza Bi. Nenelwa Mwihambi aliyeteuliwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kuwa Katibu wa Bunge na kuapishwa rasmi tarehe 19 Mei, 2021.

Nawashukuru pia Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husssein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald

Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mussa Azzan Zungu**, Mb**
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**
Mei, 2021

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Vicent Paul Mbogo, Makamu Mwenyekiti wa hii Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mkisia makofi mengi ni kwamba Wenyeviti wanafanya kazi nzuri ya kulea Makamu Wenyeviti wa Kamati. Mheshimiwa Zungu ndiye Mwenyekiti wa hii Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa majina hapa na utaratibu wetu sasa tutaanza uchangiaji, tutaanza na Mheshimiwa Charles Mwijage atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Esther Nicolaus Matiko ajiandae.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia bajeti hii muhimu, neno muhimu linaweza kuonekana la kawaida, lakini hii ni muhimu kwa maana ni muhimu. Unapoona mtu unalala, unaamka unatembea, una amani na utilivu, una usalama ina maana kuna watu wanaumia kwa niaba yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mukhtadha huo nishukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali ina maana Amiri Jeshi Mkuu, Mkuu wa Majeshi Makamanda na Wapiganaji wote, kazi yenu ni nzuri sana na Mwenyezi Mungu atawalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ulivyohitimisha wakati Mjumbe wa Kamati anamaliza kusoma taarifa, mimi naungana kabisa na mapendekezo yote ya Kamati hiyo ya Ulinzi ingawa mimi sio Mjumbe. Nimeisoma na nimewasikiliza nawaunga mkono. Sasa na mimi nichangie kwenye bajeti hii kwa kusisitiza mambo mahususi yanayohusu Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma yale malengo sita ya Wizara ndio utajua uzuri wa Wizara hii, nimechagua mawili katika sita. Moja ni kujenga uwezo katika tafiti mbalimbali na uhaulishaji wa teknolojia kwa matumizi ya kijeshi na kiraia, nachukua ile ya kiraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyosema Kamati kitengo chetu cha Nyumbu kilichoasisiwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kinafanya mambo makubwa, huyu naye ni ng'ombe wa maziwa sioni kwa nini Serikali tunasita kutoa pesa za kutosha kusudi Nyumbu aweze kufanya maajabu. Nimewahi kukaa nao mara nyingi na mimi nilikwenda Jeshini sio wiki mbili mwaka mzima na kwa wale wanajeshi mimi nilifundishwa na Kanali Mtono alikuwa ni *commando failure* yaani alikwenda kwenye kozi ya ukomando akashindwa, akaja kunifundisha mimi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo jeshi nalijua kwa hiyo Nyumbu ukiangalia mfumo wa Nyumbu na vitu wanavyotengeneza katika hizi zama za uchumi wa viwanda kama hawa watu wakiwezeshwa, matatizo mengi yanayotusumbua yasingeweza kuwepo. Kamati imezungumza vizuri siwezi kuzungumza zaidi naiyomba na kuishauri Serikali yetu iweze kutekeleza mapendekezo ya Nyumbu.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mwijage, babu yangu kwamba hata humu ndani kuna wanajeshi wa akiba mmojawapo ni mimi ambaye nilikuwa kikosi cha JKT Ruvu na akina Mheshimiwa Halima Mdee, kina Silinde, kina Lusinde na wengine nilikuwa nakupa hiyo taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwijage unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, amesema yeye ni mjukuu sasa babu usipokubali taarifa ya mjukuu usipochemshiwa maji itakuwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni moja ya malengo sita ya Wizara kutengeneza jeshi la akiba ndio hilo jeshi la akiba. Kwa hiyo ninachozungumizia mimi hoja iko kwenye Nyumbu, tuna-*under utilize* uwezo wa Nyumbu nizungumze mimi Nyumba naiona mbali ya kuwa ile teknolojia waliyonayo nyumbu kinapaswa kiwe chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ijipange, Wizara ya Elimu, mjipange na Nyumbu mnaweza kuchukuwa wahandisi wetu kutoka kwenye vyuo baada ya kumaliza, badala ya kukuaa mtaani wanatembea na mabahasha wakaenda kuwa *attached* Nyumbu, wale watu wamakaniko watu wa *IT* wakafanya *practice,* watawapikia, watakula, watashiba, unapotoka pale unakuwa na *competence* iko Nyumbu yako mambo makubwa. Niwashauri Waheshimiwa Waziri wanaohusika na sekta hizo basi na waende wakajifunze Nyumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapoiacha Nyumbu nizungumzie JKT na ninaizungumza kwa upole mkubwa, naishauri Wizara naishauri Serikali tuwe na mtazamo wa JKT, mtazamo ulio mpya. Tuwapeleke vijana wetu JKT awali na mwanzo, tuwaambie wanakwenda kufanya nini. Tanzania inahitaji bidhaa nyingi mojawapo ya bidhaa iliyoko JKT unayoweza kuiendesha JKT ni wana michezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kijana anaweza kukimbia, anaweza kupiga ngumi, anaweza kucheza mpira, mpeleke JKT kama nilivyoshauri mwanzoni akafundishwa hesabu na jiografia na Kiingereza acheze mpira asubuhi na jioni basi akisha fika kule siku za mwendo asiende JKT asiende JKT timu ya JKT ajiunge na kablu kubwa kama Simba aende Barcelona na Manchester. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo twende *specifically* tukiwatumia hawa watu tatizo wasiende JKT wakidhani wanataka kwenda Jeshi la Wananchi, hapana, aende kwa mfano mtu anakwenda kujifunza kilimo na nichukuwe fursa hii kuwapongeza Jeshi la Kujenga Taifa, nimeona mashamba yao ya *irrigation* kule Morogoro, ni mashamba yanaonesha yana tija kubwa. Basi hata tunapohangaikia kutafuta pesa JKT sehemu zake ziwe sehemu za vitengo vya biashara, sio kama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna rafiki mmoja yuko JKT sitamtaja nilimwambia unapojenga kiwanda JKT usijenge kiwanda cha maji, ningependa kuona majeshi yetu yanawekeza kwenye viwanda vikubwa kama wangekwenda Mchuchuma na Liganga kama wanaweza waende, lakini Jeshi letu nisingependa kuona Jeshi la Wananchi eti wana kiwanda cha maji; kiwanda cha maji mtu yeyote anaweza kutengeneza. Basi vijana wako watakaokwenda jeshini watengeneza viwanda vya maji kusudi uwape jeshi libaki kwenye *co-activities* ambazo ni *very sensitive.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini TAMISEMI niwaeleze tunazo pesa tunazowapa vijana kila mwezi kutokana na Halmashauri, unaweza kupeleke vijana kutoka kwenye

Halmashauri wakaenda JKT, wakajifunza kazi mahususi, siku ya kuhitimu, siku ya *graduation* basi ile Halmashauri ilete vifaa ambavyo mfanyakazi huyo vijana atakwenda kutumia na impe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani mtu anapata mafunzo mahususi anapotoka anakwenda moja kwa moja kazini kwa mfano, sifa ziwaendee tumewaona vijana wanafanya kazi nzuri ya ujenzi, sasa siku ya kumaliza miaka mitatu au sita huyo kijana apewe vifaa na si vifaa tu, apewe na hati kwamba yeye ni mkandarasi daraja la saba au daraja la kumi aende moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwa sababu ndio wenye miradi kupitia Wizara mbalimbali Ujenzi, Afya tunaweza kuwapa makandarasi vijana ikiwepo sifa ya kwamba ulipitia JKT. Ndio maana ya lengo lenu moja kuwajengea uzalendo unatangaza *tender* unasema tutakupa wewe mkandarasi sifa mojawapo uwe wewe mwenye kampuni ulikwenda JKT, hapo uje uone vijana watakavyokwenda JKT wao kwa upenzi wao wakitegemewa kuandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuzungumzia suala moja muhimu; Mheshimiwa Waziri katika kambi ya Kaboya walikolala mashujaa waliopigana vita ya Uganda, kando yao kuna wananchi waliopisha eneo kwa ajili ya jeshi lile wanalalamika na kwa mila za kikwetu ukiwa una marehemu wanalalamika na majirani wanalalamika mambo hayawezi kutuendea vizuri. Nikuombe kabla hatujaenda kufagia makaburi Kaboya, wale wananchi ambao tulichukua ardhi yao kwa sababu nzuri za kiusalama tutafute pesa mimi na wewe tusaidiwe twende tukawafidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale waliolala kwenye makaburi wanalalamika acha wananchi wenyewe, waliolala kwenye makaburi wanalalamika kwa sababu wenye ardhi zile wanalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, Mheshimiwa Kwandikwa, usinitupe twende tukafagie

makaburi, lakini huwezi kufagia makaburi kama hujalipa fidia ya wale uliowahamisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nasikiliza kwa makini namna ambavyo Mheshimiwa Mwaijage anautaalamu wa kuwasikia wale walioko makaburini wakiwa wanalalamika. Mheshimiwa Joseph Mkusukuma Kasheku atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicolaus Matiko, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis ajiandae.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri, lakini pili naipongeza Kamati kwa ushauri na mapendekezo yake mazuri; naunga mkona hoja zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwanza kwa kumteua Mkuu mpya wa SUMA JKT, sisi tuliokuwa kwenye Kamati ya Nishani na Madini mwaka jana tumeona kazi nyingi sana alizozisimamia na nina imani kwamba baada sasa ya kupewa rungu mambo yatakuwa mazuri zaidi, Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa napenda kushauri kuhusiana na suala la mfumo, mimi nitazungumzia sana kwenye JKT. Mfumo wa JKT kwa mzamo wangu mimi nikitizama JKT natazama kama uchumi mkubwa sana kwenye Taifa letu, lakini ukiangalia jinsi SUMA JKT inavyochagua vijana wa kwenda kujiunga na JKT inaweka vigezo vya elimu tena ina *division* na *point* na wanapoenda kule wanasoma wengine mpaka miaka mitatu wakiwa na malengo haya haya kwamba nitaenda jeshini na kule jeshini wanajua wanavyochagua baadhi ya watu wachache wanaenda, hao wengine wote wanarudi nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa shida inakuwa moja, sisi Wabunge humu wengi ikifika kipindi cha vijana wanahitajiwa JKT karibu kila Mbunge ana *message* za wazazi

wanaomba watoto wao waingie kule, lakini wakimaliza tena wakirudi nyumbani, shida inakuwa tena kwa Mbunge yule yule tusaidie kupata ajira.

Sasa mimi ushauri wangu, nilikuwa napenda kushauri kwamba kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana JKT, lakini wangeondoa masharti ya elimu, wakachua vijana wote wenye uwezo kwa sababu ninavyoitazama JKT ni kama sehemu ya kwenda kufundishwa maisha halisi ambayo tunaweza kuyafanya hata sisi ambao hatukupata elimu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtu anaenda kufundishwa uselemala, anaenda kufundishwa kulima, anaenda kufundishwa kazi za kila siku, mimi najiuliza kama wanapanda watu cheo kwa kusimamia kazi za ujenzi, inakuwaje mtu unafundishwa JKT, unakaa miaka mitatu, unarudi tena na kusubiri kuajiriwa kwa shilingi 120,000, tunawafundisha vitu gani kule yani kama mgechukua watu wa darasa la saba ambaye anajuwa mimi nikitoka huku na taaluma yangu ya ujenzi, nikitoka shuleni ni kwenda kuomba kibarua nilipwe shilingi 20,000 kwa siku ambayo nitapata shilingi 360,000.

Kwa hiyo mimi nilikuwa nadhani, tunatengeneza bomu kubwa sana na ndio maana tunaanza kuona vijana wanaandamana, wanakiukwa masharti ya kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niombe tu kwamba muone namna wenzetu wa JKT muondoe lile sharti la elimu, mchague vijana kwa uwezo na watu ambao watawaelewa na ninyi muonekane mnafundisha watu, wanaporudi huku wawe na kazi zao za kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Waziri, lakini pia nipongeze na Jeshi. Niliwahi kuchangia hapa nikazungumza suala la Mererani kwamba kulikuwa na upekuaji ambao haukuwa mzuri, lakini nikupongeze sana Waziri na Jeshi kwa sababu ule upekuaji tena hakuna. Umerudi upekuaji wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii ndiyo maana kila siku mimi nasema nidhamu ya Jeshi ni kubwa sana na ninadhani kuna watu walituelewa vibaya, lakini nadhani ninyi mlivyokwenda kuchunguza mliona hiki kitu kinafaa na sasa mmeondoa na mnakagua vizuri na watu hawana kelele tena na kudhalilisha Jeshi letu ambalo sisi tunaliheshimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, nilitoa mapendekezo; mimi nashughulika na mambo ya madini, kwenye taaluma ya *assessment* ile wanayofanya pale niliomba, mimi naamini sana Jeshi, hebu chukueni vijana 100 muwapeleke wakasome, hawamalizi miezi sita, warudi wapewe hizo nafasi. Hawa waliopo bado tunapigwa na wanajeshi wako pale pale. Kwa hiyo, nilitoa ushauri, kama utaufanyia kazi nadhani baadaye utakuja kuona mafanikio kwa sababu mimi binafsi nina imani kubwa sana na Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa ushauri na ninatoa ushauri kwa upole sana. Mimi kama ninavyosema, naliheshimu sana Jeshi la Wananchi, lakini sijui ni kwa nini wanajeshi wetu tumewaweka kama tumewasahau kidogo kwenye suala la makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Serikali inajitahidi kujenga, lakini mkarabati na za zamani. Hebu jaribuni kupita tu, mimi nachukua mfano mmoja, pengine wenzetu hawa wanajeshi hawana watu wa kuwasemea humu ndani, ukipita Mwenge pale unamuona mwanajeshi ametoka amevaa *smart,* anang'aa, angalia nyumba anayotoka. Nenda Mwanza, nenda kila sehemu, jamani hata kukarabati tu kupiga rangi kweli Mheshimiwa Waziri? Hata wewe mwenyewe ungeishi hiyo nyumba halafu unatoka nje unaendesha *V8!* Hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Jeshi letu linasifika Kimataifa, hata Wachina, Wazungu, wakija waone mwanajeshi anatoka kwenye nyumba nzuri. Tuna maghorofa, tuna majengo mazuri, kupaka tu rangi? Mheshimiwa Waziri, mimi kwenye shilingi kuhusiana na uchafu kwa kweli kwanza

mimi niko jirani nao pale Mwenge, sitakubaliana nalo kabisa kama hutokuja na maelezo mazuri. Ninapenda uje na maelezo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niliona nichangie tu hayo kwa ufupi kwa sababu Jeshi letu linafanya kazi nzuri na mimi nalipenda. Nilitaka nimshauri Waziri kwa hayo machache, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, kuna kelele fulani hivi inasikika, kila mtu aangalie *microphone* yake ili zote ziwe hazina cha kuzungumza.

Lakini nilishapata kuzungumza kuhusu elimu ya darasa la saba namna tunavyoizungumzia humu ndani. Sina hakika na shule ambazo Serikali imejitahidi kila kata ipate shule ya sekondari na sisi Wabunge kila siku tunauliza maswali kwa zile kata ambazo hazina shule za sekondari. Watoto wetu tunatamani wasome na sisi Wabunge lazima tutume ujumbe wa namna hiyo. *(Makofi)*

Tukitaka kuonesha kana kwamba mtoto akikomea mahali fulani ni sawa, hao ni wachache sana. Ni wachache sana ambao wanaweza kukomea mahali halafu mambo yakaenda vizuri. Tusisitize watoto wetu wasome. *(Makofi)*

Hoja yake Mheshimiwa Waziri atakuja kujibu, lakini nimeona niiweke hivyo vizuri kwa sababu kuna muda tunatuma ujumbe huko nje halafu watoto wetu wenyewe wanaanza kutuambia sasa mbona mnataka tusome tena, Bungeni mmesema darasa la saba ndio wanaofanya vizuri, ndio wanaofanikiwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuwe tunatuma ujumbe mzuri huko kwa sababu sisi Wabunge wenyewe tunaonesha mfano mzuri, watoto wetu wanasoma, wako shuleni. Na wale tunaowawakilisha humu ndani pia tunatamani wapeleke watoto wao shule na sheria zetu tulizozitunga humu ndani ziko wazi kabisa na ndiyo maana tunazungumza sana kuhusu

mtoto wa kike asikatizwe masomo. Kwa nini; kwa sababu tunajua lile darasa atakaloishia halimtoshi. Kwa hiyo, ujumbe uwe unakwenda vizuri; tunatamani watoto wetu wasome kwa ngazi yoyote watakayofika lakini wasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, atafuatiwa na Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipatia fursa hii na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza kwanza kwa kupitia utekelezaji wa bajeti ambayo tunatenga kwenye Wizara hii muhimu. Pamoja na unyeti na umuhimu wa Wizara hii kwa miaka yote tumekuwa tukitenga bajeti lakini haziendi kwa ukamilifu. Kwa mfano mwaka 2015/2016, Fungu 57 – Wizara ilitengewa shilingi bilioni 220 fedha ya maendeleo, lakini ilipokea shilingi bilioni 40 tu, sawa na asilimia 18; Fungu 38 – Ngome, tulitenga na kuidhinisha shilingi bilioni nane, hawakupokea chochote; Fungu 39 – JKT, tulitenga shilingi bilioni nne, hawakupokea chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016/2017 zilitengwa shilingi bilioni 230 Fungu – 57 wakapokea shilingi bilioni 34 tu, sawasawa na asilimia 15; Fungu 38 tulitenga shilingi bilioni 10 wakapokea bilioni moja tu, sawa na asilimia kumi, za maendeleo hizi. Fungu 39 tulitenga bilioni nane wakapokea bilioni moja, sawa na asilimia 12.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, 2019/2020 tulitenga shilingi bilioni 220 Fungu 57, shilingi bilioni nane Fungu 38 na shilingi bilioni sita Fungu 39. Lakini mpaka ile Machi hawakutoa taarifa yoyote kwenye hili. Lakini tumeona 2021/2022 utekelezaji wake nao unasuasua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni fedha za maendeleo, na kwa nini nimeamua kufanya hii rejea; kwanza hata fedha

ambazo tunapeleka ni ndogo sana. Ametoka kuchangia hapa Mheshimiwa Mwijage, Jeshi la Wananchi wa Tanzania na JKT kwa unyeti wake Jeshi la Wananchi wa Tanzania kulinda mipaka ya nchi dhidi ya adui kutoka nje, lakini pia Jeshi hili ni mbadala kwa nchi yetu pale ambapo inapata mkwamo kwenye sekta zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inatakiwa Jeshi hili tuliwezeshe liweze kufanya tafiti za kina, liweze hata kufanya ugunduzi wa mambo mbalimbali, mengine ambayo hatuhitaji kuyajua ambayo yanaweza yakaisaidia nchi yetu kukwamuka kiuchumi. Lakini kwa fedha ambazo tunatenga ndogo na hatupeleki hatuwezi kufika popote.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii hili Jeshi haliwezi hata kujenga maabara ya kisasa yenye teknolojia za kisasa za kuweza kufanya huu utafiti na kuweza kujihakikishia kwamba kama nchi wanaweza ku-*counter any crisis* ambayo inakuwa imetokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalani, dunia na sisi nchi tuko kwenye hili gonjwa la *Covid-19.* Kama kweli hili Jeshi tungekuwa tunaliwekeza, ndiyo maana hawa ndugu zetu wako pale kulinda mipaka ya nchi na vitu kama hivyo, yaani hawatumiki 24/7 kama ambavyo majeshi mengine yanafanya, lakini wangeweza kujiwekeza kwa kina kuweza hata kufanya tafiti za kina, wana madaktari wakaweza kugundua dawa ya *Covid,* wakaweza hata kugundua chanjo tukaachana na ma-*debate* ya kusema nchi za nje zinaleta chanjo ambazo zinaweza zikatuathiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikitokea Jeshi wakabobea kwenye sekta zote, mathalani siombei, unatokea mgomo wa madaktari nchi nzima, hawa wanajeshi wetu wanaweza waka-*counter* kuweza kuhakikisha kwamba Watanzania hawawezi kufariki pale ambapo wanaendelea kupata matibabu pale ambapo unatokea mgomo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine tunaona nchi kama Marekani, wanajeshi wale na nchi nyingine; mimi kuna

kipindi nilikuwa nanunua *blackberry* wameandika *research in motion.* Zile ni tafiti ambazo zinafanyika na wanajeshi wa Kimarekani. Lakini pia kuna wanajeshi wa nchi mbalimbali, Mheshimiwa Mwijage hapa amelalamika kuhusu Nyumbu, sasa Nyumbu itawezaje kujikwamua wakati hata haipelekewi fedha za kutosha? Tunahitaji ku-*invest* kwenye Jeshi la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo kwenye utekelezaji hafifu wa fedha za maendeleo, kunasababisha kuendelea kuwepo kwa migogoro ya ardhi baina ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wananchi ambao wamechukuliwa ardhi ile. Imechukua miaka mingi sana, ni kwa sababu tunapitisha fedha hapa, kwenye vitabu ina-*reflect* kwamba wanakwenda kupeleka kulipa fidia, lakini miaka inakwenda wananchi hawalipwi fidia na tunajua ndugu zetu hawa wanajeshi, hawatakiwi mtu kukatiza kwenye kambi yao, ukikatiza unapewa adhabu kali sana, utalimishwa, utarukishwa kichura na vingine, ndiyo hivyo *caliber* ilivyo. Sasa unakuta wakati mwingine wamechukua maeneo ambayo yako kwenye maeneo ya raia ambako watakuwa wanapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mgogoro ulioko Tarime wa Jeshi la Wananchi pamoja na wananchi wa Kenyambi na Bugosi wa Kata za Nkende na Nyamisangura, tumekuwa tukiongea hapa, wanajeshi walikuwa kwenye kambi yao Nyandoto lakini kuna kipindi yalitokea mafuriko wakakaribishwa huku ni kweli, kwa sababu walikuwa hawawezi kupita kipindi hicho hakukuwa na miundombinu, walivyokuja huku wakaamua kuchukua ile ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Bunge la Kumi, mwaka 2010, nazungumzia hili suala; pale walipo ile kambi iko katikati ya mji kabisa. Kwa hiyo raia wakipita, kuna wengine wanapita wanakwenda Kata za Bumera au Susuni, kuna wakati wakikatiza pale raia wanachukuliwa wanapewa adhabu za kulima kwa sababu wamekatiza kwenye kambi. Tukasema basi kama wameamua kutwaa ile kambi wawalipe

fidia stahiki hawa wananchi kwa wakati; ni zaidi ya miaka 17 sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka jana na mwaka juzi Serikali ilipitisha hapa ikasema inapeleka fidia, tayari wameshatenga fedha, nikshika mpaka na shilingi, ambaye sasa hivi ni Makamu wa Rais ikawa imeshapita wakasema wame-*underestimate,* wakaenda wakafanya *re-evaluation* ili watu wale walipwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini leo nimejaribu kupitia, Tarime haipo tena. Ina maana hawa wananchi wataendelea kuteseka, kukaa wamezuiliwa wasikate mti, choo kikibomoka wasijenge, hawafanyi maendeleo yoyote yale wapo tu kwenye kakiota, nyumba ikibomoka wasifanye chochote. *This is not right! This isn't right!*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mmeamua kutwaa hata kwa mujibu wa sheria na kanuni za ardhi kama Jeshi limeamua kuchukua, *which we respect,* basi lipeni fidia. *Short of that,* Wanajeshi wale warudi kwenye kambi yao kule Nyandoto, *after all* iko mbali na mji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu nyingine ni kuhusu wastaafu wetu wanaotokana na Jeshi hili la Wananchi. Tumekuwa tukishuhudia wakishastaafu wanaishi maisha ya shida sana. Kwa sababu hata hiyo *lump sum* wanayopewa ya asilimia 25 kuna kipindi wanacheleweshewa wengine hawapewi kabisa, lakini hata wakiipata haikidhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakubali wote kwamba Jeshi hili ni letu, kama vile ambavyo tunawatambua kada zingine kama Majaji na wengine, wakistaafu wanakuwa wanapata *some percent,* basi tuangalie hawa wanajeshi wetu wanapostaafu tuwape hata walau asilimia 20 ya mshahara wao wa mwanzo ili waendelee kujikimu na maisha wakiwa uraiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizingatia wanajeshi wakiwa kule kambini huwa wanapata vifaa vingi kwa ruzuku. Wameshazoea maisha hayo, wakija huku uraiani wanateseka sana. Lakini *on top of that* tuwakatie na bima ambayo anaweza akatibiwa muda wowote ule. Mwanajeshi akistaafu *any time* kuna *crisis* wanaweza wakawa-*recall* wakaingia pia kuendelea katika kunusuru nchi. Kwa hiyo, lazima tuwa-*consider* hata walau kwa asilimia 20, siyo asilimia 80 au 70 wanazopewa hao wengine, walau asilimia 20 ya mshahara ambao alikuwa akiupata wakati anastaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya *CAG* ya mwezi Machi, 2021, ameainisha kwamba SUMA JKT kuna watumishi wanadai fedha, tena Idara ya Ulinzi. Mwaka 2018/2019 walikuwa wanadai milioni 208, mwaka 2019/2020 wakawa wanadai milioni 317, hela inazidi kuongezeka. Sasa kama Idara ya Ulinzi ambayo SUMA JKT wanapeleka kwenye *private sector* na hata kwenye mashirika ya umma, ina maana kule wanawalipa vizuri, kwa nini hawa watumishi ambao wanakwenda kufanya kazi ya ulinzi wasilipwe fedha zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani mimi nafanya kazi ya ulinzi unapokea fedha, lakini hunilipi. Unaweza hata ukashawishika ukajiingiza kwenye uhalifu, badala ya kulinda ukala njama ili uweze kuja kufanya uhalifu kwenye sehemu husika. Kwa hiyo, tunaomba mhakikishe msiwakope watumishi, hasa Idara ya Ulinzi jamani, kuwa kwenye lindo *and then* unamkopa, *isn't right. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine wamezungumza kwa kina hapa, ni kweli tunapeleka vijana wetu JKT, wanapewa mafunzo, lakini hawawezi kuwa *absorbed* wote kubaki kuajiriwa Jeshini, wa JKT na JKU. Sasa wasipochukuliwa wote Jeshini wengine wanarudi uraiani na unakuta wengine hawajapata mafunzo mbadala, hawezi akastahimili kukaa uraiani hana kazi, atashawishika. Ataingia kwenye magenge ambayo ni ya uhalifu na anajua, amejifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wametoa ushauri mkubwa sana hapa, na mimi na-*cement;* Jeshi la Kujenga

Taifa likiwezesha Tanzania ya viwanda ikawezekanika, tukipeleka fedha za kutosha tutaweza kuwa na kilimo chenye tija. Maana yake vijana wetu wakienda kule watajifunza, watawezeshwa, wakiwezeshwa ina maana tutakuwa na kilimo chenye tija, tutatoa *raw material* yataenda kwenye viwanda, viwanda vitakuwa vingi kwenye majimbo na mikoa; niliona siku ile Mheshimiwa Jafo anasema viwanda mia kila mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwezeshe JKT isiishie tu kufanya mashamba machache, mimi naita mashamba darasa. Kukiwa na maonesho ya Nanenane wanakuja wametengeneza kweli *furniture* nzuri lakini wana viwanda *all over the country,* tumewawezesha hawa watu waweze kujenga nchi yetu kweli?

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nirudie tena, ukishasema taarifa mara moja unasimama. Ndiyo maana huwa naangalia mtu kasimama wapi. Mheshimiwa Mpembenwe.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba *point* anazoziongea ni za msingi na zina maana sana za kusema kwamba tuweze kuwawezesha JKT na Jeshi kwa ujumla wake, lakini nataka tu nimpe taarifa mzungumzaji kwamba mfumo wetu wa bajeti ni *cash budget system,* tunakusanya halafu ndiyo tunatumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninamuomba tu mzungumzaji mimi na yeye na Wabunge wenzangu wengine wote humu ndani tuweze kushirikiana tuwe mabalozi wa kuweza kuhamasisha watu waweze kulipa kodi tukusanye ili Jeshi liweze kuwezeshwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *cash budget with priorities,* kama tunaweza tuka-*inject trillions of money* kwenye Wizara ya Ujenzi tunashindwa nini kupeleka *trillions of money* kwenye hii Wizara ambayo tunaiita nyeti? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni *cash budgeting, yes,* lakini tunatenga shilingi bilioni 220 na haziendi zinakwenda shilingi bilioni 30 wakati kwingine unakuta bajeti imeenda zaidi ya asilimia 100. Kwa hiyo *we need to be serious* na tusaidiande kama Wabunge, tukitenga shilingi bilioni 300 na ziende zote katika *cash budgeting* hiyo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ninapenda kusahuri; tunasema ni Jeshi la Wananchi, sasa kama Jeshi la Wananchi liko pale kulinda mipaka ya nchi yetu ndhidi ya adui, lakini kama nilivyosema mwanzo, hii ya kuteua wanajeshi wetu wanakuja kwenye kupewa fursa au kuteuliwa kuwa watendaji Serikalini au Wakuu wa Mikoa, *isn't right. Civilian Government* yaani utawala wa kiraia unamuingiza tena mwanajeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na huku sisi wengine tumeshazoea, ukimuona mwanajeshi kwanza *you freeze,* yaani nikiona *DC* mwanajeshi na wanavaa yale mavazi wakiwa kwenye hizi nafasi. Mimi ninashauri sana tuangalie wananjeshi tunawatumia, sijui nieleze vipi! Sasa ukishamuingiza mwanajeshi kwenye *system* Serikalini, tena wengine, kwa sababu *DC* na *RC* ni siasa, *it's a political thing.* Yaani ukimuingiza kwenye siasa, *it isn't right.*

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Charles Mwijage.

**TAARIFA**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili la kutumia wanajeshi kwenye kazi mbalimbali, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Matiko kwamba Jeshi la Tanzania ni Jeshi la namna yake duniani. Ndipo unaweza kumkuta askari anakuja kuchumbia nyumbani kwako, mnacheza na mnakula wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingine watu wakiona wanajeshi wanatupa kila kitu, hapa sivyo. Wewe ngoja kidogo tutoke nje uje uone nitakavyogongeana na majenerali wananipigia saluti. Sisi wanajeshi ni ndugu zetu, na ukimuona mwanajeshi maekwenda sehemu, jua kuna mambo. Ukimuona Kagera amewekwa nani, Mtwara amewekwa nani, fuatilia kuna mambo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther matiko, malizia mchango wako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napokea taarifa yake, lakini msisitizo wangu ni kwamba ukiwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa, unaingia kwenye Kamati ya Siasa ya CCM ya Wilaya au ya Mkoa; *this isn't right, that's where my point is,* kwa sababu wengine tunawaweka mipakani huko.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Tulieni jamani.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, anamalizia muda wake kwa hiyo taarifa moja tu ndiyo inayoruhusiwa hapo. Mheshimiwa Amar.

**TAARIFA**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimpe taarifa mzungumzaji kwamba hao

wanaoteuliwa kuwa Wakuu wa Mikoa, ma-*DC,* wanakuwa wameshastaafu tayari kutoka Jeshini. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, malizia mchango wako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananimalizia muda wang utu; Jenerali Mbuge amekwenda hapa, amestaafu lini? *Do a bit of research* kabla hujatoa taarifa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana, wamezungumzia kuhusu nyumba za wanajeshi wetu; ni mbovu sana, dhoofuli hali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, kuna Kanuni inavunjwa, Mheshimiwa Jenista, Kanuni.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tu nimkumbushe Mheshimiwa Esther, Kanuni ya 71(h) ambayo inamzungumzia Mbunge kutokuzungumzia mwenendo wa Rais, Spika ama watu wengine wanaotoa haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nimpeleke Mheshimiwa Esther kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ninaomba aende kwenye Ibara ya 36(2) ambayo inasema; Mheshimiwa Rais atakuwa na madaraka ya kuteua watu wa kushika nafasi za madaraka na watawajibika kuweka Sera na Idara na Taasisi za Serikali na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini akienda kwenye Ibara 34(4) inazungumzia pia madaraka ya Mheshimiwa Rais katika kufanya uteuzi. Kwa hiyo, sasa kama madaraka haya ya Rais katika kufanya uteuzi yamewekwa kwa mujibu wa Katiba nadhani si sahihi sana kwetu sisi Wabunge kuanza kuyazungumza madaraka ya Rais ya kufanya uteuzi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hizi amepewa kwa mujibu wa Katiba na yeye katika Katiba hajafungwa amchague nani, amteue nani, amuache nani. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria kwa kuwa ni suala la kikanuni lakini ni suala la kikatiba haitakuwa sahihi sana sana kuanza kuzungumzia madaraka hayo ya Rais ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati akichangia Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko amesimama Mheshimiwa Jenista, akitoa maelezo kuhusu kanuni zetu namna ambavyo kwa namna moja au nyingine zinavunjwa na mchango wa Mheshimiwa Esther Matiko na ameweka maelezo yake kwenye eneo mojawapo ambalo Mheshimiwa Esther Matiko alikuwa anachangia, nalo eneo hilo linahusu wanajeshi kwenda kuwa sehemu ya Serikali huku uraiani na ametoa mifano ya namna wanavyoteuliwa kuwa Wakuu wa Mikoa na pengine Wilaya ama kuongoza vitengo mbalimbali ambavyo si vya kijeshi, lakini ni vya kiraia.

Waheshimiwa Wabunge, wakati akitusomea Mheshimiwa Jenista Kanuni ya 71(1)(a) ambayo inaelezea namna ambavyo tunakatazwa kufanya mambo kadha wa kadha hapo, lakini pia akatupeleka kwenye Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 36 na 34 kwamba Rais anapewa hayo mamlaka ya kuteua mtu yeyote ambaye yeye anaona anafaa kwenye nafasi fulani.

Sasa katika, wakati akichangia Mheshimiwa Esther hakuwa amejielekeza kwenye mamlaka ya Rais kuteua, lakini twende taratibu, hakuwa amejielekeza kwenye mamlaka ya Rais kuteua, lakini kwa sababu aliyokuwa anawazungumzia ni wateuliwa wa Rais basi Mheshimiwa Jenista ameona

kwamba tukiwajadili wale wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais ni kama vile tunazungumzia mamlaka ya yule aliyeteua kama anayo mamlaka au hana. *(Makofi)*

Sasa wacha niliweke vizuri, mamlaka ya Mheshimiwa Rais kuteua hayawezi kuulizwa kwa namna hiyo kwa zile nafasi ambazo zinateuliwa kikatiba ama kisheria, Rais mamlaka yake hayaulizwi kwa sababu hata wale wanaompa ushauri hafungwi na huo ushauri yeye anaweza kufanya jambo ambalo ameruhusiwa kikatiba muda wowote. *(Makofi)*

Sasa hoja mahsusi ya hawa ndugu ambao wanateuliwa, hii si mara ya kwanza ikizungumzwa humu ndani. Sasa wacha niweke vizuri ili wanaochangia wengine waelewe mukhtadha wake.

Amesimama Mheshimiwa Mwijage hapa ameeleza kwa upande mmoja sababu maalum zinazoweza kumpelekea yule anayeteua na kwa mukhtadha huu Rais wetu kumteua mtu fulani kumpeleka sehemu fulani, anakuwa ana sababu na ameona mtu huyu ndiye anayefaa. Sasa kwa mukhtadha huo huwezi kusema kwa nini umempeleka huyu pale.

Lakini sasa, hoja ya Mheshimiwa Esther kwamba ukiwapeleka hawa wanajeshi wakaenda kuwa sehemu ya Kamati na ametaja mahsusi Kamati ya Siasa, lakini lazima unapozungumza Ukuu wa Mkoa usiuzungumze tu kwenye nafasi ndogo ya Kamati ya Siasa ya Mkoa ama Kamati ya Siasa ya Wilaya kwa Mkuu wa Wilaya, kwa sababu pia huyu ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwenye huo Mkoa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wanapopelekwa huko maeneo ni kwamba huyu mwenye mamlaka ya uteuzi ameona kuna sababu. Kwa hiyo, ukichukulia tu hilo eneo ambalo wanaenda kuwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya na ukasema pengine haipo sawasawa hoja ya Mheshimiwa Jenista inasimama kwamba

huwezi kuuliza yule anayeteua kama anaweza kumteua nani kwenye nafasi ipi.*(Makofi)*

Lakini sasa wanaenda pia kwenye nafasi nyingine ambazo siyo za kijeshi, lakini wanaenda wanajeshi na umetolewa mfano hapa anaweza kuwa Katibu Mkuu wa eneo fulani, Maliasili, sijui Mambo ya Nje, kwa hiyo hutegemea lile ambalo huyu mwenye mamlaka ya uteuzi ameona huyo ambaye ameteuliwa akasaidie kwenye hilo eneo. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu limezungumzwa humu ndani na watu wengine huwa hawaelewi sana zile Kamati za Siasa zinafanya nini na kazi ya Mkuu wa Wilaya akiingia kwenye Kamati ya Siasa ya Wilaya kazi yake ni nini na akiingia kwenye Kamati ya Mkoa kwa maana ya Mkuu wa Mkoa kazi yake ni nini? Hiki ni Chama ambacho ndicho chenye Ilani ambayo inatekelezwa nchini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, anavyoitwa kule ni kwenda kuelezea utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwenye Mkoa wake au kwenye Wilaya yake. Sasa kwa sababu Wabunge wa CCM huwa hawalizungumzi hili kwa nini, kwa sababu wao ni sehemu ya hivyo vikao kwa hivyo wanaelewa majukumu ya huyu mtu ni yapi. *(Makofi)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge na wananchi, wala wasiwe na wasiwasi kwa Mkuu wa Mkoa ama Mkuu wa Wilaya ambaye ni mwanajeshi kwenda kuhudhuria hivyo vikao kwa sababu wanachoenda kukifanya kule ni kile ambacho ana kazi hiyo kikatiba kwa sababu nchi yetu imeweka utawala wa kidemokrasia lakini tunaongozwa na vyama vya siasa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, chama cha siasa kilichopo madarakani kile kinachotekelezwa cha kwake lazima akawaambie wenye chama chao utekelezaji unaendaje. Kwa hiyo kule kwenye Kamati ya Siasa na Kamati ya Siasa ya Mkoa na Wilaya mukhtadha ni huo na nadhani kwa maelezo hayo nimeeleza kwa kirefu nadhani tumeelewana vizuri kuhusu hizi teuzi, lakini pia namna unavyoweza kuizungumzia humu ndani uteuzi

ambao Mheshimiwa Rais ameufanya kikatiba au kuna teuzi ambazo hata pengine zinaweza kufanywa na mamlaka nyingine ambazo zimeruhusiwa kufanya hivyo. Nadhani hili limeeleweka tayari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Esther Matiko malizia mchango wako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nilikuwa namalizia kwenye makazi ya ndugu zetu. Ni dhahiri yapo duni sana sana, kwa hiyo, tunaomba Serikali iboreshe makazi ya hawa ndugu zetu, kwa sababu tusiishie tu kuwaambia jeshi letu lipo imara, lakini wawezeshwe basi hata wakiishi wajue kabisa kweli nchi yangu inanijali kama vile ambavyo naitumikia nchi yangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, ajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwanza sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa alivyowasilisha vizuri taarifa yake, vilevile kuwapongeza walinzi wetu wote waliokuwepo hapa jinsi walivyokuja na tulivyowaona na jinsi wanavyohamasisha wanapokuwepo kwenye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kidogo nilikuwa nataka kuzungumza makazi ya wanajeshi wetu waliokuwepo pale Mererani wanaolinda *Tanzanite*. Kwa kweli Kamati ilipokwenda hali tuliyoikuta pale ilikuwa siyo nzuri, maana kwa maneno ya mjini utasema hali ya *full suit,* makazi yao juu bati, kuta bati, sasa kwenye joto, kwenye baridi wanapata shida. *(Makofi)*

Sasa tungeomba wawaboreshewe yale makazi kwa sababu askari wetu wasikivu wakakamavu wanatufanyia kazi nzuri basi na makazi yao japo nyumba mbili, tatu pale

zijengwe za za kudumu waweze kufanya kazi zao kwa uweledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia tena JKT; kuhusu ujuzi, kazi ya JKT kumfanya kijana awe mkakamavu, kijana awe mzalendo, lakini vilevile kuwafanya vijana wetu wakiondoka wawe na ujuzi, mnaweza kumfanya fundi cherehani, fundi makenika, fundi ujenzi, fundi mchundo, lakini akiondoka pale tayari anakwenda mitaani ana ufundi wake mwenyewe wa kwenda kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ningependa kuwaongezea lingine, mngekuwa mnatoa elimu ya Muungano, vijana wetu akitoka pale tayari anakuwa anajua nini chimbuko la Muungano. Akifika pale anatoka anajua nini faida ya Muungano, sasa hilo mkilifundisha ninyi kule na vijana wetu wengi mnawachukua litasaidia. Hii kuzungumza nitaienzi, nitaitukuza itakuwa rahisi kule ameshapata elimu ya kutosha. Sasa ningewaomba katika masomo yenu mnayotoa chimbuko la Muungano lazima liwemo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie lingine kuhusu Ofisi ya Wizara ya Ulinzi - Zanzibar. Ofisi za Muungano ipo ni moja tu, Ofisi ya Makamu wa Rais na ipo nyingine Mambo ya Nje, lakini zote haziridhishi, kwa sababu ya Makamu wa Rais imo ndani ya makazi yake, kule haipendezi kuwekwa ofisi. Kule kuna makazi ya Makamu, ofisi lingejengwa jengo moja kama la ghorofa au jengo la chini, ikawepo Wizara ya Ulinzi, Mambo ya Ndani, Muungano, Mambo ya Nje na taasisi zote za Muungano zikawepo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu kama anashida ya jambo la Muungano anajua nakwenda sehemu fulani nitaikuta ofisi na nitamaliza mambo yangu. Mtu anastaafu aende Bara, mtu ana matatizo yake katika Wizara ya Muungano aende Bara, kwa kweli haipendezi, na hata ninyi mkija Zanzibar mtafikia *rest house*, hotelini au kambini, pia haipendezi. *(Makofi)*

Sasa ningeomba mkashirikiana na mkajenga jengo moja tukasema hili jengo la Muungano, mtu anashida anakwenda pale Wizara zote atazikuta pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nataka sehemu nyingine stahili za likizo za wanajeshi. Toka mwaka 2011 mpaka 2020 wanajeshi hawajapata stahili zao za likizo na hasa wale wanyonge, wanadai shilingi bilioni 114 kama sikosei. *(Makofi)*

Sasa na hili mliangalie, mwanajeshi hawezi kusema hana wa kumsemea, atanung'unika pembeni na hastahiki kunung'unika. Sasa kama hatukuwasemea mtu haki yake apewe. Hata mama mwenyewe analipigia kelele hili watu wenye stahili zao walipwe, sasa ningekuona na hili ukaliangalia kwa jicho la huruma na kwa jicho la imani vipi mtawasaidia wanajeshi wetu waendelee kufanya vizuri ingawa wanafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja la mwisho, Hospitali ya Jeshi iliyokuwepo Zanzibar Bububu, hospitali nzuri inafanyakazi vizuri, lakini tungeomba kizuri lazima na kingine uongeze. Mngetuongezea nyingine kama Mkoa wa Kusini mkatufanyia kama ile iliyokuwepo Bububu au moja mkapeleka Pemba kama iliyokuwepo ili tunajua kwa sababu unapotaka upate matibabu mazuri ukikimbilia jeshini, jeshini hambagui, hambagui kitu, yoyote atakayekuja mnamtibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hasa ningeona hili mliangalie kwa sababu pale pana vifaa vya kileo, pana madaktari wazuri, kuna kila sifa mnayo, mtu uzuri wake aambiwe, lakini tunataka kama itakupendeza au itawezekana mtutafutie na nyingine ikiwa mtaweka Mkoa wa Kaskazini maana hii ipo Mkoa wa Mjini Magharibi. Kama mtatuwekea Kaskazini au Kusini na nyingine Pemba kama mtaweka Kaskazini au Kusini ili kila zikiwa zipo nyingi na mambo yetu yanakuwa mazuri na ninyi kama mnapata thawabu kwa *Allah*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kwa haya machache naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mheshimiwa Saada Monsour Hussein ajiandae.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa nafasi hii, pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa mema yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Amiri Jeshi Mkuu wa kwanza Mwanamke Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, michango mingi iliyochangiwa na mimi nimeipenda sana naiunga mkono, mchango wangu ambao nataka niunge mkono kwa jitihada zote ni suala la kuhakikisha kuwa Wizara hii inapewa fedha za kutosha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba jeshi linaweza kufanya tafiti muhimu za kisayansi ambazo zinawezesha kulifanya Taifa hili liwe na nguvu zaidi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba ulinzi uliokuwepo katika siku za nyuma ni ule ambao hasa tulikuwa tunaenda, tunajipanga zaidi kwenye mipaka yetu kuona kwamba labda adui atakuja kwa njia ya silaha ya moja kwa moja. Atakuja na *SMG,* atakuja labda pengine na silaha ya aina fulani, lakini vita vya sasa hivi ni vya tofauti, ni vita ambavyo hata adui yako humuoni, lakini upo naye jirani, ni vita ambayo inaweza ikapitia teknolojia au hizi tafiti za kisayansi zikaangamiza Taifa wakati nyinyi wenyewe hamjawa na taarifa za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi letu limeonesha nguvu kubwa sana katika mambo mbalimbali, mimi ningetamani kuona kwamba hata katika Hospitali hii inayotarajiwa kujengwa katika eneo la Msalato basi Jeshi liweze kupewa na sehemu ambayo itaweza kufanya tafiti kubwa za kibailojia ambazo zitaweza kushirikiana na taasisi nyingine za kimataifa

na ndani ya Taifa kuweza kuleta matokeo chanya zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba pamoja na hayo kwa sababu Jeshi letu halijaanza leo, yawezekana katika baadhi ya sheria tulizonazo na sera zilizopo haziwezeshi kufanya hayo, kufanya hizi kazi za mashirikiano na taasisi nyingine ndani ya nchi na nje ya nchi. Kwa hiyo, ni vyema tuziangalie pia sheria zetu ili ziwezeshe kufanya Wizara hii kupitia taasisi zake au majeshi yake kuweza kufanya kazi hizi za kitafiti, kazi hizi za kiuwekezaji na kuwezesha tuweze kupata mafanikio makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwanza pamoja na kwamba umetolewa ufafanuzi mkubwa, lakini niseme kwamba hawa ndugu zetu wanajeshi wanatakiwa pia kufahamu namna ambavyo sekta mbalimbali zinafanya kazi ikiwemo masuala ya kisiasa, kwa sababu wakati mwingine unakuta kinachosababisha mpaka vita ikatokea mahali ni masuala ya kiuchokozi tu, au masuala ambayo mengine yangeweza kudhibitiwa mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hawa wanapokuwa wanapata nafasi ya kushiriki katika maeneo mbalimbali ya kiuongozi inasaidia pia kurudisha mrejesho kwenye taasisi zinazohusiana na masuala ya kiulinzi ili ziweze kujipanga vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi katika suala la ulinzi mipakani; kwanza nianzie kuzungumzia hili suala la mpaka wa Ziwa Nyasa kwa upande wa Tanzania na ndugu zetu kule Malawi. Hili suala ni la muda mrefu, watu tunakaa tunahofu, hatujui kinachoendelea, uwekezaji unakuwa wa shida basi niombe pengine jitihada zifanyike zaidi ili suala hili la mpaka liweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati huo huo mimi nafahamu mlinzi wa kwanza katika nchi ni raia mwenyewe ni mwananchi mwenyewe, lakini sasa utakuta katika maeneo ya baadhi ya mipaka ikiwemo mpaka katika eneo la Ziwa

Nyasa hali ya barabara siyo nzuri, ukitoka kule Chiwindi ukifika mpaka Lituhi uende mpaka Lipingu, Manda, Lipingu ufike mpaka Matema hali siyo nzuri, afadhali hata sisi tuna barabara ya vivumbi kidogo, lakini wenzetu unakuta wanategemea maji. Kwa hiyo ni vema ile barabara ikapewa kipaumbele na sema hayo pamoja na Wizara ya Ujenzi lakini hao Wizara hii ndiyo wadau wakuu wa kufaidika barabara itakapokuwa imeimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile eneo la Mpepo mpaka Dapori nalisemea kila siku, jamani kuna changamoto kule kubwa, hivi ninyi ndugu zetu ninyi hamshauri ninyi si mnashirikiana na hawa wenzetu wa barabara! Kwa nini hali imekuwa mbaya vile? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba katika masuala ya kuimairisha ulinzi eneo lile ni vyema lifanyiwe kazi ikiwemo daraja la Mto Ruvuma pale Mitomoni ili kuhakikishwa kwamba usalama wa maeneo yale unaimarika na unakuwa ni mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende katika suala la haki za binadamu lakini pia kutoa fursa sawa kwa wote. Kwa siku za nyuma uwe mwanajeshi au uwe polisi ukishakuwa mfupi kama mimi *Engineer* Manyanya hawakuchukui, lakini siku hizi hatuangalii urefu tu, hatuangalii maumbile tu, hawa ndugu zetu wenye ulemavu mbona hawapati fursa za kuingia Jeshini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatusemi waende wakapigane mstari wa mbele, lakini kichwa chake na mikono yake yawezekana kina uwezo mzuri katika masuala ya *ICT*, katika masuala ya kimkakati na wakafanya vizuri tu. Kwa nini sasa Serikali isiangalie kuona namna bora ya kuweza kusaidia hata kundi hilo hata kama hawatawekwa katika nafasi hiyo ya kwenda kwenye mstari wa mbele, lakini waweze kufanya kazi ambazo pia zinaweza kusaidia katika kutoa maarifa na mambo mbalimbali yanayohusiana na kuimarisha Jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naamini inawezekana, hatuwezi kusimamia tu sheria zile za zamani zinasema kwamba wewe tumekuona mkono wako umekaa hivi basi wewe huwezi kwenda. Hapana, kuna watu tena watu wenye ulemavu Mungu amewapa vipawa vikubwa sana, unaweza kukuta kwamba huyo ndio akawa *master mind* mzuri sana. Kwa hiyo, mimi nasema hili suala tuliangalie ili hilo kundi na lenyewe liweze kusaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, katika haya masuala ya JKT hawa vijana ambao wako barabarani wanaomba na wenyewe waweze kuwekewa utaratibu wa kusaidiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, si jambo la heshima kuiona Tanzania bado inakuwa na watu wengi barabarani wanaombaomba. Hapana hawa vijana wanaweza wakasaidiwa, huyo anayesemekana labda hana mzazi yawezekana kweli wazazi wake wote wawili hawapo, lakini pengine kuna wale wazazi ambao hawajali hao ni Taifa.

Kwa hiyo, mimi niombe kupitia Jeshi letu tuone pia uwezekano wa kunusuru eneo kama hilo, lakini kwa Serikali kutenga fungu maalum la kusaidia Wizara hiyo kuweza kusaidia masuala kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kwa kweli pamoja na yote niliyozungumza mimi nalipongeza sana Jeshi letu, napongeza sana sana Wizara hii inavyojitahidi katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Nampongeza sana Mheshimiwa wetu Waziri Ndugu Elias kwa kazi kubwa ambayo anaifanya, kijana mpole, lakini mambo yako makubwa. Mimi nakupongeza kwa kweli, naona kwamba ndio maana hata Jeshi letu linaendelea kutulia, lakini nizidi kusisitiza kuomba kwamba hao ndugu wawezeshwe na kwa sababu wakiwezeshwa watafanya kazi kubwa zaidi ikiwemo kuwasaidia vijana waliopo vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na sio wabakie tu kufundisha migambo kule vijijini, mbali ya mgambo wafundishwe hata hizi shughuli za kujiajiri kule vijijini, isiwe tu kutembea, kukimbia, *root matching,* hapana; lakini pamoja na masuala ya kiuchumi wakati wanapofundishwa masuala ya mgambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo niliyozungumza naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana na mimi nimefurahi Mheshimiwa Waziri ameitwa kijana kwa hiyo, na mimi katika wale vijana wanaosubiriwa Jeshini naamini na mimi nitakuwemo kabisa maana amesema vijana walioko humu Bungeni, kwa hiyo naamini na mimi nitakuwepo kwenye hiyo orodha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, atafuatia Mheshimiwa Saada Mansour Hussein, Mheshimiwa Lucy Mayenga ajiandae.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda sana nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi yote ya Ulinzi na Usalama Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa jinsi alivyoanza vizuri kazi yake hii ya Urais wa Jamhuri ya Muungano, kwa kuliwezesha Jeshi letu la wananchi wa Tanzania pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama kuweza kufanya kazi zao kwa ueledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile napenda nichukue fursa hii adhimu nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, kwa namna bora alivyowasilisha hotuba yake ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Pia napenda sana nimpongeze na kumshukuru sana Mkuu wa Majeshi ya

Ulinzi na Usalama Tanzania *CDF*, *General* Mabeyo pamoja na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi *Lieutenant General* Yacoub Mohamed kwa namna bora wanavyoshirikiana na Mkuu wa Majeshi kwa kuweza kufanya kazi zao kwa ueledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa vilevile napenda nilipongeze Jeshi letu kwa kuendelea kulinda mipaka yetu ya Tanzania na mpaka hivi sasa nchi yetu bado iko salama. Napenda nilipongeze Jeshi letu kwa kuendelea kuulinda Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar na mpaka hivi sasa tumefikia umri wa miaka 57. Vilevile napenda nilishukuru Jeshi letu kwa kuendelea kuyaenzi na kuyalinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar nayo pia yametimia umri wa miaka 57. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nilipongeze jeshi letu kwa kuendelea kushiriki katika *mission* mbalimbali za Kimataifa hususani kule DRC Congo, Darfur Sudan pamoja na Lebanon. Vilevile napenda nilipongeze jeshi letu kwa namna bora wanavyoshirikiana na wananchi wa Tanzania, hasa pale panapotokea majanga na shida mbalimbali za wananchi, wanajitokeza na kuweza kusaidia jamii ya Watanzania na hii inaonesha wazi kuwa jeshi letu ni jeshi la wananchi kweli, ni jeshi la wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu nilikuwa napenda sana nijielekeze katika mashirikiano kati ya Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi la Kujenga Uchumi Zanzibar. Katika Ilani yetu ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 157, chama chetu kimetuelekeza kushirikiana kati ya majeshi haya mawili ambayo yana dhamana ya ulinzi, lakini vilevile yana dhamana ya kukuza uchumi wetu wa pande zote mbili. Nilikuwa naomba sana ushirikiano huu uendelee vizuri japokuwa tayari umeshaanza katika kipindi kirefu, lakini nilikuwa naomba sana ushirikiano kati ya JKT na JKU kama yalivyozungumzwa katika Ilani yetu ya Uchaguzi yaendelee ili kuwapa nguvu vijana wetu wa pande zote mbili za Muungano ili kuweza kupata sifa zile za kuweza kujiajiri na kupata sifa za kuweza kuajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa hivi Taifa letu lina vijana wengi ambao hawana kazi, lakini wengi wanategemea wapate ujuzi kupitia majeshi yetu haya mawili. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana kwa upande wa JKU tangu kuasisiwa kwake jeshi hili limekuwa likijihusisha sana na masuala ya kilimo, ufugaji, viwanda vya samani pamoja na michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba sana kupitia viongozi wa Jeshi la Kujenga Taifa – JKT waweze kushirikiana vizuri na JKU ili kuweza kuwapa nguvu nao kuweza kupata nguvu zaidi za kuweza kushiriki katika mambo mbalimbali ya Taifa letu na kuweza kukuza uchumi wetu wa Tanzania na katika hili tayari viongozi wetu wameshaonesha nia njema, hivi karibuni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, amewateua baadhi ya viongozi au Maafisa Wakuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwenda Zanzibar kwenda Wakuu wa Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mategemeo yetu uteuzi huu utaweza kaleta tija katika vikosi vyetu hivi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na ushirikiano ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania pamoja na vikosi vyote vingine ambavyo kwa mujibu wa katiba yetu ni majeshi ya akiba. *(Makofi)*

Vilevile nilikuwa napenda nilikumbushe Jeshi letu pamoja na Waziri wa Ulinzi kuweza kuongeza nguvu katika ujenzi wa nyumba za askari wetu. Wenzangu wengi wamechangia suala hili, lakini la umuhimu jitihada zimefanyika, lakini naomba pia ziendelee kufanyika ili wanajeshi wetu waweze kuishi katika nyumba bora na kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana nimuombe Mheshimwia Waziri aendelee na wazo hili la kuweka bima ya afya kwa ajili ya askari wetu pamoja na familia zao. Zoezi limeanza lakini nilikuwa naomba liende kwa haraka ili

wanajeshi wetu waweze kufaidika na kupata hamu kubwa ya kuweza kufanya kazi za ulinzi na usalama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Shaurimoyo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saada Monsour Hussein, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum ajiandae.

**MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia. Kwa vile ni mara yangu ya kwanza kusimama katika Bunge hili tukufu, nakishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kuniteua. Pia nawashukuru Umoja wa Wanawake wa Tanzania Taifa (UWT) pamoja na wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kuniamini ili niwe mwakilishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia umuhimu wa Hospitali ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania iliyopo Bububu kuboreshwa. Hospitali hii ni muhimu kwa kuwa ndio hospitali kubwa ya jeshi ndani ya Zanzibar, hivyo ninashauri Wizara ya Ulinzi iongezewe fedha kwa ajili ya kuongeza majengo na vifaatiba.

Pia ninashauri Wizara hii ijengewe majengo maalum ya kutoa huduma kwa viongozi wetu wa Kitaifa pale wanapoumwa. Hospitali nyingi za binafsi za Zanzibar na za Serikali hazina faragha za kutosha kwa matibabu ya viongozi, hivyo majengo hayo yakiwepo yatarahisisha huduma na kuwa kimbilio kwa viongozi na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Wizara ya Ulinzi haina jengo la Wizara ndani ya Zanzibar, Wizara hii ni ya kimuungano, hivyo ninashauri iwe bajeti hii ama bajeti ijayo Serikali ianze mchakato wa kuanzisha ofisi ya jengo la Wizara ndani ya Zanzibar. Ofisi hiyo itasaidia shughuli za Wizara ndani

ya Zanzibar ikiwemo kutoa huduma kwa urahisi kwa askari wetu wa JWTZ wanapotaka huduma za kiwizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lucy Mayenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo, ajiandae.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kushukuru kwa kunipatia nafasi hii, ninajisikia furaha na fahari kubwa leo kwa mara ya kwanza katika miaka yangu yote ambayo nimekaa Bungeni ninasimama hapa kuchangia Wizara hii ikiwa chini ya Amiri Jeshi Mkuu mwanamke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Watanzania wote kwa ujumla wetu tumpatie zawadi kubwa moja tu Mheshimiwa Amiri Jeshi MKuu, ni tulitaje jina lake kwa wema popote tulipo ili aweze kupata moyo wa kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Jeshi letu, Jeshi hili limetuheshimisha watanzania kwa muda mrefu sana jeshi hili limekuwa likifanya kazi nyingi sana, licha ya kazi ambazo ziko kwenye Katiba yetu kisheria, lakini limekuwa likifanya kazi nyingi sana kwenye jamii yetu kwa maana hiyo na limekuwa likituheshimisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio tu kwenye nchi yetu, Jeshi hili limekuwa likifanya kazi kubwa sana na zipo kihistoria, zipo nchi ambazo haziwezi kuelezea mafanikio waliyonayo ya uhuru wao bila kutaja mchango wa Jeshi la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya maeneo mbalimbali katika nchi hii au nje ya Tanzania yamekuwa yana matatizo kadhaa, lakini Jeshi hili limekuwa likienda, matatizo yao yanakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kwa kifupi kuhusu suala zima la mchango wa jeshi letu katika *operation* za amani duniani, jeshi hili limekuwa likishiriki katika *operation* za amani katika nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kama ambavyo tunafahamu wapo Lebanon, wapo Darfur, wapo Congo na kadhalika. Kazi wanayoifanya kule ni kubwa sana na kwa kweli mimi ningeomba jeshi hili kazi hii iendelee kwa sababu inawapa *exposure* na ni faida kwao pia kiuchumi kutokana na posho wanazozipata. Lakini pia vilevile jeshi hili wanajeshi hawa wanapokwenda kule wanakuwa pia na nafasi ya kujipima uwezo wao pamoja na majeshi mengine ya nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwasababu kazi hii inafanywa chini ya Umoja wa Mataifa, kuendelea kwa jeshi letu kuaminika kwa wanajeshi kupelekwa huko kwa kweli ni sifa kubwa sana na wanastahili pongezi kubwa sana. Lakini kwenye hili mimi nilikuwa naomba, ninaomba Mkuu wa Majeshi Mabeyo, kaka yangu kwanza nikupongeze kwa kazi nzuri sana. Mimi nilikuwa naomba kwenye *operation* hizi idadi ya wanawake iongezwe, wanawake wanaweza, leo tumeona akinamama.... *(Makofi)*

**MHE. RIDHIWANI M. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pale wamechafuka mabegani, akina mama wanaweza. Kwa hiyo mimi nilikuwa naomba kwamba kwenye...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

## TAARIFA

**MHE. RIDHIWANI M. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naomba nimpe taarifa tu dada yangu tunapo mu-

*address* Mkuu wa Majeshi hatumwiti kwa jina lake, yule anaitwa *General* Mabeyo. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Haya sasa kwa sababu Mheshimiwa Lucy Mayenga anachangia Kiswahili basi ni Jenerali. *(Makofi)*

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili kabisa Jenerali Mabeyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya kazi hizi ambazo zimekuwa zikifanywa nje ya Tanzania pamoja na hapa kwetu Tanzania, sina budi kutoa pongezi kwa jeshi letu kwa kazi kubwa sana ambayo wameifanya Kibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niwapongeze kwa sababu kazi ile kwenye masuala ya kivita, mimi sijawahi kuwa mwanajeshi wala sijawahi kuwa askari, lakini ninafahamu kwamba *conventional war* ni tofauti sana na *gorilla war;* aina ya mapigano na hali iliyokuwepo kule Kibiti, ilikuwa inafanana sana na *gorilla war;* humjui adui yako lakini kazi iliyofanyika ni kazi kubwa sana na ninaomba kwenye hili pia ili na sisi Tanzania tuendelee kuwa na amani kwa sababu inavyoelezwa ni kwamba wale magaidi wametoka sasa kwa upande wa Tanzania wamehamia kwa majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Tanzania na Msumbiji au na hizi nchi zingine ambazo tuko nazo majirani Tanzania na Msumbiji hasa ambako ndio inasemekana kwamba wamekwenda kule tuko karibu sana. Kwa hiyo, ina maana kwamba na sisi tusipojiimarisha wasije tena wakaona kama tumelala lala wakarudi. Nilikuwa naomba tuongeze msimamo, tuongeze kazi, tuongeze nguvu kama ambavyo ilivyo. Na kwenye hili, ninaomba niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuteua watu ambao wakiwepo kwenye maeneo kama haya *strategically* wataweza kutusaidia. Kwa sababu hawa ni watu ambao wana mafunzo ya hali ya juu wanajua wanachokwenda kukifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi zangu kwa kulingana na *seniority* ya wanajeshi naomba niwapongeze sana Jeshi la Nchi Kavu, naomba niwapongeze sana Jeshi la Anga, naomba nipongeze sana Jeshi la Wanamaji pamoja na JKT, kwa kazi hii kubwa ambayo walikuwa wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini licha ya kuelezea kwamba wanajeshi hawa wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana, mimi niwaombe *with due respect* kwamba kuna kitu ambacho kilikuwa kinatolewa kwa wanajeshi wetu kama motisha, kwa maana ya yale maduka ambayo yalikuwa yana *duty free* ya Jeshi. Lakini pia vilevile, *mess* ambazo zilikuwa zinaendeshwa katika utaratibu wa *duty free* kwa maana ya vinywaji na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wanajeshi wanapokuwa wanakaa pamoja kwenye maeneo kama haya ya *mess* na kadhalika wanakuwa na *cohesion* lakini pia hii ni *organizational culture,* dunia nzima hivi vitu vipo. Sasa mimi nilikuwa naomba tukikaa tukasema kwamba labda pengine kuna *either* kubana matumizi au kwa njia moja au nyingine ile hali ambayo ilisababisha tukaondoa hivi vitu, mimi nilikuwa naomba tufanye tathmini kama ilikuwa kuna dosari dosari, ubadhirifu na kadhalika kwenye vitu kama hivi tujaribu kuangalia tena upya ili kama ikiwezekana tuweze kuwarudishia kwasababu hivi ndio vitu ambavyo vinawapa motisha wanajeshi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninafahamu kwamba jeshi letu limekuwa likitoa huduma mbalimbali kwa wananchi wetu, hasa katika maeneo ambayo yamekuwa yakikabiliwa na majanga lakini pia vile vile yamekuwa yakikabiliwa na matatizo mbalimbali wakati wa dharura.

Nilikuwa naomba kutoa ombi Mheshimiwa Waziri wetu wa Ulinzi Mheshimiwa Kwandikwa ambaye anafanya kazi nzuri sana, nilikuwa ninaomba Mheshimiwa Waziri wetu na ninafahamu kwamba ni msikivu uweze kutusaidia katika Mkoa wetu wa Shinyanga yapo maeneo katika Wilaya mbalimbali

Wilaya ya Kishapu, Wilaya ya Shinyanga Mjini, Wilaya ya Kahama, Majimbo yote pamoja na kwako Ushetu, kumekuwa kuna matatizo mengi sana sana sana, pia Wilaya ya Shinyanga Mjini na kadhalika kumekuwa kuna matatizo ya uharibifu mkubwa wa miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba masuala ya miundombinu yako kwenye Wizara ya miundombinu, lakini tunajua pia kwamba mchakato wa ujenzi wa madaraja kwenye maeneo mbalimbali huwa sio kitu cha mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nakuomba sana Mheshimiwa Waziri uweze kutusaidia uwepo wa madaraja kwa mfano kwa kwetu Shinyanga Mjini kuna Upongoji ambayo linaunganisha Ndala na Masekelo kuja Shinyanga Mjini, kuna Ibinza Mata ambayo inakwenda Kitangiri, kuna Uzogole kwenda Bugwandege, kuna *Old Shinyanga* kwenda Mwamalili na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wetu wamekuwa wakipata shida, nilikuwa naomba haya madaraja ya muda ambayo mnayo basi muweze kukaa chini kuweza kuangalia ni jinsi gani mnaweza kuja kutusaidia. Ndugu zangu kwenye maeneo haya ambayo nimeelezea hali huwa ni mbaya, wananchi wanasombwa na maji, magari yanasombwa na maji, hali huwa inakuwa mbaya sana. Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba sana Mheshimiwa Waziri muweze kuliangalia hilo na ninafahamu kabisa kwamba hili ukilikalia vizuri litawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho nilikuwa nataka kuzungumzia kuhusu suala zima la teknolojia. Wote tunafahamu kwamba, dunia inabadilika naomba tu kuelezea kwa kifupi, kuna kitu kinaitwa *high tech. warfare* naomba kuuliza, *are we ready?*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, atafuatiwa na Mheshimiwa Frolent Laurent Kyombo, Mheshimiwa Asia Halamga ajiandae.

**MHE. AHMED A. SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika Wizara hii Wizara ya Ulinzi. Kwanza nimpongeza kaka yangu, ndugu yangu Mheshimiwa Waziri Kwandikwa, Waziri wa Wizara hii na hoja yake nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani ilikuwa nafikiri jeshi lolote duniani kazi yake ni kupigana tu au kulinda mipaka peke yake ya nchi husika. Lakini nimekuja kujifunza Jeshi ndio nchi na nchi ndio Jeshi. Nimpongeze sana *General* Mabeyo na timu yake yote, wakati wa msiba wa aliyekuwa Rais wetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Msiba ule waliubeba ilikuwa natazama mimi *TV* nikasema kumbe jeshi ni nchi na nchi ni jeshi kuanzia hatua ya mwanzo mpaka walipokwenda kumpumzisha aliyekuwa Rais wetu John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ile sio ndogo na ni kazi moja kubwa sana. Kwa hiyo, mimi nampongeza sana, sana, sana pamoja na jeshi lote kwa ujumla wake walivyosimamia msiba wenyewe, walivyosimamia amani ya nchi, walivyosimamia maeneo yote, ilikuwa naona maeneo tu kule mipakani, kwamba sasa pasitokee na taharuki yoyote katika Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. Jeshi letu linafanya kazi kubwa, yako mambo hata kwenye hotuba hawawezi wakayasema. Mipaka yetu inalindwa na jeshi *twenty-four seven*. Kuna watu pale hawalali saa 24 wanatazama mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa nasikiliza taarifa ya habari kuna baadhi ya wakimbizi wanatoka nchi jirani kule wanaanza kukimbilia huku. Kazi kubwa hiyo inayofanywa na Jeshi letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wapo pale. Jeshi wanafanya kazi ya kulinda mipaka yetu, Jeshi wanafanya kazi ya kulinda maeneo mengi, Jeshi wanafanya kazi yanapotokea mafuriko ndani ya nchi yetu hii, kwa mfano, kuna wakati meli ilipunduka katika Ziwa Victoria, walitumwa

vijana wa Jeshi kwenda pale, lakini kwa bahati mbaya kwa sababu ya vifaa walikuwa hawana sana, walikuwa na vifaa vichache walichukua zaidi ya siku saba mpaka siku kumi kuokoa ile hali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hoja yangu hapa Mheshimiwa Waziri pamoja na Jeshi yaani uone namna ya kuongeza fedha zaidi za kutosha kwenye eneo hili la kuokoa maeneo ya hatari au kwenye mafuriko kwenye maeneo yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ikitokea kwa mfano sasa hivi treni imepundika, barabara kubwa imekatika, daraja kubwa limekatika, kimbilio letu ni Jeshi. *(Makofi)*

Sasa hoja yangu hapa, fedha hizi tunapitisha leo trilioni 2.35 na ngapi zisipungue. Ziende kama walivyojipangia wenyewe ili wakajipange sasa waweze kuweka mambo yao vizuri kwa ajili ya Nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kenya nilisikia wameanza kutengeneza risasi na baada ya mwaka mmoja wataanza kuuza. Sisi tuna karakana kubwa ya Nyumbu alivyosema Mheshimiwa Mwijage pale kubwa mno ile inaweza kuwa ya tatu Afrika au duniani ikawa moja katika sehemu moja kubwa. Hivi tunashindwaje sisi kama Jeshi wakawa na mipango ya kutengeneza risasi na silaha ndogo ndogo. Leo JKT waliwahi ku-*assemble* matrekta haya wakauza na ikafanya kazi kubwa mno na wakulima wengi wamefanikiwa kutokana na zile treka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale Nyumbu karakana ile inaweza wakaagiza *engine* tu peke yake wana karakana wanaweza kufyatua ma-*mudguard,* wakafyatua *chassis*, wakafyatua mambo mengi pale tukaagiza vitu vichache mno vikawa-*assembled* ndani ya karakana ya Nyumbu. Nyumbu pale tunaweza tukatengeneza risasi, Nyumbu pale wanaweza wakatengeneza silaha ndogo ndogo hizi ambayo kwa nchi kama nchi tunaweza tuka-*export* kwa nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyumbu ni kitu kikubwa sana wewe ukienda pale ndio unajua hapa kweli nchi ipo hapa. Ni suala la kukaa kuwekwa teknolojia, kuona bajeti yake, kuhuisha mashine zile wakakaa kama Jeshi, mimi naamini jeshi ni watu wakubwa mno na wanaelimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Jeshi kuna watu wamesoma kwelikweli, juzi tu pale kwenye msiba wa aliyekuwa Rais wetu zilivyopita zile ndege uliamini kama kuna ma-*pilot* wa aina hiyo. Ndege inaenda inabinuka inarudi namna hii.

Kwa hiyo, utaona jeshi lipo vizuri na wanaweza wakafanya kazi vizuri, yaani mimi sasa hivi nimeona jeshi la umuhimu hapa tunatembea kwa amani tu, kumbe kuna watu kule wamekaa wanatulinda. Huwezi kujua wamekaa kwa muda gani, tunafanya kazi zetu vizuri, tunafanya mambo yetu vizuri, tunafanya biashara vizuri, tunafanya vitu vyetu vizuri, nchi leo ya Tanzania hii ni nchi katika nchi tatu Afrika ambazo mpaka leo hazijawahi kuingia kwenye misukosuko ya mapinduzi kwa sababu ya jeshi letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, historia ya Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pamoja na Afrika Kusini, huwezi kusema Uhuru wa Afrika Kusini waliopata kule bila kuwataja Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Huwezi kusema Zimbabwe bila kuwataja Jeshi la Wananchi wa Tanzania, huwezi kusema leo Congo kuna vijana wetu wapo Congo, vijana wetu wapo *Central Africa,* vijana wetu wapo Lebanon, bila ya kuwataja Jeshi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo ni kazi kubwa mno wanaifanya kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nilikuwa nataka watoke hapo tuingie, tuiboreshe Nyumbu iweze kuzalisha magari kwa ajili ya matumizi ya kijeshi, wazalishe risasi kwa ajili ya matumizi ya jeshi, waweze kuzalisha bunduki kwa ajili ya matumizi ya jeshi ndani ya nchi na kuweza kuuza ikiwezekana hata kuingia *partnership* na mashirika mengine ya *private*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Urusi, risasi hizi na silaha zao zinatengenezwa na *private* sekta lakini chini ya ulinzi wa Serikali ya Urusi. Ukienda China hizi hizi risasi, hizi hizi silaha na mabomu mengine madogo madogo yanatengenezwa na *private* sekta lakini chini ya usimamizi wa jeshi la nchi husika na hiyo inawezekana tu, ni suala la kukaa, kupanga, kuona tutoke hapa sasa jeshi letu tuliwezeshe kuwa katika jeshi moja bora katika Afrika Mashariki na Afrika nzima kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya wanajeshi; wanajeshi tuwatizamie maslahi yao. Mheshimiwa Msukuma alisema nyumba bora, ni kweli, tuwatengenezee namna ambavyo watakavyoweza kuishi vizuri wanajeshi wetu. Ikiwezekana hata kuwaongezea maslahi bora kidogo. Wanajeshi wanavyofanya kazi, yaani wanakuwa na mazingira, unaweza kukuta mwanajeshi mmoja yuko sehemu huku mke wake labda yuko huku, akihamishwa huku, anatafuta ka-*chance* kadogo tu, Jumamosi, Jumapili anakwenda kumuona mke wake anarudi kwa ajili ya ulinzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wako katika mazingira magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama kuna namna yoyote ya kuweza kuona maslahi yao, tuweze kuona maslahi yao hata kuwaongeze posho au mishahara au kuwatengenezea malazi mazuri na makazi mazuri, wahisi kwamba wao wapo kwa ajili ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nimpongeze tena *General* Mabeyo kwa kazi kubwa anayoifanya mungu akubariki sana, tuko pamoja sana, tutasaidiana sana, sisi kama Bunge wala hatua wasiwasi na naunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Ahmed Ally Salum alikuwa anaeleza namna

ambavyo wanajeshi wanavyoweza kuwa wanatoka mahali kumfuata mke wake, sasa inabidi uchangie na ile sehemu ya pili; mwanamke Mwanajeshi anaweza kuwa anamfuata mumewe na ndio maana walileta wengi humu ndani leo ili mpate picha kwamba kule nao wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Frolent Laurent Kyombo atafuatiwa na Mheshimiwa Asia Halamga kama muda wetu utakuwa unaruhusu atachangia pia Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi na mimi niungane na wachangiaji waliotangulia kuipongeza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri wanayoifanya ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwamba Jeshi la Ulinzi limekuwa likifanya kazi kubwa na hasa katika Wilaya na Majimbo ambayo yapo mipakani mwa Nchi yetu kama Mheshimiwa Waziri alivyosema katika hotuba yake na Wilaya ya Misenyi ni mojawapo ya sehemu ambayo Wizara ya Ulinzi imefanya kazi kubwa kuhakikisha amani na usalama ndani ya Wilaya yetu ya Misenyi inakuwepo na hasa katika eneo la kudhibiti wahamiaji ambao walikuwa wanatoka nchi za jirani kuja kufanya machungo ya mifugo yao ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri hiyo katika eneo hilo, tunaomba maboresho kidogo katika Jeshi letu la Ulinzi. Ukiangalia katika eneo ambalo lipo mpakani kabisa eneo la Kata ya Kakunyu, vijiji vya Kakunyu, Bugango na Bugwenkoma; mpaka wa Jeshi letu upo karibu kilometa 20 kutoka mpakani, maana yake unaacha vile vijiji nyuma na nchi ya Uganda halafu wenyewe mpaka upo mbele ya vijiji. Kwa kweli pamoja na kazi nzuri ya Jeshi letu wananchi wamekuwa wakipata taabu sana kwasababu kweli lazima Jeshi letu lijiridhishe unapokuwa unatoka eneo hilo kuja Makao Makuu ya Wilaya, kwa hiyo katika msafara huo unakuta na baadhi ya wananchi wanapata kero ndogo ndogo ambazo zinaweza kudhibitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri unajua kabisa Wilaya ya Misenyi ilitenga maeneo mazuri kule kwenye mpaka kabisa zipo heka za kutosha. Mimi ningeshauri Wizara yako ione sasa ule mpaka ambao upo katikati baada ya vijiji uweze kuhamia katikati ya nchi ya Uganda na Tanzania ili wananchi wetu sasa vijiji hivyo nilivyotaja wawe huru kuendelea na shughuli zao na pale wanapokuwa wanakwenda Wilayani basi wasipate bughudha nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma Randama ya Wizara ya Ulinzi, tunaona kazi nzuri wanayoifanya na hasa katika eneo la ushirikiano na mamlaka za kiraia. Kuna kazi nzuri zimefanyika, lakini katika eneo hilo, kuna suala lingine ambalo ningeweza kushauri Wizara iboreshe. Ni mahusiano au utatuzi wa migogoro kati ya jeshi letu ulinzi na wananchi. Wilaya ya Misenyi wote tunajua kwamba ulikuwa ni uwanja wa vita vya Kagera ambavyo vilihitimishwa mwezi Juni, 1979. Kwa hiyo, umeacha maafa mengi sana katika eneo hilo na wananchi wanapokuwa wanaendelea mambo hayo kuyaona wanahisi bado tupo ndani ya vita.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1978 Jeshi letu lilikuja na wananchi walikuwa tayari kujitoa kwa ajili ya kutoa rasilimali kuwezesha jeshi letu ili kupigana vile vita ambavyo kimsingi sisi wananchi tulikuwa na maslahi nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Kyaka, Kijiji cha Kurifani, Kitongoji cha Biawamara wananchi walitoa maeneo yao kwa ajili ya kuhakikisha jeshi letu linakaa salama, linaweka nyenzo zake, zinapigana vita vizuri. Na wananchi walitoa eneo ambalo lenyewe lilikuwa liko wazi na wao wakabaki na mashamba yao na miji yao maisha yakaendelea. Jeshi likatulia pale likafanya kazi nzuri iliyotukuka na tukafanikiwa kumkimbiza Nduli Iddi Amini nje ya mipaka ya Tanzania, lakini pia na kuwakomboa Waganda. Baada ya miaka baadaye sasa Jeshi limebadilika likawa mwenyeji wale wanachi wamekuwa wahamiaji. Maana yake sasa hivi wananchi ndio wanavamia eneo la jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha kidogo, katika eneo hilo eneo ni kubwa mno na eneo ni pori kubwa mno, wananchi wana mashamba yao na miji yao, lakini hata hiyo miji hawaruhusiwi kuendeleza, huruhusiwi kulima, huruhusiwi kufanya chochote, kwamba ni eneo la jeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikuombe kupitia kiti chako, Serikali ya Wilaya imeandika sana kupeleka suala hili Wizara ya Ulinzi kwa Katibu Mkuu, lakini kitu chochote ambacho kimefanyika mpaka leo. Mimi mwenyewe nimekuja hapa Bungeni nimemuandikia Mheshimiwa Waziri ki-*note* kwamba kule Misenyi, Kyaka, Kyawamara kuna matatizo haya nafikiri kwa sababu ya majukumu yako naomba ulifanyie kazi na nikuombe Mheshimiwa Waziri twende kule ukaone hali mwenyewe kwa sababu hii ni hali ambao inatatulika ukienda mwenyewe pamoja na wasaidizi wako tuweze kuwaokoa wananchi, kutowagombanisha na jeshi letu ambalo linafanya kazi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika suala lingine Wilaya ya Misenyi, kuna eneo ambalo tulikuwa wahanga ambapo mabomu ya Iddi Amini kweli yalikuwa pale na yakabomoa eneo la kanisa, kwa sasa hivi yaliyobaki ni magofu. Tunaishukuru Serikali tukufu ambayo imeweza kujenga Kanisa na wananchi waliendelea na ibada zao katika eneo lingine. Eneo hilo liko kati kati ya Kata ya Kyaka ambayo ni mjini kabisa ambapo sasa kwa sababu lipo katika eneo la mwinuko inaonekana katika kata nzima ambayo ni mjini pale. Sasa mahema hayo yamebakizwa ni magofu ambayo ni vipande vya kuta vya hilo kanisa ambalo lilikuwepo enzi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wakiangalia yale mabaki wanahisi kama vita vinarudi au hatuna mahusiano mazuri na nchi ya Uganda au kuna nini ambacho Serikali isingeweza kutengeneza eneo hilo likawa ni zuri, likawa la kivutio la kumbukumbu nzuri badala yake limekuwa ni magugu yamejaa pale na mwananchi akikosea kidogo akapita katika eneo hilo, hivyo viboko atakavyoambulia siyo vya nchi hii.

Kwa hiyo, mimi niombe sana na niishauri Serikali eneo hilo linaweza kufanyiwa matumizi mawili *either* Jeshi likawekeza sehemu nzuri ya kuweza watu kupumzika pale. Ni *view* nzuri ya Mto Kagera ambayo kila mmoja anauona Mto Kagera kwa kona zake na Daraja la Mto Kagera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama Jeshi haliwezi, linaweza likatoa eneo hilo kwa Serikali ya Wilaya kwa Halmashauri ikawekeza kitu kizuri na wananchi au ikawa ni eneo la *open space* wananchi wakawa wanapumzika pale. *(Makofi)*

Kwa hiyo niombe sana jeshi letu liweze kuangalia masuala haya kwa mapana na hiyo ni sambamba na uwanja wa mashujaa ambao Mwalimu Nyerere alipokea wanajeshi wetu kutoka Uganda baada ya vita. Na eneo hili lipo kati kati ya nji, ni pori, ni nyasi ndefu na hivyo unakuta inaleta taswira mbaya pale maana yake inaonekana ni eneo la jeshi lisilofanyiwa usafi, ni eneo la jeshi lisiloendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niomb jeshi letu pamoja na kuwa na haki yakutunza maeneo yake ya kumbukumbu na kihistoria kwa sababu mahali pale sio sehemu ya vifaa vya kijeshi, kwa mfano; uwanja huo wa mashujaa umeshazungukwa na Halmashauri, umezungukwa na wananchi, unawezekana ukawekezwa katika taswira nzuri, ukaendelea kumilikiwa na jeshi, lakini ukatumia kwa shughuli za Kiserikali kama ambavyo wanatumika. Ni eneo ambalo viongozi wetu wa Kitaifa wakija pale tunafanyia mikutano. Tukiwa na makongamo tunafanyia mikutano pale, lakini kwa kweli ukiuona uwanja huo ni uwanja ambao haupo nadhifu na kwa kweli ukisema kwamba majeshi yetu yalikuja yakapokelewa na Mheshimiwa Amiri Jeshi Mkuu wakati huo inakuwa haileti tija nzuri kwa taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niombe sana, mheshimiwa Waziri pamoja na Wasaidizi wake baada ya kipindi hiki cha Bajeti twende Wilaya ya Misenyi wakakague sehemu ya Byawamara, maeneo ambayo yanaleta changamoto kwa wananchi, wakaangalie lile eneo la kanisa

ambalo limebaki kama kumbukumbu, wakaangalie uwanja wa mashujaa ndani ya Wilaya ya Misenyi, uweze kuwekewa mkakati madhubuti viboreshwe na viweze kuwa ni kumbukumbu njema kwa ajili ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwashukuru Jeshi wanaendelea kufanya kazi, sisi ambao tupo mipakani tunaona mchango mkubwa wanaoufanya na niendelee kumshukuru pia na Mkuu wetu wa Wilaya lakini kimsingi ni tunda la Jeshi ambaye ni Kanali Dennis Mwila ambaye amekuwa ni nguzo kubwa katika eneo letu kuhakikisha ulinzi wa Wilaya ya Misenyi unakuwepo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nipende pia kusema kwamba baadhi ya maeneo kama wachangiaji wengine walivyosema tunahitaji kuwa viongozi ambao wamepitia katika vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanaweza kulindwa vizuri na amani wananchi hao inaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nikushukuru kwa nafasi naunga mkono hoja. Niombe basi Mheshimiwa Waziri baada ya majukumu hayo akaitembelee Wilaya ya Misenyi tuweze kutatua hizo changamoto za wanachi. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Asia Halamga atafuatiwa na Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Kwanza niendelee kuwapongeza kwa sababu wao wamekuwa ni sehemu kubwa ya maandalizi ya vijana weledi na wenye uzalendo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kutumia Randama ya bajeti yao ambayo imegusia mfano

wa kilimo cha mpunga kule Chita mkoani Morogoro. Kilimo hicho cha mpunga ambacho kinafanywa na wenzetu wa JKT wameweza kutumia mwaka 2019/2020 katika bajeti, wametumia fedha shilingi milioni 775 katika kulima kilimo cha mpunga. Lakini matarajio yao watakapouza wanatarajia kuuza kwa shilingi milioni 778. Na ukienda kuangalia faida watakayokuwa wamepata watakuwa wamepata milioni 22 kwa hali ya kawaida ni hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nini mchango wangu; mchango wangu; kwa kutambua kazi kubwa inayofanywa na JKT na hasa vijana wanapopelekwa makambini na kutumia muda mrefu kukaa kambini na baadaye kurudi mitaani, bado kulalamika tatizo la ajira. Mchango wangu ninaiomba Wizara ya Kilimo iweze kushirikiana na JKT kwa maana ya kutoa mbegu pamoja na pembejeo za kilimo ili kuweza kufikia uchumi wa viwanda ule ambao tuanutarajia kwa sababu tayari tuna watu wa uhakika wa uzalishaji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niombe pia kutumia Wizara ya Elimu, kwa maana ya kupeleka mafunzo yanayotolewa *SIDO* pamoja na *VETA* ili tuweze kuwaandaa vijana hawa katika ujasiriamali wa kilimo na waweze wao wenyewe kutengeneza viwanda ili wanapotoka huku nje sasa waweze kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika ninaiomba Wizara ya Viwanda na Biashara kuweza kuingia na kuungana na JKT kwa maana ya haya mazao ambayo tunayaandaa na kuyalima Wizara ya Viwanda ikiangalia hapa Chita tayari wanaenda kupata hasara kwa sababu kwanza hawajapata soko la uhakika. Lakini kama Wizara ya Viwanda na Biashara ikiwatengenezea soko la uhakika watu wa JKT kwa namna ambavyo wanazalisha tutakuwa na uhakika wa moja kwa moja viwanda vyetu kuwa na nafaka na rasilimali ya kutosha na hatimaye kukidhi soko la ndani na baadaye kwenda kwenye soko la nje. Lakini hapa kwenye soko la nje bado nitaiomba Wizara ya Mambo ya Nje kuendelea kutafuta masoko ya uhakika ili baadaye tuweze kupata fedha za

kigeni na hii itatusababishia baada ya vijana hawa kumaliza mafunzo yao kambini basi wasitegemee ajira ya moja ya moja kwenda Jeshi la Wananchi bali tuwe tumezalisha vijana ambao wao wenyewe wakitoka nje watakuwa ni wazalishaji na tunaposema uchumi wa viwanda basi tayari tutakuwa na watu wa uhakika lakini pia tunatengeneza walipa kodi wa baadaye ambao ni wazalendo na wenye tija katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau katika Wizara hizo, Wizara ya TAMISEMI pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia mifuko ya uwezeshaji kijamii ili tunapokuwa tumewaandaa vijana hawa na wameanza kushirikiana na Wizara hizi vijana hawa watapata mikopo ya moja kwa moja. Kwa hiyo, tutakuwa tumewatengeneza watu ambao wakitoka baada ya mafunzo yao miaka mitatu kumaliza Jeshini, basi tunakwenda kuwapa vijana ajira ya moja kwa moja bila kutegemea kuajiriwa tu Jeshini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo hakika suluhisho la ajira litakuwa limepatikana kwa vijana wengi katika nchi yet una hasa vijana wa kizalendo ambao wanatengenezwa na JKT. JKT inafanya kazi kubwa na nzuri sana ya kuwatengeneza vijana lakini bado tunawapa mzigo wa lawama. Wizara hizi zote zikiweza kushirikiana, ni uhakika kwamba Jeshi letu litakuwa linatengeneza vijana wenye tija na hakutakuwa na malalamiko bali tutakuwa na wafanyabiashara na wazalishaji wakubwa wa ndani na nje ya nchi kwa maana ya masoko. Tutakuwa na masoko ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee hapo hapo kwa kutolea mfano. Tunayo Kambi ya Makutupora, hali kadhalika makambi haya yanapoanzishwa yanakuwa ni kwa ajili ya operesheni maalum. Sasa kambi ya Makutupora yenyewe ni kwa ajili ya kilimo cha zabibu na alizeti. Serikali ikiamua kuwekeza vizuri katika kilimo na hasa vijana hawa wanapoingia huko ndani na wanakuwa na tija, tukiwawezesha ni dhahiri kwamba baada ya muda mfupi hatutakuwa na changamoto ya kupata hata mafuta ndani

ya nchi. Tutakuwa na uhakika wa kuzalisha mafuta ndani ya nchi lakini pia kukidhi soko la ndani na hatimaye kwenda kwenye soko la nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyachangia hayo, niendelee kushukuru na sasa niende kwenye maombi; ninaiomba Wizara hii, vijana wanapoingia kambini kuna posho ambayo wanapewa kila mwezi. Posho ile ilipangwa kwa muda mrefu. Kulingana na gharama na mahitaji ya sasa hivi, fedha zile kwa sasa haziwatoshi wale vijana kule makambini. Kwa hiyo, tunaomba Wizara ilibebe hili na ichukue iweze kuongeza fedha za kujikimu ili walau hata wanapotoka waweze kubana fedha na hatimaye wakitoka nje wawe wamejiwekea mtaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue tena nafasi hii kuendelea kuiomba Wizara, vijana hawa wanapomaliza mafunzo, wanapata nafasi mbalimbali za kwenda kuajiriwa na makampuni binafsi, lakini wanapoajiriwa na makampuni binafsi, vijana hawa hawapewi mikataba.

Sasa tuombe Wizara isaidie, ni kweli, vijana hawa wanasaidia na kampuni binafsi kupata ajira, lakini ajira hizo zinakuwa hazina uhakika kwa kuwa hawana mkataba wa kudumu ambao unaweza kuwasababishia wao kwanza kujiamini kazini kwamba ajira moja kwa moja, lakini pia wakishakuwa na mkataba watatusaidia hata kuingiza mapato Serikalini kwa sababu tutakuwa walipa kodi wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo majeshi yetu ambayo kwa muda fulani huwa yanafanya kazi maalum. Mfano, kule Mererani, pale tunavyo vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama na wanapata posho fulani hivi ya kujikimu, lakini kwa wenzetu Jeshi la Polisi wapo eneo moja. Naomba nsivitaje vyombo kwa majina, lakini vyombo vya ulinzi na usalama vinavyolinda katika eneo la Mererani vinapata posho, lakini Jeshi la Polisi askari polisi walioko pale hawapati posho.

Naiomba Serikali ilione basi kwa kuwa hawa wote ni vyombo vya ulinzi na usalama basi wote waweze kupewa posho ya kuweza kujikimu ili wasipate tamaa ya wao kuona ni sehemu hata ya kutorosha hiyo mizigo inapokuwa hapo bali na wao wajisikie ni sehemu ya Jeshi, sehemu ya ulinzi, wote wawe na furaha kuliko hawa wanapewa, hawa hawapewi. Na hii iwe sio tu kwa Mererani, kwa maeneo yote ambapo kuna kazi maalum na vyombo vya ulinzi fulani vinapata posho na vyote viko pamoja basi wote waweze kupewa posho hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa kumalizia, ninaomba bima za wanajeshi na familia zao; wameshatoa fedha lakini bado hawajapatiwa bima zao za afya, Waziri naomba uliangalie hili wapatiwe bima zao kwa wakati. Lakini pia katika bajeti hakujatengwa hela ya tafiti. Tuombe sasa ili Jeshi letu liweze kufanikiwa zaidi tunahitaji fedha ya tafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na kuniachia dakika. Shsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Almas Maige.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nakushukuru sana kuniruhusu nichangie wa mwisho.

Kwanza nianze na pongezi, naipongeza sana Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa lakini pia niwapongeze viongozi wa Jeshi. Nianze na ndugu yangu Jenerali Mabeyo, lakini pia Mnadhimu Mkuu Jenerali Yacoub Mohamed, Makammanda wote wa Jeshi letu. Wamefanya kazi kubwa kuituliza nchi baada ya tukio kubwa hili la kupotelewa na Mheshimiwa Rais Marehemu Magufuli.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, huyu Mnadhimu Mkuu wa Jeshi ni Luteni Jenerali maana nafikiri

nchi inakuwa na Jenerali mmoja halafu wengine wanakuwa ni Majenerali wastaafu.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunisahihisha. Luteni Jerenali Yacoub Mohamed. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo mimi nimejielekeza kwenye malengo ya Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na nianze na lengo la kwanza, kuwa Jeshi dogo lenye ufanisi mkubwa. Jeshi hili litakuwa na ufanisi mkubwa kama litapewa vifaa na zana hasa zana za *EW (electronic warfare).* Vita imeacha kupiganwa sana sana kwa mizinga na bunduki, lakini *electronic warfare* au vita vya elektroniki vinafanya kazi imara. Jeshi letu litakuwa na nguvu sana sana kama litapewa hela za kutosha kununua vifaa na zana hizi za *EW. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye utafiti ambao ni lengo la Wizara lengo la tatu (c ). Hapa ndipo tunapata taabu sana na Jeshi letu, hawana hela za kufanyia utafiti. Jeshi litakuwa la kisasa, usasa ule na weledi utatokana na tafiti ambazo wanazifanya wao wenyewe. Huko tulikopita Jeshi lilitakiwa liandike andiko lipeleke *COSTECH* likasome, ndiko hela zipo, halafu wazipe Jeshi. Andiko la Jeshi ni la siri, haiwezekani raia wasome andiko la Jeshi wafanya maamuzi ya kuwapa hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iweke hela za utafiti wa Jeshi kama kweli tunataka amani ya nchi hii na utendaji wa Jeshi ufanyike. Wapeleke hela Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa au moja kwa moja Ngome. Wafanye utafiti wa silaha, utafiti wa maisha ya watu ili waweze kuwalinda. Utafiti haufanyiki na matokeo yake Jeshi hili haliwezi kuwa dogo likawa na nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niongelee eneo (d) kuimarisha Jeshi la akiba. Jeshi la akiba zamani tulilitita mgambo lilifanya kazi kubwa sana wakati wa vita vya Kagera, mimi nilikuwepo. Jeshi la akiba ni jeshi muhimu sana.

Sasa hivi Wizara haina hela ya kuendeshea au kulifanya Jeshi hili liendelee kuwepo. Mafunzo na mazoezi ya jeshi la akiba ni muhimu sana, hela hakuna. Mimi nashauri Serikali iipe Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Jeshi lenyewe hasa ili waweze kuendeleza uwepo wa jeshi la akiba. Wamelitaja kama ni lengo la tatu katika malengo ya Wizara. Napendekeza, ni muhimu sana jeshi la akiba liendelee kuwa imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la JKT; JKT imefanya kazi kubwa sana ya kuwafanya Watanzania wawe wazalendo. Suala hili naona kama lililegalega huko nyuma mpaka Jeshi lenyewe la JKT likaacha kuchukua vijana. Limeanza kuchukua vijana sasa hivi, lakini hawatoshi. Wafanyakazi, Mawaziri walioko leo madarakani ni watendaji wazuri wa Serikali, wana uzalendo kwa sababu walipita JKT. Katikati hapa vijana walianza kutawanyika bila kueleweka wewe ni Mtanzania au sio Mtanzania kwa sababu hawakuwa na uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa ndicho chombo pekee kinachojenga uzalendo kwa Watanzania. Naomba hela zipelekwe ili watu wanaotakiwa kwenda kupita JKT wapiti, wale wa kwa mujibu wa sheria na wale wa kujitolea. Mimi nasema uzalendo ndiyo chombo muhimu sana. Leo hii tungesema tupigane vita vya Kagera tungepata taabu sana. Mwaka ule wa 1978 wanajeshi wanasimamisha magari wanapeleka *front line,* mstari wa mbele. Leo mtu atasema nilipeni kwanza hela zangu ndipo niwapeni gari langu, uzalendo umepungua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chombo pekee cha uzalendo ni Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Naomba sana Serikali ifikirie kurudisha hela nyingi kwenye chombo hiki ambachi kimetusaidia sana kuleta amani na utulivu nchini. Watu wakiwa wazalendo hawawezi kutoa maneno ya misonge misonge kwa sababu watasema sisi ni Watanzania. Tunasema, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi lendelee. Inaendelea kwa sababu kuna uzalendo rohoni, hawasemi tu mdomoni, kazi iendelee, hapana! Tunasema kwa sababu

tunasema kweli na tumefundishwa na JKT. Kwa hiyo, Jeshi la Kujenga Taifa ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee sasa eneo la mwisho kuhusu *SUMA guard,* wanafanya kazi nzuri sana lakini ni sehemu ya sekta ya ulinzi binafsi, ni wanachama pia wa Chama cha Sekta Ulinzi Binafsi *(TSIA).* Liko tatizo, *SUMA guards* leo wanapewa kazi bila zabuni. Ni sehemu ya kazi za makampuni ya ulinzi binafsi pia, lakini wao wanapewa kazi bila zabuni. Lakini pia wanaomba zabuni kwenye kazi nyingine hizi. Kumekuwa na utata kidogo, kuna kusukumana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya ulinzi binafsi inazimika kwa sababu kazi zote za Serikali ambazo walikuwa wanalinda na wao pia wanapewa JKT, lakini na wao pia ni kampuni za ulinzi. Sasa hivi kumekuwa na mkorogano zaidi, hata Jeshi la Magereza nao wameanzisha, wanaita *SHIMA.* Mkorogano huu unaleta migongano na kuua ufanisi hasa wa sekta ya ulinzi binafsi.

Mimi nashauri *SUMA guards* washiriki zabuni, lakini pia waoneshe kwamba wanafanya kazi kweli sehemu ya ulinzi binafsi. Sasa ilivyo kuna upendeleo mkubwa huu ambao unavuruga mfumo mzima wa sekta ya ulinzi binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Nimemaliza.

**NAIBU SPIKA:** Ameshamaliza muda wake. *(Kicheko/ Makofi)*

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Uzuri wake Mheshimiwa Sophia Mwakagenda anachangia mchana kwa hiyo naamini hicho alichotaka kukisema atapata fursa ya kukisema mchana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa sehemu hii ya kwanza ya Bunge.

Sasa niwataje baadhi ya Wabunge watakaoanza kuchangia mchana ili waweze kujiandaa; Mheshimiwa Juma Mohamed Ali, Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa na wengine tutaendelea kuwataja kadri muda utakavyoenda na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 07:04 Mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Juma Mohamed Ali, atafuatiwa na Mheshimiwa Maulid Saleh Ali, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi tayari nimeshachangia.

**NAIBU SPIKA:** Wewe ni Mheshimiwa Juma Mohamed Ali?

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, jina langu Ali Juma Mohamed, lakini kwenye kishkwambi wanatumia hiyo Juma Mohamed Ali. Niliomba kwenye kishkwambi na nikapeleka jina kwa Katibu pale.

**NAIBU SPIKA:** Sawa, ahsante sana.

Mheshimiwa Maulid Saleh Ali atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda ajiandae.

**MHE. MAULID SALEH ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai, afya njema kuweza kukutana hapa, lakini vilevile niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Welezo kwa kunichagua kwa wingi na kunipa imani kubwa ili niwe mtumishi wao, lakini vilevile nimshukuru sana na kumpongeza Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kutupa matumaini makubwa kabisa kuendeleza yale ambayo yameachwa na Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake wa bajeti yake hii nzuri. Nimpongeze Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, lakini na Makamanda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nianze kwa kuchangia bajeti hii kwanza kwa kuanza na ile dhimay a Wizara. Dhima ya Wizara hii ni kuendeleza juhudi, kulinda

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui na aina yoyote katika ndani na nje ya nchi yetu, lakini vilevile niwapongeze sana jeshi letu kwa kuwa makini na kuonesha umahiri makini katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimeona bajeti yao hii fedha zile ni kidogo. Niiombe Serikali iwaongezee fedha hizi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao, lakini hasa kuweza kupata zana zile za kisasa, kuboresha maslahi yao na makazi. Kama wao wametuahidi kulinda na kuitetea nchi yetu kwa muda wote ule, basi na sisi lazima tuwatetee maslahi yao, ili kuwa na hamu ya kuweza kulinda nchi yetu kwa makini kabisa. Na hii inasababisha nchi yetu kupata maendeleo makubwa. Bila ya jeshi hili kulinda amani na mipaka yake basi hatuwezi kuleta maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitagusa kidogo kuna huduma zile za afya, bahati nzuri na mimi nimebahatika kule katika jimbo langu ninacho Kikosi cha 672 ambacho tuna hospitali, lakini hospitali ile kidogo haiko vizuri ingawa inatoa huduma, lakini niombe Serikali sana ipeleke dawa zile na kuboresha kile kituo maana hakiko katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nimeona na mavazi yao, kidogo; unajua wanafanya kazi ngumu sana, lakini ukiangalia yale mavazi yao kidogo yaani siku zote mimi siku hiyo nakwenda kule, basi tujitahidi kidogo Mheshimiwa Waziri angalau wawe na sare tatu, nne waweze kubadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile nitilie mkazo katika ujenzi na uboreshaji wa Hospitali ya kule Bububu. Ni kweli viongozi wetu endapo itatokea wamepata maradhi kidogo kwa kule kwetu shida, mpaka wasafirishwe waletwe Tanzania Bara. Niombe Serikali iboreshe, hususan Hospitali ile ya Bububu ili viongozi wetu hawa wanapokwenda pale wapate matibabu mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niwapongeze sana vijana wa JKT kwa kupata mafunzo mazuri ili kuweza

kupunguza ule ukali wa maisha na hii niombe Serikali iwape mitaji pale ambapo wanapomaliza tu kule basi wanapokuja uraiani huku wapate nyenzo ili waendelee na maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache niwapongeze sana kwa kuchapa kazi vizuri, kwa bidii, uvumilivu, uzalendo,uadilifu na utii na nidhamu ya hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama mpaka jioni hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kutoa pongezi za dhati kwa Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Tanzania, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Mama Samia Suluhu Hassan, lakini napenda kuwapongeza Wakuu wa Majeshi yetu yote. Napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa inayofanywa ambayo inahakikisha usalama wa nchi yetu, ulinzi wa nchi yetu na pia kushughulikia mambo mbalimbali ya ustawi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli napenda kuwapongeza kwa dhati majeshi yetu haya ya ulinzi, nchi iko salama, mipaka ya nchi yetu iko salama na hii inatokana na umahiri wao, lakini uzalendo wao, kujitoa kwao, kujituma kwao na kuwa waadilifu, wakweli na wasikivu kwa nchi yao na Taifa lao. Nawapongeza pia na majeshi yetu yote nchini Tanzania kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu kwenye Jeshi la Kujenga Taifa; kazi kubwa inafanyika ya kuandaa vijana wetu, lakini na mimi napenda kuishauri Serikali, katika maandalizi yetu haya ya vijana wetu wa Jeshi la Kujenga Taifa tuendelee kuwapa *skills* ambazo zitawasaidia kujiajiri, lakini pia zitasaidia kuongeza kipato chao, lakini kipato cha nchi na uchumi wa nchi. Na Jeshi letu hili la Kujenga Taifa tuhakikishe wanaporudi kwenye mitaa yetu au kwenye maeneo yetu wanatumika vizuri na sio badala yake kutumika vibaya. Tuwape *scheme* au *skills* ambazo zitawafanya watumike vizuri kwa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea jeshi letu la ulinzi limeanza tangu mwaka 1964 na katika miaka hiyo ya 1964 kwa mfano kwa upande wa Zanzibar mwaka 1964 kumekuwa na kambi nyingi za kijeshi ambazo kwa maeneo hayo kwa wakati huo ilikuwa ni porini na wananchi hawajawahi kufika huko, lakini kwa mazingira ya sasa hivi baadhi ya kambi zimezungukwa na raia. Tayari zimezungukwa na maeneo ya wananchi, hata magari, madaladala baadhi ya maeneo yanapita chini ya kambi. Wasiwasi wangu ni kwamba kunaweza kukatokea hatari ya kambi yenyewe au hatari kwa kambi yenyewe au kwa wananchi ambao wako jirani na kambi, apa ndio ushauri wangu unapokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema sasa jeshi letu au Wizara yetu hii ya Ulinzi ikawasiliana na Serikali zetu kubadilisha matumizi ya maeneo yale na kuomba maeneo mapya kwa ajili ya kuzihamisha zile baadhi ya kambi ambazo ni hatarishi kwa maisha ya wananchi, lakini pia ni hatarishi kwa jeshi lenyewe. Na kwa kipindi cha mpito nashauri kuna baadhi ya kambi ukipitia nje unawaona walioko ndani na kinachofanyika ndani. Ni vyema basi tukazungusha uzio angalao ile staha ya ile kambi ipatikane, wakati tunajiandaa na kutafuta mbadala wa kambi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hayo yako kwa maeneo mengi ya nchi yetu, kambi zimezungukwa na maeneo ya rai ana raia wamekuwa jirani na hizo kambi na nyingine ndio wanachunguliwa mpaka ndani wanaona kinachofanyika

ndani. Lile ni jambo hatarishi kwa kambi zetu na usalama wa wanajeshi wenyewe waliomo mle ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwenye mipaka ya nchi, naomba Serikali ilione hili la kuhakikisha tunaongeza fedha ili mipaka sahihi ya nchi yetu iwekwe ili kuepusha mkanganyiko wa kugombaniana mipaka na kuleta taharuki kwa nchi. Sasa tuko salama, lakini miaka inakwenda na mambo yanabadilika na mahitaji yanaongezeka kwa kila nchi kwa hivyo ni vyema tukawekeza pia kuchanganua mipaka yetu kwa usahihi baina ya nchi na nchi, baina ya maeneo na maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea na mimi kuchangia kwamba jeshi letu lipewe nyenzo za kisasa zinazolingana na teknolojia ya kisasa na vijana wetu wanajeshi wapewe mafunzo yanayolingana na hali ya kisasa na mabadiliko mbalimbali ya kidunia yanavyojitokeza katika ulinzi wa nchi, mipaka ya nchi na usalama wenyewe wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulipongeza jeshi let una vikosi vyote vya ulinzi kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhakikisha nchi yetu iko salama, lakini pia nawapongeza yanapotokea majanga, maafa. Kwenye furaha na kwenye shida wanakuwa pamoja na wananchi bega kwa bega kuhakikisha nchi yetu inafanikiwa katika matukio yote likiwemo tukio la juzi tu la tangu kumuaga na kumsindikiza mpendwa wetu, Rais wetu mpendwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye sasa ni Hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Jeshi hili halikulala usiku wala mchana, lilifanya kazi kubwa kuhakikisha kwanza nchi iko salama, wananchi wako salama na mambo yote yanatekelezeka kwa wakati muafaka na hakuna tatizo lolote lililojitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hilo tuwape hongera kwa umahiri wao pamoja na majemadari wao, makamanda wao kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi letu ni tiifu na bila ya utiifu jeshi hili kusingekuwa na amani hii tunayoizungumza hivi sasa, lakini nalipongeza jeshi letu ni tiifu sana, ni wasikivu na naomba wapokee pongezi zangu hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na katika kuwapongeza hivyo na wao tuwaone kwa sababu mcheza kwao hutunzwa. Wanatusaidia, wanatufurahisha, wanatutengenezea mambo yetu na sisi tuwatunze, tuwaone kwa mahitaji yao zikiwemo nyumba bora, mishahara minono, marupurupu mengine ambayo yatawasaidia kustawisha maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba niunge mkono hoja, nakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana na mimi kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu. Mimi nitazungumzia suala la hati za kambi za jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyojua mimi kwa uzoefu mdogo kwa sababu nilikuwa mtoto wa *quarter* ninajua kambi nyingi za jeshi zilianza kuwepo, lakini kwa kutokuwa na hati za kumiliki ile ardhi watu wanaingia, mwisho wa siku inaonekana kwamba, jeshi limewavamia wananchi au wananchi wamelivamia jeshi.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa ninaomba Serikali iweze kujipanga na ninajua pale jeshini kuna wasomi waliosomea wanaweza kujipimia wenyewe bila kutegemea Wizara ya Ardhi, mambo mengine yakafanywa baadaye, lakini angalau wakajipimia wakajua maeneo yao ni yapi wanayoyamiliki, ili iweze kuondoa migogoro mbalimbali ambayo inaonea majeshi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba jeshi siku zote lilikuwa linakaa mbali na wananchi na linakuwa na *square meter* nyingi, lina *square meter* nyingi kwa ajili ya kumiliki lile eneo, lakini usipopima mtu akaja akajenga mwisho wa siku mwenye hati ndio mwenye mali. Hivyo basi, tunaomba Wizara na ninajua Mheshimiwa Kwandikwa kwa kuja kwako unaweza ukahahakikisha mnapata fedha za kupima kambi za jeshi nchi nzima na kuweza ku--*identify* maeneo yenu kwa usalama zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia wanawake katika jeshi, leo hii Mheshimiwa Waziri ametuletea Majenerali tumewaona tunashukuru, lakini bado tuna haja ya kuongezewa vyeo kwa wanawake zaidi jeshini, hasa kada za chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua wanawake wanaweza, sasa katika wote hatujajua ni wangapi, hatuna *statistics* kama Bunge tulioletewa kwamba wanawake wangapi ambao wana vyeo hivyo. Sawa leo wamekuja majenerali tunawapongeza na tumeyasema haya mwaka jana na mwaka juzi na miaka iliyopita, lakini bado kada ya masajenti na kuendelea mpaka makapteni waongezeke zaidi wanawake ili waweze kuongezewa vyeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia nyumba za askari; nimesema mimi nimezaliwa kambini; kiukweli kwa mfano *flats* za pale Keko njia panda ya kwenda uwanja wa Taifa tumehamia pale mwaka 1973, lakini mpaka leo hii maghorofa yale hayajawahi kupakwa rangi. Tunaomba tafadhali Mheshimiwa Kwandikwa pamoja na kwamba, maghorofa mengi yamejengwa kwa ajili ya askari, tunaomba ukarabati wa nyumba za askari uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini si tu hivyo, bado askari wa *rank* za chini wanaishi uraiani. Unapokuwa na wanajeshi wanaokaa uraiani kunakuwa hakuna udhibiti wa wale askari kwa sababu hawa watu wanaweza wakaitwa wakati wowote kwa ajili ya kwenda kufanya kazi yoyote kwa muda wowote. Anapokuwa na mama mwenye nyumba mwenye

funguo za geti anakaa nazo chumbani, hii si sawa tunaomba jeshi lijenge nyumba zaidi hasa kwa askari wadogo waweze kupata makazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazungumzia habari za upandishwaji wa v eo nimeshalisema, lakini mwisho wa siku ajira kwa wanajeshi. Tumeona Kamati ya Nje, Ulizni na Usalama (NUU) imezungumza hapa kwamba kuna upungufu wa wafanyakazi jeshini, tunaomba sana ikama inayosimamia wafanyakazi jeshini waweze kuajiriwa. Na tunao vijana wa JKT wengi ambao wamemaliza JKT, kama ni kigezo cha kwenda jeshini basi wachukuliwe vijana wetu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiondoka kwenye jeshi nikaingia kwenye JKT. Leo hii JKT ina vijana wengi sana walinzi, ametoka kuongea Mbunge mchana wa leo kwamba JKT haifanyi *tender,* mimi sikubalini. Ninaamini katika JKT kupewa malindo mbalimbali katika Taifa hili, tunaogopa sana kuwa na walinzi kwenye benki, kuwa na walinzi kwenye kampuni za kiserikali na mashirika ya umma kutoka nje ya kampuni binafsi. Tunatamani JKT iajiri vijana wengi zaidi kwenye kampuni hizi, lakini shida kubwa iliyopo kwa JKT wanawalipa mshahara mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wewe mwenyekwe ukiwa unaelekea Mbeya ukipita pale kwenye Bwawa letu la hapo Mtera utakuta vijana kwenye mazingira magumu, mishahara wanayoipata ni midogo. Tunaomba sana kwa sababu unapokwenda kumnunua mlinzi kwenye kampuni unaweza ukawa unapewa laki tano kwa askari mmoja, lakini wale vijana mshahara wanaoupata ni chini ya shilingi 200,000 tunaomba muwaongezee mishahara kusudi wafanye kazi kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia JKT hao hao wenzetu sasa wanafanya mambo mengi ikiwemo mambo ya maji kuna mmoja amasema wafanya mambo makubwa zaidi, lakini sio vibaya kuanza na madogo ili uende kwenye makubwa.

Mimi ninashauri mradi wa maji kutoka JKT mashirika yote ya umma, Wabunge na maeneo mengine yote yanayohusiana na Serikali tusitumie maji ya mashirika ya watu binafsi, tulazimishe tutumie maji ya JKT kama kuwasaidia wala msishituke kwa sababu tunataka kuisaidia JKT ili iweze kutoa ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuelezea suala la Kiwanda cha Nyumbu; wenzangu wengi wameelezea na mimi ninaamini kuna fedha nyingi wamekwisha kupata tunaposema Tanzania ya viwanda tunataka Jeshi letu kwa sababu wao wana dhamana kabwa kwetu tuwekeze fedha nyingi kwao waweze kuzalisha. Nyumbu kama walivyosema waliotangulia ni sehemu ambayo ingekuwa mfano, waliwahi kutengeneza gari, wanatengeneza magari ya zimamoto, tuwekeze fedha ili waweze kutuzalishia zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo siungi hoja, nasisitiza fedha ziongezewe na zile zilizopangwa ziweze kuwafikia wahusika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani nilifafanua hoja ya Majenerali asubuhi sina haja ya kuirejea tena. Jenerali nchini anakuwa ni mmoja tu halafu ukisikia Jenerali mwingine maana yake amestaafu kwa hiyo hawa waliopo hapa ni Mabrigedia Jenerali, Luteni Jenerali, Meja Jenerali ndio vyeo vyao, hawa waliopo hapa hakuna Jenerali, Jenerali leo hayupo jamani. Jenerali ni Venance Mabeyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, Mheshimiwa Hassan Mtenga ajiandae.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nipate kuchangia mawazo yangu na mawazo ya wananchi wa Jimbo la Chakechake kwenye Wizara hii ya Ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kuwa Amiri Jeshi Mkuu wa kwanza mwanamke wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri ambayo ametuelezea dira na mwelekeo wa Wizara yake katika mwaka wa fedha 2021/2022 nimpongeze sana kwa kazi iliyotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo sipo vizuri sana kiafya, kifua kidogo na homa homa kwa hiyo utanivumilia, nilipanga kusema mengi lakini inawezekana katokana na hiyo hali nikapunguza kidogo yale ya kusema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sisi tunaotoka kwenye majimbo ya visiwani Zanzibar tukisema ile dhana ya *local content* kwa mfano kwenye maeneo ambayo Mungu amewabariki kuwa na migodi inaweza isiwe inafahamika vizuri kwenye akili za wengi wanaotoka kwenye visiwa. Kwa sababu sisi hatujabarikiwa kupata maeneo ambayo yana uchimbaji wa dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi tumebarikiwa kupata maeneo mengi ambayo yamezungukwa na Kambi za Jeshi, kwa hiyo, ile dhana ya *local content* inaweza ikatumika *mutatis mutandis* kutoka kwenye dhana ya wenzetu ambao Mungu amewabariki kupata migodi na sisi ambao tumezungukwa na kambi za Jeshi. Dhana ya *local content* kwenye kambi za Jeshi ni vile tunavyoweza kutumia uwepo wa kambi za Jeshi kwenye maeneo yetu kama fursa. Kambi za Jeshi zikiwepo kwenye maeneo yetu kwenye majimbo yetu maana yake hiyo ni fursa ya wewe kupata Kituo cha Afya ambacho kitajengwe ndani Kambi ya Jeshi, kupata shule ambazo zinajengwa ndani ya kambi za jeshi na huduma za kijamii nyingine, kwa mfano, mimi kwenye Jimbo langu sina Kambi ya Jeshi lakini jirani yangu Jimbo la Wawi wao wanazo kambi za jeshi zaidi ya moja, ipo hospitali katika Kambi ya Jeshi ya *Ali Khamis Camp* ambayo imekuwa ina

msaada mkubwa kwa wananchi wa Wawi na wananchi wa Chakechake, maana yake nje na zaidi ya Jimbo ambapo kambi ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali imekuwa ikihudumia watu, raia wengi wamekuwa wakienda kwenye hospitali hizo kupata huduma, kwa hiyo rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri ni kwamba hizi hospitali zinatakiwa zipewe uwezo kwasababu sasa zimekuwa ni sawa sawa na hospitali za kiraia kwa jinsi zinavyohudumia hata wasiokuwa wanajeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya nzima ya Chakechake sisi tumebahatika kuwa na hospitali moja ya Wilaya ambayo ndio ina sehemu za kuhifadhia maiti/ majokofu ya kuhifadhia maiti. Ushauri wangu ni kwamba tunaomba kuongezewa uwezo kwa hospitali ya Jeshi iliyoko kwenye kambi ya *Ali Khamis Camp* ili iwe na uwezo wa hifadhi maiti, kwa sababu Hospitali ya Chakechake haitoshi inakuwa inamezwa na mzigo, inabebeshwa mzigo mkubwa wa kuhifadhi maiti jambo ambalo halina uwezo huo. Kwa hiyo mbadala ni kuiwezesha kambi ili hospitali iliyopo kwenye *Ali Khamis Camp* ili liwe na Mortuary ambayo itasaidia hii Hospitali ya Chakechake kubwa ya Wilaya pale inapotokea mahitaji maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nilitaka kuchangia ni suala la uwekezaji wa jeshi kwenye tafiti za kisayansi, hili limesemwa sana jirani yangu *Engineer* kalisema, Mzee wangu Mheshimiwa Maige kalisema na Wabunge wengi waliochangia mwanzo wamelisema kwa msisitizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo sasa yameshakwenda mbele zaidi kwenye maendeleo ya kisayansi na teknolojia huko duniani ni uwekezaji na utumiaji wa sayansi kwenye majeshi; *in terms* ya silaha, *in terms* ya mbinu za kupigana, hizo *drones* tunazoziona (ndege zisizo na rubani) zimegundulika kutokana na vyuo vya kitafiti vya kijeshi. Kwa hiyo na mimi nataka niweke msisitizo hapa, dunia haipo

tena tulipo sisi, watu walishakwenda mbele zaidi, leo watu wanateknolojia za kuzuia makombora kabla ya kufika maeneo yao yakiwa yamelengwa kuelekea kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wana *launch rocket* za kijeshi, kwa hiyo hatuwezi kufika huko kama hatujawekeza fedha nyingi kwenye maabara za kijeshi za kuweza kufanya tafiti za kisasa ili na wao jeshi letu tulipe uwezo wa kufanya ugunduzi wa silaha mpya na teknolojia mpya za kjeshi ambazo zitalipa uwezo jeshi letu kwenye kulinda mipaka na kufanya ile kazi waliyopewa kikatiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka 2000-2005 wakati tunamaliza *form four* kulikuja ile dhana ya mapinduzi ya wasomi ndani ya jeshi, tulikuwa tunashawishiwa kwa sababu mimi wakati ninamaliza muda huo nilikuwa ninasoma shule ya jeshi, kwa hiyo, tulikuwa tunashawishiwa tuingie jeshi tulikuwa tukiambiwa kuna mapinduzi ya kwamba jeshi sasa linataka wasomi kwa hiyo ili hao wasomi wawe na faida ambazo sasa hivi wapo wengi ndani ya jeshi ni wengi wengi wengi wapo, ili wawe na faida ni lazima tuwekeze kwenye maabara za kisasa za kisayansi zitakazowasaidia wasomi wetu kutumia elimu zao ili kulisaidia jeshi letu la ulinzi na usalama kutulinda kisayansi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu pia ambalo nilitaka kulisema ni kuhusiana na suala la ajira; juzi kulikuwa kuna kikao cha kiutendaji baina ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mheshimiwa Mchengerwa kilifanyika Zanzibar tarehe 12 Mei, 2021; moja katika vitu walivyovijadili ilikuwa ni nafasi sawa za ajira katika vyombo vya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi ni chombo cha Muungano, kwa hiyo, zinapotoka nafasi za ajira utaratibu tunatakiwa Zanzibar wapewe asilimia 21 ya nafasi hizo za ajira. Kwa hiyo ninasisitiza na hili Mheshimiwa Waziri alichukue na alifanyie kazi zinapotoka nafasi za ajira tunao vijana wengi mimi ndani ya Jimbo langu Chakechake wapo vijana wengi

wasomi wamemaliza *degree*, wamemaliza *form six,* wamemaliza *form four,* wapo mtaani na wao wanahitaji hizo ajira zikiwa zinatoka itazamwe Zanzibar kwenye hiyo asilimia 21 ili na sisi tupate nafasi ya kuwa sehemu ya Jeshi la Ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema chochote kuhusiana na yale maelezo ambayo uliyasema pale maana yake yale maelezo yalijitosheleza kuhusiana na dada yangu Mheshimiwa Jenista alipotoa utaratibu wa Kanuni ya 71 wa Kanuni za Kudumu za Bunge pamoja na Ibara ya 34 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini cha kushangaza mtu anashangaa kwa nini mwanajeshi anakwenda kwa Mkuu wa Mkoa, lakini mtu hashangai kwa nini mwanajeshi ni daktari anatibu raia wake wenye jamii. Unaogopa mwanajeshi akiwa Mkuu wa Mkoa tu na magwanda...

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramandan kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**T A A R I F A**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumpa taarifa Mheshimiwa Ramadhan kwamba kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 63(2) na (3) imetoa mamlaka kwa Bunge kuishauri na kuisimamia Serikali na vyombo vyake. Kwa hiyo, pale nillikuwa ninatimiza wajibu wangu wa kuishauri Serikali kwa mujibu wa Katiba kama Mbunge. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, humu ndani humu, Kanuni zetu ziwe zinatuongoza vizuri. Nilitoa mwongozo kuhusu utaratibu ulioombwa na Mheshimiwa Jenista na sasa amesimama Mheshimiwa Esther Matiko akieleza kwamba yeye alifanya jukumu lake, nadhani nilieleza kwa kirefu kabisa kwamba Rais hafungwi na ushauri unaotolewa, kwa hiyo

wewe umefanya kazi yako na yeye anachangia vile aonavyo bora kama wewe ulivyofanya ya kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan malizia mchango wako.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naendelea, ni kwamba wanajeshi hawa hawa ndio madaktari wetu kwenye hizo jamii zetu na magwanda yao wanatutibu na wala hatuwaogopi, ni walimu mimi kwenye Jimbo langu wapo wanajeshi ni walimu mpaka wa madrasa. Kwa hiyo wamefanya urafiki na jamii kiasi kwamba wao kwa sababu ni ndugu zetu, hao hao wanajeshi baadaye wanarudi kwa sababu ni baba au ni mjomba unamuogopaje mjomba! Hiyo ndio ambayo nilitaka nichangie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nilitaka kuishia hapo, ahsante sana kwa kupata hii fursa na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Mtenga, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate ajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi pia nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi na nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa Ulinzi kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo machache ya kuchangia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Biharamulo nadhani taarifa zangu nilishakaa na Waziri pia lakini ningeomba jambo hili niliweke sawa kwa ajili ya *records* na kwa ajli ya wale ambao wamenituma, maana nilikuwa Jimboni juzi na jana kelele kubwa ni kwa ajili ya mgogoro wa muda mrefu kati ya Kikosi cha 23KJ na wananchi wa Kata ya Nyarubungo katika Vijiji vya Rusabya na Kata ya Ruziba vile

vile katika vijiji vya Ruziba lakini na kata ya Biharamulo mjini sehemu ya ng'ambo Lukoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 1984 wakati kambi ya jeshi inaletwa pale Biharamulo tayari wananchi walikuwa wanaishi katika vijiji hivi na ikafanyika tathmini, ilipofanyika tathmini wananchi wakaamuliwa wasifanye maendelezo yoyote yale kwa sababu tayari ilikuwa ni sehemu ambayo imetengwa kwa ajili ya kufanya mazoezi ya kikosi cha 23KJ na hivyo wananchi wakabaki *stranded* kwa sababu hawakutakiwa kuendeleza nyumba wala kulima au kufanya chochote kile. Lakini tangu mwaka 1984 wananchi wale hawakulipwa wala hawakufikiwa chochote kile. Kwa hiyo ninavyosimama kuongea ni miaka 37 tangu wakati ule, wanachi wamekuwa katika sintofahamu ya muda mrefu na zaidi wakiendelea kuilaumu Serikali kwa kitu hiki ambacho kilifanyika, lakini pia mwaka 1998 iliundwa kamati nyingine ndogo iliyohusika viongozi wa kijiji, ilihusisha viongozi wa Wilaya pale, Afisa Ardhi na watu wengine wakapitia tena upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninasema sio mgogoro ila ni changamoto ambayo imekuwepo kwasababu hata jeshi lenyewe ambalo limechukua eneo lile ni eneo ambalo lipo ndani *perimeter* ya kilometa tano kutoka katikati ya mji wa Biharamulo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hata jeshi lenyewe ni kwamba haliwezi kutumia eneo lile ambalo limetengwa kwa sababu ni eneo ambalo lilitengwa kwa ajili ya kufanyia mazoezi, lakini kwa sababu wananchi wale hawakulipwa inaonekana sio mali halali ya jeshi kwa sababu jeshi haliwezi kusema kwamba ni male yake kwa sababu bado halijawalipa wananchi, lakini wananchi waliamuliwa wasiendelee kufanya kazi yoyote. Kwa hiyo kumekuwa na mvutano mdogo mdogo ambao unaendelea. Wananchi wale wanachoka kwasababu sasa ni eneo la mjini unapomtoa pale na ukampeleka sehemu nyingine ni kwamba wamekosa sehemu za kufanyika kazi, maana hata maeneo yale ambayo ilibidi wakimbilie wamekimbilia kwenye

kata moja ya Nyamahanga eneo moja linaitwa Kibale lakini hata kule walipo bado ni maeneo ambayo wameenda na kuwakuta watu wengine kwa hiyo wameenda kuanzisha mgogoro na watu wengine tena pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilichokuwa naomba kipindi Waziri ana-*wind up* tuje na majibu sasa tujue wananchi hawa ambao wamekaa kwa miaka 37 wakisubiria kujua hatima yao ni nini kinaendelea, maana kabla ya mimi kuingia Bungeni niliambiwa kwamba mwaka jana kuna Tume ziliundwa na Mawaziri nadhani wakazunguka kupitia maeneo ambayo yalikuwa na migogoro, lakini kwa Biharamulo hawakufika na maswali ambayo nimekumbana nayo sana na wananchi wale bado wanalalamika kwasababu wanasikia watu walienda sehemu nyingine Biharamulo hawakufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa ninaomba Serikali itupe majibu ya kina na ya ufasaha ili wakazi hao ambao wameachia maeneo yao, maeneo ya Rubasya, maeneo ya Ruziba, maeneo ya Ng'ambo ili wajue hatma yao ni nini *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hata jeshi nalo pia haliwezi kuyatumia maeneo yale kwasababu kuna kipindi katika kufanya *range* walipiga risasi wakati wanajeshi wanafanya majaribio pale wananchi wakaja kuokota maganda wakaleta *complain* nyingi sana kwamba ni kama vile wameshambuliwa na nini.

Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba hili jambo liangaliwe kwa sababu ninachoelewa kazi kubwa ambalo jeshi linayo pale ni kazi ya kuhamasisha, kuelimisha wananchi juu ya masuala ya ulinzi wa nchi yetu ili waweze kushiriki katika kulinda mipaka ile na mkizingatia sisi tupo mipakani kule.

Sasa wananchi wale ambao inabidi muwaelimishe na watusaidie kulinda mipaka ile, wanapokuwa wana-*feel* kwamba kama wameonewa au wamedhulumiwa eneo lao sidhani kama watakuwa walinzi wazuri wa mipaka kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyote ni mashahidi kwamba sisi ambao tupo maeneo yale wenzetu wa nchi jirani wakati mwingine wanaingia na ndio hao wanatumika, lakini mlinzi wa kwanza ambae anawatambua wale kabla ya Serikali au vyombo vya ulinzi na usalama mlinzi wa kwanza lazima awe mwananchi. Kwa hiyo kama mwananchi ameshirikishwa vizuri ataweza kutusaidia kulinda maeneo yetu ya mpakani kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilichokuwa ninaomba mimi sina maneno mengi sana kwa ajili ya ku-*save* muda lillilonisimamisha hapa kwenye Wizara hii ni hilo moja ya kwamba sasa tupate majibu ya uhakika ya Serikali mkwamo huu wa tangu mwaka 1984 ambao ume-*consume* miaka 37 leo tunaumalizaje ndani ya Bunge hili iliwananchi hawa wa Biharamulo waweze kupata haki yao na hatimaye jeshi pia liweze kuwa *free* kuyatumia maeneo yale kwa ajili ya kufanyia mazoezi wanajeshi. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Ameshamalizia kuchangia.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Mtenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba ajiandae.

**MHE. HASSAN S. MTENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nijumuike na wenzangu kumshukuru Amiri Jeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama yetu Samia Suluhu. Lakini pia nichukue fursa nayo kumshukuru Waziri wa Ulinzi, kwa kweli nina kila sababu ya kuzungumza na Waziri wa Ulinzi jinsi anavyojiweka kwetu, tunavyozungumza naye na ni Waziri

ambaye yupo tayari kuzungumza na kila Mbunge mmoja wapo iwe nje au ndani, kwa kweli ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze kwenye masuala ya barabara ya ulinzi. Katika mipaka yetu inawezekana tukazungumza suala la ulinzi kiujumla, lakini suala la ulinzi kama hatujalipa kipaumbele inawezekana majeshi yetu tukawapa kazi kubwa sana kwenye ulinzi. Mfano nataka nizungumzie mpaka wa Mtwara na Msumbiji tuna barabara hapa ya ulinzi ya kilometa 300; unatoka Mtwara hadi Tunduru. Barabara hii kwa hali jinsi ilivyo haiwezi kupitika kwa urahisi iwapo litatokea janga lolote la kitaifa au la uvamizi hawa wanajeshi wetu hawawezi kufika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu nadhani Waziri wa Ulinzi wafanye mazungumzo na Waziri wa Ujenzi barabara ile ya ulinzi ambayo iko madhubuti kabisa kwa ajili ya ulinzi wa mpaka wa kusini iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wamezungumza sana kuhusu migogoro ya ardhi, kuhusu makambi ya majeshi yetu; kule kwangu ni sehemu pale Mtwara ni sehemu ya waathirika wa makambi hayo. Ukienda kwenye Kata ya Ufukoni ina watu takribani zaidi ya 12,000 lakini katika kata hiyo watu 12,000 kuna watu zaidi ya 4,000 wana mgogoro na Kambi ya Jeshi, na hili ni lazima nilizungumze kwa sababu kwenye mgogoro ule utawakuta wanajeshi/makamanda wako wana viwanja na wamejenga nyumba za kisasa. Kwa hiyo, rai yangu nataka nizungumze kwamba niombe muda wa bajeti hii ikishaisha tumemaliza hili Bunge ikimpendeza Waziri twende tukatatue mgogoro ule haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima tunaozungumza vijana wetu wa JKT; wenzangu wamezungumza sana, vijana hawa wa JKT tumekuwa tunawapa mafunzo na mafunzo haya wanayopewa ni mafunzo ya kijeshi. Lakini nataka nitoe angalizo kwa Serikali,

vijana hawa tunapokwenda kuwapa mafunzo ya kijeshi na baadaye tukaendelea kuwaacha *idle* nje, iko siku hawa watabadilika sasa kuwa watu wabaya ndani ya Serikali yao. Kwa sababu tayari tumewapa mafunzo, lakini tunashindwa sasa kuwatumia kimafunzo sahihi.

Nashauri wenzangu wamezungumza sana kuhusu viwanda, lakini wenzangu wamezungumza kuhusu *activity* nyingi kuhusu vijana hawa. Kama ikikupendeza na Serikali ikiipendeza naomba vijana hawa sasa waandaliwe shughuli mahususi wanapotoka kwenye mafunzo ya jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili la ulinzi tukirudi nyuma kwenye historia ya nchi yetu tumepigana vita kule na Uganda, lakini wakati tunapigana vita na Uganda tulifika mahala tukaathirika kama Watanzania na Jeshi letu. Baada ya daraja letu ambalo tulikuwa tuna daraja pale Kagera halikuwa na uwezo wa kuwa na daraja kama daraja. Haya nayazungumza kwenye historia hii, natoa mfano sasa tunazungumza Mtwara na Msumbiji na nimekuwa nikizungumza sana Bunge hili, lakini nimekuwa naishauri sana Serikali juu ya kujenga daraja baina ya Msumbiji na Mtwara kwa pale ambapo tunasema barabara yetu ya ulinzi ya mpaka ule ndiyo inapoanzia basi twendeni sasa tujenge daraja ili jambo lolote litakalotokea kuwepo na unafuu wa kuweza kuboresha jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niendelee kulipongeza Jeshi hili, nalipongeza Jeshi katika nchi zetu za Kiafrika ni jeshi la kwanza ambalo halijayumba na hili lazima tukubaliane kwamba tayari tuna majemedari ambao wamefika mahali wamegeuka kuwa wazalendo ndani ya nchi yao. Lakini ukiangalia kwenye nafasi zao na maudhui jinsi wanavyoishi pale kwangu Mtwara tunazo nyumba za wanajeshi nyumba zile zilijengwa takribani miaka ya 1980.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyumba zile ukienda kuziona siku ya leo na ukaangalia ukaona kwamba nyumba hizi wanakaa wanajeshi wetu, ni aibu kubwa sana. Niiombe na Serikali twendeni tukazikarabati zile nyumba kwa sababu

ufanisi wa jeshi letu, ufanisi wa wafanyakazi wetu lazima wafike mahala wajue yale maudhui wanayoishi kwenye Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nazungumzia wanajeshi kukaa nje ya makambi; mimi nataka niishauri Serikali hawa wenzetu wanafanya mazoezi mazito sana na kwa bahati nzuri asilimia kama 20 ya mazoezi hayo mimi nayafahamu. Lakini wanapojumuika na wananchi ndiyo tunasema hawa ni rafiki sawa na wananchi lakini yako mambo ya msingi ambayo wanajeshi kama wanajeshi kwenye taaluma yao haitakiwi kujichanganya na wananchi. *(Makofi)*

Sasa hili natoa angalizo kwa Serikali leo tumeona maeneo mengi nasikia jeshi wamempiga mwananchi huko, jeshi wamempiga siyo kwamba wanakusudia kufanya vile kwasababu hawa wanajeshi huwezi kumpeleka jeshi aende akalinde benki siyo kazi yake na siku utakayomchukua mwanajeshi kwenda kulinda benki, inawezekana maudhui ya yeye na mteja yakawa ni mambo mawili tofauti. Kwa sababu siyo kitu ambacho wamesomea au wamejifundisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi niiombe Serikali twendeni sasa tuwajengee mazingira ya kuishi kwenye makambi na wale maafisa ambao tunasema maafisa wetu hawakai kwenye makambi wanakaa uraiani, tutengeneze sasa nyumba za kisasa kwa ajili ya kukaa hawa wanajeshi wetu. Suala hili la ujenzi wa nyumba halikuanza jana wala juzi, kwa kumbukumbu zangu kabla sijaingia Bunge hili, lakini mabunge yaliyopita Wabunge wengine walizungumza sana kuhusu ujenzi wa nyumba za wanajeshi. Kwa hiyo na mimi niungane na wenzangu nikuombe Naibu Spika na Serikali kwa ujumla hebu twende sasa tuwaangalie wanajeshi wetu haswa kwenye makazi salama ambayo wanaishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wanajeshi wetu wanafanyakazi kubwa sana na kama Serikali itafika mahala tukatenga bajeti leo tunazungumza kuhusu vijana hawa wanaotoka JKT, wanafanya shughuli gani tunawaacha *idle,*

kama tumeweza kupeleka fedha tukatunga sheria, tukasema sasa tunatoa asilimia 10 kwa ajili ya wajasiriamali kwenye manispaa zetu, kwanini Serikali sasa isijiwekeze tukasema sasa tunaamua sasa tutengeneze kiwanda kimoja kikubwa ndani ya nchi yetu tutafute wabia, lakini hawa vijana wetu kwa sababu wengi wanakuwa wataalam kutoka huko jeshini waende wakafanye kazi kwenye viwanda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii rai naitoa kwasababu hawa vijana wako wengi sana na kila muda tunapowachukua kuwapeleka kule Jeshini kwenye mafunzo *reaction* yake inakuwa kubwa ya ukomavu wale vijana. Lakini kwenye ukomavu wao hatuwajengei *sympathy* ya kurudi kule kwenye maeneo wakawa wana uwezo wa kujitegemea. Tutengeneza mazingira, kama tumeelemewa basi twende na njia mbadala sasa ya kufika mahali tukasema sasa vijana wetu hawa tunawatafutia *activity* yoyote ile ambayo inawezekana wakaweza kuishi na kufanya shughuli zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru na niunge mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi na mimi kuchangia Wizara hii muhimu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa nguvu kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Kyerwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya lakini pia nimpongeze kwa unyenyekevu ambao kwa kweli amekuwa akiuonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni Wizara ambayo ni muhimu mimi naweza nikasema ndiyo moyo wa nchi, ni

Wizara ambayo imetuletea heshima kubwa ndani na nje ya nchi kwa kweli Jeshi letu linasifika sana na ninawapongeza na niseme moyo huo wa kujitolea kuhakikisha Taifa linakuwa salama, uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo machache ambayo mimi nitashauri; kwa upande wangu mimi ninapakana na nchi ya Rwanda na Uganda, mipaka yetu iko salama, lakini nilikuwa ninaomba kuna Kata ya Kitwechenkula pale kuna mambo ambayo yanafanyika kwenye mpaka wetu kwa raia wetu siyo mambo mazuri. Niliombe Jeshi letu liangalie na ikiwezekana pale hatapawepo na kambi itapendeza kwa sababu wenzetu upande wa pili wao wana kambi na sisi tukiweka pale kambi nafikiri tutaheshimiana vizuri. Kwa hiyo niombe sana Serikali na Wizara hii iliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ambalo mimi nilete pale kwenye Kata ya Kaisho kuna kambi isiyo rasmi, ile kambi iko katikati ya raia na unajua raia hawajazoea kuona majeshi kama hakuna ulazima wa ile kambi kuwepo pale iko barabarani kwanza hata kwa wanajeshi wetu inaweza wasiwe salama kwa sababu wako katikati ya wananchi hakuna uzio ni barabarani kwahiyo niombe sana Wizara iliangalie kama hakuna ulazima wa kambi ile kuwepo pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine Jeshi letu limefanyakazi kubwa sana na mkiona Taifa hili liko salama ni kwa sababu ya kazi nzuri inayofanywa na Jeshi letu sasa mimi nilikuwa ninaomba wakati mwingine wameeleza hapa ukiangalia nyumba za askari wetu kwa kweli unajiuliza hawa watu wanaosababisha Taifa liwe salama leo hii tuko hapa tumetulia kwasababu ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama mipaka yetu iko salama. Nchi nyingine hawawezi wakakutana namna hii hebu tuangalie namna gani tunaweza tukaboresha makazi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi nimekuja na hoja nyingine ikiwezekana hawa wanajeshi wanapostaafu wawe

na bima ya maisha, kwa sababu tumeshawatumikisha wamechoka wanapostaafu hata hawana uwezo tena hawana nguvu kwa sababu nguvu kubwa wameiwekeza huku kupigana na kuhakikisha mataifa mengine yanakuwa salama.

Kwa hiyo, tuhakikishe tunawapa bima ya maisha kama zawadi kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya. Kwa hiyo hilo ndilo ombi langu ambalo nimelileta kwenu na Waziri aliangalie pamoja na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, atafatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Taska Mbogo ajiandae.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ambayo ndiyo inachukua moyo wa nchi kwa maana ya usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameweza kutujaalia wote angalau kufikia siku ya leo na kuweza kushiriki kwenye mjadala huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu nimpongeze Mheshimiwa Waziri, unaweza ukamuona yuko kimya, lakini anapeleka mambo yake vizuri. Mheshimiwa Waziri hongera sana kwa kazi kubwa unayoifanya. Lakini kupitia Wizara hii Serikali yetu inafanya kazi kubwa ambayo inahakikisha kwamba mipaka iko salama na sisi tuko salama na wananchi wanafanya shughuli zao. Mheshimiwa Waziri na Serikali yote hongereni sana kwa kuhakikisha kwamba mipaka yetu iko salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji hawa wanafanyakazi kubwa na nikichukua mfano Mkoa wa

Kigoma, unapakana na nchi nyingi ikiwemo Kongo, Burundi, Rwanda, Na kadhalika, mpaka ni mkubwa na kwa maana ile inahitajika kuwe na doria ya hapa na pale. Lakini watu hawa maafisa hawa maaskari wetu hawana vitendea kazi hasa magari. Niombe wapatiwe magari kwa sababu kutokana na kwamba mfano kwa mpaka wetu wa Kigoma maana yake kuna muingiliano wa watu wa kutoka nchi mbalimbali kuna wanaoingia wanaotoka maana yake inahitajika ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha kwamba mpaka uko salama, lakini hawana vyombo hawana magari niombe sana katika bajeti hii Mheshimiwa Waziri uhakikishe kwamba hawa watendaji, hawa maaskari wanapata magari kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanafanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vipo vikosi mbalimbali ambavyo vimeteuliwa na Jeshi letu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mipaka iko salama katika Wilaya yetu ya Kakonko uko mpaka katika Kijiji cha Rumashi, upo mpaka katika Kijiji cha Nyakayenzi, kipo kikosi katika Kijiji cha Kabingo, kipo kikosi katika Kijiji cha Nyagwijima na kipo kikosi katika Kijiji cha Kakonko. Kote huko kama ambavyo wenzangu wamezungumza maaskari hawa hawana majengo, hawana nyumba za kuishi badala yake wanaishi kwenye nyumba za kupanga. Si rahisi sana kutimiza wajibu wao vizuri kwasababu wamechangamana na jamii niombe wajengewe nyumba zao maalum kama walinzi wetu ili ziwasaidie kuishi salama na waweze kutimiza wajibu wao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya yetu ya Kakonko inavyo vikosi ambavyo nimevitaja, lakini ukichukua kutoka Biharamulo ambako kuna kambi maalum ya ulinzi katika mpaka wa Mkoa wa Kagera na mkoa wetu, kikosi kingine kipo Kigoma, kwa hiyo, hapa katikati hakuna kikosi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba ulinzi upo. Niombe sana kianzishwe kikosi katika Wilaya ya Kakonko ambacho kazi yake itakuwa ni kuhakikisha kwamba mpaka umelindwa na wananchi wetu wanaendelea kuishi vizuri na kwa usahihi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nikushukuru na naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, atafatiwa na Mheshimiwa Taska Mbogo, Mheshimiwa Maimuna Pathan ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu Rais wetu wa Jamhuri ya Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya na niwaombe Waheshimiwa Wabunge kwa heshima na taadhima kabisa kwa kutoa heshima kwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tugonge meza mara mbili ili tuonyeshe heshma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ninaomba nimpongeze Jenerali Mabeyo kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya ya kudumisha amani katika nchi yetu hii ya Tanzania. Lakini pia niipongeze Wizara na Waziri Mheshimwia Elias Kwandikwa, jirani yangu, kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya katika Wizara hii ya Ulinzi lakini mwisho kabisa niwapongeze majenerali na mabregedia wote walioko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa na mimi nianze kuchangia katika hotuba ya bajeti hii. Moja kabisa tunafahamu ya kwamba JKT kwa sasa wameingia katika ushindani wa kuwekeza lakini wameenda mbali Zaidi katika kuhakikisha ya kwamba wana-*compete* zabuni mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kuchangia kwa maana ya kuiomba Wizara hasa JKT kumekuwa na ucheleweshaji wa miradi inayotekelezwa na jeshi letu la JKT. Nimuombe Waziri Mheshimiwa Waziri utakuwa ni shahidi katika Jimbo langu la Msalala tunao mradi mkubwa wa ujenzi wa jengo la Utawala katika Halmashauri ya Msalala ambayo inatekelezwa na JKT na Mheshimiwa Waziri niseme tu kwamba ukiangalia fedha iliyotengwa walitoa *certificate* ya

kiasi cha shilingi milioni 515 kwa ajili ya hatua za awali za ujenzi wa jengo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sambamba na hilo ucheleweshaji umeendelea kuimarika jengo hilo mpaka tunapozungumza sasa bado halijakamilika japo kuna jitihada ambazo zinaendelea. Niombe Wizara Mheshimiwa Waziri unanisikia upo hapo ndugu yangu, jirani yangu, tunapata tabu sana wananchi wa jimbo la Msalala Halmashauri yetu tumekaa katika sehemu ya kupanga tumebanana tunahitaji sasa tuhamie kwenye jengo hilo, niiombe Wizara, niwaombe JKT kumaliza mradi huu kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko juu ya wastaafu wetu, juu ya namna gani kuiomba Wizara na Serikali waweze kuwaongezea *pension.* Kama unavyofahamu wastaafu hawa baada ya kustaafu wanarudi vijijini kuja kujumuika na wananchi, kumekuwa na changamoto nyingi juu ya changamoto za kimaisha katika wastaafu hawa. Niiombe Wizara iweze kuona ninamna gani basi wanaweza kuongeza walau *pension* kidogo ili wasaidie wastaafu wetu hawa kuendesha maisha yao huko walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa kuwa Jeshi linatoa mafunzo mbalimbali, nikuombe kabla wastaafu wetu hawa hawajastaafu basi ni vyema Wizara ikae na kupanga waone namna gani basi wanaweza wakaanzisha *short course* ya kuwaandaa wastaafu wetu hawa wanapostaafu waende wakakabiliane na maisha ya huko vijijini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni ukweli usiopingika kwamba wazee hawa, wastaafu hawa wanapokuja kule ni kweli usiopingika kwamba wanazalilika sana maisha ni magumu mno, wanapokuja kuanza ku-*adopt* mazingira ya kule vijijini wanapata taabu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kwamba kumekuwa na malalamiko kwamba Mbunge mwenzangu amechangia hapa juu ya namna gani askari wetu wanajeshi

wetu hawa wanapatiwa mavazi *pair* chache na ameshauri kwamba ikiwezekana walau waweze kupatiwa *pair* tatu. Lakini ni ukweli usiopingika kwamba Jeshi lina taratibu zake na taratibu za namna gani kuweza kutoa mavazi haya unaona kabisa hapa wanatakiwa wapewe mavazi mapya ya ndani ya miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa ninavyozungumza bado baadhi ya wanajeshi hawa hawajapatiwa mavazi hayo mapya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri, vijana wetu hawa wanafanya kazi kubwa sana, lakini pia na wao wanahitaji wapate mavazi haya ili waonekane *smart* kama watu wengine, niiombe Wizara kama kunauwezekano basi Wizara ione namna gani inaenda kuwapa mtaji Jeshi la JKT, ili wafungue kiwanda cha kushona mavazi hawa wanajeshi wetu. Kwa kufanya hivyo tutasaidia kutengeneza ajira, lakini tutakuwa tumewajengea vijana wetu ili tuweze kuondokana na adha ya upungufu wa mavazi na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho nimalizie kusema kwamba kumekuwa hakuna usawa juu ya usaili wa vijana wetu huko chini katika ngazi za chini katika kujiunga na Jeshi letu. Taarifa katika baadhi ya maeneo zinakuja leo kesho usaili umekwisha, kwa hiyo, niiombe Wizara ione namna gani inapotoa taarifa za usaili za vijana wetu hawa wapeleke mapema kule, lakini kumekuwa kuna urasimu pale mikoani, vijana wetu hawa baadhi wanaobahatika kuingia katika nafasi hizo wanapofika mkoani wanapewa vikwazo vingi vingi na wengine wanatolewa majina yanakuwa yameandaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe Mheshimiwa Waziri, sisi wana Mkoa wa Shinyanga ni waathirika wa hilo, hebu tuangalie tuone namna gani sasa Wizara inaenda kujipanga kuonesha ya kwamba inaondoa urasimu huo ili vijana na wao wapate sifa ya kujiunga na Jeshi letu hili la wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba niendele kuwapongeza na ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Taska Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Maimuna Pathan, Mheshimiwa Hamis Tabasam ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia Wizara nyeti, Wizara ya Ulinzi. *(Makofi)*

Kwanza kabisa napenda nimpongeze Mheshimiwa Kwandikwa kwa hotuba yake nzuri sana aliyeitowa leo napenda niwapongeze wanajeshi wote nchini Tanzania kwa kazi nzuri sana ambayo wanaifanya kutulinda sisi wananchi, lakini pia kulinda mali zetu na kulinda nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu wa leo kabla sijaenda kwenye hoja ya Mheshimiwa Kwandikwa, napenda nizungumzie Mkoa wangu wa Katavi. Kwenye Mkoa wangu wa Katavi pale Mpanda Mjini mwaka 1984 kuna mnara uliwekwa pale maeneo ya Kampuni, lakini mwaka 1993 Jeshi liliondoa huo mnara, badaye mwaka 2020 ule mnara ulirudishwa pale na mwaka 2021 waliweza kufunga hiyo *radar. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ni nini yale maeneo yanazungukwa na kata tatu, Kata ya Ilembo, Kata ya Mpanda Hotel, na Kata ya Msukumilo na hoja iliyopo Jeshi lilipokuja mwaka 1984 lilikuwa na hekari 100, liliporudi mwaka 2020 liliongeza yale maeneo na kuwa na hekari 2,200. Sasa katika maeneo yale walioongeza kuna shughuli za kijamii zinaendelea pale, kuna watu wanalima wanafuga, lakini pia kuna nyumba za watu ambazo zilikuwemo katika eneo hilo. Ombi langu kwa Wizara ya Ulinzi na kwa Mheshimiwa Waziri ni kwenda kutatua ule mgogoro ili wananchi pamoja na wanajeshi waweze kukaa kwa amani, kwa sababu kwa sasa hivi kinachoendelea wale wananchi wanapokatiza lile eneo la Jeshi kwenda kuangalia shughuli zao wanajeshi

wanawapiga, lakini pia wanachoma nyumba zao na kuwanyang'anyia mali zao kama mabati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, ili kuwe na amani na ili Jeshi kwa sababu ni Jeshi la wananchi, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri atafute muda ili aende Mkoani Katavi pale kwenye Wilaya ya Mpanda Mjini akaangalie hilo tatizo na aweze kulimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri; Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ameeleza changamoto ambazo anazikabili kwenye ukurasa wake wa 19; aya ya 78, 79 mpaka aya 80.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba tatizo analokabiliana nalo ni ukomo wa bajeti, ili nchi iweze kufanya mambo mengine, ili nchi iweze kutatua tatizo la maji, tatizo la umeme, tatizo la barabara, lakini pia ili wananchi waweze kufanya kazi kwa amani lakini pia wanajeshi wale wanatakiwa waongezewe marupurupu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiona bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi inaukomo sasa bajeti ikiwa na ukomo na Mheshimiwa Waziri katika hizi aya nilizozitaja ameeleza kwamba ameshindwa kutoa mafunzo kwa wanajeshi, ameshindwa kuwapeleka kusoma, kununua vifaa, lakini pia ameshindwa hata kutoa yale mahitaji muhimu yanayohitajika pale Jeshini kwa sababu ya ukomo wa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali bajeti ya Ulinzi, isiwekewe ukomo wa bajeti na hii itatusaidia sana sisi wananchi wa Tanzania ili tuweze kuishi kwa amani, lakini pia ili tuendeleze amani yetu iliyopo sasa hivi. Suala hili ni muhimu, nimeliona nilizungumze hapa la ukomo wa bajeti ili tuweze kuangalia tunalifanyia vipi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningependa kulizungumza leo ni mipaka ya nchi yetu. Mipaka ya nchi yetu mingi hakuna barabara na ndiyo maana tuna wahamiaji

haramu wengi wanaingia nchini kwetu, utaweza ukajiuliza uko pale Mbeya au uko Dodoma mhamiaji haramu ameingiaingia vipi mpaka akafika hapa Dodoma na ameingilia wapi? Jibu unaweza ukajijibu mwenyewe kwamba ameingilia kwenye uchochoro wa mpakani kwa sababu hakuna barabara. *(Makofi)*

Kwa hiyo niiombe Serikali na nimuombe Waziri awasiliane na Waziri wa Ujenzi waangalie ni jinsi gani wataweza kuitengeneza barabara zinazozunguka nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni muhimu kwa sababu nchi yetu inapakana nan chi nyingi, inapakana na nchi za Rwanda, Burundi, Uganda, Msumbiji, lakini na nyingine nyingi. Sasa ili tuwe na uimara wa mipaka yetu na hili wale walinzi wa mipakani ambao ni wanajeshi wetu waweze kuwagundua kwa mapema wale wahamiaji haramu ni muhimu barabara zikawepo. Kwa sababu ukosefu wa barabara, mlinzi atakuwa amesimama hapa kwenye lindo, lakini yule mhamiaji haramu anapata upenyo wa kupita eneo lingine kwa sababu hakuna barabara inayonyooka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba suala la barabara za mipakani lizingatiwe, lakini pia mipaka yetu ioneshwe, sisi tupo lakini kuna siku tutaondoka katika dunia hii, tunatakiwa kizazi kitakachokuja kikute mipaka ya nchi yetu ikiwa inafahamika vizuri. *(Makofi)*

Suala la mipaka nchi nyingi zimeweza kugombana kwa ajili ya mpaka wa hatua moja au mbili. Mheshimiwa manyanya alizungumza leo asubuhi kuhusu mpaka ulioko Ziwa Nyasa ndiyo utaangalia jinsi gani umuhimu wa kuweka mipaka yetu sasa hivi ili kizazi kinachokuja kikute mipaka yetu iko wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala ambalo wengine wamelizungumza hapa kuhusu nyumba za wanajeshi wetu na kukaa uraiani. Ili kuweka ile dhana ya kusema huyu sasa

ni mwanajeshi turudi kama jeshi lilivyokuwa zamani wale wanajeshi wakae katika kambi zao, wasikae uraiani, kwa sababu hii kwanza kikanuni inaweza ikapunguza ile sijui nitumie neno gani? Hali ambayo mwananchi anamuona kwamba huyu mwanajeshi ni mlinzi wa amani ya kwangu na ni mlinzi wa nchi, sasa inakuwa kwamba yule mwanajeshi anakaa nyumba moja na mwananchi wanatumia geti moja, labda wanatumia bafu moja, naona kama inapunguza kitu cha namna fulani, nimeshindwa kuweka maneno gani mazuri hapa, lakini maana yangu ilikuwa ni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba tulilirudishie jeshi letu heshima yake ya toka mwanzo kama jinsi lilivyoanzishwa. Nafahamu yapo mapungufu lakini kama tunaweza kutatua hili tatizo la makazi ya wanajeshi litatusaidia sana, majeshi yakae mahali pao, polisi wakae mahali pao japokuwa siyo bajeti yao hii, lakini nilitaka tu kusema hivi wale watu ambao kwa sababu wanajeshi wenyewe uwezi kumkuta mwanajeshi ameingia baa au polisi ujuwe huyo siyo mwanajeshi halali. Sasa kama huko kuna miiko basi na ukaaji vilevile wasichanganyike na rai ndiyo suala ambazo nilipenda kulizungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nilitaka kusema ni suala la la vile viwanda ambavyo vimeanzishwa na Jeshi letu la wananchi, kulikuwa wanajeshi waliwahi kutengeneza gari inaitwa Nyumbu, lakini sijui gari hiyo iliishia wapi.

Kwa hiyo wangekuwa wamewezeshwa na wale wataalamu waliokuwa waliotengeneza hiyo gari nafikiri sasa hivi wangeshatengeneza magari mengi, lakini pia Jeshi lina kiwanda cha kutengeneza *uniform,* kwa hiyo sioni hoja ile ya kusema mwanajeshi anakosa *uniform* wakati kuna kiwanda cha kutengeneza *uniform* na nilivyosoma kwenye hii taarifa ya Mheshimiwa Waziri kile kiwanda kina uwezo wa kutengeneza *uniform* 400 kwa siku. Sasa kama kina uwezo wa kutengeneza 400 kwa nini mwanajeshi akose *uniform,* ni kwamba sisi tumekosa kuwapa zile fedha/mitaji ya kununua zile material ili waweze kutengeneza hizo *uniform*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ombi langu kwa Serikali ni kuangalia hivi vitu ambavyo viko viwanda na tunafahamu wanaviwanda wanamambo ya kilimo ambayo yameanzishwa na wanajeshi na ambayo kwa kweli yanawasaidia sana kujitegemea wao wenyewe kwa wenyewe.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sisi tuweke input tuporeshe kama ni hivyo viwanda Serikali iweke pesa hizo *uniform* zitengenezwe hakuna haja ya kusimama hapa na kusema kwamba wanajeshi hawana *uniform* wakati wanakiwanda cha kutengeneza *uniform* zao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maimuna Pathan atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Tabasam, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi kwanza napenda Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na sisi wote kuwa hai kwa siku hii ya leo. *(Makofi)*

Napenda pia kumpaongeza Rais wetu mpenzi Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na timu yake yote. Pia napongeza Waziri wa Ulinzi kwa hotuba yake nzuri ambayo ametusomea leo asubuhi, kwa kweli imeshiba, inapendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mwenyeji wa Mkoa wa Lindi, kule kwetu Lindi na Mtwara tupo mpakani kabisa, mwaka jana kuanzia mwezi wa sita/wa saba mpaka kumi kidogo tuliishi kwa mashaka. Watu walikuwa hawawzi kufanya kazi zao, kazi kubwa ambayo inafanywa na wakazi wa Mkoa wa Lindi na Mtwara ni uvuvi na kilimo. Kipindi kile watu walikuwa wanashindwa kwenda mashambani kwao kwa sababu kuna watu waliingia ambao sio watu wazuri kutoka kwenye nchi za wenzetu japokuwa siwezi nikasema

ni nchi gani, lakini inaonekana kuna watu waliingia wakawa wanafanya matendo ambayo hayafurahishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nashukuru sana nilipongeze Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania walichukua jitihada za haraka wakatuma vikosi vya Jeshi kwenye mipaka ile na ulinzi uliimarishwa, hatimaye hali ikarejea vizuri sana kwa kweli tunawapongeza sana tunasema ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Lindi na Mtwara kwa sasa wanaamani wanaendelea na kufanya kazi zao na tunaona bajeti iliyowekwa hapa tunaomba ipitishwe tu kwakweli tusishike shilingi ipitishwe vizuri kwa sababu wanaonesha wanania ya kulinda mipaka na walilinda mipaka ipasavyo, tunaomba bajeti yao iende vizuri ili kazi iendelee kusiwe na mkwamo wowote wa ulinzi na usalama wa mipaka yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuliongelea ni suala la nyumba za wanajeshi, katika Wilaya ya Nachingwea kuna kikosi cha Jeshi kinaitwa Majimaji na *Old Camp*, nyumba zilizopo pale ukiziona kwa kweli zinakatisha tamaa na ukiambiwa wanaishi watu/wanajeshi kwa kweli inatisha. Ombi langu kwa Serikali kwa Wizara ya Ulinzi mfanye marekebisho ya zile nyumba ili watu wanaoishi mle wajisikie ni watu kama watu wengine wanaishi vizuri, zile nyumba zimechoka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi lingine nililonalo kwa Wizara ya Ulinzi ni ofisi zao, nimeshaingia kwenye ofisi zao mara nyingi hata pale Kikosi cha Mgulani ofisi zao kwa kweli haziko vizuri. Tunaomba Waziri wa Ulinzi ulichukuwe hilo ujaribu kuangalia kuboresha ofisi za jeshi kwa sababu zile ni ofisi kama zilivyo ofisi nyingine, tunaomba uboreshe ziwe vizuri ili na wao wafanye kazi vizuri, wajisikie wanapotimiza majukumu yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine napenda kuliongelea ni kuhusu barabara za mipakani. Wabunge wengi

wameongelea hizo barabara, tunashukuru Serikali yetu kupitia Wizara ya Ujenzi wamejitahidi kutengeneza barabara hizo. Ila tunaomba tunatia msisistizo kwamba barabara zile ziendelee kuimarishwa ili ziwe vizuri hata kama kukitokea suala lolote kusiwe na tatizo jinsi ya kupita kwenye zile barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sina mengi ya kuongea kwenye Wizara hii ila ombi langu naomba tusishike shilingi tuwaache Wizara hii wapewe pesa zao vizuri ili waweze kufanya majukumu yao vizuri, kwa kweli wanajitahidi, wanafanya kazi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hamis Tabasam, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Ester Bulaya ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Segerema naomba kuchangia mchango wangu katika hotuba ya Waziri wa Ulinzi kama ifuatavyo; nimeusikiliza mchango wa Mheshimiwa katika maombi yake ya kupitisha bajeti, lakini kazi nzuri zinazofanywa na wanajeshi wetu katika ulinzi wa mipaka ya nchi hii, lakini kufanya kazi za kijamii katika nchi hii tunaomba tushauri kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba Wizara ya Ulinzi lazima iwe na kitengo cha kisayansi, leo tumekutwa na gonjwa kubwa kama hili la *Covid,* lakini wanajeshi wetu wangefanya kazi hii, na wao ndio wangekuwa wa mwanzo katika mstari wa mbele kwenye tiba na kila kitu. Tunayo Hospitali yetu ya Lugalo kule Mwanza tunayo Hospitali ipo Pasiansi kule. Lakini wanazo hospitali zao nyingine za kijeshi ambazo zingeweza kutumika katika hali hii ya kupambana na hali kama hii kwa sababu kwa mfano mwishoni mwa mwaka jana hospitali zetu zote zilielemewa, lakini hatukuona jeshi kuchukuwa msaada katika jambo hili wanayo mahema,

wana kila kitu sasa inamaanisha kwamba jeshi limeandaliwa kwenda kupigana vita tu, sasa ni hatari sana kuwa na jeshi la namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunahitaji jeshi kama nafasi za kuajiri basi waajiri wataalamu, hii ni jambo ambalo kwenye mpango wenu kama jeshi basi mgeweza kuajiri wataalam na wakapelekwa katika nchi ambazo zimeendelea sana kisanyansi, mfano Cuba, labda India wakapelekwa China, Urusi hawa wangekuja kama madaktari wa akiba wakuja kufanya kazi za kuokoa nchi kama hiko katika hali mbaya kama hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ambalo nataka kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, ni kwamba wanajeshi sasa hivi tabia zimebadilika, wanajeshi wetu sasa hivi wanaishi na raia sio kwa ugomvi kama ulivyokuwa mwanzo. Mara nyingi sasa kungekuwa na mikutano hata kama kuna hali ya mipaka, wanajeshi sasa hivi wanakaa na wananchi. Kwa mfano kule kwangu katika eneo la Sengerema wana uwanja wao waliacha kambi ya jeshi ilihamiishwa kutoka Sengerema kuhamia Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi hii inakuwepo miaka 1980 na 1985 sasa tumesikia tena wanajeshi wanakuja kuchukuwa eneo hilo ambalo lile eneo lilibakia kwa Halmashauri.

Sasa tunamuomba waziri pamoja na kazi nzuri mnayofanya hili eneo letu la Sengerema katika eneo la Nyatukala mnakuwa na eneo lingine katika eneo la Nyamterera eneo lingine mlikuwa kule eneo la Nyamazugo kama sehemu ya mafunzo ya kijeshi na eneo la kambi, kwa sababu maeneo haya mliyakabidhi basi tunakuomba Mheshimiwa Waziri hili lenyewe uliangalie limekuwa ni shida, leo mkitaka kuja kudai maeneo yenu kule, wananchi wameshajenga, Serikali imejenga ofisi ya kata, imejenga ofisi yake ya Idara ya Ujenzi, tunayo shule ya msingi Mweli pale, zote ziko katika eneo ambalo tayari mnadai kwamba mipaka hii ni ya kwenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea jeshi hili sasa ni Jeshi la Wananchi, likisha kuwa Jeshi la Wananchi basi hebu pelekeni mipango mizuri kwa wananchi, maeneo mengine yapo Sengerema tunayo maeneo ambayo mnaweza mkaja mkachukua kule ambayo yako vizuri sana kwa ajili ya ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kwamba tuna ujenzi wa daraja kubwa la shilingi bilioni 700 kuna eneo la *Kigongo Ferry* ambalo kama mlipanga kama jeshi leo na lenyewe lile lina miaka kama 40 halijafanyiwa kazi. Basi ni vizuri Mheshimiwa Waziri katika hotuba yako ukija katika majumuhisho basi uangalie hilo eneo la *Kigongo Ferry* mwende kiustaarabu na huku Sengerema mje muangalie maeneo mengine Halmashauri inaweza ikawapa, lakini hili eneo la Sengerema Mjini kweli itakuwa ni shida kwa wananchi wa Sengerema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mimi kama mwakilishi wao nitakuwa niko katika hali mbaya sana kwa sababu kwanza hatuwezi kubishana na jeshi, kwa nafasi yenu na mamlaka ya ulinzi wa nchi, basi maeneo kama haya yapo nchi nzima, basi ni vizuri mkayapitia upya muone kama kuna maeneo ambayo sasa hivi wananchi wameshavamia wako katika maeneo hayo, basi jeshi linaendelea kutafuta eneo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ndio huo, nakupongeza sana Mheshimiwa kwa usikivu wako na nina imani hili utalisikia kwa ajili ya wananchi wa Sengerema na kwa nchi nzima, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, mtoa hoja ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niwe mmoja wapo wa kuchangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze sana kwa kumpongeza Jemedari Mkuu Samia kwa kazi nzuri ambayo anaifanya ndani ya nchi yetu. Lakini nimpongeze sana Waziri Kwandikwa kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika Wizara hii ya Ulinzi. Jeshi la Wananchi ni mali ya wananchi na wananchi ni mali yao sasa Kwandikwa namna anavyojichanganya anaendana na jeshi la wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Kwandikwa tunakupongesa sana kwa namna unavyojichanganya na sisi Wabunge wenzako, umekuwa karibu na sisi hongera sana kwa kazi ambayo unaliongoza jeshi hili. *(Makofi)*

Lakini pili nimpongeze sana *CDF* Mabeyo, pamoja Makamishna wake wote, kwa kazi nzuri wanayetulinda mipaka yetu na kadhalika, tuko salama tuko kwa sababu wao wapo, wanaliongoza jeshi vizuri kupitia wewe tunakushukuru sana Mabeyo na wenzako kwa kazi nzuri ambayo unaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile niungane na wenzangu kwamba Mabeyo na timu yake na wewe Waziri baada ya kifo cha Jemedari wetu....

**NAIBU SPIKA:** Jenerali Mabeyo.

**MHE. DEO K. SANGA:** ...kwa kazi nzuri aliyoiongoza kuituliza nchi, juu ya kifo cha kilichotokea cha Dkt. Magufuli amefanya kazi kubwa sana na nitampongeza sana kwa kusimamia mazishi yale chini ya Waziri Mkuu ambaye naye pamoja akisaidiana na Mheshimiwa Jenista, dada yetu kwa kazi nzuri ya kuongoza mazishi yale Jenista tunakupongeza sana kwa kazi nzuri ile ambayo umeifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, mimi nina mambo machache, nimesikiliza sana michango ya Wabunge, kuna migogoro baina ya mipaka ya wananchi na jeshi. Ombi langu Mheshimiwa Waziri na timu yako mkae

na Waziri Lukuvi na timu yake ili muone muorodheshe maeneo yenye migogoro kati ya wananchi, na jeshi hili yatatuliwe. Litakuwa ni jambo jema sana nitoe mfano mdogo tu pale kwangu Makambako, Mkuu wa Kikosi cha Jeshi la Makambako anafanya kazi nzuri haijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yuko jirani na wananchi, anashiriki maendeleo na wananchi, anashiriki kuchangia maendeleo ya shule yetu iko jirani pale ya Kipagamo na maendeleo mengine anafanya, kwa kweli tunampongeza sana Mkuu wa Kikosi chetu cha jeshi pale. *(Makofi)*

Ombi langu kuna eneo dogo ambalo wananchi walipanda vitindi vya ulanzi. Vitindi ndugu zangu kule kwetu ulanzi ule unagemwa, unaota kutoka chini unagemwa wananchi wanauza, wanapata riziki. Kwa hiyo, sasa wananchi wamekosa kwa sababu jeshi eneo lile wanasema ni mali yao. Ombi langu Mheshimiwa waziri na timu yako tafuta muda, njoo uone eneo linalozungumzwa hili paweze kutatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilikuwa na ombi lingine Mheshimiwa Waziri wamezungumzia wenzangu Waheshimiwa Wabunge hapa kwamba Jeshi kwa sababu wanafanya kazi nzuri, wajengewe nyumba nzuri za kuishi. Sasa na mimi nazungumzia juu ya jeshi lililopa Makambako, tuna nyumba ambazo mlizijenga miaka mingi sana za kuishi wanajeshi pale, nyumba hizi hazijamaliziwa zaidi ya miaka 15; nikuombe Waziri fedha ya Serikali iko pale, kuna nyumba zaidi ya tisa, ombi langu nyumba hizi zimalizwe ili wanajeshi waweze kukuaa kwenye nyumba zile. kwa sababu zimekaa hazimaliziwi kwa hiyo niombe sana jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni kuhusu vijana wanaojiunga kwenda JKT nilikuwa nadhani Serikali itafute namna ambavyo vijana hawa wanapokwenda kujiunga kule, kazi ya JKT ninavyojua mimi ni kwenda kujenga uzalendo wa nchi yao. Sasa tutafute namna ambavyo tuongeze hela/bajeti hili vijana hawa wajiunge kule kwa ajili ya kwenda kujenga uzalendo, tukiacha miaka kadhaa bila

ya kupeleka vijana JKT mimi naiona kwamba itakuwa hatari. Waende huko ili wakajenge uzalendo juu ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho Mheshimiwa Kwandikwa na timu yako juu ya Jemedari wetu Mama Samia Suluhu Hassan, mimi nawaombea sana kwa Mungu, kwa kazi ambayo mnaifanya ya kulinda nchi hii, mipaka yetu na sisi kwa kweli tuko salama ni kwa sababu yenu. Lakini vilevile pamoja na kwamba si Wizara yake leo pamoja na *IGP* Sirro na Jeshi lake la Polisi na vyombo vingine vya ulinzi tuko salama ni kwa sababu yao, Mungu akubariki endelea na kazi nzuri ambayo unaifanya ndugu yangu Kwandikwa, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa wanajeshi kama kujenga nyumba za kuishi pamoja na kununua vitendea kazi kama magari na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ihakikishe JKT inawezeshwa ili kuzalisha chakula cha kutosha kwa matumizi na biashara. Pia Serikali kuendelea kulisimamia Shirika la SUMA JKT kuendeleza viwanda na ujenzi wa majengo mbalimbali ya Serikali kuongeza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kusimamia na kuondoa migogoro ya ardhi na mipaka baina ya Jeshi letu la wananchi pamoja na wananchi wanaoishi jirani na kambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waziri na Naibu Waziri na Makatibu Wakuu pamoja na Mkuu wa Majeshi kwa utendaji kazi wenye weledi kwa kuimarisha ulinzi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ISSAAY Z. PAULO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuungana na viongozi wa Taifa letu kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote kama Taifa kupitia majanga mbalimbali hususan janga la corona, kimbunga cha jobo kule Mtwara na mengi kadha wa kadha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupokea uongozi wa Taifa letu. Hivyo tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu amjalie ulinzi na baraka katika kuongoza Taifa letu tuwe kielelezo mbele ya mataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge letu navipongeza sana vyombo vyetu vyote vya ulinzi na usalama, kama nchi siyo rahisi kutambua haraka kujua kazi kubwa ya vyombo vyetu vya ulinzi ndani ya nchi na nje ya nchini. Nayasema haya kwa sababu majeshi yetu ni nguzo ya tunu ya amani na utulivu ulioko nchini kwetu. Hivyo basi sisi kama Bunge tuwe mstari wa mbele tuwatetea kupata stahiki zao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini nachukua nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2015 na 2020 kwa jimbo langu la Mbulu, hongereni sana wadau mbalimbali walioshiriki kwa kwa hali na mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naungana na Watanzania wote kumwombea sana Mheshimiwa Hayati John Pombe Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano kwa kweli kama Taifa mchango wake tutaukumbuka daima. Ee Mwenyezi Mungu umpokee mtumishi wako mwaminifu, mzalendo, mtiifu mwana mapinduzi wa Afrika katika ufalme wako wa milele mbinguni, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha naungana na waheshimiwa viongozi wa Taifa letu, Bunge zima, Watanzania

wote kwa ujumla kutoa pole nyingi kwa msiba wa kifo cha mpendwa wetu Mheshimiwa Hayati Khatib Said Haji, Mbunge wa Jimbo la Konde, Mwenyezi Mungu ampokee katika ufalme wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kutoa ushauri wangu kupitia bajeti hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa nikianza na kutokana na changamoto kubwa sana ya makazi ya askari, upungufu wa magari na vitendea kazi hivyo Serikali ijitahidi kupeleke fedha zote zinazopangwa kwenye bajeti zetu kwani hali ni mbaya sana ili majeshi yetu yatekeleze majukumu yao kwa weledi mkubwa kuendana na utandawazi mkubwa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema hayo kwa sababu nimehudumu kwenye Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Serikali yetu haijafanikiwa kupeleka fedha za maendeleo kwa zaidi ya 50% zinazopangwa.

Pili, kutokana na vijana wengi kujiunga na JKT na baada ya kuhitimu wanarudi uraiani. Ni wakati sasa wa kuona kuwa na matawi ya SUMA JKT kwa ngazi ya mikoa ili kuchochea fursa za ajira kupitia matawi hayo. Kuna umuhimu wa kutoa maelekezo ya Serikali kuajiri vijana wote kwenye ulinzi katika taasisi za umma kama vile halmashauri, elimu, afya na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iangalie umuhimu wa dhana ya uraia na uzalendo ambao ndiyo nguzo muhimu sana kwa kila Mtanzania ili kuwajengea vizazi vyetu na Watanzania kwa ujumla kwani ni dhahiri kuwa vijana wote wanaohitimu JKT hawataweza kupata nafasi za ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vijana wengi wanaojiunga na JKT toka awali hawajiandai kisaikolojia kuwa lengo lake ni kujiari hivyo ni muhimu toka mwanzo wa kujiunga vijana wetu waulizwe hulka yake ni nini katika kujiajiri kama sekta za kilimo, ufundi, ufugaji ili kubaini anapaswa kwenda kambi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga hoja mkono asilimia 100 na naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukurani zangu za dhati kwako kwa kinipatia fursa hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Pili, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kutayarisha na hatimaye kuiwalisha katika Bunge lako tukufu kwa umakini mkubwa na kwa ufasaha wa hali ya juu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika kutoa mchango wangu kwa Wizara hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; kwanza ni kuhusu Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jeshi la Kujenga Taifa ni kitengo muhimu sana katka nchi yetu, ni kitengo kinacholea vijana na kuwaelekeza namna bora ya kuishi katika nchi yetu na katika jamii kwa jumla. Jeshi hili ni lina vitengo muhimu sana katika maisha ya kiuchumi na kuwawezesha wananchi kiuchumi, kwa mfano uvuvi, mifugo na kilimo. Jeshi hili lina wataalam wa kutosha katika maeneo hayo. Aidha, maeneo hayo yanahitajika sana na wananchi wa maeneo hayo huku uraiani ili kuweza kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Wizara na Serikali kwa jumla ni kuushusha utaalam huu kwa raia kwa kuwaelimisha namna ya kuendeleza miradi hii.

Kuhusu makazi ya wanajeshi, napenda kuipongeza Serikali yetu kwa namna inavyochukua juhudi kubwa ya kuwawezesha wanajeshi wetu katika maeneo kadhaa ili kuwafanya wanajeshi wetu kuweza kufanya majukumu yao ya kila siku. Lakini wanajeshi wetu bado wanakabiliwa na tatizo dogo la makazi. Wanajeshi wetu kama binadamu wengine wanahitaji mambo yote ya kimsingi (chakula na makazi). Serikali inachukua jitihada kubwa kwa kuwapatia

chakula cha kutosha na bora. Lakini bado wanajeshi wetu makazi yao hayaridhishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado katika maeneo kadhaa wanajeshi wetu wanafanyakazi makambini lakini wanalala uraiani. Hii ni hatari kwa usalama wa wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali kuendelea kuchukua juhudi za makusudi ili kutatua tatizo hili la makazi kwa wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha mchango wangu wa maandishi katika wizara hii ya Ulinzi.

Kwanza napenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa inayoifanya kwa kuhakikisha Taifa linakuwa salama muda wote. Tunatambua uzalendo wao kwa Taifa hili na sisi kama wawakilishi wa wananchi tutakuwa nao bega kwa bega.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na pongezi hizo tuna changamoto katika Mkoa wa Katavi wa mgogoro baina ya jeshi na wananchi wa Mpanda Manispaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro umekuwa wa muda mrefu sana, namuomba sana Mheshimiwa Waziri kupitia Serikali watoe tamko kwani wananchi hao wamekuwa wakifanya shughuli za maendeleo katika maeneo hayo kwa muda mrefu kutokana shughuli za jeshi katika eneo hilo imesababisha mgogoro na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali itoe tamko ili wananchi wajue hatima yao kwani mpaka sasa wananchi hawajui nini hatima ya mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sikusimama Bungeni kutoa mchango wangu wa kawaida naomba nichagie kidogo kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na kumpongeza Mheshimiwa Waziri *Engineer* Elias Kwandikwa, Katibu Mkuu na watendaji wote Wizarani pamoja na Mkuu wa Majeshi *(CDF)* pamoja majeshi yetu kwa kazi nzuri wanazofanya za ulinzi wa Taifa letu, lakini pamoja na majukumu mengine wanayoagizwa na Amiri Jeshi Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jeshi letu linafanya vizuri sana na linasifika hata nje ya mipaka yetu. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamechangia mengi mazuri kuhusu bajeti iliyoletwa kwetu na mimi naomba nichangie jambo moja tu ambalo naliona ni la muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida wanajeshi wanatekeleza majukumu yao kwa amri na amri zote ni halali. Ni kwa ajili hiyo mataifa mengine mengi yanatumia majeshi yao kama nyumba ya kufanyia tafiti za kisayansi kwa sababu ya nidhamu ya kijeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nchi yetu nayo ni sehemu ya dunia ya leo ya ki-TEHAMA, nashauri Serikali iangalie ni namna gani tunaweza kutumia majeshi yetu kama nyumba ya kufanyia tafiti za kisayansi *(atomic, molecular, medical etc)* na hata ujenzi wa viwanda vya kutengeneza magari ya kisasa na vifaa tiba na vya kijeshi pamoja na vifaa vya ujenzi wa miundombinu. Hili linaweza kufanyika kwa kutenga fedha na kuchukua vijana wetu wenye vipaji maalum watunzwe na kuhakikishiwa maisha mazuri na kutengenezewa maabara za kisasa kwa ajili ya tafiti ambazo tunazihitaji kitaifa kwa ajili ya maendeleo ya kisayansi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda atafuatiwa na mtoha hoja.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nipende ku-*declare interest* yangu

hapa, mimi nimezaliwa jeshini, ni mwanajeshi niliyefanya kazi jeshini miaka 33; kati ya hiyo miaka 13 nilikuwa nimewekwa *attachment* Wizara ya Mambo ya Nje, kwa hiyo....*(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pinda, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Esther Matiko.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru nakumbuka kumbukumbu zangu ukiwa umekalia kiti hapo ulitupa mwongozo tukisema una-*declare interest* au maslahi jambo unalozungumzia labda uwe unapata fedha *direct.* Sasa Mheshimiwa Pinda naomba nikupe taarifa kwamba kukaa kambini sio kwamba una maslahi, wengi tumekaa kambini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda unaipokea taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mtoa hoja hajaelewa ninachokisema, kwa hiyo naomba nimuhurumie tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema kwamba mimi ni uzao wa jeshi na nimetumika jeshini miaka 33 na hivyo basi ninaposimama kama Naibu Waziri wa Katiba na Sheria najisikia raha sana kwa sababu nimetokea kwenye chombo hiki ambacho leo kimewasilisha bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili ya kuchangia; kwanza niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ya pekee jinsi ambavyo mmechangia, mmetoa mawazo makubwa sana, nadhani Wizara ya Ulinzi mwakani tutakaa mkao mzuri ili kuandaa bajeti inayolingana na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge kwa sababu mmegusa maisha ya wanajeshi kwa karibu sana na hili ni

jambo muhimu sana kwa sababu wakati mwingine tungekuwa tunashuhudia tu nashika shilingi, lakini kumbe nimebaini kwamba mnajua umuhimu wa hiki chombo ambacho ni chombo muhimu sana hasa kwa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninaomba tu niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba katika kufikia uchumi wa kati, jeshi limechangia sana kwa sababu bila utulivu tumeshuhudia nchi nyingi zinakimbia kimbia, hakuna muda wa kuzalisha. Hivyo basi niwaombe mkawe mabalozi huko ambako vikosi vyetu vya jeshi vipo karibu na wananchi, mjaribu kutusaidia kuelimisha wananchi kuelewa umuhimu wa hivi vikosi vya jeshi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hakuna Kikosi cha Jeshi kinachowekwa bila mpango maalum wa umuhimu katika ulinzi wa nchi. Kwa hiyo utaona maeneo mengi ambayo vikosi hivi vipo vina malengo maalum katika kulinda mipaka ya nchi yetu na kuwalinda wananchi wake ambao tunalala na kuamka salama bila hata kuchomwa na sindano na maadui zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na migogoro ya ardhi kwenye maeneo ya jeshi; makambi na vikosi vya jeshi la Ulinzi la wananchi wa Tanzania (JWTZ) vinaundwa kulingana na sheria ya ulinzi ya Taifa Na. 24 ya mwaka 1966 ambayo imefanyiwa marekebisho na kuwa Sura ya 192 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 1966 hadi 1979 Serikali imetenga maeneo mengi na makubwa mbalimbali mbali na miji na vijiji kwa matumizi ya jeshi. Miaka ya hivi karibuni kumezuka migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo kadhaa ya jeshi, kwa sababu mbalimbali zikiwemo maeneo ya jeshi kutopimwa kuchelewa kulipa fidia mapungufu ya sheria za ardhi kupanuka miji midogo kuwa miji mikubwa wananchi wasio wahaminifu kuvamia maeneo ya jeshi. Hata hivyo Wizara inachukuwa hatua mbalimbali kutatua migogoro hiyo ikiwa ni pamoja na kupima maeneo

yake kufanya uthamini na kufanya vikao vya usuluhishi na wadau wa migogoro husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ambayo tayari upimaji umefanyika na ramani zake kusajiliwa. Wizara inafanya jitihada za kuandaa hati miliki, hadi sasa Wizara ya Ulinzi imeweza kupima maeneo yake yapatayo 121 kati ya 203; maeneo matatu tayari hati miliki zimepatikana na maeneo 62 yapo katika mipango ya kuomba kuandaliwa kwa hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na mwaka wa fedha 2020/2021 imeweza kulipa fidia kwa maeneo kumi yakiwepo *Kigongo Ferry* na Ilemela shilingi 6,824,544,927; Nyagungulu na Burihahela shilingi 3,534,295,165.58; Mwanza Mlangalini na Mashono huko Arusha shilingi 1,548,490,247.88. Kwa upande wa Kilwa ni shilingi 624,236,405 Makoko ni shilingi 1,109,841,249 na Nyabange Musoma shilingi 203,646,661 na Airport Chato, Geita ni shilingi 972,218,036.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Wizara inatarajia kulipa maeneo yafuatayo Nyamisangula Bugosi na Kanyambi - Tarime shilingi 1,631,984,692.76; Kaboya - Muleba shilingi 4,440,346,998.25; Kikombo - Dodoma shilingi 2,261,604,837.45; Mitwero - Lindi shilingi 187,888,88 na Duluti - Arusha shilingi 4,694,000,000 idadi ya maeneo yaliyotarajiwa kulipwa fidia kwa mwaka wa fedha 2021/2022 yataongezeza kutokana na timu ya wataalam walioko uwandani hivi sasa wakifanyia upimaji na uthamini kwa sababu timu hiyo ipo Mikoa ya Lindi na Mtwara wakiendelea kutekeleza majukumu ya upimaji na thamani yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo niombe tu kwenu mjaribu kuwapelekea wananchi wawe watulivu kwenye maeneo yale ambayo bado hatua za uthamini zinaendelea, lakini Serikali inaendelea kupunguza ulipwaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa kilimo kwa upande wa JKT; katika kuhakikisha kwamba JKT inajitosheleza kwa chakula, umeandaliwa mpango mkakati 2019/2020 - 2024/2025 ambao unalenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kwa ajili ya kujitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya mkakati huu ambayo yamefanyika ni pamoja na kuandaa andiko la mkakati, upimaji wa ukubwa wa mashamba na afya ya udongo katika maeneo ya vikosi, upatikanaji wa pembejeo na kuweka miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba. Aidha, kwa kuanzia JKT imeanza ujenzi wa skimu ya umwagiliaji katika Shamba la Chita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza mkakati huu JKT imeingia makubaliano na Wizara ya Kilimo katika maeneo ya utaalam na teknolojia ya kilimo, mafunzo ya utaalam, mbinu za uzalishaji bora wa mazao, upatikanaji wa pembejeo za kilimo, masoko ya mazao na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo makuu ya mkakati huu ni kuongeza uzalishaji wa mazao ili kujitosheleza kwa chakula na kuwajengea vijana uwezo wa kujiajiri kupitia sekta ya kilimo na hatimaye kuchangia ukuaji wa uchumi wa viwanda nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matarajio ya Jeshi la Kujenga Taifa ifikapo mwaka 2024/2025 ni kuhakikisha linaongeza maeneo ya kilimo kutoka ekari 14,200 zinazolimwa sasa hadi kufikia ekari zaidi ya 28,000 sanjari na kuongeza eneo la umwagiliaji katika shamba la Chita kutoka ekari 2,500 zinazojengwa kwa sasa hadi kufikia ekari 12,000 ifikapo 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hiyo basi, mimi naamini wazi kwamba hata baada ya muda huu vijana watapata nafasi ya kujiajiri kwa sababu sasa hivi ni kweli vijana wetu wanapoambiwa wanakwenda JKT wazo la pili walilonalo ambalo wanaondoka nalo ni kupata ajira. Lakini

ukweli ni kwamba JKT inakwenda kuwajengea uwezo wa kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa naamini wazi kabisa kwamba tukihamasika hata sisi Wabunge kuwatumia wale vijana waliomaliza JKT kuwaweka katika makundi ya uzalishaji kwenye maeneo yetu, watakuwa na tija ya kutosha kabisa. Kwa hiyo, nipende tu kusema hayo, lakini naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Mhandisi Elias John Kwandikwa, ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba uniruhusu nimshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu na kuweza kuhitimisha hoja yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe mwenyewe kwa kutupa nafasi hii, lakini nakushukuru sana kwa kuweza kuongoza mjadala huu kwa umahiri na weledi mkubwa, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kurudia kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuniteua, kuniamini na kunipa nafasi hii ili niweze kulitumikia Taifa kwa kuiongoza Wizara hii, namshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nilikuwa na pacha wangu hapa, Mheshimiwa Mwanaidi, utaona kwamba nilikaa kwa utulivu. Unajua ukikaa na mama mambo yanakuwa barabara, sikuwa na *pressure*, nilikuwa napata ushauri wa kutosha. Kipekee nimshukuru sana, lakini pia nimefanya zoezi la kudumisha Muungano wetu. Ninamshukuru sana. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepata wachangiaji wengi, Waheshimiwa Wabunge 26 kama sikosei wamechangia kwa kuzungumza, nilipata pia michango ya Waheshimiwa Wabunge wawili ambao waliitoa kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nitumie nafasi hii kuwapa pongezi nyingi sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao, lakini nipokee pia pongezi nyingi ambazo Waheshimiwa Wabunge mmezitoa kwa wingi sana, lakini pia mmewapongeza wenzangu hapa, Jenerali pamoja na timu yake na Wizara kwa ujumla. Kwa hiyo, hizo pongezi nazichukua na ninazifikisha kwa kweli kwa uzito ule ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, niwashukuru mmeonesha dhamira ya dhati ya kuona kwamba Wizara yangu inapata fedha za kutosha na sina mashaka Waheshimiwa Wabunge kwamba mtatupitishia bajeti hii ili twende tukafanye kazi yetu, tukatimize jukumu letu. Kikubwa hapa ni kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu maneno yenu yametutia moyo sana, pia mmetupatia maeneo ambayo sisi tukitoka hapa kwa michango na ushauri wenu tunakwenda kuufanyia kazi, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kumshukuru sana Mheshimiwa Pinda, amezungumza kwa kirefu juu ya masuala ya ardhi. Lakini ninafikiri nianze na hilo na niongezee kidogo kuwatoa hofu Waheshimiwa Wabunge, nimewasikia Waheshimiwa Wabunge, Mbunge wa Biharamulo umezungumza hapa juu ya eneo la Biharamulo na changamoto zake, na siyo hapa tu, Waheshimiwa Wabunge hawa tumekuwa na mijadala na majadiliano kule nje ya Bunge ili kuhakikisha kwamba changamoto ambazo zipo kwenye masuala ya ardhi tunakwenda kuzitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba nimewasikia, nimemsikia

Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara, nimekusikia ndugu yangu Mheshimiwa Tabasam kule Sengerema na ulizungumza na kunipa historia ya muda mrefu sana na maeneo mengi kwa kweli yenye mgogoro ni migogoro ambayo ilikuwa imekaa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siiti mgogoro, naona tu kwamba ni changamoto ambazo zilijitokeza kwa sababu maeneo ya Jeshi ni mengi, tunayo maeneo mengi na wakati mwingine wananchi ulifika wakati wakaona labda saa nyingine hatuyahitaji, lakini maeneo yote tuliyokuwa nayo tunayo kwa ajili ya kuona kwamba lile jukumu la ulinzi linakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimewasikia Waheshimiwa kule Kyerwa na Katavi kwa Mheshimiwa Taska Mbogo, mchango wa maandishi wa Mheshimiwa Martha Mariki naye alizungumza kuhusu mgogoro ambao upo. Lakini kimsingi ninataka niseme tu kwamba katika maeneo yote tunakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo hili pia tulisikia kuhusu kule Kaboya kama sikosei, lakini pia tulikuwa tumezungumza hapa na ananitazama hapa Mheshimiwa Dkt. Bashiru kwamba ile *issue* ya maeneo yale, nitakwenda lakini taarifa ambazo zipo ni kwamba pia wenzetu wa milki, kwa sababu tulianzisha Kitengo cha Milki ili kurahisisha uratibu na kuhakikisha kwamba changamoto ambazo ziko kwenye maeneo ya ardhi tunakwenda kuzimaliza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kuishukuru Serikali, tumepokea fedha kwa ajili ya kuifanya ile timu yetu ambayo inakwenda kuhakiki maeneo yetu ambayo yana changamoto, inakwenda kufanya kazi. Na nikuhakikishie tu kwamba kati ya maeneo 94 yaliyokuwa na changamoto likiwepo eneo ambalo Mheshimiwa Esther Matiko amelizungumza, lenyewe limefikia katika hatma yake, fedha zipo, wataalam wamekwenda, tunakwenda kulimaliza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na maeneo yako mengine kama 44 hivi ambayo kwa sasa timu yetu ya milki imepata fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya kwenda kumaliza mgogoro katika maeneo haya. Kwa hiyo, niseme maeneo yote Waheshimiwa Wabunge nimewasikia yaliyokuwa na changamoto ya migogoro hii ya ardhi, tutakwenda kuimaliza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba nimepokea pia ombi la kwenda kwenye maeneo kadhaa, na baada ya Bunge lako hili tutakwenda kule na mimi napenda nikienda katika maeneo haya niende wataalam wakiwa wamemaliza changamoto zilizokuwepo kwenda kuwatia moyo wananchi wetu na kuhakikisha kwamba tunasonga mbele. Na tunafanya zoezi la kuhakikisha kwamba tumekwenda kutengeneza maeneo haya yawe na hati miliki. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Pinda kwa ufafanuzi wake kama alivyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nigusie kidogo maeneo ambayo Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama imetoa mapendekezo hapa. Niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali ni sikivu, na mimi ninaamini kabisa Waheshimiwa Wabunge Kamati hii ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama watakubaliana na mimi kwamba tumekuwa na mijadala mizuri ya kuhakikisha kwamba tunafanya Jeshi letu linakwenda kutekeleza majukumu yake kisawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote ambayo wameonesha kwenye ripoti, yako mengi ambayo tayari tumeshachukulia hatua nzuri, yako kwenye hatua nzuri na yako mengine ambayo yako kwenye mipango mizuri ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kuyatekeleza. Ninaamini kabisa maelekezo na ushauri wa Kamati utakwenda kutuboreshea utendaji kazi wetu katika Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kueleza machache yaliyoko kwenye ripoti ya Kamati, ninaomba nitoe ufafanuzi kwamba takwimu za utekelezaji wa bajeti kwa

mwaka wa fedha 2020/2021 ambazo nimezionesha zilikuwa ni kwa kipindi ambacho kinaishia hadi Aprili, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ninataka niseme kwamba kiwango kikubwa cha bajeti ambacho tumepokea baada ya Aprili, 2021 kwamba tumepokea fedha nyingi kwa ajili ya kukamilisha na kuendelea na shughuli zetu za mafunzo ya Jeshi, upande wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, ukarabati wa miundombinu na shughuli za mashirika ambayo tunayasimamia katika Wizara. Kwa hiyo, tumeendelea kupata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Mambo ya Nje imeshauri pia Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha za maendeleo kwa Fungu 39 kwa mtiririko uliopangwa, aidha, itoe kwa ukamilifu fedha zote za maendeleo ambazo bado hazijatolewa katika Fungu 38 – Ngome na Fungu 57 – Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka niseme tu kwamba katika mwaka wa fedha 2020/2021, Fungu 39 liliidhinishiwa shilingi bilioni nne kwa fedha za maendeleo, lakini mpaka ninapozungumza tumepokea shilingi bilioni 3.5 na ushehe hivi. Kwa hiyo utaona kwamba karibu asilimia 100 ya fedha zote tulizotengewa tunazipata. Ninao uhakika mpaka tutakapokwenda kumaliza mwaka tutakuwa tumepokea asilimia 100. Naishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Fungu 57 – Wizara kupitia Fungu 58 – Ngome tumepokea shilingi bilioni 83.8 kati ya shilingi hizo bilioni 150. Lakini pia tulipokea shilingi bilioni 9.694 kati ya shilingi bilioni kumi mtawalia. Ninataka nioneshe tu kwamba kuanzia kipindi kile cha Aprili mpaka sasa hivi mtiririko wa fedha kwa kweli tunashukuru sana, ni mzuri. Tunakwenda vizuri sana.

Kwa hiyo, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tu kwamba ninaamini kabisa kwa makubaliano na Wizara ya Fedha kwa mazungumzo tulifanya na tukakubaliana, mpaka kufikia Juni tutakuwa tumefanya mapokezi makubwa na saa nyingine itakuwa kwenye rekodi

nzuri katika kipindi hiki kwamba ninaweza nikasema haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilitushauri kukamilisha mpango wa kuwapatia wahitimu wote wa kidato cha sita mafunzo ya JKT. Tunashukuru kwamba tumeendelea kupata fedha, ndiyo maana utaona kwa rekodi ya wanafunzi waliomaliza kidato cha sita kwa sasa hivi kwa fedha tulizopata tutakwenda kupokea wanafunzi hawa 35,000 ukilinganisha na kipindi kilichopita tulipokea wanafunzi 21,000. Kwa hiyo, unaona kwamba mambo yanakwenda barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokea pia pesa kama nilivyosema, kwa ajili ya JKT, hizo shilingi bilioni 3.5 kati ya bilioni nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishauri kwamba tukamilishe haraka mpango wa kuwezesha vijana kujitolea kwa ajili ya mafunzo ya JKT kwa kuwapatia mitaji kwa kushirikiana na sekta na taasisi nyingine. Huo mpango ndiyo upo kama nilivyowahi kueleza hapo awali pia, kwamba tunafungamanisha sasa mafunzo haya ili tuweze kuwapokea watoto kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali zikiwemo Wizara kama ya Kilimo, Mifugo, Viwanda na Fedha ili tuone kwamba tutakuja na mpango kwamba vijana wetu wote ambao wanamaliza na kupata ujuzi tunakwenda kuwawezesha ili sasa yale mafunzo yao yalete maana kwa maana ya kwamba waweze kupata kazi ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niaombe tu Waheshimiwa Wabunge wakiwemo Wabunge vijana ambao mmezungumza kwa uchungu sana kuhakikisha kwamba hawa vijana ambao tunawaanda ili tutakapowarudisha wakirudi kule wakiwa wamepata mafunzo wamesheheni mambo mbalimbali, sasa waweze kwenda kujitegemea lakini pia kutoa mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, mambo yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala ambalo pia Kamati imetushauri kwamba katika miradi yetu Kamati imeona kwamba wakati mwingine tunapata fedha hizi za ufadhili zinakuwa na utaratibu wa kuwa labda imehitaji mshauri elekezi akatoka sehemu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri huu pia tumeuchukua kwamba tutaendelea kuona kwamba tunaisimamia vizuri ili pale tunapopata fedha au tumefadhiliwa, lakini mshauri mwelekezi awe sehemu yetu ili tuweze kufanya kulingana na mahitaji yetu. Kwa hiyo na hilo tumeweza kulichukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo mchango Waheshimiwa Wabunge wamezungumza juu ya kuliimarisha Shirika letu la Nyumbu pamoja na mashirika mengine. Nataka niseme tu kwamba tunayo mashirika, tuna Shirika letu hilo la Nyumbu *(TATC),* lakini pia tuna Shirika letu la Mzinga na SUMA JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumza juu ya Shirika letu hili la Nyumbu, kwanza tumepata fedha ambapo sisi wenyewe kupitia Nyumbu tunakwenda kutengeneza nguzo zile za umeme na kazi imeanza. Naishukuru sana Serikali, tumepata fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya maboresho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mpango wa kwenda kufanya ufufuaji, ip0 mitambo 116 ambayo kipindi cha nyuma ilifanya kazi vizuri, lakini pia kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia; upande wa Serikali tumejipanga vizuri, tumepata ule mpango wa maendeleo kwa ajili ya kuinyanyua Nyumbu. Na hii imekubalika Serikalini sasa tunakwenda kufanya maboresho makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, yako mambo mengi yatakwenda kufanyika kule Nyumbu na tunapenda pia Nyumbu iwe kitovu. Tutakwenda pia kuzingatia kuwachukua vijana ambao watakuwa na weledi wa tofauti, wabunifu. Tutajitahidi kuhakikisha kwamba

tunaifanya iwe *center* wale vijana wote ambao tunaona wanaweza kuwa na uwezo wa kitofauti tutawachukua. Lakini kazi yetu sisi ni kuwatengeneza na pia kuweza kuwatoa katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuona kwamba ule ujuzi wao tunauendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejipanga vizuri, tunakwenda kuiboresha Nyumbu na tutakwenda kuweka fedha za kutosha kabisa na utaratibu unakwenda sawasawa. Kwa hiyo Nyumbu tutakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mzinga tunafanya uzalishaji – Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanachangia, Mheshimiwa Ahmed alichanganya kidogo Nyumbu na Mzinga; Mzinga ndiyo tunazalisha yale mazao muhimu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tumejipanga vizuri kuhakikisha kwamba tunakwenda kufanya sasa uzalishaji wa mazao ya kutosha kwa sababu sisi wenyewe mahitaji ya yale mazao ni makubwa sana, lakini bado ziko taasisi nyingi za kiulinzi hapa nchini zinahitaji kupata huduma ya kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali pia muda siyo mrefu tumepokea fedha nyingi sana na tumeshaagiza mitambo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunakwenda kuzalisha kwa hali ya juu, kwa hiyo tumejipanga vizuri. Kule Mzinga tutakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengine ambayo tunakwenda kufanya maboresho kama nilivyozungumza, kule SUMA JKT. Kwa sababu taasisi zetu hizi zimejipanga sasa kwenda kufanya uzalishaji wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo niwatoe hofu tu kwamba tumejipanga kweli kweli na yako maeneo mengine tutakwenda kufanya maboresho ya sheria zetu ili kufanya taasisi zetu zifanye kazi, zitumie weledi, tuwatumie wataalam tuliokuwa nao vizuri bila kuwa na kikwazo chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo haya yote yanalenga kuhakikisha kwamba ile historia ambayo Waheshimiwa Wabunge mmekuwa mkiirejea kwamba tunayo historia ya taasisi zetu hizi kipindi cha nyuma tuliweza kutengeneza magari, tuliweza kutengeneza mpaka nyambizi, tutakwenda kufanya hivyo. Lakini tutakwenda kujikita zaidi pia kwenye eneo hili la utafiti, na ndiyo maana upande wa Serikali tumejiandaa na tulikuwa na andiko ambalo niko nalo hapa ambalo linalenga kwenda kuboresha taasisi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla niseme kwamba Wabunge walivyochangia nilikuwa najaribu kuangalia, angalau kuweka kwenye ma-*group* maeneo ambayo wamezungumza, kwa ujumla wake nikijaribu kupitia ninaona kwamba kulikuwa na masuala ya bajeti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini niseme tu kwa hali ya bajeti hii ambayo naiombea sasa hivi hapa kumekuwa na ongezeko la bilioni 217 kama nilivyozungumza, hii ni asilimia kumi, siyo haba. Lakini bado Serikali imeonesha nia kwamba huko tunakokwenda tutakwenda kufanya maboresho makubwa sana ya ongezeko la bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sana kwa *concerns* zenu, lakini naishukuru pia Kamati kwa sababu Kamati imezungumza vizuri sana na kutoa maelekezo. Kwa sababu uko umuhimu wa kupata fedha za kutosha ili hizi zana ambazo tunazimiliki tuweze kuzitunza, tuweze kuzifanyia mazoezi, kwa sababu ili tuweze kuwa vizuri zaidi upande wa mazoezi ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa masuala ya kibajeti mmezungumza masuala ya pensheni. Tumeanza kughughulikia suala la pensheni, tumeanza na *level* ya *Major Generals* na *Lieutenant General* na majenerali kuhakikisha kwamba ile sheria ambayo ilipitishwa tunakwenda kuitekeleza. Kwa hiyo, tunaendelea kuifanyia kazi kuona maslahi ya askari wetu tunayaweka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia yale masuala ya pensheni Waheshimiwa Wabunge mmezungumza hapa tunachukua ushauri wenu, lakini pia mmetoa pia masuala ya kibajeti juu ya ununuzi wa vifaa na hili tupo nalo vizuri, vifaa vya kwetu tulivyokuwanavyo tunavyo vya kisasa, tupo vizuri. Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi, tupo vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wamezungumza pia juu ya stahili za wanajeshi ni kweli zipo changamoto, lakini upo ukweli kwamba changamoto hizi tumezizungumza wenzetu wa Hazina, na ni ukweli kwamba tumewasilisha mahitaji yetu na mahitaji ya wanajeshi wetu ambayo wanadai na uhakiki unaendelea kukamilishwa kwa sababu tayari tumeshakuwa na mwelekeo na makubaliano kwamba tutakwenda kulipa haya madeni ya vijana wetu ambayo yamekaa muda mrefu. *(Makofi)*

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge nimewasikia na imetia moyo kuona mnawajali sana vijana wetu, Jeshi hili ni la kwetu, vijana hawa ni wa kwetu, lazima tuwahudumie ili waweze kutufanyika kazi nzuri, waendelee kufanya kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuhusu stahili zao na maboresho ya maslahi niliambie tu Bunge lako na mimi mwenyewe nipo mstari wa mbele kuhakikisha kwamba ninakuwa na jeshi ambalo ni la kisasa lakini jeshi ambalo linahudumiwa na jeshi ambalo sasa linakuwa na morali na motisha ya kutosha kwenda kufanya kazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili halina wasiwasi tumefanya vikao kadhaa kwa nia ya kufanya maboresho. Waheshimiwa Wabunge, niwatoe hofu tunakwenda kufanya mapinduzi makubwa ili jeshi letu hili zuri lenye sifa nzuri tuendelee kuona kwamba tunawatendea haki vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na kuhusu maeneo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla mmechangia ni juu ya mafunzo ya JKT, Mheshimiwa

Musukuma ulizungumza sifa, sifa zipo ndiyo maana tunaonesha sifa ya vijana wa kujitolea tumeionesha kuanzia darasa la saba tunakwenda, kwa sababu tunakata hata yule kijana ambaye hakubahatika kwenda shule, lakini akija kwetu tutamtengeneza, akirudi kule kijijini anakwenda kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sifa zipo zinamuonyesha kijana ambaye tutaweza kumchukua kwa ajili ya kujitolea na wale vijana kwa mujibu wa sheria. Kama mlivyozungumza kwamba sifa zipo tutaendelea kufanya hivyo, pale ambao patalazimika kuwa na kutengeneza sifa za ziada kulingana na mazingira ambayo tupo nayo tutafanya hivyo kwa nia hiyo hiyo yakuona kwamba tunaendelea kuwatengenezea vijana sifa nzuri, uzalendo, uchapakazi na kuweza kutoa mchango wao kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimuarifu tu Mheshimiwa Matiko hapa alizungumza kwamba kuna deni kule *SUMA guard,* labda hii rekodi ya miaka mingi lakini mpaka ninapozungumza sasa hivi kwa vijana ambao wameajiriwa huko *SUMA guard* hatuna deni. Kwa hiyo hii, kama labda saa nyingine sikukuelewa naomba tu baadaye tunaweza tukazungumza nikupate sawa sawa, eeh si ndiyo haina mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niseme tu pia ipo michango ilitolewa kuhusu ushirikiano wa JKT na JKU na ushauri uliotoka Mheshimiwa tumeupokea lakini niseme tu, nakuliarifu Bunge lako tangu mwaka 2001 yapo mashirikiano ambayo tunayafanya, tunabadilishana uzoefu, tunabadilishana mafunzo, tunabadilishana hata vijana kwa ajili ya kuona kwamba tunakwenda sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo niwatoe wasiwasi ndugu zangu na mimi hata nimetembelea kule Zanzibar na nina programu za kwenda Zanzibar pia, kwa hiyo nikitembelea kule nitaendelea pia kufanya mijadala kwa ni hiyo hiyo ya kuona kwamba tunafanya majeshi yetu

yanafanya kazi kwa ushirikiano wa hali ya juu ili kuona kwamba sisi wote tunakwenda sawa, kwa hiyo, Unguja nilikwenda na Pemba nitakwenda siyo mara moja, nitaendelea kwenda kwa nia hiyo hiyo ya kuona kwamba tunaweza kujiweka vizuri ili tuone kwamba tunatembea wote pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko la bajeti kama nilivyozungumza kwa ajili ya mafunzo kule JKT na pia kuna ushauri uliotolewa kwa ajili ya elimu ya muungano kupitia majeshi yetu tutaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu nilikuwa naona *record* pia ya bajeti hata ya JKT kwa maana ya mafunzo kwa mujibu wa sheria imeongezeka kutoka shilingi bilioni 16 kwenda bilioni 21.6 hii siyo jambo dogo, nilijaribu kuonyesha tu kwamba tunajitahidi sana kuomba fedha ili tuendane sambamba na mahitaji ya kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mambo mengine ambayo yalizungumzwa kwa ujumla ilikuwa ni ujenzi na ukarabati wa miundombinu ushauri tumeuuchukua, hata mimi nimetembelea hizi nyumba katika maeneo kadhaa tunahitaji kupaka rangi, tunahitaji kufanya maboresho na hiyo ni jambo la kawaida. Huwezi kujenga nyumba ukakaa nayo muda wote bila kuwa uliifanyia ukarabati na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mapungufu kadhaa ambayo tumeyaona hata tulivyokuwa na Kamati, tumejipanga kwenda kushughulikia upungufu wa nyumba lakini upo mpango pia wa kuendelea kujenga nyumba kwa ajili ya wanajeshi wetu, mmeshuhudia nyumba nyingi zimejengwa kwa kipindi kifupi, lakini mpango ule siyo kwamba umeisha tunaendelea kwenda kuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengine walizungumza juu ya mchango wa jeshi letu kwa ajili ya ulinzi wa amani. lakini pia Mheshimiwa Lucy Mayenga alizungumza juu ya kuongeza idadi ya akinamama katika *operation* zetu. Niwahahakishie tu asilimia 6.5 ya wanajeshi waliopo kwenye

*operation* tunao akinamama, yapo mahitaji mengine ni maalum yanahitaji akinamama wanajeshi kuwasaidia wenzetu katika maeneo ya *operation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kunapokuwa na machafuko maeneo kadhaa waathirika wakubwa ni akina mama na watoto, tunahitaji pia kuwa na weledi kupitia jeshi letu kuweza kusaidia. Kwa hiyo tutaendelea kuongeza idadi kadri itakavyokuwa kwa sababu yapo makubaliano ambayo tunayafanya na wenzetu tunapokuwa tunapeleka askari kwenye *operation.* Kwa hiyo, tutaendelea kuona hivyo na tunafanya mijadala mingi ili kuona kwamba tunakidhi mahitaji ya wanajeshi wetu katika ulinzi wa amani katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu, kama nilivyozungumza juu ya upimaji na uthamini wa ardhi kwamba mambo tumechukua lakini Wabunge wengi pia walizungumza juu ya huduma za afya, ndiyo maana tumejipanga na Waheshimiwa Wabunge msiwe na wasiwasi kwa wale ambao mngeweza kupata nafasi ya kutembelea kule Lugalo mnaweza kuona kwamba tumetengeneza eneo maalum kwa ajili ya kumudu magonjwa hatari ikiwemo *Ebola* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule utaona, tunavyo vifaa maalum. Mheshimiwa Kuchauka, yapo maeneo ukifika kule utashangaa maana yake mimi nilishangaa na mimi kidogo nina uzoefu kidogo, sasa wewe uliyetoka Liwale nafikiri ukienda kule nikukaribishe uone mambo mazuri ambayo yanafanyika kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejipanga kwa ajili ya kupokea hatari yoyote ikitokea kwa sababu wanajeshi wetu wanapokwenda kwenye *operation* pia kuna maeneo yana hatari sana, kwa hiyo tumejipanga hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini zaidi ya hapo kama nilivyozungumza kwenye hotuba yangu asilimia 80 ya huduma tunazotoa kwenye hospitali zetu ni kwa raia wetu

kwa watanzania wenzetu. Kwa hiyo, unaona kwamba tunavyoimarisha hospitali zetu inalengo pia ya kwenda kuwahudumia wananchi wa watanzania na tunaendelea kufanya hivyo ndiyo maana tumeona kwa sababu Serikali sasa imehamia hapa Dodoma tumeanza ujenzi pale Msalato na ujenzi huu fedha tunazo, tutasimamia kuhakikisha hospitali hii inakamilika ili sasa tuweze kugawana kutoa huduma katika maeneo ya kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani muda upo kwenye nafasi yangu, nimalizie tu, kukushukuru sana, nikushukuru sana kwa kuendesha mjadala, lakini Waheshimiwa Wabunge nimeona leo wametulia sana, kwa hiyo, ninawashukuru sana, walikuwa makini sana na nilifikiria kwamba saa nyingine tutakuwa na wachangiaji wachache, lakini tumepata michango mingi sana, na saa nyingine niseme tu siyo rahisi michango yote niweze kuizungumza moja kwa moja, lakini niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge tumewasikia na leo timu yangu ilikuwa kubwa kwa sababu ya kuhakikisha kwamba hatuachi neno hata la Mheshimiwa Mbunge mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ndiyo jeshi letu, jeshi letu limejipanga vizuri kama mnavyoliona hakuna mashaka, jambo lolote Waheshimiwa Wabunge mmelizungumza hapa tunaenda kulifanyia kazi kwetu sisi ndiyo mmetupa kazi ya kuweza kuhakikisha kwamba tunawatumikia watanzania kwa weledi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kuwapongeza sana Katibu Mkuu yupo hapa na viongozi wote wa Jeshi wapo hapa, kazi nzuri inafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata nafasi kadhaa ya kuzungumza na wenzetu kutoka nje ya nchi na kwenye mashirika mbalimbali, jeshi letu linatamanisha sana liwepo maeneo mengi, mchango wake ni mkubwa na mchango wake ni mzuri sana, jeshi letu lipo katika ubora wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa NaibU Spika, kwa hiyo mimi naendelea kuwapongeza najisikia furaha sana kuwa Waziri katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza na Kitabu cha Pili, Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ukurasa wa 386.

**FUNGU 57 – WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management*......Sh. 17,953,760,700

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Fungu hili ndilo lenye mshahara wa Waziri kwa hivyo kuna Wabunge wanahitaji ufafanuzi, ninalo jina moja tu hapa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, sina dhamira ya kushika shilingi, lakini nataka ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri sote tumesikiliza mijadala ya Wabunge wengi kuhusiana na migogoro iliyopo ya ardhi kati ya wananchi na Jeshi la Wananchi la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2021 kuna maeneo tulipitisha fedha hapa kwamba wanaenda kulipa fidia kama Kikombo, Duluti na kwingineko, mwaka 2019/2020 zilipitishwa fedha hapa mfano Tarime na wakasema *evaluation* ni ndogo ya *1.4 billion* wanaenda kufanya *re-evaluation* na mwaka 2021 Waziri wa Ulinzi ambaye sasa hivi ni Rais wa Zanzibar na Waziri wa Fedha *by then* ambaye sasa hivi ni Makamu wa Rais wakasema fedha zipo na shilingi tulishika akasimama Naibu Waziri akasema fedha zipo zinaenda, lakini hazikwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo wakati Naibu Waziri wa Katiba anajibu Duluti ya Arusha imeshushwa fedha kutoka *7.4 billion* wanasema mwaka huu wanaenda kulipa *4.9 billion* na ilitakiwa ilipwe kwa mwaka wa fedha uliopita na Kikombo, Tarime imebaki ileile ya mwaka 2019/2020 na maeneo mengine yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nataka *commitment* ya Serikali na wala siyo kwenye wizara yako, najua tatizo lipo kwenye Wizara ya Fedha kwa masikitiko wapo hapa kujibu, nataka *commitment* ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri mwenyewe umeanisha maeneo mengi hapa ambayo yanahitaji utatuzi wa migogoro, tunataka *commitment* Serikali ipeleke fedha ambazo umepitisha hapa maeneo uliyoyataja ikiwepo Tarime, lakini watafute na fedha zingine kuweza kutatua migogoro yote ambayo ipo ili sasa Jeshi la Wananchi wa Tanzania waweze kukaa kwenye zile kambi kwa *harmony* na wananchi waweze kuendeleza maisha yao huko kwingine

watoke kwenye haya maeneo ambayo mmeamua kuyatoa. Naomba *commitment* ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Matiko amesema hana hata nia ya kushika shilingi, lakini nilitaka tu nimhakikishie Mheshimiwa Matiko na Waheshimiwa Wabunge kwamba tupo *committed* na kwa kushirikiana kama mwenyewe alivyoliweka sawasawa kwamba tunashirikiana na wenzetu wa Ardhi, tunashirikiana na *Chief Valuer*, tunashirikiana na viongozi wa Serikali za Mikoa na Wilaya.

Kwa hiyo, na kwa kuongezea ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na uratibu mzuri ndiyo maana tumeanzisha sasa Kitengo Maalum cha Milki ambacho wakilala wakiamka ni kwa ajili ya kwenda kuhakikisha kwamba migogoro inaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na matokeo yake yameonekana kama nilivyozungumza kwamba yapo maeneo kwa idadi, kwa uwingi ambayo tayari migogoro imeisha; na yapo maeneo ambayo yapo kwenye hatua nzuri na ikifika masuala ya fedha na haki za wamiliki wa maeneo lazima twende kwa umakini.

Kwa hiyo lile zoezi la uhuwishaji kama tulivyokuwa tumechelewa kule nyuma ndiyo nilileteleza kuona kwamba tunahakikisha kwamba huyu mwananchi wa Tarime na mwananchi wa sehemu nyingine anaenda kupata haki yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna wakati mwingine kama kulikuwa na uchelewashi ni kwa sababu ya kuhakiki kwamba tumeenda kutenda haki. Sasa kwa mfano kama saa hizi fedha za Tarime tunazo isingekuwa rahisi sasa tuzibebe tu twende tukaanze kulipa halafu tukabakia hatukuwa tumewatendea haki wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Matiko wala usiwe na wasiwasi tumejipanga vizuri na ndiyo maana unaona tumepokea zaidi ya bilioni nzima kwa ajili ya kuiwezesha hii timu ninayoitaja ya Milki kuhakikisha kwamba tunaenda kumaliza migogoro ambayo ilikuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na migogoro tisini na nne, lakini karibu asilimia 50 yote tumeshaimaliza na kasi ipo kubwa, tupo *committed* kuhakikisha kwamba hawa Watanzania ambao wanalipenda jeshi lao ambalo wameachia maeneo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba jeshi linafanya kazi yake nzuri na wao lazima tuwandee haki kuona kwamba wanapata haki zao.

Kwa hiyo Mheshimiwa Matiko wala usiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit* ... ... Sh. 180,321,900
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Division* ... ...Sh. 485,934,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*... ... ... ... ... ... Sh. 172,246,000
Kifungu 1005 - *Procurement Management Unit*..Sh. 131,060,000
Kifungu 1006 - *Legal Services Division* ... ... ... ...Sh. 95,109,300
Kifungu 1007 - *Government Communication Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 131,651,000
Kifungu 1009 - *Information and Communication Technology* ... ... ... ... ... ... ... Sh. 177,680,200
Kifungu 2001 - *Industries, Construction and Agriculture Division* ... ... ... ... ... ...Sh. 260,770,000
Kifungu 2002 - *Military Research and Development Division* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 308,021,400
Kifungu 2003 - *Building Consulting Unit* ... ... ... ... ... ... ...Sh. 0
Kifungu 2004 - *Estate Management and Building Consulting Division* ... ... ... ... ... Sh. 269,766,900

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi ya bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 38 – NGOME**

Kifungu 1001 - *National Defence Headquarter... ... ... ... ... ...* Sh. 1,770,317,585,700

**MWENYEKITI:** Rudia.

Kifungu 1001 - *National Defence Headquarter... ... ... ... ... ...* Sh. 1,770,317,585,700
Kifungu 1006 - *Defence forces Headquarter Command ... .... ... ... ... ...* ...Sh. 1,596,916,800
Kifungu 1007 - Land *Forces Command ... ...*Sh. 2,454,362,000
Kifungu 1008 - *Air Defence Command ... ... ...* Sh. 2,277,404,700
Kifungu 1009 - Navy *Command ... ... ... ... ...* Sh. 1,283,488,400
Kifungu 1010 – *Military Hospitals ... ... ... ... ...*Sh. 1,545,527,400

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi ya bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 39 - JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Kifungu 1001 – *The National Service Force*...Sh. 382,474,955,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tujielekeze kwenye Kitabu cha Nne – Matumizi ya Maendeleo, Fungu 57 ukurasa wa 146.

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 57 – WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Division... ...* Sh. 350,000,000
Kifungu 1009 – *Information and Communication Technology Unit... ... ... ... ...* ...Sh. 3,500,000,000
Kifungu 2001 – *Industries, Construction and Agriculture Division... ... ... ...*Sh. 23,500,000,000

Kifungu 2002 – *Military Research and Development Division*... ... .. Sh. 97,350,000,000
Kifungu 2004 – *Estate Management and Building Consulting Division*... ... ... Sh. 15,300,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 38 – NGOME**

Kifungu 1001 – *National Defence Headquarter (NDHQ)*... ... ...... ... ...Sh. 32,578,424,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 39 - JESHI LA KUJENGA TAIFA**

Kifungu 1001 – *The National Service Force*... ...Sh. 4,000,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 Kanuni ya 123(3)(a) na (b) naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako likikaa kama

Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwamba, kile alichokuwa amekiomba kupitia bajeti yake Bunge limepitisha bila kutoa shilingi.

Kwa hiyo, tunakutakia kila la kheri wewe na watendaji wako ambao wako hapa, tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa bajeti hii. Na kwa maelezo uliyoyatoa awali kwenye kitabu chako cha bajeti lakini pia kwenye ufafanuzi kwenye hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, tunaamini ili kuidhinisha hayo maombi uliyoyaleta basi mambo mengi yanaenda kutekelezwa na kwa kweli ule utulivu tunaouona, tunaamini utaendelea kuwa hivyo na pengine utaongezeka zaidi pale ambapo migogoro ambayo umeisema yote mnaenda kuifanyia kazi. Basi tunaamini mambo yatakuwa mazuri, tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yenu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nichukue fursa hii pia kuwashukuru sana wenzetu wa Kamati inayoongozwa na Mheshimiwa Zungu kwa kazi nzuri wanayoifanya kuisimamia Wizara hii muhimu kabisa na nyeti. Tunafahamu wanajitahidi sana pengine wakati mwingine wanapata na taarifa za ziada, lakini wanajitahidi kujizuia, ndio maana nchi yetu inaendelea kuwa salama. Kwa hiyo, tuwapongeze sana

Kamati hii na Wajumbe wote pamoja na uongozi wa Kamati hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini pia michango yenu leo imeashiria kwamba uelewa ni mkubwa kwenye mambo haya ya ulinzi na usalama wa nchi yetu na ni dhahiri kwamba, pamoja na kufuatilia lakini michango mingi imeashiria kwamba tunafahamu mipaka yetu yapi tuongee na yapi tusizungumze. kwa hiyo, ninawapongeza sana sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Sasa ulifika mahali nikawa nasikiliza kuna Wabunge wanataja silaha kutengenezwa na mambo kama hayo, lakini nadhani ni mambo ya kawaida kwa ile Kamati itakuwa inaelewa, lakini sisi wengine basi tukisema hayo msione kama tunataka vile muanze kutueleza tuna vifaru vingapi na ndege ngapi na risasi mnatengeneza au hamtengenezi na mambo kama hayo. Lakini hii inaashiria kwamba, pamoja na uelewa mkubwa wa Waheshimiwa Wabunge ni muhimu kama Wizara kuangalia mambo machache ambayo mnaweza kuwa mnafundisha. Kuacha wale watu wa kamati peke yao, lakini Bunge zima kuelewa utaratibu wa mambo yanavyokwenda, ili hata sisi kwasababu wakati mwingine huwa tunasafiri, tujue mambo gani tunaweza kuzungumza. *(Makofi)*

Maana mtu anaweza akaenda huko akasema yaani nchi yetu sisi hatufanyi kitu chochote au asijue kwamba haruhusiwi kusema, lakini akaenda sisi tuna Shirika kule linatengeneza mambo fulani, kwa hiyo, ni vizuri tukifahamu mambo haya. Nafahamu huwa mna huo utaratibu lakini ni vizuri pengine na Wabunge kwa ujumla wapate hiyo fursa ya kufahamu. Tunawashukuru sana, tunawapongeza sana na Wajeshi wetu karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilitaka kukumbusha mambo mawili; la kwanza, ni jambo ambalo limetokea sasa nawakumbusha kidogo kwa sababu ya utaratibu wetu, mafunzo tunafanyia hapa hapa ndani. Mbunge anaruhusiwa kuwaambia pengine Wabunge wengine wamuunge mkono kwenye hoja anayoweza kuwa amesema, ama wamuunge

mkono kwenye mawazo yake yaani kwamba na wao wachangie kwa namna hiyo ili Serikali ielewe.

Lakini Mbunge hawezi kuzungumza na Wabunge ili wafanye kitendo fulani humu ndani kwa sababu Mbunge ili aweze kuzungumza lazima aruhusiwe hapa mbele, ili aweze kusimama aruhusiwe hapa mbele. Kwa hiyo sasa, ukisema Waheshimiwa Wabunge naomba mpige makofi unakuwa kidogo umeenda nje ya utaratibu, maana umewafanya Wabunge wafanye kitendo ambacho hawajaambiwa na mimi wafanye.

Kwa hiyo, sasa tukifanya hivyo itakuwa mtihani mtu atakuja kupata msiba mahali akasema, naomba tusimame tuwakumbuke marehemu halafu Kiti kikakataza, itaonekana kama yaani hawa jamani mbona wanakuwa wakali sana hawajui kama kuna watu wamefariki sehemu.

Kwa hiyo, hizi ni taratibu tutaendelea kujifunza nawakumbusha tu, ni mazingira hayo ndio unaweza kuwaomba Wabunge wenzio na unavyowaomba sio kwamba wanakujibu kwamba ndio tutakuunga mkono, yaani unawashawishi kwamba watakapochangia wafanye hivyo ama unawaomba wakuunge mkono, ambapo hawazungumzi chochote saa ya kukuunga mkono wanasimama tu na mimi nitawaona.

Kwa hiyo, Mbunge haruhusiwi kuwaambia watu wengine wasimame, wapige makofi, ama washangilie au wafanye hivi, ama hata wazomee, haruhusiwi kusema sasa tumzomee fulani. Kwa hiyo, nadhani hilo limeeleweka vizuri. *(Makofi)*

Jambo la pili, ambalo ningependa kusisitiza Waheshimiwa Wabunge ni jambo lile la kupima. Mheshimiwa Spika, ameleta watu wazito hapa jamani wataalam mbalimbali kwa ajili ya kupima afya za Wabunge na hawa watu wapo mpaka wiki ijayo, niwasihi sana mkatazame afya zenu kwa sababu tunakaa sana kwa hiyo ni muhimu ukifahamu afya yako. Sasa hapa anayekaimu nafasi ya

Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni yeye ameonesha mfano mzuri.

Kwa hiyo, naamini watu wote wa Serikali watamfata Kaimu Kiongozi hapa kwenda kupima, yeye ameshaenda kupima jamani na majibu yake kachukua leo, kwa hiyo msiwe na wasiwasi kwamba pengine hajachukua majibu. *(Makofi)*

Kwa upande wa walio wengi wameongozwa na Mheshimiwa Jenista naye ameshaonesha mfano wa kupima lakini, katika wale wapimaji ambao mimi nimewaona maana hata mimi imebidi nioneshe mfano maana watu wanaweza kusema yeye mwenyewe ameenda jamani kupima? *(Makofi/Kicheko)*

Mimi mwenyewe nimepima na ninao mashahidi wengi kabisa humu ndani mkiwaona watu wanapiga makofi ujue ndio mashahidi wangu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa upande wa wanaume kidogo ni wachache, wale ambao mimi nimeonana nao mwenyewe ni Mheshimiwa Lukuvi, Mheshimiwa Geophrey Pinda na Mheshimiwa Tabasam; nataka kuamini kuna na wengine wameenda lakini basi muende wengi, kwa sababu yaani wanaume niliowaona mimi ni watatu, halafu wanawake nikiwataja wanaweza kufika 20 au nitaje mifano? *(Kicheko)*

Haya mimi mwenyewe moja, Mheshimiwa Jenista, Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Stella Fiyao kuna mtu anahisi nimemsahau Mheshimiwa Mama Sitta hawa wote niliwakuta pale. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge niwaombe twende huko, Mheshimiwa Felista Njau naye alikuwepo, jamani tujitahidi tukapime. Zoezi hili ni la muhimu sana sana sana kwetu sote na inampa picha pia Mheshimiwa Spika kujua Wabunge wake afya zao zikoje ili ajipange vizuri, si ndio jamani. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, nawatakia kila la kheri katika hilo zoezi la upimaji lakini ukishapima ukachukue majibu, sisi tumekuonesha mfano hao wote niliowataja hapa wamepima na wameenda kuchukua majibu. Kwa hiyo, usipime tu halafu ukaondoka. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kama tulivyokuwa tumesema asubuhi, kesho ni siku ya Jumamosi lakini Bunge litaendelea.

Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.33 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi, Tarehe 22 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*